*TANZANIA OSAKA ALUMNI*

# Kitabu cha

# Mbinu Bora 4

**Ofisi ya Rais**
**Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**
**P.O. Box 1923,**
**Dodoma.**

**Desemba, 2017**

# KITABU CHA MBINU BORA 4

# (2017)

**Kimeandaliwa kwa ajili ya Tanzania Osaka Alumni (TOA) na:**
**Paulo Faty, Mhadhiri, Chuo Kikuu Mzumbe;**
**Ahmed Nassoro, Mhadhiri Msaidizi, LGTI; na**
**Michiyuki Shimoda, Mshauri Mwanadamizi, OR-TAMISEMI**

**Na kuhaririwa na:**
**Liana Hassan – Makamu Mwenyekiti, TOA**
**Stella Paschal – Afisa Serikali za Mitaa Mkuu, OR-TAMISEMI**
**Emmanuel Mkongo – Mchumi Mwandamizi, OR-TAMISEMI**
**Honorina Ng'omba – Mtaalamu Mshauri Kitaifa, OR-TAMISEMI**

# Yaliyomo


| Yaliyomo | Ukurasa |
|---|---|
| Vifupisho | i |
| Dibaji | iv |
| Utangulizi (TOA) | v |
| Utangulizi (JICA) | vi |
| SURA YA KWANZA:MASUALA YALIYOIGWA KUTOKANA NA UZOEFU WA JAPANI | 1 |
| SURA YA PILI:JITIHADA ZA JAMII KWA AJILI YA HUDUMA BORA | 20 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Lindi: Ujenzi Shirikishi wa Barabara za Vijijini | 23 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea: Ushiriki na Jitihada za Jamii Katika Ujenzi wa Boma | 32 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Masasi: Jitihada za Jamii Katika Ujenzi wa Zahanati ya Mapili | 41 |
| Halmashauri ya Mji wa Masasi: Jitihada ya Jamii Kuboresha Elimu ya Msingi | 49 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya: Jitihada za Jamii katika Miradi ya Barabara na Maji | 57 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Momba: Jitihada za Jamii Katika Kujenga Madaraja Bembea | 65 |
| Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya: Jitihada ya Marafiki wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Mbeya | 73 |
| SURA YA TATU: UGATUAJI WA MASUALA YA FEDHA NA UBORESHAJI WA MAPATO | 82 |
| Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni: Mfumo wa Digitali wa Ukusanyaji Mapato | 84 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba: Matumizi Mkakati ya Mapato ya Ndani Kukidhi Mahitaji ya Jamii | 95 |
| SURA YA NNE: USHIRIKISHWAJI WA JAMII KATIKA UTOAJI WA HUDUMA | 104 |
| Halmashauri za Lindi, Kilwa, Ruangwa na Chunya: : Uboreshaji wa Huduma Kupitia Utunzaji Shirikishi wa Misitu | 107 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo: Upangaji Shirikishi wa Mji wa Lwangwa | 126 |
| Halmashauri ya Manispaa ya Ilala: Usafi, Ujanishaji na Upendezeshaji Mazingira Katika Shule za Msingi | 139 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Ileje: Ujirani Mwema Kati ya Tanzania na Malawi | 147 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Newala: Uboreshaji wa Huduma za Elimu Kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Elimu | 156 |
| SURA YA TANO: MAENDELEO YA JAMII KIUCHUMI | 163 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga: Uboreshaji wa Kipato Kupitia Uzalishaji Bora wa Zao la Kahawa | 166 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Masasi: Uboreshaji wa Umwagiliaji kwa Uhakika wa Chakula na Kipato | 176 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru: Uzalishaji wa Mpunga na Uongezaji wa Thamani | 183 |
| REJEA | 193 |

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| ALAT | Association of Local Authorities In Tanzania |
| AMCOs | Agricultural Marketing Cooperatives |
| AMSDP | Agricultural Markrting Systems Development |
| ASDP | Agriculture Sector Development Programme |
| ATM | Automatic Teller Machine |
| BOQ | Bill of Qauantitie |
| BOT | Bank of Tanzania |
| CDO | Community Development Officer |
| CG | Central Government |
| CHF | Community Health Fund |
| CHMT | Council Health Management Team |
| CMT | Council Management Team |
| COBET | Complementary Basic Education |
| CPU | Coffee Processing Unit |
| CRC | Convention on the Rights of the Child (1990) |
| CUF | Civic United Front |
| DADPs | District Agricultural Development Plans |
| DAIO | District Agricultural and Irrigation Officer |
| DANIDA | Danish International Development Agency |
| DAS | District Administrative Secretary |
| DbyD | Decentralization by Devolution |
| DC | District Council |
| DED | District Executive Director |
| DEO | District Education Officer |
| DIDF | District Irrigation Development Fund |
| DIDT | District Irigation Development Team |
| DLNRO | District Lands and Natural Resources Officer |
| DLO | District Land Officer |
| DSM | Dar es Salaam |
| ELCT | Evangelical Lutheran Church of Tanzania |
| E-PRA | Extended Participatory Rural Appraisal |
| ESD | Education for Sustainable Development |
| FMD | Foot and Mouth Disease |
| FSC-UK | Forest Stewardship Council – United Kingdom |
| FST | Forest Scout Teams |
| FY | Financial Year |
| GIS | Geographical Information System |
| GPS | Global Positioning System |
| HOD | Head of Department |
| HQ | Headquarters |
| ICT | Information Communication Technology |
| IT | Information Technology |
| IWRM | Intergrated Water Resource Management |
| JICA | Japan International Cooperation Agency |
| KATC | Kilimanjaro Agricultural Training Centre |

| | |
|---|---|
| KIMRECOM | Kinondoni Municipal Revenue Collection Manager |
| LAT | Local Allocation Tax Grant |
| LG | Local Government |
| LGA | Local Government Authority |
| LGDG | Local Government Development Grant |
| LGRCIS | Local Government Revenue Collection Infromation System |
| MATI | Ministry of Agriculture Training Institute |
| MC | Municipal Council |
| MCCCO | Mbinga Coffee Curing Company Limited |
| MCDI | Mpingo Conservation Development Initiative |
| MHIMINA | Mtandao wa Hifadhi Misitu Nangaru |
| MHIMIRU | Mtandao wa Hifadhi Misitu Rutamba |
| MIVARF | Market Infrastructure Value Addtion and Rural Financing |
| MJUMITA | Muungano wa Jumuiya za Uhifadhi Misitu Tanzania |
| MoU | Memorandum of Understanding |
| MRRH | Mbeya Regional Referral Hospital |
| MUST | Mbeya University of Science and Technology |
| NBS | National Bureau of Statistics |
| NEDF | Newala Education Development Fund |
| NFRA | National Food Reserve Agency |
| NGOs | Non - Governmental Organizations |
| NHC | National Housing Cooperation |
| NHIF | National Health Insurance Fund |
| NMB | National Microfinance Bank |
| NORAD | Royal Norwegian Agency for Development |
| NSSF | National Social Security Fund |
| O&OD | Opportunities and Obstacles to Development |
| OJT | On the Job Training |
| OPD | Out Patient Department |
| OVOP | One Village One Product Movement |
| PFM | Participatory Forest Management |
| PO - PSM | President's Office, Public Service Management |
| PO - RALG | Presidents' Office, Regional Administration and Local Government |
| POS | Point of Sales |
| POT | Post Osaka Trainings |
| PPP | Public –Private- Partnership |
| PRA | Participatory Rural Appraisal |
| RAS | Regional Administrative Secretary |
| RC | Regional Commissioner |
| RCH | Reproductive and Child Health |
| RHMT | Regional Health Management Team |
| RIPS | Regional intergrated Programme Support |
| RMO | Regional Medical Officer |
| RS | Regional Secretariat |
| SACCOs | Savings and Credit Cooperative Societies |
| SAP | Structural Adjustment Programme |
| SIDA | Sweden International Development Agency |
| TACOBA | Tandahimba Community Bank |
| TACRI | Tanzania Coffee Research Institute |
| TANROADS | Tanzania Roads Agency |
| TASAF | Tanzania Social Action Fund |
| TATEDO | Tanzania Traditional Energy Development Organization |

| | |
|---|---|
| TC | Town Council |
| TCB | Tanzania Coffee Board |
| TCCIA | Tanzania Chamber of Commerce Industry and Agriculture |
| TCFCN | Tanzania Community Forest Conservation Network |
| TFCG | Tanzania Forest Concervation Group |
| TFDA | Tanzania Food and Drugs regulatory Agency |
| TKL | Tutunze Kahawa Company Limited |
| TOA | Tanzania Osaka Local Government Reform Alumni |
| TPO | Town Planning Officer |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| UMICHITA | Uhifadhi Misitu Kata ya Chikonji na Tandangongoro |
| UMIKIWAMI | Uhifadhi wa Misitu Kiwawa na Mihola |
| UNDP | United Nations Development Programme |
| UNICEF | United Nations Childrens' Fund |
| UPE | Universal Primary Education |
| URT | United Republic of Tanzania |
| UTT | Unit Trust of Tanzania |
| VEO | Village Executive Officer |
| VETA | Vocational Education Training Authority |
| VNRCs | Village Natural Resources Committees |
| WDC | Ward Development Committee |
| WEO | Ward Executive Officer |
| WHO | World Health Organization |
| WWF | World Wide Fund for Nature |
| ZITSU | Zonal Irrigation Technical Services Unit |

# Dibaji

Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania yamelenga katika utoaji bora wa huduma wa Serikali za Mitaa kwa kuzingatia sera za kitaifa za Serikali Kuu. Maboresho yamekaribisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, washirika wa maendeleo na wadau wengine tangu awamu ya kwanza hadi sasa. Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) iliwekwa dhahiri mwaka 1998 na utekelezaji wake wa maboresho ya Serikali za Mitaa ulianza mwaka 2000. Kupitia ushirikiano huu maboresho ya Serikali za Mitaa hapa Tanzania yamefanikiwa kuleta Serikali za Mitaa za kidemokrasia, matumizi bora ya raslimali watu, kuongozeka kwa ruzuku toka hazina, kuimarika kwa utawala bora katika Serikali za Mitaa, kuongezeka kwa ushiriki wa wananchi na kwa ujumla kuongezeka kwa uhuru wa Serikali za Mitaa katika utoaji wa huduma.

Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania yametekelezwa kwa mkakati wa jumla ambao umejumuisha kujifunza jitihada za maboresho na utekelezaji wake katika nchi nyingine, Afrika na kwingineko na kuunda mkakati sahihi wa utekelezaji wake na mbinu mbadala kwa Tanzania. Tangu mwaka 2002 Serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM – TAMISEMI – Wakati huo) na Serikali ya Japani kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani (JICA) kwa pamoja wameendesha mafunzo kuhusu Ugatuaji nchini Japani kupitia mafunzo ya Osaka. Mafunzo haya yamehudhuriwa na Wakurugenzi na Watumishi wengine toka OR – TAMISEMI, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) na wadau wengine wa maboresho ya Serikali za Mitaa. Mafunzo haya pia yalitolewa kwa Makatibu Tawala Wasaidizi, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na wakuu wa idara kupita mafunzo ya mikoa baada ya mafunzo ya Osaka (Reginal Post Osaka Training).

Mafunzo ya Osaka na yale ya Mikoa yametoa fursa kwa watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kujifunza uzoefu wa ugatuaji madaraka wa Kijapani, kuchagua mbinu bora za ugatuaji wa Kijapani na kutekeleza mbinu hizo katika Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hili limeibua umuhimu wa kutoa taarifa za utekelezaji wa mbinu hizi bora kupitia kitabu, ili kuzifanya Sekretarieti za Mikoa na MSM kuona na kujifunza utekelezaji na siri zake humuhumu nchini.

Kitabu hiki cha Nne ni mwendelezo wa juhudi za pamoja kati ya OR – TAMISEMI na JICA kuimarisha sera ya ugatuaji wa madaraka Tanzania. Kitabu hiki kinaanza kwa kuonesha historia ya mafunzo ya Osaka na mbinu bora kama ifuatavyo; Sura ya Kwanza inaonyesha kwa ufupi Masuala mazuri yaliyoigwa toka Japani; Sura ya pili inahusu Jitihada za Jamii kwa Ajili ya Huduma Bora ikiwasilisha Mbinu Bora kutoka Halmashauri za Wilaya za Lindi, Nachingwea, Masasi, Mbeya na Momba, Halmashauri ya Mji wa Masasi na Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya. Sura ya Tatu inahusu Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato ikiwasilisha Mbinu Bora kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kinodoni na Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba. Sura ya Nne inahusu Ushiriki wa Jamii katika Utoaji Huduma ambayo inawasilisha Mbinu bora kutoka Halmashauri za Wilaya za Lindi, Kilwa, Ruangwa, Chunya, Busokelo, Ileje na Newala, na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. Sura ya Mwisho inahusu Maendeleo ya Jamii Kiuchumi na inawasilisha Mbinu Bora za Halmashauri za Wilaya za Mbinga, Masasi na Tunduru.

OR – TAMISEMI inashauri watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na wa MSM na wadau wote wa maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania kusoma kitabu hiki, kufahamu jitihada za ndani, kujifunza siri za mafanikio na kutumia fursa zilizopo kwenye maeneo yao kuonesha utendaji mzuri katika mazingira ya ugatuaji wa madaraka.

**Mhandisi Mussa Iyombe**
**KATIBU MKUU**
**OR-TAMISEMI**

# Utangulizi (TOA)

Kitabu cha Mbinu Bora cha Nne ni matokeo ya jitihada za pamoja za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia OR – TAMISEMI na Serikali ya Japani kupitia JICA tangu mwaka 2002 kwa kuendesha mafunzo huko Osaka na mafunzo baada ya Osaka katika kila Mkoa juu ya uzoefu wa Ugatuaji Madaraka huko Japani. Mafunzo haya yalitoa fursa kwa watumishi wa Sekretarieti za Mikoa, MSM na wadau mbalimbali wa maboresho hapa Tanzania kujifunza uzoefu wa Kijapani kuhusu Ugatuaji katika maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa na Usimamizi wa Raslimali Watu, Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato, Upangaji na Utoaji Huduma Shirikishi na Maendeleo ya Kiuchumi katika MSM hasa kupitia wimbi la OVOP. Masuala mazuri yaliyoigwa yametekelezwa katika Sekretariati za Mikoa na MSM nyingi kwa lengo la kuboresha utoaji huduma kwa jamii ndani ya sera ya ugatuaji, yaani "D by D". Mbinu Bora nyingi za utekelezaji zimeonyesha mafanikio na matokeo chanya kwa jamii. Kamati ya Utendaji ya TOA imeamua kutoa Mbinu Bora ambazo zimewasilishwa kwenye toleo hili la Nne. TOA itaendelea kutoa matoleo mengine ya kitabu hiki siku za mbele sambamba na utekelezaji unaondelea wa Masuala mazuri yaliyoigwa kwenye mafunzo ya Osaka na yale ya Mikoa.

Kukamilika kwa kitabu hiki cha Nne cha Mbinu Bora kumetokana na misaada kutoka taasisi na watu binafsi mbalimbali. TOA inapenda kutambua na kutoa shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kufikia makubaliano na Serikali ya Japani, kufadhili na kuruhusu watumishi wa Tanzania kuhudhuria mafunzo ya Ugatuaji nchini Japani toka mwaka 2002 hadi sasa. Pili, TOA inaelekeza shukrani za dhati kwa Serikali ya Japani na JICA kwa kuandaa, kusaidia na kufadhili mafunzo ya Osaka na Mafunzo ya Mikoa na uzalishaji wa kitabu hiki. TOA pia inapenda kutambua na kushukuru juhudi za utekelezaji wa yale yaliyojifunzwa za Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa MSM na utayari wao wa kuandika Mbinu Bora kamilifu kama zinavyoonekana kwenye kitabu hiki.

Uchambuzi na uunganishi wa Mbinu Bora zilizopo kwenye kitabu hiki ulifanywa na Bwana Paulo F. Faty (Mhadhiri - Chuo Kikuu Mzumbe) na Bwana Ahmed Nassoro (Mhadhiri Msaidizi - Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo), pia Masuala yaliyoigwa Japani yamechambuliwa na Bwana Michiyuki Shimoda (Mshauri Mwandamizi, OR – TAMISEMI). TOA inapongeza kwa dhati mchango wao na inawashukuru sana.

Mwisho TOA inapenda kuwashukuru watumishi wote wa OR – TAMISEMI na JICA kwa kushiriki katika mikutano mbalimbali iliyoboresha na kuunda kitabu hiki. Siyo rahisi kutaja wote waliochangia katika kazi hii, hata hivyo TOA inaheshimu michango yote iliyotolewa na Taasisi na Watu mbalimbali.

Mwisho kabisa, ingawa Watu na Taasisi nyingi zimechangia katika kitabu hiki, TOA na timu ya uchambuaji wanawajibika kwa makosa na mapungufu yanayoweza kuhisiwa na wasomaji wa kitabu hiki.

------------------------------------------------------

**Mhandisi MUSSA NATTY**
**MWENYEKITI WA TOA**

# Utangulizi (JICA)

Wasomaji Wapendwa!

Utekelezaji wa sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) umechukua zaidi ya miaka 10 sasa ukiwa na lengo la kuboresha huduma kwa kugatua shughuli, majukumu na raslimali toka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa.

Kutokana na ukweli huu hapo juu Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani (JICA) limejikita katika kusaidia utekelezaji wa sera hii hasa katika kuimarisha utoaji huduma katika ngazi za msingi kwa kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na maendeleo ya sekta za afya, kilimo, maji na barabara.

Toka mwaka 2002, JICA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) imekuwa ikiendesha mafunzo kuhusu maboresho katika Serikali za Mitaa yanayoitwa "Osaka Training". Mafunzo haya yalilenga Maofisa wa juu wa Menejimenti katika maboresho ya Serikali za Mitaa, yaani Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa MSM, Maofisa wa OR – TAMISEMI na Vyuo vya Elimu ya Juu kwa malengo ya kujifunza uzoefu wa Kijapani katika maboresho ya Serikali za Mitaa. Katika kurudi kwao, waliwasilisha na kujadiliana uelewa na uzoefu walioupata kwenye warsha za mafunzo za mikoa (2003 – 2007). Matokeo yake Umoja wa Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa MSM (TOA) ulianzishwa mwaka 2006 ili kuwa na jukwaa ambalo wajumbe wa TOA wanapata fursa ya kubadilishana uzoefu, mbinu bora na changamoto zilizopo. JICA imekuwa ikisaidia uimarishaji wa taasisi ya TOA.

Kutokana na utekelezaji wa Masuala yaliyoigwa kwenye mafunzo ya Osaka, Mbinu Bora nyingi ziliwasilishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika warsha za Mikoa zilizofanyika katika kanda sita mwaka 2011/12 pamoja na warsha za Mikoa zilizofanyika tangu mwaka 2014 na 2015. Baada ya uhakiki na uchambuzi wa mbinu hizi bora, toleo la kwanza, la pili, la tatu na hili la Nne la "kitabu cha Mbinu Bora" hatimaye limetoka. Kitabu hiki kinathibitisha kuwa ***"tunatakiwa kujifunza siyo tu kutoka nchi nyingine bali katika jitihada nyingi zilizopo ndani ya nchi".***

Nitafurahi kama mtajifunza vipengele muhimu kutoka kitabu hiki na kuchukua hatua ndogo lakini za uhakika ili kuboresha utendaji katika eneo husika.

JICA ina mpango wa kuisaidia TOA kuendesha mafunzo ya Watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na Wakuu wa Idara katika Mikoa yote kwa kutumia vitabu hivi. Tungependa kufuatilia na kujua mbinu bora zitakazofuata zilizotokana na kitabu hiki na mafunzo yake. Tunatarajia kuanzisha jukwaa la kujifunza wenyewe kwa wenyewe (Horizontal Learning) katika ngazi za Msingi.

**Toshio Nagase**
***Mwakilishi Mkuu – Ofisi ya JICA Tanzania***

# Sura ya Kwanza: Utangulizi; Masuala Yaliyoigwa Kutokana na Uzoefu wa Japani

## 1.0 MAFUNZO YA OSAKA

Kitabu hiki kimeandaliwa na Umoja wa Washiriki wa Mafunzo ya Osaka kuhusu Serikali za Mitaa wanatoka Tanzania (TOA). TOA ni Umoja wa washiriki wa kozi inayotolewa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA). Mafunzo yenyewe yanaitwa "Mafunzo yenye Mrengo wa Nchi – Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania", lakini yajulikanayo sana kama "Mafunzo ya Osaka". Umoja una wanachama ambao ni Makatibu Tawala wote wa Sekretarieti za Mikoa na Wakurugenzi wote wa Halmashauri nchini.

Mafunzo ya Osaka yalianza mwaka 2002. Kipindi cha miaka mitano ya mwanzo, Makatibu Tawala wote kutoka Mikoa 21 (kipindi hicho) pamoja na Wakurugenzi wa Halmahauri wawili kutoka kila mkoa walihudhuria. Pia maofisa wa juu toka OWM – TAMISEMI (wakurugenzi na wakurugenzi wasaidizi)[1], Katibu Mkuu wa ALAT na baadhi ya wanataaluma mashuhuri walihudhuria kozi hii.

Kutokana na mafanikio na matokeo dhahiri, JICA iliamua kuendelea na mpango huu, kwa kupanua wigo wake kwa kuongeza nchi nyingine tatu za kiafrika ambazo zilikuwa zikipanga maboresho ya ugatuaji, yaani Kenya, Uganda na Zambia, pamoja na Tanzania. Mpaka leo zaidi ya viongozi 100 wa maboresho wanaojumuisha Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri wamefaidika moja kwa moja na mafunzo ya Osaka. Pia washiriki hawa waliporudi katika mikoa yao waliendesha warsha za ndani zijulikanazo kama "mafunzo ya Post Osaka" ili kubadilishana uzoefu na uelewa walioupata Osaka kwa kuwaalika Wakurugenzi waliobaki pamoja na wakuu wa idara. Hivyo wafaidika wa mafunzo haya waliongezeka mpaka kufikia zaidi ya 1,500, ingawa uanachama wa TOA ulibakia kuwa wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri.

Kutoka katika Masuala mbalimbali yaliyoigwa Osaka na mafunzo ya Post Osaka, Halmashauri zilizohudhuria ziliandaa mipango kazi ya kuboresha utendaji wao. Kukiwa na zaidi ya miaka 10 ya utendaji, imethibitishwa kuwa kuna idadi kubwa ya mbinu bora zinajitokeza katika Halmashauri nyingi kwa kutekeleza ile mipango kazi ambayo ni vyema kuwashirikisha wengine. Kwa hiyo TOA iliamua kuhakiki na kuchambua kesi hizo za mbinu bora na kutengeneza kitabu hiki, ili viongozi wa Halmashauri waweze kuzirejea kesi hizi na kuzitumia pale wanapoona zinafaa na zina tija, katika kuboresha kazi zao.

[1] Pamoja na Makatibu wakuu wawili wa Zamani wa OWM-TAMISEMI, yaani, MS. Tarishi M.K. na Bwana H.A. Katanga

Kabla ya kuingia kwenye kesi zenyewe za mbinu bora, ni vyema katika sura hii tukaangalia kwa nini JICA iliamua kutoa mafunzo haya kwa viongozi wa maboresho wa kitanzania, nini ilikuwa maana ya mafunzo ya Osaka kwa Tanzania na Masuala gani yalijadiliwa kwenye mafunzo haya.

## 2.0 HISTORIA YA MAFUNZO YA OSAKA

Kwa nini JICA iliamua kutoa mafunzo haya? Na yalikuwa na maana gani kwa Tanzania?

### 2.1 Maoni ya JICA Kuhusu Msaada kwenye Ugatuaji

JICA ina maoni ya kiza Jamii kuhusu misaada kwenye utawala ambayo yanaweza kutofautiana na maoni ya washirika wengine wa maendeleo. JICA imeshuhudia programu kubwa kubwa za maboresho zikifanywa katika nchi zinazoendelea na washirika wa maendeleo kama Programu wa kurekibisha Miundo ya Uchumi (SAPs) na maboresho ya utawala ikiwa ni pamoja na Ugatuaji wa madaraka. Inaweza kusemwa kuwa programu hizi na maboresho haya yaliyofanywa katika nchi zinazoendelea ni sawa kabisa na yale yanayojaribiwa sasa katika nchi zilizoendelea bila kujali tofauti iliyopo ya kihistoria na mazingira kati ya nchi hizi. Pia mara kwa mara inajidhihirisha kuwa maboresho haya yanatekelezwa kwa msukumo mkubwa toka kwa wafadhili, bila kuzingatia asili ya mchakato wa maendeleo na umiliki wa nchi husika.

Kutokana na machungu ya kushindwa kufikia malengo katika ushirikiano wa kimataifa wa aina hii, JICA imekuwa na msimamo ufuatazo katika kusaidia ugatuaji.

(i) Hakuna mfumo wowote unaoweza kutumika katika nchi zote.
(ii) Ugatuaji wenyewe siyo lengo bali ni njia ya kufikia lengo fulani.
(iii) Kuasilisha na kukuza mfumo ndani ya nchi kupitia majadiliano ya kitaifa ni muhimu.
(iv) Jinsi gani ya kuhakikisha viwango vya chini vya kitaifa vya huduma[2] vinafikiwa ni muhimu katika kuandaa maboresho ya Ugatuaji.
(v) Maboresho ya Ugatuaji ni mchakato mrefu, ambao hautakiwi kuchukuliwa kama Mradi au Programu tu.
(vi) Maboresho ya Ugatuaji ya haraka haraka yanaweza kuleta fujo. Katika kila maboresho ya Ugatuaji (d by d), ni lazima kuhakikisha kuna mazingira sahihi kwa upande wa Halmashauri na wanajamii kupokea majukumu makubwa yanayogatuliwa.

## 2.0 Changamoto Kubwa Iliyogunduliwa katika Programu ya Tanzania ya Maboresho ya Serikali za Mitaa na Ujumbe wa Maandalizi ya Mafunzo wa Mwaka 2002

Baada ya maombi ya Serikali ya Tanzania kuhusu kuwepo kwa Mpango wa mafunzo wa maboresho katika serikali za mitaa mwaka 2001, JICA iliamua kutuma ujumbe kwenda kuchambua hali ilivyo ili kuunda kozi ya mafunzo yenye maudhui ya kumaliza Masuala muhimu.

[2] Viwango vya chini vya kitaifa vya huduma ni nadharia kuwa kiwango fulani cha huduma lazima kifikiwe hata kama ni katika jamii maskini vijijini sawa na kwenye miji mikubwa.

Ujumbe ule ulipofika Tanzania, Novemba mwaka 2002, uligundua kuwa Programu ya maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania ilikuwa na changamoto zifuatazo;

(i) Jedwali kubwa na lenye hatua nyingi za utekelezaji (Zaidi ya kurasa 80)
(ii) Programu ya maboresho ilikuwa ukitekelezwa kwa jedwali zuri sana lakini halikuruhusu maboresho/mabadiliko zaidi. Ujumbe uliona kulikuwa na nafasi ndogo sana iliyoachwa ya kuweza kubadili lolote ili kuruhusu majaribio ya suala ambalo ni muhimu. Ujumbe uliona kuwa kila kitu kimeshadhamiriwa, na Serikali ya Tanzania ililazimika kufuata reli hiyo bila kwenda pembeni au kurudi vyuma.
(iii) Programu iliandaliwa kwa msaada mkubwa kutoka kundi la wafadhili.
(iv) Wafadhili wa kawaida waliopo kwenye mfuko "Basket funding" waliunda kamati ya msukumo pamoja na serikali. Kuandikwa kwa Programu yenyewe kulifanywa na wataalamu washauri wa nje na hata utekelezaji wenyewe. Ujumbe ulihofia kuwa Programu ya maboresho iliandaliwa bila kupitia mchakato stahiki wa kujenga uelewa ndani ya nchi na kupata makubaliano yanayohusu mahitaji ya mabadiliko.
(v) Hatari ya kukimbilia kwa haraka Ugatuaji wa Madaraka (D by D).

Sera ya ugatuaji (D by D) iliyokuwa ikihamasishwa na Serikali ilidhihirika kwenye ujumbe huo kuwa ni kama vile Tanzania ilikuwa inatekeleza ugatuaji wa madaraka sawa na ule wa nchi zilizoendelea. Swali likawa; Je ni kweli uwezo na mtazamo wa Halmashauri na Wizara zote ulikuwa tayari kwa mabadiliko haya ya haraka? Ujumbe huu uliaona changamoto zifuatazo katika hili;

- Upinzani kutoka Wizara za kisekta
- Ukosefu wa majadiliano ya kina kuhusu ugatuaji katika jamii
- Hakukuwa na uwezo kamilifu kwa upande wa Halmashauri kuchukua majukumu yote yaliyogatuliwa

**2.3 Uwezekano wa Umuhimu wa Uzoefu toka Japani katika Ujenzi wa Taifa na Maboresho ya Ugatuaji - Ujumbe kutoka Japan kwenda Tanzania kupitia Mafunzo ya Osaka.**

Baada ya kuona hali halisi ya Tanzania iliyoelezewa hapo juu, JICA iliamua kuwa uzoefu wa Japani kwenye ujenzi wa Taifa na Maboresho yaliyokuwa na mchakato wa muda mrefu ya Ugatuaji ungeweza kuwa unastahili na muhimu kwa viongozi wa maboresho wa Tanzania kujifunza na kupitia upya maboresho yao.

Japani ni nchi ndogo huko Bara la Asia isiyo na ustaarabu wa Magharibi, ambayo ilianza ujenzi wa taifa kama nchi iliyo nyuma kabisa lakini ikafikia maendeleo ya ajabu. Japani ina uzoefu mwingi wa aina yake wa kutumia mifano (models) ya nje (mfano wa Magharibi) ambayo wafadhili wengine hawana. (Mataifa ya Ulaya yamekuwa mara zote mstari wa mbele na katikati ya dunia na hujiona hayana sababu ya kujifunza toka nje). Kwa kweli, Japani ilianza Ujenzi wa taifa na maendeleo, kwa kujaribu kuiga mifano ya Magharibi lakini ikashindikana mwanzoni kabisa. Tokea hapo ikawa ni mchakato mrefu wa kujaribu na kushindwa mpaka hatimaye ilipofikia Japani ikaunda mfumo wake wa kiza Jamii unaoitwa "Nusu kijapani nusu Magharibi". Japani inaamini

kuwa aina hii ya uanzishaji wa mfumo, pamoja na umiliki wake thabiti kupitia kujaribu na kushindwa mara nyingi ni muhimu sana kwa maendeleo endelevu ya nchi.

Mchakato huu ambao Japan ilitumia ili kuanzisha mfumo wake wa serikali za mitaa na maboresho ya Ugatuaji ni tofauti kabisa na mifano ya Ulaya ambayo nchi zinazoendelea zinajaribu kuanzisha kwa sasa. JICA ilifikiri kuwa kuwasilisha "mfumo huu tofauti" unaweza kuwa muhimu, kwani kuwa na mfano mmoja tu, inaonekana kama vile "ndio njia za Jamii" hakuna nyingine. Lakini kukiwa na mifano zaidi ya miwili, wanaweza wakaanza kulinganisha na kuona ni mfano upi unafaa zaidi katika mazingira yao, na ni hatua ipi iwe ya kwanza katika kuandaa mfumo wao wenyewe.

Ifuatayo ni mifano tu ya kuvutia ya vigezo vinavyoweza kuigwa toka mfumo wa kijapani kati ya mengi yaliyopo;

**(1) Mchakato wa Maboresho wa Polepole Sana Lakini wa Uhakika**

Japani ilitumia miaka 110 toka ilipoanza kuunda mfumo wa Serikali za Mitaa na Ugatuaji; ingawa tunahesabu miaka 55 ya Maboresho Makuu baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia hadi kufika ugatuaji halisi (D by D) mwaka 2000. Serikali ilijaribu kuhakikisha kuwa Halmashauri zimeshajengewa uwezo wa kutosha kabla ya kugatua majukumu, na siyo kukimbilia kurekebisha taasisi za Ugatuaji (D by D). Uzoefu huu wa Japani unaipa Tanzania fursa ya kufikiria mara mbili kama mwendo wa maboresho siyo kasi sana, na kama nchi inataka kuendelea na mwendo kasi uliopo, basi haina budi kuhakikisha kuna ujenzi wa uwezo stahiki kwa upande wa Serikali za Mitaa.

**(2) Ukasimishaji wa Shughuli/Majukumu kwa Wakala (Agency Delegated Functions)**

Katika kipindi tajwa cha miaka 55, serikali ilichagua mfumo wa "kukasimu" unaoitwa ADF kama hatua ya mpito, badala ya kurukia Ugatuaji moja kwa moja. Kwa sababu ya mfumo huu Japani ilipingwa sana na nchi za Magharibi kwa kipindi kirefu kuwa haijafanya Ugatuaji sahihi, na mwishoni kabisa Serikali ikaamua kuingia katika Ugatuaji halisi mwaka 2000 na kuondokana na mfumo wa kukasimu (ADF). Hata hivyo sasa hivi imethibitika kuwa ADF ilichangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa mfumo mzuri wa Serikali za Mitaa na kupelekea kufikiwa kwa ugatuaji halisi (D by D) nchini Japani; hasa katika vipengele vifuatavyo;

- Shukrani kwa ADF, Halmashauri zilifanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na Wizara husika, na zikaweza kujenga uwezo wao kupitia mafunzo kazini (on the job training) kukiwa na usaidizi wa kitaalamu wa karibu toka wizarani. Kila walipopata changamoto, maofisa wa Serikali za Mitaa waliweza kuwasiliana na maofisa wa wizara husika kwa simu na maofisa wa wizara waliweza kusaidia kwa wema na kumaliza changamoto hizo pamoja. Haya yote yaliwezekana kwa sababu kimsingi shughuli zote zilikuwa ni wajibu wa Wizara na zilikasimishwa tu kwa Halmashauri. Hivyo hakukuwa na upinzani wowote toka wizarani, zaidi ya ushirikiano ilipofikia Ugatuaji wa shughuli; kinyume kabisa na yanayotokea katika nchi zinzoendelea zinapotekeleza ugatuaji.

- Hoja ya msingi ilikuwa ni kuhakikisha kuwa raslimali ambazo ni chache zilizopo ndani ya nchi zinaweza kutumika vizuri zaidi kuelekea upande mmoja yaani maendeleo ya nchi, badala ya kuzigawa na kutengeneza tofauti kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.
- Ilikuwa ni muhimu sana katika hatua za mwanzo ambapo Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa na uwezo dhaifu. Bila mfumo wa kukasimu (ADF) kipindi hicho Halmashauri zisingeweza kufanya vizuri shughuli zao za kuhudumia watu wala uwezo wao usingejengeka.
- Sababu nyingine muhimu ilikuwa mafunzo kazini (OJT). Shukrani kwa mchakato wa mafunzo kazini (OJT), kwa miaka 55, watumishi wote wa Serikali za Mitaa pamoja na muundo wao kwa ujumla walijenga uwezo thabiti, kwa kupokea ufahamu na utaalamu kutoka wizarani, na kuwa tayari Serikali Kuu ilipoamua kugatua madaraka (D by D).

Uzoefu huu wa Japan unaleta swali moja la msingi kwa Tanzania juu ya namna gani nchi inaweza kujithibitishia uhakika na ubora wa mchakato wa kuzijengea uwezo Halmashauri ilihali Ugatuaji (D by D) ukiendelea; kuhakikisha matumizi mazuri ya raslimali chache zilizopo nchini na kukwepa kabisa upinzani toka Wizara za kisekta.

**(3) Mfumo wa Kubadilishana Watumishi kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa**

Nchini Japani, kipindi cha hatua za mwanzo za maboresho, mtindo wa kubadilishana watumishi kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ulitumika sana kama mbinu bora kabisa ya (a) kujaza upungufu wa watumishi hasa wenye sifa katika Halmashauri za pembezoni na (b) kuhakikisha uhamishaji wa ujuzi na utaalamu kutoka kwa wasomi wa Wizara kwenda kwa watumishi wa Halmashauri waliokuwa na ujuzi na uzoefu mdogo ili kujenga uwezo wa Halmshauri hizo.

Serikali iliunda jopo kubwa la maofisa wataalamu katika wizara ya Serikali za Mitaa na kuwapeleka kwenda kwenye Halmashauri zilizokuwa na uwezo mdogo huko pembezoni ili kuzisaidia. Hatua hii ya uhamisho wa muda ilidumu kwa muda wa miaka 4 - 5 na baadaya watumishi hawa walirudishwa kwenye nafasi zao za kawaida kwenye wizara zao. Kadri walivyokuwa na uwezo wa kitaalamu kuwezesha wengine ndivyo walivyopelekwa kwenye Halmashauri za mbali na zenye udhaifu mkubwa. Pale walipofaulu na kutenda vizuri katika vituo hivi vipya, waliahidiwa kupanda vyeo zaidi wanaporudi, ambayo iliwapa motisha wataalamu hawa waliobobea kwenda kwenye sehemu zisizovutia kwa hamasa ya juu kabisa. Pia Halmashauri nyingi zilipeleka watumishi wao kwenye wizara mbalimbali kufanya kazi, katika misingi ya mafunzo kazini kwenye maeneo ambayo Halmashauri husika ilihitaji.

Baada ya kurudia mizunguko kadhaa ya kubadilishana watumishi, ujuzi na utaalamu wa kutosha ulihamishwa kikamilifu toka Wizara kwenda Halmashauri, kitu ambacho kilisaidia sana kujenga uwezo wa Halmshauri nchini Japanni. Sasa Halmashauri zinajitegemea katika raslimali watu bila kuitegemea Serikali Kuu tena.

Nidhahiri kuwa ugatuaji wa raslimali watu ukifanyika kwa ukamilifu wake bila kuwa na mbinu za kutatua matatizo, hupelekea upungufu mkubwa wa watumishi kwenye Halmashauri ambazo zipo katika maeneo maskini na pembezoni. Ni kwa sababu hii Tanzania iliamua kurudisha Masuala ya raslimali watu kwa sehemu kubwa Serikali Kuu. Hata hivyo haina mantiki kuendeleza Ugatuaji wa madaraka (D by D) bila Ugatuaji halisi wa raslimali watu. Badala ya "0 au 100", serikali inatakiwa kutafuta mkakati wa namna ya kugatua raslimali watu na wakati huohuo kukwepa kutengeneza upungufu katika maeneo ya vijijini, na kujiridhisha kuwa kuna mchakato wa kujenga uwezo wa baadaye wa Halmashauri.

## 3.0 MASUALA YALIYOJITOKEZA NA KUJADILIWA WAKATI WA MAFUNZO YA OSAKA

Kutokana na upungufu wa nafasi Masuala machache tu ya msingi yameweza kuwasilishwa kwenye sehemu hiyo hapo juu, kati ya mambo mengi yanayotokana na uzoefu wa Japani ambayo Tanzania imepewa. Hapa vipengele vingine vitatajwa na kuelezewa kwa kifupi.

### 3.1 Masuala ya Jumla

Masuala na Maswali yafuatayo yalijitokeza na kujadiliwa wakati wa mafunzo ya Osaka:

**(1) Umuhimu wa kukuza uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama kigezo cha mafanikio ya Ugatuaji wenyewe**

- ➢ Je hakuna hatari ya kudidimiza utoaji huduma, kugatua wajibu mkubwa kiasi hiki ndani ya muda mfupi?
- ➢ Ni namna gani ya kukabiliana na hali halisi kuwa Halmashauri zinahitaji uwezo zaidi ili kutekeleza shughuli zilizogatuliwa?
  - Vipi kuhusu ajira? Namna gani itawezekana kupata watumishi wenye sifa katika Halmashauri zilizopo kwenye maeneo maskini na pembezoni?
  - Ni jinsi gani ya kuziba pengo kati ya ujuzi na utaalamu katika Serikali za Mitaa na kuziendeleza? Je siyo muhimu kwanza kuweka mbinu za kuhamisha ujuzi na utaalamu, pamoja na usaidizi wa kitaalamu kutoka serikali kuu kwenda Halmshauri? Siyo muhimu kwanza kuimarisha mahusiano ya ushirikiano kati ya Serikali Kuu na Halmashauri badala ya kutegemea misaada toka nje?

**(2) Ugatuaji na Maendeleo**

- ➢ Ili kuweza kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi na kwa raslimali chache zilizopo, ni muhimu kutafuta mbinu mkakati ya kuzitumia raslimali hizi (hivi ndivyo ambavyo Japani imekuwa ikifanya kujiletea maendeleo yake)
- ➢ Namna gani unaweza kusimamia maendeleo ya nchi na ugatuaji kwa pamoja wakati mara kadhaa hupingana? Unawezaje kujiridhisha kuwa hakutakuwa na utengano wa raslimali na tofauti (kutokuelewana) kati ya Serikali Kuu na Halmashauri au kati ya Halmashauri zenyewe?

**(3) Ugatuaji na Viwango vya chini vya kitaifa**

- Jinsi gani ya kusimamia ugatuaji na kuzingatia viwango vya chini vya kitaifa? Ni jinsi gani itahakikishwa kuwa Halmshauri zilizopo vijijini zitakuwa na uwezo wa kutosha kama zilivyo zile tajiri katika kigezo cha utoaji huduma kwa watu? (uwezo wa watumishi na fedha).

**(4) Ukweli Kuhusu Uwezo wa Halmashauri kuweza Kutoa Huduma**

- Swali liliulizwa; Ni Maofisa Ugani wangapi waliopo katika Halmashauri ukijumuisha na wale ambao wanatumikia katika kata na vijiji? Swali hili liliulizwa kwa washiriki ili kuwafanya waelewe hali ilivyo mbaya ambayo Halmashauri za Tanzania zinatakiwa kukabiliana nayo. Ukichukua Mkoa mmoja kama mfano, Mkoa wa Nagano nchini Japani, ni mkoa mdogo kabisa ulioko maeneo ya vijijini lakini una maofisa ugani wa kilimo wapatao 1500. Pia kuna Halmshauri 77 za ngazi za chini katika Mkoa huu ambazo kila moja inaajiri maofisa ugani kati ya 20 – 30. Maana yake kuwa wakulima katika Mkoa (prefecture)[3] wa Nagano wanafurahia huduma zinazotolewa na zaidi ya maofisa ugani 3,000 wa Halmshauri ikilinganishwa na wakulima wa Tanzania ambao wana maofisa ugani wasiozidi 100[4]. Pia nchini Japani kuna mashirika mengi ya binafsi yanayouza mashine za kilimo, mbolea, madawa, mbegu n.k pamoja na taasisi za ushirika zilizo imara; zote hizi hutoa huduma mbalimbali za ugani na ushauri wa kitaalamu.
- Ni vyema kutambua hali ngumu iliyoelezewa hapo juu na kuanzisha mkakati mpya. Hatutakiwi kuota ndoto kwamba Tanzania inaweza kufikia kutoa huduma nzuri kama za nchi zilizoendelea kwa idadi ndogo hivi ya watumishi kwenye eneo lote hata kama Serikali Kuu itaamuwa kufanya kila kitu peke yake.

**(5) Umuhimu wa Juhudi za Wananchi na Ushirikiano kati ya Halmashauri na Jamii**

- Kutokana na Ukweli ulioongelewa hapo juu, haikwepeki kutumia kwa kiasi kikubwa Uwezo wa watu na Juhudi za kujitegemea ili kutoa huduma zilizo bora.
- Ni imani ya JICA kuwa kama watu wataongozwa na kuwezeshwa vizuri, wana uwezo wa kufanya mambo mengi wenyewe, kama kujenga shule za msingi, zahanati, barabara zao na kuzitunza.
- Kwa Japani pia, kipindi cha hatua za mwanzo za Maendeleo, Serikali haikuwa na uwezo wa kujenga shule za msingi. Kwa mfano, ilikuwa ni watu katika jamii zao waliochangia

---

[3] Mkoa (prefecture) huko Japani ni karibu sawa na wilaya za Tanzania kwa ukubwa wa eneo. (Ingawa Wilaya nyingine za Tanzania ni kubwa sana kuliko Mikoa ya Kijapani).

[4] Pia si kwamba Japani ina hali nzuri katika maana hii. Kinyume chake, Japani ni nchi ambayo ina idadi ndogo kabisa ya watumishi kwa idadi ya watu waliopo ikilinganishwa na nchi zilizoendelea. Maana yake ni kuwa Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Italia n.k wana watumishi wengi zaidi wa serikali.

kutoka mifukoni mwao na wakafanya kazi pamoja kujenga na zaidi wakatafuta watu wanaoweza kufundisha na wakawalipa mishahara yao. Ndiyo maana shule nyingi za kipindi hicho hazikuwa za “umma” bali “binafsi”, kwa maana ya “shule zinazomilikiwa na jamii; ilikuwa ni baada ya miongo kadhaa, serikali ilipotajirika na ikaanza kuzimiliki na hatimaye kuwa shule za umma.

- Inahitaji mabadiliko ya mtazamo wa Serikali na Watu, kutoka fikra kuwa ni jukumu la Serikali kutoa huduma zote kwa watu kuelekea mtazamo kuwa watu wanaweza kufanya mengi sana kwa juhudi zao wenyewe na serikali ikawezesha tu mchakato huo badala ya Serikali kutekeleza peke yake.

**(6) Umuhimu wa Kuainisha Ukubwa Sahihi wa Sehemu za Serikali za Mitaa; na Kuunda Mbinu Mpya za Kuzifikia Jamii kutoka makao makuu ya Halmashauri**

- Kutokana na vigezo hivyo hapo juu ni lazima kuunda mbinu imara sana za Halmashauri kuzifikia jamii. Hapa Tanzania, Halmashauri za Wilaya ni kubwa mno, hivyo ni muhimu kufikiria jinsi ya kujenga daraja kati ya Halmashauri na jamii.
- Kutoka kwenye wazo la kukuza mtazamo wa watu kuwa na uhuru wao, eneo la Halmashauri linatakiwa kuwa dogo sana ili watu waweze kuona kuwa sehemu hiyo kweli ni yao. Kwa upande mwingine sehemu hii ndogo ya Serikali za Mitaa inatakiwa iwe na uimara wa kutosha kutoa huduma za kutosha ambayo inahitaji kiasi cha raslimali fedha na watu. Haya ni mahitaji muhimu mawili yanayopingana.
- Kuweza kutoa majibu kwa swali hili hapa juu linalojipanga lenyewe, sahihisho lililopo ni kuwa na mfumo wenye ngazi nyingi kutoka Halmashauri hadi jamii. Kwa Japani mfumo huu wa ngazi nyingi unafanya kazi vizuri. Lakini Tanzania pia ina mfumo mzuri wenye wilaya – kata – kijiji – kitongoji. Hii inasaidia sana kukuza uhuru wa jamii na jitihada shirikishi za maendeleo kati ya Halmashauri na jamii. Zaidi ya hayo, Mfumo wa Upangaji Mipango Shirikishi Jamii (O&OD) unaweza kuwa jukwaa zuri zaidi la kuboresha mfumo huu na kuuwezesha kufanya kazi vizuri zaidi.

## 3.2 Usimamizi na Ugatuaji wa Raslimali Watu

Kama ilivyo kwenye sehemu iliyotangulia, mafunzo ya Osaka yalitoa tahadhari kwa Viongozi wa Tanzania katika miaka michache ya mwanzo kuwa waangalifu kuhusu kutoharakisha kugatua na kupeleka madaraka maarufu kama *D-by-D*. Hata hivyo, kuhusu ugatuaji wa masuala ya raslimali watu, ujumbe ulikuwa tofauti kidogo kwa vile ilionekana kwamba madaraka haya yalikwisha anza kurudishwa Serikal Kuu; kwani uteuzi wa Wakurugenzi wa Halmasahuri na Wakuu wa Idara unafanywa na Wizara pamoja na kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Ajira ili kuendesha mchakato wa ajira kwa kada nyingine za watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Nchi ya Japani haikugatua madaraka na kuyapeleka Halamashauri kwa haraka, bali Serikali Kuu ilendelea kuhodhi baadhi ya shughuli. Kwa mantiki hii, ugatuaji nchini Japani haukuwa umekamilika kwa miaka mingi mpaka ilipofika mwaka 2000. Hata hivyo, kuhusiana na kugatua

masuala ya usimamizi wa raslimali watu, Japan ilihakikisha kwamba madaraka haya yamegatuliwa na kupelekwa Halmashauri kikamilifu tangu mwanzo kabisa wa maboresho.

Hii ni kwa sababu kugatua masuala ya usimamizi wa raslimali watu ndiyo jambo la muhimu sana na msingi wa ugatuaji. Kulingana na mfumo wa Serikali za Mitaa Japani, masuala yote huamuliwa na kutekelezwa ndani ya Mamlaka za Serikali Mitaa husika bila kuingiliwa na Serikali Kuu, yaani kuajiri na kufukuza, kuendesha mafunzo, kupanga ngazi za mishahara, kufanya uhamisho, kupandisha vyeo , mpaka kustaafu. Mamlaka za Serikali za Mitaa Japani huajiri wahitimu wapya kutoka vyuo vikuu kila inapofika mwezi Aprili kulingana na mahitaji yao. Wahitimu walioajiriwa na Mamlaka fulani ya Serikali za Mitaa, wataitumikia Mamlaka husika kwa maisha yao yote mpaka watakapostaafu. Hakuna kanuni ya uhamisho kutoka Mamlaka moja ya Serikali za Mitaa kwenda mamlaka nyingine.

Zaidi ya hayo, Wenyeviti au Mameya ni wanasiasa na huchaguliwa na wananchi kwa njia ya kura, na ndio wakuu wa Tawi la Utawala/Utendaji sambamba na Tawi la Baraza la Madiwani la Halmashauri husika. Watendaji wanawajibika kwa Meya/Mwenyekiti na siyo kwa Madiwani, kwa hiyo masuala ya watendaji hulindwa na huwakilishwa na Meya/Mwenyekiti katika Baraza la Madiwani.

Kwenye mafunzo ya Osaka, mambo matatu yafuatayo yalitiliwa mkazo kwamba ndivyo vitu muhimu katika kufikia uwezo wa juu wa raslimali watu katika Halmashauri:

1) Kuajiri
   Kuajiri watumishi wenye sifa kuliko wote na wanaofaa katika kufikia dhima/malengo ya mamlaka husika; na
2) Mafunzo
   Baada ya kuajiri, kuwapa mafunzo yanayolenga na kuwezesha kufikiwa kwa dhima/malengo ya mamlaka husika (siyo malengo ya mtu binafsi); na
3) Kujipanga
   Kuhakikisha kuwa uwezo wote wa Raslimali watu katika Halmashauri unatumika kikamilifu ili kutimiza malengo ya mamlaka husika

Kwa minajili hiyo, Japani iliona kuwa ni jambo lisilokwepeka kutangulia kugatua madaraka yahusuyo usimamizi wa raslimali watu ili kila Halmashauri iweze kuchambua hali halisi, kupanga mipango, kuajiri, kutoa mafunzo, kupanga majukumu na kudhibiti watumishi. Mtumishi wa Halmashauri lazima awe mtu anayelipenda eneo husika na watu waliopo, anayefanya kazi kwa bidii kwa ajili ya watu, anayeelewa vizuri kuhusu hali ya eneo husika, anayewafahamu watu vizuri na kuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa karibu na wakazi wa eneo husika; hii ndiyo mantiki ya ugatuaji. Ni uzoefu wa nchi ya Japani kwamba, kwenye Halmashauri zenye mafanikio ya kuridhisha, kuna maofisa na watendaji wanaofanya kazi kwa kujituma hasa katika kuwahudumia watu, na kushirikiana na wakazi; na walio wengi wao ni wale watendaji waliozaliwa na kukulia katika maeneo hayo na wanayapenda makazi hayo, pamoja na uongozi thabiti wa Meya/Mwenyekiti ambaye naye ni mzawa.

Jambo jingine muhimu linalozifanya Halmashauri za Japani ziwe na nguvu ni juhudi waliyonayo katika kuwapa watumishi wao mafunzo. Halmashauri za Japani zinawekeza sana kwa watumishi kwa kuwapeleka kwenye mafunzo pamoja na mpango wa mafunzo kazini ambao uko kimkakati kulingana na mahitaji ya kitaasisi (siyo mahitaji binafsi) na kwa mtazamo wa mbali.

Hili linawezekana kule Japani kwa sababu hakuna uhamisho wa watumishi toka Halmashauri moja kwenda nyingine ya na kiwango cha kubakiza/kushikilia watumishi kazini ni kikubwa sana, hivyo Halmashauri huwekeza bila hofu kwamba baada ya kuwasomesha watakimbia.

Kinyume chake, Tanzania kuna uhamisho wa mara kwa mara wa watumishi muhimu kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine na hivyo ni vigumu sana kuwabakiza/kuwashikilia watumishi kwenye Halmashauri moja. Katika hali kama hii, changamoto kubwa ni jinsi ya kuhakikisha kwamba matokeo yatokanayo na mafunzo ya watumishi yanabaki ili yalete maboresho katika utendaji kazi wa mamlaka husika, na kuzifanya Halmashauri ziwe na bidii katika kujenga uwezo wa watumishi licha ya uwezekano mkubwa wa kuwapoteza baada ya kuwasomesha. Swali moja liliulizwa kwenye mafunzo ya Osaka kama Tanzania inaweza kuandaa na kutekeleza mpango mkakati na thabiti wa muda mrefu wa mafunzo ya kuwajengea watumishi wake uwezo katika hali hii.

Kwa upande mwingine, mafunzo ya Osaka yaliibua suala la “kufanya kazi kama timu” ili kuweza kutumia asilimia 120 ya uwezo wa nguvu kazi iliyopo na kuyafikia malengo ya kitaasisi. Kule Japani, kuna mambo kadhaa kuhusu mfumo wa usimamizi wa raslimali watu ambayo yamefafanuliwa kwa uangalifu mkubwa kwa ajili hiyo, kama vile:


1) Ngazi za mishahara zimewekwa makusudi kwa lengo la kuondokana na rushwa na kuchochea watumishi wafanye kazi kwa bidii hadi watakapostaafu;
2) Mfumo wa kiza Jamii wa Japani “kuchelewesha upandishaji vyeo” ili kumfanya kila mtu afanye kazi kwa bidii kwa miaka mingi kabla ya kupandishwa cheo (kukamua asilimia 120 ya uwezo wa kila mmoja);
3) Watumishi kufanya kazi kwa kuzunguka kila idara ya Halmashauri husika na mtindo wa kuweka kumbukumbu za kila mwaka za utendaji wa kila mtumishi ili kufanya za tathimini kwa haki na kwa malengo na kuchagua wale wenye uwezo mkubwa na wanaostahili kupandishwa vyeo kuwa Wakurugenzi;
4) Shughuli zote zinazohusu raslimali watu ziko chini ya Idara ya Uendelezaji Raslimali Watu ili iwezeshe namba 3) hapo juu;
5) Mazingira ya kiza Jamii ya Japani yanawezesha “utendaji kazi kama timu”, usimamizi unaofanywa na wakuu/viongozi, na mafunzo kazini yanayoendeshwa na wasimamizi, mtindo unaojulikana kama mtindo wa “chumba kikubwa” yaani ofisi ya wazi mithili ya ofisi za benki.

Yote yaliyoelezwa kwenye sehemu hiyo hapo juu yamewekwa na kanuni zinazotawala Mamlaka za SM za Japani ili kuhakikisha mambo matatu yahusuyo usimamizi wa raslimali watu yanazingatiwa mfano 1) Kuajiri; 2) Mafunzo; na 3) Kushughulika kwa bidii. Swali liliulizwa, katika mazingira ya sasa ya Halmashauri za Tanzania, ni kwa jinsi gani zinaweza kutekeleza mambo haya matatu.

### 3.3 Fedha za Serikali za Mitaa na Ugatuaji wa Masuala ya Fedha

**a) <u>Misingi ya kifedha katika Halmashauri</u>**

Michoro (1) na (2) inaonyesha japo kwa ufupi hali ya Halmashauri za Japani kuhusu masuala ya fedha.




**Mchoro (1) Uwiano wa Matumizi ya SK na SM kwa kila sekta**
Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010
(Ministry of Home affairs of Government of Japan)


Mchoro (1) unaonyesha ukubwa wa majukumu ya Halmashauri katika matumizi ya kutoa huduma ndani ya kila sekta. Ukiangalia sekta ya afya, Halmashauri hutumia 94% ya fedha iliyotengwa kwenye bajeti ya afya ya taifa na Serikali Kuu hutumia 6% tu. Kwenye elimu uwiano kati ya Halmashauri na Serikali Kuu ni 85% kwa 15%. Ukizingatia uhusiano wa karibu uliopo kati ya uzito wa majukumu na matumizi,

Halmashauri za Japani zinafanya sehemu kubwa zaidi ya majukumu ya Serikali ya kutoa Huduma. Kwa upande mwingine, ni muhimu kutambua kwamba kiasi kikubwa cha bajeti <u>hutengwa</u> kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri kutekeleza majukumu mazito yaliyogatuliwa na kupelekwa kwao.


Je hali ikoje Tanzania? Ukweli ni huu, ukiangalia majukumu yote yaliyogatuliwa na kupelekwa kwenye ngazi za msingi katika Halmashauri Tanzania, ukubwa wa majukumu ni sawa tu yale ya Halmashauri za Japani. Lakini, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Halmashauri Tanzania, ilikuwa pungufu ya TZS trilioni 3 ya bajeti ya taifa ya zaidi ya TZS trilioni 11 ya mwaka 2011/12.

Ulinganisho unaofanywa, ni ule unaohusu bajeti za Halmashauri zenye kuwa na masharti au uhuru wa matumizi. Mchoro (2) unaonyesha viwango na vyanzo mbalimbali vya mapato ya Halmashauri za Japani. Kama ilivyothibitishwa na takwimu hizi, 51% ya mapato hutokana na vyanzo vya ndani ( kodi ushuru na malipo mbalimbali). Pia kuna <u>ruzuku ambazo hazina masharti yoyote ya matumizi</u> zinazoitwa "ruzuku toka SK kwenda SM " (ruzuku za LAT). Ruzuku ya LAT ni <u>fedha nyingi inayotoka SK kwa mara moja</u> kwenda SM na serikali za mikoa. Fedha hii inahamishwa toka Wizara ya Fedha kwenda kwenye akaunti kuu ya kila Halmashauri <u>siku ya kwanza ya kila robo mwaka</u>. Ukijumlisha mapato ya ndani na ruzuku za LAT toka SK, Halmashauri za Japani zina aslimia 75% ya bajeti yao isiyo na masharti na wanaweza kutumia kama wanavyoamua wenyewe.

Mchanganuo huu ni wa muhimu sana kwa Halmashauri SM za Japani katika kufikia malengo ya mipango yao ya maendeleo, kwani wana bajeti ya kutosha na ya uhakika kila mwaka. Washiriki toka Tanzania walipochunguza hali za Halmashauri za kwao, walithibitisha kwamba zina hali mbaya ya kifedha pia fedha nyingi wanayopokea ina masharti ya matumizi kama ilivyo kwenye Mchoro, (3).




**Mchoro(2): Vyanzo na viwango vya mapato ya SM za Japani**
**Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010 (Ministry of Home Affairs of Government of Japan)**





**Mchoro (3): Muundo wa vyanzo mapato ya SM za Tanzania**
**Chanzo: Ni hesabu zilizofanywa na mwandishi toka tovuti ya serikali ya Tanzania**

Ama kwa hakika, hata kwa hali hii ingelikuwa jambo la maana kama 94% ya ruzuku wanayopokea isingelikuwa na masharti ili Halmashauri ziwe na uhuru wa kuzitumia. Bahati mbaya, kuna ruzuku mbalimbali zinazokuja zikiambatana na masharti katika matumizi. Hivyo basi, hata kama Halmashauri itaanda mipango mizuri ya maendeleo, ni vigumu sana kutekeleza miradi yao ya vipaumbele kwa sababu ya ruzuku zenye masharti, ambazo husababisha mipango ya maendeleo isitekelezeke kirahisi.

Ikumbukwe kwamba kiasi cha fedha inayotengwa kwenye bajeti za Halmashauri ni kidogo mno cha Shilingi trilioni 3 kati ya trilioni 11 za bajeti ya taifa (2011/12). Hizi Shilingi trillioni 3 ni sawa na 94% ya bajeti nzima ya Halmashauri, na hii inathibitisha jinsi ambavyo hawana vyanzo vya ndani vya kutosha.

Mafunzo ya Osaka yaliwataka viongozi wa Serikali ya Tanzania kutenga kiasi cha kutosha cha bajeti kutekeleza wingi wa majukumu ya Halmashauri yaliyogatuliwa na kupelekwa kwao kama kweli wameazimia kufikia ugatuaji wa madaraka. Fedha hii inaweza kuwa zile kutoka vyanzo vya

ndani au katika ruzuku isiyo na masharti[5]. Kama hakuna bajeti ya kutosha inayotengwa, basi hakuna sababu ya kugatua majukumu kwenda ngazi za Halmashauri. Vinginevyo, shughuli hizo hazitatekelezwa na mwishowe jamii itateseka kwa kukosa huduma. Kama tulivyoona kwa Halmashauri za Japani, ikitokea kwamba 85% ya majukumu ya kutoa huduma za elimu yamegatuliwa na kupelekwa ngazi za Halmashauri, basi kiasi cha kutosha cha bajeti ya kutekeleza majukumu hayo hugatuliwa na kupelekwa Halmashauri ili kufikia malengo. Vinginevyo si haki hata kidogo kwa Halmashauri na hasa kwa watu wanaotegemea huduma.




**Mchoro (4): Aina za Kodi kwenye Majiji/Miji**
**Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010**
**(Ministry of Home Affairs of Government of Japan)**

## b) <u>Kodi za Ndani kwa ajili ya Uendelevu na ushamiri wa Serikali za Mitaa</u>

Kule Japani, kuna sababu zilizo wazi kabisa kuhusu aina zote za kodi zinazotengwa kwenye ngazi zote mbili za SM. Prefectures(SM za Wilaya ndiyo ngazi ya juu za SM) na Municipalities (Miji na Majiji) ndiyo ngazi za chini za SM[6]). Japokuwa Wilaya (Prefecture) ndiyo ngazi ya juu ya SM ya Japani, zinaweza kulinganishwa na Halmashauri za Tanzania kwa ukubwa wa eneo. Kuhusu majukumu, ngazi za chini za SM Japani (Municipalities) ndizo zinalinganishwa na ngazi za Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa/Jiji kwa Tanzania. Hata hivyo kule Japani, huduma zote za muhimu kwa jamii hutolewa na Majiji/Miji (Municipalities) kwa sababu ndizo ngazi za msingi zilizo karibu na watu, huku Prefecture/Wilaya wanahusika hasahasa na maendeleo ya kiuchumi kwa vile majukumu haya yanahitaji eneo kubwa kwa ajili ya mipango na kuyatekeleza kimkakati.

Kulingana na majukumu yalivyo na wajibu wa Majiji/Miji, zifuatazo ni kodi ambazo zinaweza kutozwa na Majiji :

Kama inavyoonekana katika mchoro (4), kodi za nyumba na mali zisizo hamishika ni sawa na 45.3% ya mapato yatokayo na kodi, ambayo ni karibu na nusu ya mapato yote yatokanayo na kodi. Ukijumlisha na "Kodi ya mkazi"(kodi ya Kichwa) pamoja na "kodi ya mipango miji", inakuwa ni zaidi ya 80% ya mapato yatokanayo na kodi. Kodi za nyumba na kodi ya mipango miji hutozwa kwenye ardhi na majengo na hizi ni kodi ambazo hakuna awezaye kuzikwepa. Kama ardhi yote na majengo yote yamesajiliwa na kuthaminiwa vizuri, basi hivi ni vyanzo vya uhakika kwa serikali za Mitaa.

[5] Kwa hatua zilipofikia kwa sasa, bado haishauriwi kugatua madaraka ya kifedha na kuwapa SM mamlaka makubwa ya kutoza kodi. Hii ni kwa sababu hali hii itaziumiza zile SM zilizo kwenye maeneo yenye ufukara ya vijijini, kwa vile hazina vyanzo vya uhakika vya kodi, huku zile SM tajiri za mijini zitakuwa na mapato mengi kutoka vyanzo vyao vya ndani . Kwa hiyo ni busara zaidi kuendelea kutoa ruzuku kutoka chanzo kimoja, lakini SM ziwe na uhuru na maamuzi wa kuzitumia kulingana na vipaumbele vyao kwa sasa.

[6] Kuna Prefecture/Wilaya 47 na (Munispaa) 1,742 hadi kufikia Octoba 2012. Manispaa za Japani zinajumuisha Majiji**<u>, Miji na Vijiji</u>**, na tofauti na mgawanyiko wa ngazi za SM za Tanzania.

"Kodi ya kila mkazi wa Halmashauri za Japani" ni "kodi ya kichwa" iliyofutwa hapa Tanzania ambayo ni "kodi ya maendeleo"[7]. Chanzo hiki cha kodi pia huwa ni chanzo cha kuaminika kwa sababu wakazi wote wameandikishwa na Halmashauri inajua wanapoishi. Tukiangalia hali ya Tanzania, vyanzo vingi vya mapato ni vile vinavyohusiana na shughuli za kiuchumi, mfano ushuru wa mazao (23%), ushuru wa huduma (18%), ushuru wa nyumba za kulala wageni(3%), leseni (10%), karo na malipo mbalimbali (17%), ambazo hubadilika kulingana na mabadiliko ya hali ya uchumi wa eneo husika, na cha kushangaza ni kwamba kodi ya majengo ni 8% tu ya mapato yatokanayo na kodi.

Mafunzo ya Osaka yaliwapa viongozi wa Tanzania changamoto kwamba ili Halmashauri ziweze kutoa huduma endelevu zinazohitajika kwa wakati na viwango vinavyotegemewa, ni lazima kujenga wigo mpana na mfumo wa uhakika wa kukusanya kodi ndani ya Halmasahuri zenyewe. Uzoefu wa Japani unaonyesha kwamba bila kuweka msisitizo kwenye vyanzo vyenye uhakika vya kodi/ushuru kama vile kodi za majengo, kodi ya kichwa/kodi ya maendeleo, siyo rahisi hata kidogo kwa Halmashauri kutekeleza majukumu yake. Kwa mazingira haya, ni muhimu kuwa na mfumo wa daftari la kuandikisha ardhi na mali zisizo hamishika pamoja na daftari la wakazi wote kwa kila Halmashauri, hii itasaidia nchi nzima siyo tu kwenye masuala ya kukusanya mapato, bali kwa matumizi mengine mengi.

Kuhusu utaratibu huu, inafaa kusema kwamba tayari Tanzania kuna mifano ya kufurahisha na inayotia moyo ya Halmashauri zinazotekeleza kile kinachopendekezwa hapa, rejea kisa mkasa cha Manispaa ya Mtwara Mikindani kwenye Sura ya Tatu.

### 3.4 Maendeleo ya Kiuchumi ya Serikali za Mitaa – Uzoefu wa kufurahisha wa dhana ya ki-Japani ya "Kijiji kimoja zao moja" au (OVOP)"

Hitaji la maendeleo ya kiuchumi ya Halmashauri limekuwa likisumbua vichwa vya Wakurugenzi wengi wa Tanzania. Kuhusiana na hili, kuna uzoefu maarufu nchini Japani wa dhana ijulikanayo kama "zao moja kwa kijiji kimoja" maarufu kama OVOP, iliyoanzia kwenye wilaya/ Prefecture ya Oita ambayo hapo awali ilikuwa moja ya wilaya fukara kuliko zote nchini humo. Uzoefu unaotokana na dhana hii unaweza kuwa muafaka kwa Tanzania kama utatafsiriwa na kutumika inavyostahili kulingana na mazingira ya Tanzania.

#### (a) Zao moja kwa kijiji kimoja (OVOP) ni nini?

Vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" au OVOP ni mkusanyiko wa ubunifu wa shughuli za maendeleo ya jamii zilizobuniwa na kupata msukumo wa viongozi kutoka jamii husika katika Wilaya (Prefecture) ya Oita, ambao waliipenda jamii yao na wakahuzunishwa kutokana na hali ya ufukara uliokuwa umekithiri huko miaka ya nyuma. Japokuwa juhudi kama hizo za mtu mmoja

[7] Tofauti pekee ni kwamba kodi ya kichwaTanzania hutozwa kwa kiwango sawa kwa kila mtu, kwa Japani kodi ya mkazi hutozwa kulingana na viwango vya kipato cha kaya. Kama hakuna kipato cha kiasi fulani kinachokubalika, basi wanakaya wa kaya hiyo hawana sababu ya kulipa kodi ya mkazi.

mmoja zilikuwepo hapa na pale kwenye Wilaya (Prefecture)ya Oita tangu miaka ya 1960, dhana yenyewe ya "zao moja kwa kijiji kimoja" au OVOP ilianzishwa rasmi mwaka 1979 na Dr. Morihiko HIRAMATSU, akiwa Gavana[8] wa Wilaya hiyo kwa kuanza kuzitambua baadhi ya juhudi za jamii zilizokwisha anza na kuziendeleza.

Dr. HIRAMATSU, alikuwa ni msomi mwenye mafanikio makubwa akiwa mtumishi wa cheo cha juu kwenye Wizara ya Biashara za kimataifa na Viwanda yaani "Ministry of International Trade and Industry (MITI)". Hii ilikuwa Wizara yenye nguvu sana, lakini aliamua kuacha kazi hiyo na kurudi kwenye Wilaya ya Oita yaani nyumbani kwao. Kilichomsukuma ni kwa sababu alihofia sana kuwa Wilaya ya nyumbani kwake iliendelea kubaki nyuma kimaendeleo na kuwa miongoni mwa Wilaya fukara kuliko zote nchini Japani kwa wakati huo.

Baada ya kurudi kwao, aligombea na kushinda cheo cha Ugavana wa Wilaya ya Oita. Alipoanza kazi hii jambo la kwanza alilolifanya ni kutembelea vijiji vyote kwenye Wilaya hiyo. Wakati akifanya matembezi haya, alikuta kuna miradi ya maendeleo na jitihada mbalimbali za watu wenyewe kujaribu kujinasua huko vijijini. Aliguswa sana na jitihada hizo za wananchi wakiongozwa na viongozi wao wenye mapenzi mema na juhudi hizi zilikuwa hazijulikani kwa serikali. Alithamini sana juhudi za jamii, na akawatia moyo waendelee na jitihada za kujikwamua. Kwa wanavijiji, wengi wao walikuwa hawajawahi kutoka nje ya vijiji vyao, kwa hiyo kwao ilikuwa ni faraja kubwa kutembelewa na mtu mkubwa kama Gavana na kusifiwa kwa kile walichokuwa wanakifanya!. Hawakuwahi kuwaza kwamba kile walichokuwa wanakifanya kilikuwa ni kitu cha kiza Jamii na cha thamani machoni pa wengine. Tangu Gavana wao Dr. HIRAMATSU alipofanya matembezi haya, juhudi hizo za jamii zilipewa msukumo mkubwa na watu wakahamasika zaidi na kujisikia fahari wenyewe.

Kwa upande wake, Dr. HIRAMATSU alifikiri ni jukumu muhimu kwa Serikali ngazi ya Wilaya kuunga mkono na kuendeleza juhudi za thamani kubwa zilizoanzishwa na wananchi kutaka kuboresha maisha yao wenyewe, kuzieneza zaidi na kubadilisha uzoefu huu mzuri na viongozi wa vijiji vingine ndani ya Wilaya yao.

Vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" yaani OVOP ina mambo muhimu yanayolitofautisha na dhana nyingine kwani Vuguvugu hili hupelekea kuzalisha bidhaa za kiza Jamii (ikijumuisha utalii), ili kupata maendeleo kwa kutumia raslimali zilizopo ndani ya jamii husika. Hata hivyo, jambo jingine la tofauti kwenye vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" ni kwamba: kuna uzoefu dhabiti wa jamii unaopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi midogo ya maendeleo ya shughuli za kiuchumi ngazi za msingi. Wananchi husika huunganisha uwezo wao wa kujipanga na kutekeleza mustakabali wa maisha yao; jamii zimejijengea uwezo, zimeamka na zina ujasiri; Jamii zimeimarika na zimefikia uwezo wa kujitawala na kujiendesha wenyewe kama kijiji. Ukweli uliopo hapa ni kwamba wananchi wana uzoefu wa kufanikiwa na wakati mwingine kushindwa (lakini wamejijengea uwezo na tabia ya kujikwamua katika kushindwa huko), siyo tu kwamba jamii inategemea kupata mafanikio ya kiuchumi za Jamii, bali pia jamii inatarajia kujijengea uwezo,

[8] Cheo cha Gavana wa Prefecture ni cheo cha juu zaidi kwenye SM za juu Japani ikilinganishwa na Meya wa kwenye SM za Tanzania (Ona "3.2. Usimamizi wa Rasilimali Watu na Ugatuzi wa madaraka" kwa Meya.)

uzoefu na ujasiri na kupata nguvu zaidi katika mchakato huo. Ukweli huu ni muhimu ufahamike ili kulielewa vizuri vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja”. Ikumbukwe kwamba ni rahisi sana kupata mafanikio au faida ya mara moja katika biashara au mradi fulani kutokana na msaada wa mara moja kutoka nje ya jamii, lakini kama jamii hiyo itakumbana na vikwazo fulani fulani baadaye, hawataweza kuvishinda kama watakuwa hawajajijengea uwezo kupitia michakato iliyotangulia ya kutatua matatizo yao kwa nguvu na jitihada zao wenyewe.

Kwa mantiki hii, ni vyema kutambua kwamba nyingi kati ya juhudi zilizojitokeza kwenye Vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja” kule Oita, zilipitia mchakato ufuatao:

- Kabla ya vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja”au OVOP, wanavijiji wa Oita walikuwa fukara sana, walikuwa wamekata tamaa kuhusu mabadiliko, wenye kijicho na kuoneana wivu wao kwa wao, kutokana na hali hii haikuwezekana kushirikiana baina yao ili kuboresha maisha kwa pamoja. Hata hivyo, kupitia Vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja” walianza kujitambua kwamba “Ndiyo, tunaweza kama tunataka!” Haya ni mafanikio makubwa katika mchakato wa kubadili fikra.
- Katika badiliko la fikra hapo juu, wanavijiji walianza kujijengea uzoefu wa kushirikiana kwenye shughuli mbalimbali ndani ya jamii, wakizikabili changamoto wanazokutana nazo na kuzishinda kwa pamoja. Mchakato huu uliwafanya waweze kujipanga vizuri na vizuri zaidi.
- Kupitia mchakato huo huo, waliimarisha mahusiano na taasisi za nje zenye usaidizi ikijumuisha Halmashauri na Asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali.
- Pamoja na ujenzi wa uwezo wa jamii ulioelezwa hapo juu, jamii husika zilifanikiwa kupata matokeo dhahiri ya maendeleo ya kiuchumi.

**(b) Dr. HIRAMATSU alifanya nini akiwa Gavana wa Wilaya?**

Kwanza kabisa, ieleweke vizuri kwamba vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja” halikuwa ni programu ya lazima(“maamrisho ya kutoka juu kwenda ngazi za msingi”) iliyoandaliwa na Dr. HIRAMATSU na kwamba watu hawakuambiwa cha kufanya. Kwa bahati mbaya, baadhi ya nchi zinazoendelea ambazo zilivutiwa na Vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja”, waliuelewa vibaya ukweli huu. Walizingatia tuu zile faida za kiuchumi zinazotokana na OVOP na kujaribu kuendeleza vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja” kama sera ya taifa na kutoa maamrisho kutoka juu kwamba kila kijiji kizalishe kitu ambacho kinaweza kuuzwa hapa nchini au nje ya nchi. Kinyume chake sasa, alichokifanya Dr. HIRAMATSU kwenye Wilaya ya Oita ilikuwa ni, kwanza, kutembelea vijiji vyote, kuzitambua juhudi za wananchi za thamani ambazo zilikwishaanza, akawasifia na kuwatia moyo.

Pili, alivishirikisha vijiji vingine na viongozi wao kuhusu mambo mema yanayofaa kuigwa ili habari hii iwe kichocheo, waanze na wao kufikiri kuhusu maendeleo yao wenyewe kwa kutumia raslimali zilizopo kwenye maeneo husika, badala ya kulalamika eti hawana chochote kwenye vijiji vyao na kukata tamaa.

Tatu, alipotambua bidhaa fulani za kiza Jamii kwenye baadhi ya vijiji, alisaidia kutafuta soko la ndani na nje ya Wilaya ya Oita. Alitumia maarifa yake, uzoefu na mitandao ambayo alikwisha

jijengea alipokuwa afisa wa ngazi za juu Wizara ya Biashara ya Kimataifa na Viwanda. Alizitangaza bidhaa hizi nchi nzima.

Nne, aliwezesha suala zima la kubadilishana uzoefu baina ya viongozi wa vijiji mbalimbali ili wajifunze na kuhamasika kutokana na kujifunza kwa watu walio kwenye ngazi moja na siyo kujifunza kwa ngazi tofauti ya maendeleo. Alianzisha shule ya kuendeleza raslimali watu[9]" iliyoitwa "*Toyonokuni*[10]. Juhudi hizi za Gavana, zilisaidia kuchochea ari ya viongozi na hii ikapelekea kuibuka kwa miradi mingi yenye sura ya "zao moja kwa kijiji kimoja" yaani OVOP.

Kama inavyoonekana hapo juu, dhamira ya vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" au OVOP ilikuwa ni Halmashauri kuzitambua, kuzisifia, kutia moyo juhudi za kimaendeleo zinazojitokeza kwa jamii. Jukumu la Halmashauri ni "uwezeshaji" na siyo "utekelezaji" au "uelekezaji". Dr. HIRAMATSU hakuwaambia wanavijiji jambo la kufanya katika kuendeleza vuguvugu hili, bali aliheshimu juhudi zao na umiliki wao, pamoja na nguvu zao. Mafunzo ya Osaka yanasisitiza vuguvugu la"zao moja kwa kijiji kimoja", kwani ni dhana muafaka kwa mazingira ya Tanzania, na inaaminika kwamba tayari zipo juhudi za namna hiyo kwenye Vijiji na wapo viongozi wazuri wanaojali maendelo ya nyumbani kwao. Ingelikuwa ni jambo la manufaa makubwa kwa Tanzania kuunga mkono vuguvugu hili na kutoa fursa ya wazalishaji kujifunza kwa wenzao walio ngazi moja. Mafunzo ya Osaka yaliwataka viongozi wa Tanzania kudhani kwamba eti hakuna chochote kwenye vijiji vyao. Kuna mambo mengi mazuri yanayostahili kuigwa lakini pengine wao ndio hawajayatambua. Ni wajibu wa viongozi wa Halmashauri kuanza kuzitambua juhudi za jamii zilizopo, kuzitia moyo, na kubadilishana uzoefu na wengine. Ingekuwa ni njia yenye tija zaidi ya wazalishaji kujifunza kutoka kwa wenzao walio kwenye ngazi moja kuliko kujifunza watu wa ngazi tofauti au kutoka kwenye vitabu. Ni kutokana na mtizamo huu ndipo kitabu hiki kikaandaliwa.

### 3.5 Masuala Mengine

Kuna mengi ambayo hatukugusia hapo juu kutokana na kukosa nafasi. Lakini, yapo ambayo ni ya muhimu kugusia ambayo yanafaa kwa Tanzania kama vile kisamkasa cha Minamata na uzoefu unaotokana na "Ugonjwa wa Minamata"(Minamata Disease) na jinsi walivyoweza kuhuisha jamii kutokana na mkasa huo; Upangaji mipango shirikishi jamii; mipango miji; mipango ya matumizi bora ya ardhi na marekebisho ya ardhi, uzoefu wa Japani kuhusu maendeleo ya kiuchumi na mchango wa Halmashauri katika mkasa huo, n.k.

Kuhusu kisamkasa cha Minamata, mafunzo ya Osaka yanaweka msistizo kwenye umuhimu wake, na inaaminika kwamba nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania zina mengi ya kujifunza kutokana na kisa mkasa hiki. Masuala ya kisa hiki yatagusiwa kwa undani kwenye kitabu kinachofuata.

---

[9] Inaitwa "shule" lakini hakuna majengo. Huwa ni aina fulani ya mafunzo kwanjia ya warsha kwa ajili ya viongozi ili kuwakutanisha pamoja.
[10] "Toyonokuni" jina la kienyeji la eneo hili la Wilaya ya Oita

## 4.0 MAENDELEO BAADA YA MAFUNZO YA OSAKA YALIYOSABABISHA KUCHAPWA KWA KITABU HIKI

Kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya 1 hapo juu, mafunzo ya Osaka yalikuwa yameandaliwa mahsusi kwa nchi ya Tanzania kwenye miaka mitano ya mwanzo(2002 – 2007), yaliendelea kwa miaka mingine sita lakini wigo wake ukapanuliwa na kuingiza nchi nyingine tatu (2008 – 2012). Mafanikio makubwa katika miaka hii 11 hapa Tanzania ni kule kuanzishwa kwa Umoja wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi waliosoma Osaka, kwa kifupi TOA. Huu ni mfano wa za Jamii Duniani kuwa na Umoja wa Wahitimu wa kozi ya aina moja ukijumuisha Wadau Maarufu ambao ni viongozi wa maboresho kama vile Makatibu Tawala wa Mikoa (RAS) na Wakurugenzi wa Halmashauri pamoja na wakuu wengine kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI). Japokuwa haikutegemewa, lakini ni jambo la kupendeza hata kwa JICA ambao wanaendesha maelfu ya kozi za mafunzo duniani kote.

Kwa nyongeza, TOA wameshaanza kuendesha semina mbalimbali na warsha za mafunzo kama vile Mafunzo baada ya Osaka na Warsha za Mafunzo za Kanda kwa ajili ya kubadilishana uzoefu baina ya Halmaushauri wanachama. Fursa hizi, siyo tu kwamba zina saidia kubadilishana maoni baina ya Halmashauri wanachama, bali yametoa uwanja ambao ni nadra kuupata wa majadiliano na kuhusu uhalisia wa Ugatuaji wa Madaraka, hususan changamoto wanazokutana nazo katika kutekeleza maboresho ya Serikali za Mitaa.

Mpaka sasa, hakuna asasi ya namna hii hapa Tanzania, inayowahusisha Watendaji wa Serikali za Mitaa na wale wa Sekretarieti za Mkoa. Jumuia ya Serikali za Mitaa (ALAT) ipo, lakini wahusika wake wakuu ni Wenyeviti wa Halmashauri, Mameya na Wabunge. Vikao vya Jumuiya hii haviwapi fursa Wakurugenzi wa Halmashauri kushiriki kikamilifu na kutoa ushauri wa kitaalamu ingawa wao pia ni wajumbe. Kwa mantiki hii, TOA ina uwezekano mkubwa wa kukua hadi kuwa Umoja wa Watendaji Wakuu wa Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa yaani Wakurugenzi wa Halmashauri na Makatibu Tawala wa Sekretarieti za Mikoa ambao ni wataalamu na watekelezaji wa ugatuaji wa madaraka na maboresho nchini. Hawa ndio wanaoshughulika kila siku kwenye mstari wa mbele wa maboresho. Maoni na mapendekezo yao ya pamoja yanaweza kuwa ni ya maana sana na ya kuongeza ufanisi kwenye kutekeleza maboresho.

Kuhusu mambo mema yanayofaa kuigwa, tayari Tanzania imekwishajijengea uzoefu kwa zaidi ya muongo mmoja wa utekelezaji Ugatuaji wa Madaraka kwenda ngazi za msingi katika kila Mamlaka ya Serikali za Mtaa. Lazima kutakuwepo na idadi kubwa ya mambo ya kufurahisha na uzoefu mzuri kwenye Halmashauri nyingi kote nchini ambao unafaa kushirikisha Halmashauri nyingine. Japani inaamini kwamba aina hii ya kujifunza kwa taasisi zilizo kwenye ngazi zinazofanana inaweza kuwa muafaka zaidi kuliko kujifunza kutoka nje ya nchi yaani kutoka kwenye ngazi tofauti au ya juu sana. Tanzania inaweza kujifunza vizuri kutokana na uzoefu ulioko ndani mfano shughuli za OVOP kama zilivyoelezwa kwenye 3.4. hapo juu. Kitabu hiki cha rejea kiliandaliwa kwa kuzingatia maelezo na msingi huo ulioelezwa hapo juu. Ni matumaini ya TOA na mafunzo ya Osaka kwamba yatachangia kuboresha utendaji ndani ya Mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa, kila moja ikimchochea mwenzie, na kuendeleza mambo mema yanayojitokeza, ambayo yatapelekea kwenye ufanisi na mafanikio ya ugatuaji wa madaraka katika nchi hii.

Mwishowe, inastahili kusema kwamba kutokana na matokeo ya kufurahisha yaliyotokana na mafunzo ya Osaka kwa nchi ya Tanzania, ambayo yameelezwa kwenye sura hii, Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japani (JICA) limeaamua kuendelea kutoa mafunzo ya Osaka kwa miaka mingine mitano, yakilenga Tanzania kwa mara nyingine tena na litatoa msisitizo maalumu katika kuwezesha shughuli za wanaumoja wa TOA na juhudi zake za ujenzi wa kitaasisi. Hii ina maana kwamba, viongozi wengine wengi wa maboresho Tanzania watafaidika kutokana na mafunzo ya Osaka ili waweze kuchangia utekelezaji mzuri zaidi wa maboresho ya ugatuaji wa madaraka kwenda ngazi za msingi nchini.

# Sura ya Pili: Jitihada za Jamii kwa Ajili ya Huduma Bora

Mtazamo wa Jitihada za Jamii ni mfumo mpya katika eneo la maendeleo vijijini, ambao lengo kuu ni maendeleo vijijini. Malengo Mahsusi ya mfumo huu ni kuongeza ubora wa maisha ya watu maskini, na kuboresha miundombinu. Ni mfumo wa hiari wa kundi la watu wanojiendesha wenyewe wakiwa na tabia zinazofanana za kijamii na kiuchumi, ambao wanaungana ili kuanzisha fikra zitakazochochea maendeleo endelevu. Mtazamo wa Jitihada za Jamii kwa ajili ya Maendeleo Vijijini katika hali ya kendesha mipango ya kiuchumi huleta ajira, miondombinu ambayo jamii inaweza kujitengenezea, stadi za kazi pamoja na shughuli mchanganyiko. Pia mtazamo huu huleta mipango ya ustawi wa jamii ili kuboresha afya, lishe na maslahi ya jamii kwa ujumla.

Jitihada za Jamii huwa na maana ya majaribio ya jamii kupambana na changamoto zinazoikabili kijamii na kiuchumi bila kusubiri miradi mikubwa kutoka serikalini. Jitihada za Jamii hujumuisha maazimio ya kutatua matatizo ya jamii kupitia jamii kujipanga, kushiriki na kutekeleza. Katika haya yote jamii yenyewe huona hitaji, hupanga namna ya kufikia hitaji, hutafuta raslimali zilizopo zinazohitajika kufikia hitaji, hujipanga katika makundi ya utekelezaji na kutekeleza mradi.

Mara nyingi Jitihada za Jamii huwa na maana ya uundaji wa vyama vya hiari katika jamii, ambapo wanchama huwa na malengo yanayofanana, hujipanga na kuratibu mipango wakiwa na lengo mahsusi la kuboresha hali ya kijamii na kiuchumi katika jamii yote. Tafiti zinaonesha  kuwa vikundi katika jamii kwa miaka mingi vimefanikiwa kujiendesha katika kujenga barabara, vituo vya afya, madaraja na nyumba, kulima mashamba, kufadhili masomo, na kuanzisha taasisi za viwanda, kutaja machache. Ushahidi wa haya umeleta ongezeko na kupanuka kwa uanachama na jitihada za Jamii katika jamii za vijijini.

Hapa Tanzania, Jitihahada za Jamii na Ushiriki wa Jamii vimekuwa dhahiri kutokana na historia ya itikadi ya kijamii na kiuchumi ya kujitegemea. Tangu Uhuru, jamii katika vijiji vyao zilishauriwa kuishi kwa pamoja na kutumia mbinu za ushirika katika kutatua matatizo yao. Kileleni kabisa mwa itikadi hii kati ya miaka ya 1960 na 1970 na hasa baada ya Azimio la Arusha, jamii zilianzisha miradi mbalimbali na kuitekeleza katika namna za ujenzi wa shule na zahanati, kuchimba visima na mabwawa madogo, kulima barabara na kuendesha kilimo cha ushirika.

Pamoja na kuwa mbinu hizi zilipungua katika miaka ya 1990 kuelekea milenia mpya kutokana na madai ya serikali kuwa inaweza kutoa huduma zote, kuna jamii ambazo, siku za karibuni zimetumia Jitihata za Jamii kwa kina katika ujenzi wa shule, zahanati, madarasa na majengo ya serikali; vyote vikilenga kuboresha utoaji wa huduma.

Katika sura hii, mbinu bora mbalimbali zimewasilishwa kutoka Halamshauri za Wilaya za Lindi, Nachingwea, Mbeya, Momba na Masasi, Halmashauri ya Mji wa Masasi na Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya. Zimeelezwa kwa kifupi hapa chini.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Lindi inahusu ujenzi shirikishi wa barabara ya Mvuleni – Kitomanga, ambacho ni kipande muhimu cha barabara ambayo kukosekana kwake kulileta matatizo makubwa. Kupitia jiihada za Jamii, jamii iliweza kujenga barabara inayopitika mwaka mzima kwa kutumia uhamasishaji jamii na ujenzi wa uelewa kwa wanakijiji, kuazimia na kujumuisha ujenzi wa barabara ya Mvuleni – Kitomanga kwenye mpango wa kijiji. Halmashauri ilipeleka mhandisi katika eneo la ujenzi, ilitenga fedha na vifaa, ilitangaza zabuni na hatimaye kuingia mkataba na mkandarasi na pia kutenga fedha kwa ajili ya matengenzo ya mara kwa mara ya barabara ya Mvuleni – Kitomanga.

Mbinu Bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea inaonesha ushiriki jamii na Jitihada za Jamii katika ujenzi wa Boma (ofisi ya Serikali). Kabla ya Mwaka 2008 H/W ya Nachingwea ilishuhudia utoaji duni wa huduma kutokana na kutokuwepo kwa jengo na vifaa vya kisasa vya ofisi. Baadaye Bazara la Madiwani liliweka azimio la kujenga Boma la Kisasa. Katika Mkutano huu, Mkuu wa Wilaya (Marehemu Bwana Leonidas Gama) alikuwa mwalikwa. Mikakati iliyotumika kufikia malengo ni pamoja na uundaji wa kamati ya utekelezaji, uendeshaji wa mikutano ya kuhamasisha jamii katika ngazi zote na kukusanya michango kutoka kila Kata na Kijiji. Michango hii ilikuwa mchanga, mawe, mbao, changarawe, chakula cha wafanyakazi, matofali ya kuchoma na mirunda kwa kutegemea upatikanaji wa maliasili katika eneo husika. Pia, Halmashauri ilijikita katika kutoa taarifa kuhusu michango ya jamii na matumizi yake, na utekelezaji bora chini ya usimamizi wa mhandisi wa Halmashauri.

Mbinu Bora ya H/W ya Masasi inahusu Jitihada za Jamii za Jamii katika ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Mapili. Kijiji hiki kilichopo 80km kutoka makao makuu ya Halmshauri ni mojawapo ya vijiji 126 ambavyo havijawahi kuwa na Zahanati toka kuanzishwa kwa Halmashuri mwaka 1978. Wanakijiji walikuwa wakitembea 25km kwenda Hospitali ya Wilaya ya Newala kupata huduma za msingi za afya, jambo ambalo lilileta changamoto nyingi. Wanakijiji walianza kwa kutoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya, kuchangia fedha taslimu na baadaye waliunda kamati ya ujenzi, kwani wanakijiji walitambua kuwa Serikali ya Kijiji ilikuwa na majukumu mengi ya kila siku. Halmashuri ilisaidia katika kuandaa na kupitisha makadirio bora ya gharama za ujenzi ambazo zilitumiwa na wanakijiji kununua vifaa vya ujenzi vya viwandani na kuanza ujenzi rasmi wa zahanati ya Mapili kwa kutumia mafundi waliopo kwenye jamii. Ujenzi ulianza tarehe 23 Februari, 2009. Mgawanyo asilia wa majukumu kijinsia ulielekeza ushiriki wa wanaume na wanawake katika shughuli za ujenzi. Ukusanyaji zaidi wa fedha ili kukamilisha ujenzi ulitumia mfumo wa manunuzi wa Korosho uliorahisisha ukusanyaji wa michango ya jamii (stakabadhi mazao ghalani).

Mbinu Bora ya Halmshauri ya Mji wa Masasi ni jitihada ya jamii kwenye kuboresha elimu ya msingi katika kijiji cha Mpekeso. Kabla ya mwaka 2010, uandikishaji wa wanafunzi ndani ya Halmashauri uliporomoka sana kutokana na umbali ambao wanafunzi wenye umri mdogo walilazimika kutembea kuzifikia shule, ukosefu wa mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia na uelewa mdogo kati ya wazazi kuhusu umuhimu wa elimu ya mtoto. Kijiji cha Mpekeso kilikuwa kati ya vijiji vilivyo athirika sana na tatizo hili. Kijiji kiliazimia kuboresha elimu ya msingi kwa kujenga uelewa kwa jamii, kukusanya michango, kujenga madarasa mawili, kushirikisha wanakijiji katika utambuzi wa eneo la ujenzi, utengenezaji wa matofali na ujenzi rasmi wa jengo la kwanza la MEMKWA. Watu walishiriki pia katika uandikishaji wa wanafunzi, uanzishaji wa shule mpya ya msingi kijijini na ujenzi wa madarasa mawili na matundu 6 ya choo. Mwisho, msaada wa Halmashauri kwa shule ya msingi Mpekeso ulfanyika kupitia programu ya TASAF ambayo ililenga uendelezaji wa miundombinu ambapo Halmashauri iliunda kamati ya uendeshaji wa mradi. Timu hii ya TASAF iliwezesha jamii kuchagua na kuthibitisha kamati ya uendeshaji wa mradi.

Jitihada Za Jamii kwenye Miradi ya Barabara na Maji katika H/W Mbeya inawasilisha uzoefu wa Kata za Tembela, Ijombe, Itewe, Maendeleo na Inyala. Wananchi waishio katika Vijiji vya Maendeleo, Tembela, Ijombe na vijiji vya ndani zaidi katika kata za Ulenje na Itewe walikuwa na shida sana katika kufikia masoko

kwa ajili ya mazao yao ya kilimo kutokana na ukosefu wa barabara ya uhakika kwa misimu yote na ukosefu wa maji safi na salama kwa ajili ya jamii za Kata ya Ijombe. Mwaka 2012/2013 Jamii za Kata za Tembela, Ijombe, Itewe, Maendeleo na Inyala ziliunganisha nguvu na Halmashauri ili kuboresha barabara ya Tangamo-Ijombe-Itewe na kujenga Daraja la Nkunywa katika barabara ya Ntangano – Ijombe. Hili lilihusisha uanishaji na utambuzi wa hitaji la barabara na daraja, ukusanyaji wa fedha taslimu, ushiriki katika shughuli za ujenzi na matumizi ya akaunti maalum (Force account). Mikakati kama hii ilitumiwa pia katika mradi wa maji ingawa kupima skimu, kuunda kamati za watumia maji na kutoa mafunzo ni mikakati ya jamii kwani mradi wa maji unasimamiwa na jumuia za vijiji za watumia maji.

Mbinu Bora ya H/W ya Momba ni ya kipekee. Inahusu jitihada za Jamii katika ujenzi wa madaraja ya kuning'inia yaitwayo "kiteputepu". Jamii za Momba zilizoea kutumia ngalawa na madaraja ya kienyeji ya miguu kuvuka mto momba; ingawa kwa hofu kuu kuhusu usalama wao. Kutatua changamoto hii jamii iliamua kupanga na kufanya maamuzi kwa msaada wa wawezeshaji kutoka Halmashauri; kwa kutumia mfumo wa Fursa na Vikwazo Kwa Maendeleo (O&OD). Kati ya mwaka 2004 na 2006, ujenzi wa uelewa, ukusanyaji wa michango ya kaya na maombi ya usaidizi wa Halmashauri vilifanyika na kuwezesha ujenzi wa madaraja ya kuning'inia 16. Madaraja haya yameboresha sana mawasiliano ya watu na usafirishaji wa mazao ya kilimo.

Mbinu Bora ya Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya imepewa jina la " Jitihada ya Marafiki wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya" kwa sababu utekelezaji wake ni wa kipekee kwani ujenzi wa njia za ndani ya Hospitali ulitekelezwa kwa ushiriki thabiti wa wasamaria wema wenyeji tu. Hadi mwaka 2014 kulikuwa hakuna njia za hospitali kuunganisha idara mbalimbali kama idara ya wagonjwa wa nje, Wazazi, Maabara, Stoo, Wadi za wanawake, wanaume na watoto na chumba cha kuhifadhia maiti. Lakini kupitia kutambua hitaji, ushawishi na uratibu wa wadau, kushirikisha hitaji kwa utawala wa hospitali, kuendesha mikutano ya wadau na kukusanya fedha toka kwa Marafiki; ujenzi wa njia za ndani za hospitali uliwezekana. Jitihada hii imefanikisha kuwepo kwa kundi la Marafiki wa hospitali hii lenye wanakikundi 22, maeneo ya hospitali yaliyoboreshwa na watumishi wenye motisha.

Sura hii inahimiza Serikali za Mitaa kuzihamasisha jamii kuainisha changamoto zinazokabili utoaji wa huduma na kuunganisha nguvu kuzitatua. Inarejesha mfumo wa kujitegemea kwa jamii, ambapo jamii zinakuwa mbele kutambua mahitaji yao, kupanga kutatua changamoto, kutekeleza mikakati ya kuondoa changamoto na kufurahia maboresho. Sura hii inaonesha jitihada za Jamii za jamii na usaidizi kutoka Halmashauri na Serikali kuu katika utoaji huduma bora na endelevu. Nadharia ya mipango na utekelezaji kuanzia chini kama ilivyo katika Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD) imekuzwa na mbinu bora zilizoelezewa kwa kina katika sura hii na inazitaka Halmashauri zote Tanzania kuziwezesha jamii kutatua matatizo yanayowakabili kupitia jitihada na mipango shirikishi kwa kutumia mfumo wa O&OD.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA LINDI


**UJENZI SHIRIKISHI WA BARABARA ZA VIJIJINI**



***BARABARA YA MVULENI – KITOMANGA***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Lindi ni mojawapo ya Halmashauri sita za Mkoa wa Lindi. Halmashauri hii ilianzishwa tangu mwaka 1984 chini ya Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Na. 7 ya 1982. H/W ya Lindi inapatikana kati ya Latitudo $9^0$.3' na $10^0$.45' Kusini na Longitudo $38^0$.4' na $40^0$ Mashariki. H/W ya Lindi hupakana na H/W ya Kilwa upande wa Kusini, Bahari ya Hindi upande wa Mashariki, Mkoa wa Mtwara upande wa Kusini na H/W ya Ruangwa upande wa Magaharibi. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, H/W ya Lindi ina wakazi 194,143 (91,647 ni wanaume na 102,496 ni wanawake). Kiutawala, H/W ya Lindi imegawanyika katika majimbo mawili ya uchaguzi ambayo ni Mchinga na Mtama. Kuna tarafa 9, Kata 31, Vijiji 140 na Vitongoji 748.




***Ramanani ya H/W ya Lindi (Tarafa na Kata)***

H/W ya Lindi ina misimu miwili ya mvua, mvua fupi (vuli) kati ya Novemba na Januari, na mvua za masika kuanzia Machi hadi Mei. Kwa ujumla, Halmashauri hupata mvua kwa wastani wa 1000mm kwa mwaka, kukiwa na mabadiliko ya kiasi mwaka hadi mwaka na mvua chache kiasi upande wa ndani ya nchi kuliko pwani.

Kwa ujumla, Halmashauri bado inategemea wakulima wadogo wadogo wanaotumia kilimo cha kuhamahama; takribani 95% ya wakazi hutegemea kilimo (RIPS, 2004). Uvuvi pia ni muhimu kwa maisha ya vijiji vilivyopo pwani, lakini upatikanaji wa samaki ni mdogo na vifaa vya kuvulia ni vya kienyeji. Shughuli nyingine za kiuchumi ni biashara ndogondogo, uvunaji wa mazao ya misitu, na viwanda vidogovidogo.

Vijiji vya Mvuleni na Kilolambwani huunda sehemu ya Kata ya Kilolambwani katika H/W ya Lindi. Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012 wakazi wa Kata ya Kilolambwani walikuwa 6,286. Kata hii ina vijiji saba ambavyo ni Dimba, Kijiweni, Kilolambwani, Maloo, Mnang'ole, Mvuleni A and Mvuleni B. Wakazi wa vijiji hivi huishi kwa kilimo cha kuhamahama na biashara ndogondogo tu huku wakipata huduma chache za kijamii na kiuchumi kutoka makao makuu ya Halmashauri kutokana na miundombinu duni; hasa barabara za vijijini.

**2.0 TATIZO**

Barabara za vijijini ni zile zinazounganisha maeneo ya kilimo na masoko vijijini na kutoka masoko hayo kuelekea mtandao wa barabara kuu. Barabara za vijijini ni barabara ndogo, njia na mapario katika maeneo ya vijijini ambayo yana idadi ndogo ya vyombo vya moto vya usafiri. Kimsingi barabara hizi huunganisha vijiji na vijiji vingine au vijiji na mitandao ya barabara kuu.

Ufunguaji na uboreshaji wa barabara za vijijini ambao pia huitwa matengenezo ya mara kwa mara ya barabara zilizopo hutia chachu katika maendeleo kwa namna mbalimbali. Husaidia usafirishaji wa pembejeo na mazao ya kilimo kutoka na kwenda kwenye masoko pamoja na kuboresha kupatikana kwa huduma kama elimu, afya, teknolojia, elimu na taarifa za kilimo. Ufunguaji wa barabara husaidia mabadiliko katika bei za bidhaa zisizo za kilimo na za kilimo, mabadiliko katika mifumo ya uzalishaji, kuimarika kwa ubobezi, kuibuka kwa shughuli zisizo za kilimo, kuongezeka kwa fursa za vipato na hatimaye maisha ya viwango vya juu. Husaidia kuimarika kwa uhamaji toka vijijini kuelekea maeneo ya mijini na kuunganisha maeneo ya vijijini. Mwisho husaidia kuboresha ukakika wa chakula kwa wakazi wa vijijini vipindi vya uhaba wa chakula. Kwa maneno mengine, usafirishaji huchangamsha maendeleo ya masoko vijijini.

H/W ya Lindi ilikuwa na tatizo la upungufu na ubora duni wa miundombinu ya barabara za vijijini kwa miaka mingi kabla na baada ya Uhuru iliyojidhihiridha katika utendaji duni wa Halmashauri katika kutoa huduma. Mwaka 2008, Halmashauri ilikuwa na mtandao wa barabara wa 621km. Jedwali lililopo hapa chini linaonesha hali ya barabara mwaka 2008.

**Jedwali 1: Mtandao wa Barabara H/W Lindi Mwaka 2008**

| No. | Aina ya Barabara | Umbali kwa km | Lami | changarawe /Udongo | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | changarawe | Udongo |
| **1** | Barabara Kuu | 198km | 103km | 95km | – |
| **2** | Barabara za Mikoa | 78km | | 22km | 56km |
| **3** | Barabara za Halmashauri | 308km | | 40km | 268km |
| **4** | Barabara za Vijijini | 37km | – | – | 37km |
| **5** | Madaraja | 5 | | | |
| **6** | Kalavati | 36 | | | |

Kati ya Vijiji vilivyokuwa na changamoto kuu ya barabara ni Mvuleni na Kilolambwani. Changamoto kuu zilizovikabili vijiji hivi viwili zilijumuisha ongezeko la umbali wa 70km kupitia makutano ya Mchinga ili kufikia huduma za rufaa katika kituo cha afya cha Kitomanga na usafirishaji wenye usumbufu wa bidhaa kutoka na kwenda vijiji vya Mvuleni na Kilolambwani hadi barabara kuu ya Lindi – Dar es Salaam. Hali hii ilipelekea kuwepo kwa vifo vya wagonjwa, kuoza kwa mazao ya shambani na upungufu wa bidhaa muhimu zitokazo nje. Kupambana na changamoto hizi jamii iliona haja ya kufungua barabara ya 18km kuunganisha vijiji vya Mvuleni na Kilolambwani na barabara kuu ya Lindi – Dar es Salaam na Kituo cha afya cha Kitomanga. Uamuzi wa kufungua barabara ya 18km ulileta changamoto nyingine. Hizi zilijumuisha msitu mnene, mabonde makubwa ya mito na yenye udongo wa mfinyanzi ambavyo vilifanya kazi ya ujenzi wa barabara kuwa ngumu. Changamoto hizi zilisababisha gharama kubwa katika kusafisha eneo, kushindilia udongo na ujenzi wa kalavati na madaraja.

**3.0 MALENGO**

Lengo kuu la kufungua barabara ya 18km lilikuwa kuunganisha vijiji viwili vya Mvuleni na Kilolambwani na barabara kuu (DSM-Lindi) na kufikika kwa urahisi kwenye huduma za rufaa katika Kituo cha Afya cha

Kitomanga. Sambamba na lengo hili kuu wanakijiji wa vijiji hivi viwili walilenga kurahisisha usafiri wa mazao ya Kilimo (Korosho, Karanga, Ufuta na mazao ya uvuvi kama samaki) kwenda barabara kuu, kuboresha uingizaji wa bidhaa na huduma muhimu (ndizi na mihogo) kutoka Matapwa (Mpingo) na kuimarisha huduma nyingine za Halmashauri.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Wana jamii wa Mvuleni na KiIolambwani walianza kuona umuhimu wa kuwa na barabara ya uhakika kuunganisha Mvuleni na Kitomanga tangu miaka kumi kabla. Kwa mara ya kwanza, mwaka 2005 walianza kujipanga wenyewe ili kusafisha eneo la barabara kutoka Mvuleni hadi Kitomanga. Kwa bahati mbaya, mwanakijiji mmoja alipata ajali iliyomfanya apoteze jicho jambo ambalo liliwakatisha tamaa kuendelea na usafishaji wa eneo la barabara. Ajali hii ilihusishwa na uchawi na kusababisha kusimama kabisa kwa zoezi za ufunguaji wa barabara. Mwaka 2010 Halmashauri iliamua kutumia Viongozi wa Kisiasa, yaani Mbunge wa jimbo la Mchinga na Diwani wa Kata ya Kilolambwani pamoja na Mhandisi na Afisa Maendeleo Jamii wa Halmashauri kuwaamsha na kuwapanga wanajamii wa Mvuleni na Kilolambwani kuanza tena ufunguzi wa barabara. Awamu hii ya utekelezaji ilihusisha shughuli mbalimbali zilizoelezwa hapa chini.

Uhamasishaji na Ujenzi wa Uelewa kupitia Vikao vya Kijiji; jamii ya Mvuleni na Kilolambwani walisitisha usafishaji wa eneo la barabara ili kuwa na barabara fupi kutokana na imani za kichawi kuwa ukataji wa miti ya porini ili kutengeneza barabara ingeleta balaa na tendo la kufuru ambalo lingepelekea majanga mengi kwa jamii. Sehemu kubwa ya jamii iliamini katika mtazamo huu. Pili, ushindani wa kisiasa katika vijiji ulileta upinzani katika uwepo wa jitihada za jamii kwani baadhi ya vyama vya siasa na wagombea wao walidai kuwa ujenzi wa barabara na utoaji wa huduma nyingine za umma ni shughuli mahsusi kwa serikali tu. Sehemu kubwa ya jamii pia ilikubaliana na mtazamo huu. Kuweza kujenga barabara, serikali ya kijiji, ikishirikiana na Mbunge wa Jimbo la Mchinga, Diwani wa Kata ya Kilolambwani na watumishi mbalimbali wa Halmashauri walitembelea kila Kitongoji na kukutana na wanaume kwa wanawake kuwashawishi kushiriki katika usafishaji wa eneo la barabara ambayo ni fupi kwenda Kitomanga. Serikali ya Kijiji pia iliendesha mikutano mingi ili kubadili fikra za wanajamii na kuelezea kwa kina faida za barabara ya Mvuleni – Kitomanga. Mwishoni mwa mwaka 2012 jamii ilikuwa imepata uelewa wa kutosha na utayari wa kushiriki katika shughuli zote za ujenzi wa barabara.

Kufanya maamuzi na kuingiza barabara ya Mvuleni – Kitomanga katika Mpango wa Kijiji; kupitia uwezeshi wa Diwani wa Kata ya Kilolambwani, vijiji hivi viwili viliibua vipaumbele, vikafanya tathmini na kuviwasilisha katika Kamati ya Maendeleo ya Kata (KMK). Kipaumbele kilichoongoza katika mapendekezo ni ujenzi wa barabara ya Mvuleni – Kitomanga. Mikutano ya Wanakijiji wote katika vijiji hivi viwili ilipitisha kipaumbele hiki na kushauri kiingizwe kwenye Mipango ya Kijiji. Kukazia uamuzi huu, vijiji hivi viliunda mpango kazi uliohusisha awamu za usafishaji wa eneo, uchimbaji na utengenezaji wa mifereji ya kutolea maji barabarani.

Usafishaji wa eneo la Barabara; usafishaji wa eneo la barabara huhusisha uondoaji wa miti ili ardhi itumike kwa malengo mbalimbali ikiwemo maendeleo, uundaji wa makazi na matumizi mazuri ya ardhi. Katika jitihada hii usafishaji wa eneo ulifanyika kwa lengo la kujenga barabara mpya. Kupitia mikutano ya vitongoji na vijiji, jamii iliamua kuwa wanaume wote katika vijiji vyote viwili washiriki katika zoezi la kusafisha eneo la barabara. Zoezi hili lilifanyika kwa kutumia vifaa vya kienyeji kama mundu, majembe, shoka na mapanga. Mapato ya Kijiji yalitumika kuwapatia wanaume chakula na vinywaji katika eneo la kazi na ni wanawake ambao walipewa jukumu la kupika na kusafirisha chakula na vinywaji kwenda kwenye eneo la kazi.

Kupelekwa kwa Mhandisi wa Wilaya kwenye eneo la ujenzi wa barabara; H/W ya Lindi ilipewa taarifa na Diwani wa kata ya Kilolambwani kuwa wanakijiji wameamua kuanza kusafisha eneo la barabara na kuchimba barabara ya 18km kutoka Mvuleni hadi Kitomanga. Baada ya kupata taarifa hii na kujiridhisha kuwa kazi inaendelea Halmashauri ilituma wahandisi na mafundi kwenda kwenye eneo. Jukumu la wataalam hawa lilikuwa kuwaongoza wanakijiji katika masuala ya kitaalam kama upimaji, uainishaji wa aina za udongo, utambuzi wa kokoto zinazotakiwa kwenye kusawazisha barabara, ujenzi wa madaraja na uchimbaji wa mifereji ya kutolea maji. Wanakijiji walihamasika sana kufanya kazi na wahandisi waliobobea kutoka makao makuu ya Halmashauri.

Halmashauri Kutenga Raslimali Fedha na Vifaa; licha ya kutuma wataalam kuwasaidia wanakijiji katika kufungua barabara, baadaye H/W ya Lindi ilitenga kwenye bajeti na kutoa fedha za kuboresha barabara kufikia kiwango cha Changarawe. Katika mwaka 2013/14 Baraza la Madiwani lilipitisha uboreshaji wa barabara ya Mvuleni – Kitomanga na kutenga fedha (zilizoonyeshwa chini) kwa ajili ya kukodi mitambo ya Ujenzi wa barabara ili kushindilia na kusawazisha barabara, kuboresha mifereji ya kutolea maji, kujenga madaraja na kuimarisha maeneo ambayo hutuwamisha maji kipindi cha mvua.

Uaandaaji wa Zabuni na Mkataba wa Ujenzi wa Barabara ya Mvuleni – Kitomanga; msaada wa kitaalam uliotolewa na mhandisi wa Halmashauri kwa jamii ya Mvuleni na Kilolambwani uliwezesha kuingizwa kwa barabara hii katika mpango wa Halmashuri wa mwaka 2013/2014. Ili kutekeleza mradi huu Halmashauri iliandaa zabuni na kuzitangaza kupitia vyombo vya habari. Wazabuni kadhaa waliwasilisha mapendekezo yao na uchambuzi ulifanyka ili kumpata mzabuni mmoja aliyetekeleza mradi huu. Maelezo ya utekelezaji wa mradi na shuguli halisi za ujenzi yalihusisha kushindilia na kusawazisha barabara, kuboresha mifereji ya kutolea maji, kujenga madaraja na kuimarisha maeneo yanayotuamisha maji kipindi cha mvua.



***Shughuli za ujenzi, Barabara ya Mvuleni – Kitomanga***

H/W Lindi kutenga fedha za matengenezo ya mara kwa mara kila mwaka; Halmashauri iliiweka barabara hii kwenye mipango yake ya marekebisho ya barabara na ilianza kuiingiza kwenye bajeti ya mfuko wa barabara tangu 2012/2013, 2013/2014 na 2014/2015. Maamuzi haya muhimu yalifanyika baada ya kutambua jitihada zilizofanywa na watu wa Vijiji vya Mvuleni na Kilolambwani

**5.0 RASLIMALI**

Shughuli za ujenzi wa barabara pamoja na barabara za vijijini kwa asili ni za gharama sana. Mwaka 2012 wanavijiji wa Mvuleni na Kilolambwani waliazimia kujenga barabara ambayo ilihusisha raslimali mbalimbali kwa namna ya michango ya jamii kupitia nguvukazi, ukodishaji wa mitambo na utoaji wa

chakula chenye thamani ya shilingi 5,000,000. Kwa upande mwingine mwaka 2013/14 Halmashauri ilichangia jumla ya shilingi 392,891,000 kutoka katika mfuko wa barabara kwa ajili ya kukodi mitambo, kushindilia na kusawazisha barabara, kuboresha mifereji ya kutolea maji, kujenga madaraja na kuimarisha maeneo yanayotuamisha maji kipindi cha mvua. Jumla ya raslimali kutoka kwa jamii na Halmashauri ziliwezesha kuwepo kwa barabara muhimu ya 18km kutoka Mvuleni hadi Kitomanga; moja ya miundombinu ya kudumu ambayo imechangamsha ukuaji wa uchumi, utoaji wa huduma na utawala.

**6.0 MATOKEO**

Tangu awali, jitihada za jamii zilikuwa suala la kawaida hapa Tanzania. Karibu makabila yote yalikuwa na mifumo ya jitihada za Jamii kama Msaragambo, Harambee, Umoja na Ujamaa. Jitihada za Jamii za vijiji vya Mvuleni na Kilolambwani katika kujenga barabara zimefanikiwa kupata matokeo yaliyoelezwa hapa chini.

Jamii za Mvuleni na Kilolambwani sasa zinajivunia kuwa na barabara yenye kiwango, uhakika na kupitika mwaka mzima ikiwaunganisha na barabara kuu ya Kitomanga na Manispaa ya Lindi ambapo shughuli nyingi za biashara (jumla na rejareja) zinafanyika. Uwepo wa barabara ya uhakika umewardhisha sana wanakijiji kwa sababu ya nafuu walioipata kupitia muda uliopungua waliokuwa wakitumia kusafiri kutoka vijiji hivi kwenda maeneo mengine ya Mkoa wa Lindi na ndani ya nchi.




***Barabara na Daraja, Mvuleni-Kitomanga***

Utekelezaji wa mradi huu kwa mfumo wa jitihada za jamii umeifanya jamii kuunganika zaidi na kuwezesha utekelezaji rahisi wa miradi mingine mingi katika sekta za maji na kilimo. Kutokana na programu kubwa za uhamasishaji na ujenzi wa uelewa zilizofanywa ili kufanikisha mradi huu, watu wa Mvuleni na Kilolambwani wamejenga mtazamo chanya kuhusu ushiriki katika miradi yao ya maendeleo, mahudhurio bora katika mikutano ya Vitongoji na Vijiji na utayari wa kuchangia fedha katika jitihada mbalimbali za vijiji kama ujenzi wa madarasa, maabara na ununuzi wa madawati kwa ajili shule za Vijiji na Kata.

Sababu moja kuu iliyosukuma ujenzi wa barabara ilikuwa kufika kwa urahisi kwenye huduma za rufaa za afya mbali na vijiji hivi viwili na katika huduma za juu za afya. Ujenzi wa barabara umeleta urahisi wa kufika katika huduma za rufaa za afya katika kituo cha afya cha Kitomanga. Hili limeimarishwa kwa kuwepo gari la wagonjwa ambalo linaweza kutumia barabara hii ya 18km kwa urahisi na uhakika kutoa huduma za kukimbiza wahitaji, hasa wanawake na watoto.




***Gari la Wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Kitomanga Kilichopo Barabara kuu ya DSM-Lindi***

Wakazi wa Mvuleni na Kilolambwani walizoea kuwa matatizo makubwa katika usafiri wa raia katika vijiji vyao na kati ya vijiji hivi na barabara kuu kwenda Lindi na Dar es Salaam. Hali hii kwa sasa imekuwa Historia kwani jamii zimeshuhudia usafiri wa raia ulioimarika. Afisa Mtendaji wa Mvuleni anasema *"……barabara hii unayoiona imefanya maajabu au tuseme miujiza, mabasi yanayopeleka watu Lindi na Kitomanga yameongezeka kwa idadi na ubora, tulizoea kuwa na basi moja tu ambalo lilikuwa baya na zee sana, …….sasa tuna mabasi zaidi ya manne yakipishana kupeleka watu kwenda Lindi……..vijana sasa wameajiriwa kwenye huduma za bodaboda, baadhi yao huwakimbiza watu kwenda Kituo cha afya cha Kitomanga, wengine hutoa huduma za usafiri ndani ya kijiji……..wengine husafiri hadi Lindi na bodaboda zao kununua na kuuaza bidhaa kutumia barabara hii tuliyojenga kwa mikono yetu wenyewe…..wanakijiji wanafurahia sana barabara na huduma ya usafiri, siyo tu katika afya, elimu na utawala bali pia katika kilimo na biashara……."*



***Wananchi wakitumia barabara iliyoboreshwa***

Ujenzi wa barabara ya Mvuleni – Kitomanga umeleta ongezeko la shughuli za kilimo na uvuvi kwa sababu ya usafiri ulio bora kutoka sehemu ya uzalishaji hadi sokoni. Ufuta ni moja ya mazao ambayo jamii imeongeza uzalishaji wake kwa ekari na uzalishaji kwa hekta.



***Shamba la Ufuta kandokando ya barabara ya Mvuleni-Kitomanga***

Mazao mengine ni mihogo, nazi na jamii za kunde. Shughuli katika uvunaji wa misitu, uvuvi, na biashara zimeongezeka kutokana na uhakika wa barabara na usafirishaji kwa kutumia malori, magari madogo ya kubebea mizigo (pickups) na pikiki za matairi matatu. Aina hizi mbalimbali za usafiri zinapatikana kwa urahisi na gharama zinazokubalika.

Maboresho katika huduma za afya, usafirishaji, uzalishaji katika kilimo na shughuli za biashara kutokana na ujenzi wa barabara yanaleta ongezeko katika kipato cha mtu binafsi na kaya. Kumekuwa na ongezeko la safari za Lindi na Dar es Salaam ishara kuwa kipato kimeimarika na wanachi wameridhika. Matokeo ya muda mrefu ya jitihada hii yanatarajiwa kuwa kuimarika kwa ustawi wa wakazi wa Mvuleni na Kilolambwani ikienda pamoja na ukuaji dhahiri wa uchumi, kupanuka kwa shughuli za biashara na maboresho katika utawala na utoaji huduma.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Baada ya kushuhudia mafanikio katika ujenzi wa barabara na faida zinatokana na jitihada za Jamii, jamii ya Mvuleni na Kilolambwani inafahamu kuwa kuna matukio yenye athari kadhaa yanayoweza kutokea endapo mikakati thabiti ya uendelevu haitabuniwa na kutekelezwa. Baadhi ya matukio haya ni kuharibika kwa barabara kutokana na mvua, magari makubwa kubeba mizigo zaidi na kutokuwepo kwa uratibu wa matengenezo ya mara kwa mara ya barabara. Kuhakikisha kuwa barabara inakuwa endelevu vijiji hivi na Halmashauri vimeweka mikakati iliyoelezwa hapa chini.

Kuanzishwa kwa kamati ya usimamizi wa barabara; kila kijiji kimeteua wajumbe kuunda kamati ya usimamizi wa barabara ambayo imepewa majukumu yanayojumuisha kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kubaini maeneo yanayohitaji matengezo ya haraka, kuandaa taarifa za robo mwaka kuhusu hali ya barabara na kuziwasilisha kwenye Halamshauri ya Kijiji na kuwasimamia wanakijiji wakati wa matengenezo ya barabara. Kamati hii pia huwafikia na kuratibu watumiaji mbalimbali wa barabara na wadau ili kuhakikisha ushiriki wao thabiti katika kutunza barabara. Katika suala hili wamiliki na watumiaji wote wa  magari makubwa hulazimishwa kuchangia kwa ajili ya matengenezo.

Kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara; Kata ya Kilolambwani ina vijiji na wakazi wengi wanaohitaji huduma endelevu kutoka Halmashauri. Barabara iliyoanzishwa na vijiji hivi viwili imewezesha na kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma. Kwa sababu hii Halmashauri imeipandisha daraja barabara hii kutoka barabara ya kijiji na kuwa barabara ya Halmashauri na tangu mwaka 2013/2014. Halmashauri hupanga na kutenga fedha kwenye bajeti kwa ajili barabara ya Mvuleni – Kilombwani. Hii husaidia matengenezo walau kila mwaka.

Mahusiano bora na endelevu na viongozi wa kisiasa; mwisho wa mkakati huu ni kuwafanya wanasiasa kuwatia moyo na kuwaunganisha wana vijiji mara kwa mara kukarabati barabara. Mbunge, Diwani na wenyeviti wote wa vijiji na vitongoji wameshauriwa kushirikiana kati yao na wanajamii kuhakikisha kuwa barabara ni ya uhakika kipindi cha kiangazi na masika.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Jitihada za Jamii  kwa kawaida hutokana na mahitaji ya jamii yenyewe. Ujenzi wa barabara ya Mvuleni – Kitomanga ulifanikiwa kwa sababu ulitokana na hitaji la jamii. Mahitaji ya jamii ni mabadiliko yanayoonekana ya lazima kwa sehemu kubwa ya jamii ili kurekebisha mapungufu wanayoyaona katika eneo lao. Katika hili, wakazi wa vijiji hivi viwili kiuhalisia walilitambua hitaji lao la barabara kwa ajili yakuzifikia huduma mbalimbali. Hali hii ilileta ridhaa na utayari wa kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa barabara. Siri nyingine zilizowezesha mafanikio ya jitihada hii ni pamoja na:

(i) Programu kubwa za uhamasishaji na ujenzi wa uelewa,

(ii) Utayari wa jamii kuchangia na kushiriki katika shuhuli za ujenzi wa barabara,
(iii) Uwepo wa mafundi wa kijijini waliowaongoza wanacnhi katika shughuli za ujenzi,
(iv) Juhudi na Utayari wa Halmashauri kutambua jitihada za Jamii, kuzitia moyo jamii na kutoa misaada ya fedha na utaalamu.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NACHINGWEA


**USHIRIKI NA JITIHADA ZA JAMII KATIKA UJENZI WA BOMA**



***UZOEFU WA H/W YA NACHINGWEA***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea ilianzishwa Desemba 31 mwaka 1983 kutokana na vifungu namba 8 na 9 vya Sheria ya Serikali za Mitaa na. 7 ya 1982 (Mamlaka za Wilaya). Ilianza rasmi shughuli zake Januari 1984. H/W ya Nachingwea inapatikana Kusini Mashariki mwa Tanzania Bara na mojawapo kati ya Halmashauri 6 za mkoa wa Lindi. Halmashaauri hii ipo kati ya Latitudo $10^0$ – $11^0$ Kusini na Longitudo $38^0$ – $39^0$ Mashariki. Mwinuko wa kuanzia 200m – 900m juu ya usawa wa bahari. Halmashauri hii inapakana na H/W za Ruangwa upande wa Kaskazini Mashariki, Masasi Kusini Mashariki, Tunduru Kusini Magharibi, na Liwale Kaskazini. Halmashauri ina Tarafa 5, Kata 34, Vijiji 127 na Vitongoji 527. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 Halmashauri ina wakazi 162,081.




***Ramani ya H/W ya Nachingwea ikionesha mipaka ya utawala***

H/W ya Nachingwea ina eneo la 7,070 km$^2$; kati ya hizo 5,337km$^2$ zinafaa kwa kilimo na 152.685 km$^2$ (29.7%) tu ndizo zinalimwa. Eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni 260ha; eneo linalomwagiliwa ni 60ha. Halmashauri in uoto wa savanna wenye aina mbalimbali za majani, miti na vichaka. Halmashauri hupata mvua za mwaka kati ya 800mm – 1000mm na ina msimu mmoja tu wa mvua ambazo hunyesha kati ya Novemba na Aprili. Kuna mito ya msimu ya Lionja, Lukuledi, Kihatu and Mbwemkuru ambayo hujaa maji wakati wa masika. Mvua huongezeka kulingana na mwinuko, hivyo ukanda wa chini huwa mkavu zaidi ikilinganishwa na ukanda wa juu. Joto la mchana huwa kati ya nyuzi joto $25^0$ C na $31^0$C na unyevu wa hewa huwa kati ya 71% na 86%.

**2.0 TATIZO**

Kabla ya mwaka 2008 H/W ya Nachingwea ilikuwa na hali mbaya ya utoaji wa huduma kutokana na kukosekana kwa jengo la ofisi na vifaa vya kisasa. Mkurugenzi Mtendaji alikuwa akitumia jengo la ofisi ambalo ni dogo sana na chakavu ambalo liliweza kuchua idara chache tu. Matokeo yake yalikuwa, msongamano wa idara na watumishi katika vyumba vichache, vilivyobanana na vichafu. Idara nyingine zote za kisekta zilitawanyika kila kona ya mji mdogo wa Nachingwea na kuwepo kwenye majengo ambayo hayakujengwa kwa ajili ya ofisi bali kwa makazi duni, na kufanya mawasiliano na ofisi ya Mkurugenzi

Mtendaji kuwa magumu. Pia utoaji wa huduma kwa wananchi ulikuwa mgumu kwani wananchi walilazimika kutembea umbali mrefu kutoka idara moja hadi nyingine kutimiza mahitaji yao. Hakukuwa na vyumba vya kutosha vya mikutano kwa ajili ya watumishi na Madiwani. Pia nafasi ya kuhifadhi nyaraka na vifaa vya ofisi ilikuwa ndogo sana na kusababisha uharibifu na upotevu wa taarifa nyingi za siri na nyaraka za serikali.



*Ofisi ya zamani ya Mkurugenzi*



*ofisi ya zamani ya Mkuu wa Wilaya*

Hali hii ilikuwa hivyo hivyo na kwa Mkuu wa Wilaya. Mkuu wa Wilaya na watumishi wote walitumia jengo la ofisi ambalo kabla lilikuwa ghala la Korosho. Jengo hili lilikuwa na hali mbaya ya mwanga, nafasi ndogo, kutokuwepo kwa vyumba vya mikutano, na lilikuwa ni kero kwa wananchi na watumishi. Mazingira ya jengo hili yalikuwa ni ya vumbi msimu wa kiangazi, matope msimu wa masika na machafu mwaka mzima. Utoaji wa huduma ulikuwa duni kutokana na watumishi kukosa motisha kutokana na kusongamana katika ghala la korosho. Pia ofisi ya Mkuu wa Wilaya ilijitenga na ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji na kuleta changamoto kwa wananchi wenye uhitaji wa huduma za serikali.

Majengo yote mawili ya ofisi hayakuakisi sura ya Halmashauri kwa hadhi ya Serikali ya Tanzania, utajiri wa jamii ya Nachingwea na umri wa Halmashauri ambayo ilianzishwa tangu mwaka 1993 na kuanza kutoa huduma mwaka 1984.

**3.0 LENGO**

Katika menejimenti ya kisasa, ubora, mahali majengo ya ofisi yalipo na nafasi ya kutosha ni muhimu kwa heshima, motisha kwa watumishi, uwepo wa watumishi, wepesi katika utoaji wa huduma na usalama wa watumishi, kazi na nyaraka. Lengo kuu la jitihada ya Nachingwea lilikuwa kuboresha na kutoa huduma za kisasa kwa wananchi. Mahsusi kabisa Halmashauri kwa kushirikiana na ofisi ya Mkuu wa Wilaya ililenga;

(i) Kuimarisha mahusiano ya kikazi kati ya Serikali Kuu (ofisi ya Mkuu wa Wilaya) na Serikali za Mitaa (ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji),
(ii) Kuwa na ofisi za kisasa, zenye ubora na nafasi ya kutosha kwa ajili ya watumishi wa serikali, vifaa na nyaraka,
(iii) Kuboresha mazingira ya kazi ya watumishi wa serikali kwa kuwa na ofisi zilizopangwa vizuri, zenye hewa na mwanga wa kutosha na zenye samani bora,
(iv) Kuchochea ushiriki wa jamii kwenye utekelezaji wa miradi kwa kuwachangamsha watu wa Nachingwea ili kujenga mtazamo kuwa maendeleo katika Halmashauri ni jukumu la wadau wote na siyo serikali peke yake,

(v) Kupunguza gharama za ulinzi uliotokana na kutawanyika na uchakavu wa ofisi. Ukweli kuwa boma jipya lingeunganisha ofisi ya Mkurugenzi na ofisi ya Mkuu wa Wilaya ungeunganisha gharama za ulinzi, maji na nishati, na hatimaye kupungua kwa gharama za uendeshaji.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Ushiriki wa jamii katika utekelezaji wa miradi hapa Tanzania ulikuwa ni jukumu la kila mwanajamii. Viongozi mara baada ya Uhuru waliamuru mikoa, Halmashauri, vijiji na jamii kuhakikisha kila mwanajamii anashiriki katika mchakato wa maendeleo. Watu kupitia vijiji na mitaa walishiriki kwa pamoja katika kuzalisha na kumiliki mifumo mikuu ya uzalishaji. Baada ya mabadiliko katikati ya miaka 1980 na 1990, ari ya ushiriki wa jamii na uchangiaji iliporomoka. Ushiriki wa jamii huzifanya jamii kuwa na hamu ya umiliki wa miradi iliyopo katika jamii suala ambalo huleta uendelevu. Ushiriki wa jamii katika ujenzi wa Boma Nachingwea ni mojawapo ya mifano ambapo jamii ilitoa raslimali zake kujenga ofisi ya Mkuu wa Wilaya na ya Mkurugenzi wa Halmashauri.

Kwa miaka mingi H/W ya Nachingwea ilikuwa na mipango ya kujenga jengo lake la kisasa na bora. Badaye mpango huu uliwasilishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani kwa ajili ya kupitishwa ambapo Mkuu wa Wilaya (Marehemu Leonidas Gama) alikuwa mwalikwa. Wakati wa Mkutano Bwana Gama alifurahishwa na mpango huo na akauboresha kwa kuanzisha wazo la kuwa ofisi mbili ndani ya jengo moja. Baada ya majadiliano ya muda mrefu ilikubalika ujenzi wa boma ujumuishe ofsi zote mbili za serikali, yaani ofisi ya Mkuu wa Wilaya na ofisi ya Halmashauri.

Julai 23, 2001 Halmashauri iliendesha mkutano ulioshirikisha wakuu wa idara, wakuu wa mashirika ya umma, viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa taasisi za dini na wadau wengine. Ilikubalika kuwa ujenzi wa boma uanze kwa kutumia jitihada na michango ya wadau na jamii. Mkuu wa Wilaya bwana Leonidas Gama na mwenyekiti wa Halmashauri bwana John Malibiche walipewa jukumu kuongoza mapambano ya kuzihamasisha jamii ili kufikia kuwa na Boma la Wilaya ya Nachingwea. Baada ya jitihada za dhati za kukusanya raslimali kutoka kwa jamii, shughuli za ujenzi zilianza rasmi Novemba 2002. Shughuli za ujenzi na kukamilisha Boma zimeelezwa kwa kina hapa chini.

Kuunda Kamati ya Utekelezaji; ilikuwa muhimu kugawa majukumu kwa makundi mbalimbali kwa mfumo wa kamati. Iliundwa kamati kuu ambayo ililkuwa na wajumbe 20 na kamati ndogo 4, yaani kamati ya fedha na mipango, kamati ya ujenzi, kamati ya uhamasishaji na kamati ya uratibu. Kamati hizi zilikuwa na wajumbe kutoka makundi mbalimbali ya jamii ikiwa ni pamoja na wazee 9 katika kila kamati. Kamati zote zilitakiwa kujihusisha na shughuli za uhamasishaji ili kupata fedha zaidi na kukusanya vifaa vya ujenzi kutoka ngazi zote za jamii ya Nachingwea. Kwa ajili ya uwajibikaji, ilikubalika kuwa viongozi wote wa Halmashauri waachane na usimamizi wa moja kwa moja wa masuala ya fedha na wajikite katika ufuatiliaji.

Kuendesha Mikutano ya Uhamasishaji katika ngazi zote; timu ya uhamasishaji ilitembelea jamii zote katika Halmashauri ili kujenga uelewa kuhusu sababu na faida za kushiriki kikamilifu kwenye mradi. Kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya kata na vijiji vyote vilifikiwa na timu hii na kupatiwa taarifa za kina kuhusu maboresho katika utoaji wa huduma kama boma litajengwa kwa viwango na kuakisi hadhi ya ofisi za juu kabisa katika Halmashauri. Kushawishi wananchi kuelewa umuhimu wa kujenga ofisi ulileta mafanikio katika michango ya fedha taslimu na vifaa kutoka kwa jamii na wadau wengine.

Ukusanyaji wa Michango; kila Kata na Kijiji kilipangiwa kukusanya kiasi kadhaa cha vifaa vya ujenzi kama mchanga, mawe, mbao, kokoto, vyakula kwa ajili ya wajenzi, matofali ya kuchoma na mirunda kulingana na upatikanaji katika eneo husika. Ukusanyaji wa michango hii mbalimbali ulifanywa na Maafisa watendaji wa Kata na Vijiji. Maofisa hawa waliandaa rejesta ya wananchi wote wenye uwezo na kukusanya michango

yao yote kwa awamu hadi ahadi zote zilipokamilika. Makusanyo yote yaliwasilishwa kwa Kamati ya Fedha na Mipango ambayo ilikuwa na wajibu wa kugawa fedha kwenye shughuli mbalimbali za ujenzi wa Boma.

Utoaji taarifa wa michango ya jamii na matumizi yake; ilikubalika kuwa kwa sababu mradi ulikuwa wa jamii katika ngazi zote za Halmashauri, mapato na matumizi yote yatolewe taarifa kwa jamii kupitia Madiwani wao katika kila robo mwaka ili kuhakikisha kuwepo kwa uwazi na kuongeza mwitikio. Mkakati huu ulichochea uhakika katika makusanyo ya fedha taslimu na vifaa vya ujenzi kwani jamii zilijivunia jitihada zao hivyo kuongeza ari ya kushirikiana na kamati na timu za ujenzi kuelekea ukamilishaji thabiti wa mradi.

Ujenzi na ugawaji wa ofisi; tangu hatua ya michoro ilikubalika dhahiri kuwa ujenzi wa Boma utatekelezwa na mhandisi wa Halmashauri. Katika Baraza, iliamuliwa pia kuwa chini ziwepo ofisi mbalimbali za Halmashuri na juu ghorofani iwepo ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Ugawaji na utaratibu huu wa ofisi ulikuwa na sababu zake kutokana na ukweli kuwa ofisi za Halmashauri huwa na wateja wengi zaidi kwa maana ya watumishi na wananchi. Kupunguza usumbufu kwa wasaka huduma ilikubalika vyumba vya chini viwe ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji.

## 5.0 RASLIMALI

Ujenzi wa majengo ya serikali kimsingi hufanywa na Serikali kupitia bajeti za maendeleo za mwaka. Uamuzi wa Baraza la Madiwani kujenga jengo la Halmashauri ni wa kipekee na wa gharama kwa jamii. Ujenzi wa boma ulihusisha aina mbili za michango; vifaa vya ujenzi kutoka kata na vijiji na michango ya fedha taslimu kutoka kwa wadau mbalimbali.

(a) Michango ya Vifaa vya Ujenzi toka Vijijini; vijiji vyote vilifikiwa na kuombwa kuchangia vifaa vya ujenzi kulingana na raslimali zilizopo katika Vijiji au Kata husika. Jedwali hapa chini linaonesha michango kutoka vijiji mbalimbali.

**Jedwali 1: Michango ya Vifaa toka Vijiji na Kata**

| Na | Aina | Idadi ya vijiji | Idadi ya vifaa | Thamani | Jumla (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mbao | 67 | 9200 | 7,000 | 64,400,000 |
| 2 | Matofali | 9 | 550000 | 50 | 27,500,000 |
| 3 | Kokoto | 14 | 185 lori | 20,000 | 5,550,000 |
| 4 | Mawe | 6 | 75 lori | 20,000 | 1,500,000 |
| 5 | Mchanga | 1 | 1900 | 15,000 | 28,500,000 |
| 6 | Vifusi | 1 | 160 | 15,000 | 2,400,000 |
| 7 | Mirunda | 3 | 10000 | 400 | 4,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | | | | **133,850,000** |

(b) Michango ya Fedha taslimu; michango ya fedha ilikuwa lazima katika mradi huu na iliandaliwa kwa namna ambayo kila mtu mwenye sifa achangie kulingana na kipato chake. Watumishi wa serikali walichangia shilingi 6,000 kwa mwaka na wakulima walichangia shilingi 2,000 kwa mwaka. Wafanyabiashara walichangia kulingana na thamani na ukubwa wa biashara zao. Michango hii ya kila kundi imeoneshwa kwenye jedwali 2 chini.

**Jedwali 2: Michango ya fedha toka wadau mbalimbali**

| No | Wadau | Kiasi | % |
|---|---|---|---|
| 1 | Wakulima kupitia mazao ya biashara | 469,957,080 | 89 |
| 2 | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | 340,000,000 | 4 |
| 3 | Wananchi | 9,352,250 | 2 |
| 4 | Watumishi | 8,329,250 | 2 |
| 5 | Mauzo ya Nguo zilizotumika | 6,928,500 | 1 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6 | wafanyabiashara | 9,737,800 | 2 |
| | **Jumla ndogo** | **844,305,880** | **100** |

(c) Usafirishaji wa vifaa vya ujenzi; lori la Halmashauri lilitumika kusafirisha vifaa toka vijijini.
(d) Michango ya Serikali Kuu; serikali kuu ilichangia kukamilisha ujenzi kama ilivyoainishwa hapa chini.

- Mwaka 2007/2008 TZS 100,000,000 zilitengwa na Katibu Tawala wa Mkoa.
- Mwka 2008/2009 ongezeko la TZS 200,000,000 lilitengwa kwa ajili ya kufunga umeme, mifumo ya maji na kufunga milango na madirisha.
- Mwaka 2009/2010 Wizara ya Fedha ilitoa TZS 200,000,000 kwa ajili ya kujenga uzio na ikawa ndio mwisho wa ujenzi wa Boma.

**6.0 MATOKEO**

Jamii ya Nachingwea na Utawala ilifanya kazi ngumu kwa miaka mingi kukamilisha ujenzi wa jengo la kisasa na bora kwa ajili ya ofisi ya Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya. Kukamilika kwa mradi huu mgumu kunajidhihirisha kwa faida mbalimbali zilizoelezwa hapa chini.

Ofisi za Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri zipo katika jengo jipya. Sehemu ya juu imechukua ofisi za Mkuu wa Wilaya, idara na watumishi wake wakati sehemu ya chini imepangwa vizuri kwa ajili ya utoaji huduma na imechukua ofisi ya Mkugenzi Mtendaji na na watumishi wengi wa Halmashauri. Idara zote na vitengo ukiondoa Afya, Maji, na Ujenzi zipo kwenye jengo jipya lenye samani nzuri. Ofisi ilifunguliwa rasmi na Dr. Jakaya Mrisho Kikwete; Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Desemba 2 mwaka 2012. Wakati wa uzinduzi rasmi wa Boma, watumishi wa serikali walivaa fulana zenye maneno "''HONGERA WANANCHI WA NACHINGWEA KWA UJENZI WA BOMA''.



***Boma la Wilaya ya Nachingwea lililojengwa kwa Michango ya Wadau***

Kuboreshwa kwa utoaji wa huduma; jamii, wadau mbalimbali na watu binafsi sasa wanafurahia huduma zilizoboreshwa na urahisi wa kufika kwenye ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya. Afisa Mtendaji mmoja wa Kata alikuwa na maneno haya ya kusema *"…… kabla ya kukamilisha jengo hili tulikuwa tunazunguka sana ….na ilikuwa mbaya zaidi kama ulikuwa na masuala yanayohusu ofisi ya Mkurugenzi, idara za kisekta, na ofisi ya Mkuu wa Wilaya, ungehitaji siku tatu kukamilisha suala ambalo*

*leo linachukua saa moja au mawili na linahusisha ofisi zote…..tunafurahia kupata huduma za haraka, kwenye ofisi zenye ubora na nafasi za kutosha za kusubiria maamuzi ya kiofisi…..".*

Mazingira ya kazi yaliyoboreshwa; watumishi wote wa Halmashauri na ofisi ya Mkuu wa Wilaya sasa wanafanya kazi katika ofisi ambazo zina mwanga na hewa, samani na nafasi ambavyo vimerahisisha kazi na utoaji wa huduma. Ukaribu kati ya ofisi za Halmashauri na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya umeleta mahusiano bora kati ya makundi mawili ya watumishi wa Serikali. Matokeo ya hili ni ongezeko la motisha, uwepo kazini na kuridhika kwa watumishi ambavyo kwa pamoja vimeleta utoaji huduma ulioboreshwa kwa wadau mbalimbali na wananchi.




***Baadhi ya ofisi Sehemu ya Chini ya Boma***

Kuimarika kwa ushiriki wa jamii; ari ya ushiriki wa jamii iliimarika kupitia jitihada ya ujenzi wa boma. Ukusanyaji thabiti wa raslimali kutoka vijijini, taasisi mbalimbali na jamii nzima ya Nachingwea viliamsha mfungamano wa asili ndani ya jamii kushiriki katika miradi ya maendeleo. Programu za uhamasishaji jamii pamoja na ujenzi wa uelewa zilizoleta mafanikio katika jitihada hii zimebadili watu wa Nachingwea na kuwafanya kuwa waitikiaji wa mahitaji ya maendeleo na kuyakabili kama jamii kwa ari ya juu katika kuchangia ili kutatua matatizo katika Vijiji na Kata. Ujenzi na kukamilika kwa Boma viliongeza ari ya michango ya jamii. Kwa mfano, siku za karibuni jamii za Nachingwea zimefanya jitihada mbalimbali kuifanya Nachingwea iwe mahali bora pa kuishi kwa kutekeleza miradi mbalimbali kama ujenzi wa maabara wenye thamani ya shillingi 130,000,000 katika shule ya sekondari ya wasichana ya Nachingwea na ujenzi wa madarasa katika shule ya sekondari ya wasichana ya Nachingwea uliofanywa na kampuni ya Ngwena ambapo jamii ilichangia shilingi 36,000,000 na Halmashauri ilichangia shilingi 4,000,000 tu. Mradi mwingine wa siku za karibuni wa jitihada za jamii ulikuwa ujenzi wa ofisi ya Kata ya Nangowe kwa jitihada za jamii na Halmashauri. Wakati wa ujenzi wa ofisi hii, jamii ilijenga ukuta mpaka kwenye lenta na Halmashauri ikaunga mkono kwa kukamilisha shughuli za kumalizia zenye thamani ya shilingi 16,000,000.




*Maabara za Fizikia, Kemia na Baiolojia katika sekondari ya Wasichana ya Nachingwea*



*Darasa katika Sekondari ya Nachingwea*



*Ofisi ya Kata ya Nangowe*

## 8.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Moja ya matokeo makuu ya ujenzi wa Boma ni hali ya umiliki iliyojengeka katika jamii ya Nachingwea. Kupata huduma katika Boma imeleta hali ya umiliki na ushuhuda kuwa nguvu zao katika machakato wa ujenzi wa Boma umefanya Halmashauri kuwa na ofisi nzuri kwa ajili ya watumishi wao wanaofanya kazi makao makuu ya Halmashauri. Hii imedumisha ari ya kuendelea kushiriki katika miradi mingine kutokana na ukweli kuwa kama waliweza kujenga jengo kubwa kiasi hiki wanaweza pia kutekeleza miradi mingine katika maeneo yao.

Halmashauri imeweka mikakati ya kutumia uongozi wa kisiasa kuendeleza uelewa wa jamii kuhusu thamani ya jitihada za Jamii katika sekta zote kama elimu, maji, afya na kilimo. Halmashauri pia imedhamiria kutumia kwa kina mfumo wa fursa na vikwazo kwa maendeleo (O&OD) ili kuainisha vipaumbele vya jamii, kupanga na kutumia jitihada za jamii kutekeleza miradi badala ya kusubiri Serikali katika hatua zote za utekelezaji wa miradi.

## 9.0 SIRI ZA MAFANIKIO

Ushiriki wa jamii mara nyingi hukwamishwa na ukosefu wa uelewa, mawasiliano duni na upashanaji habari mbovu, mgawanyo mbovu wa nafasi na majukumu, ukosefu wa stadi za menejimenti katika ngazi mbalimbali na ukosefu wa raslimali fedha kwa ajili ya uratibu wa shughuli. Changamoto kama hizi kwa hakika ziliukabili uongozi wa H/W ya Nachingwea katika kuhakikisha ujenzi unafanikiwa na kwa kutumia ushiriki wa jamii na wadau. Mafanikio yalipatikana kwa sababu ya siri zilizotajwa hapa chini.

(i) Ujenzi thabiti wa uelewa kwa jamii ya Nachingwea kuhusu sababu za kuchangia na kushiriki katika utekelezaji wa Mradi wa Boma.

(ii) Kufanya kazi kama Timu kati ya Viongozi wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya, Mwenyekiti wa Halmashauri, na Mkurugenzi Mtendaji ambao walitoa nguvu zao kwa ajili ya maendeleo ya Wilaya ya Nachingwea.

(iii) Ujenzi wa Boma lilikuwa hitaji halisi la jamii ya Nachingwea.

(iv) Ushikishwaji thabiti wa jamii katika utekelezaji wa mradi (kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kufanya tathmini) kulijenga hali ya umiliki na ndio chanzo cha mafanikio.

(v) Uwazi katika mapato na matumizi wakati wa utekelezaji wa mradi vilijenga uaminifu na utayari wa kuchangia.

(vi) Uwepo wa zao la korosho ulitengeneza fursa kwani michango ya wakulima ilikatwa moja kwa moja wakati wa mauzo ya zao la korosho (stakabadhi ya mazao ghalani).

# HALMASHAURI YA WILAY YA MASASI


JITIHADA ZA JAMII KATIKA UJENZI WA ZAHANATI YA MAPILI



*UZOEFU WA KIJIJI CHA MAPILI*

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ni moja kati ya Halmashauri 9 za Mkoa wa Mtwara ambayo ina fursa kubwa ya maendeleo na kushamiri kiuchumi. Halmashauri ina hali nzuri ya hewa na ardhi inayofaa kwa kilimo na uwekezaji mwingine wa kiuchumi. H/W ya Masasi hupakana na H/W za Nachingwea kwa upande wa Kaskazini, Lindi na Newala kwa upande wa Mashariki, Nanyumbu upande wa Magharibi na Jamhuri ya Msumbiji upande wa Kusini. Halmashauri hii inapatikana kati ya Latitudo $10^0$ na $12^0$ Kusini na Longitudo $36^0$ na $38^0$ Mashariki ipo umbali wa 214km kutoka makao makuu ya mkoa ya Mtwara. Halmashauri ina jumla ya eneo 3,829$km^2$ sawa na 20.8% ya eneo lote la Mkoa wa Mtwara (16,720$km^2$).




***Ramani ya H/W ya Masasi***

Kisiasa na kiutawala, H/W ya Masasi ina Majimbo mawili ya uchaguzi ambayo ni Lulindi na Ndanda pamoja na Tarafa 5 za Lisekese, Mchauru, Mkundi, Chiungutwa and Lulindi. Halmashauri ina Kata 34, Vijiji 166 na Vitongoji 889. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 Halmashauri ina wakazi 260,854, kati yao 125,151 ni wanaume na 135,703 ni wanawake. Ukuaji wa wastani wa idadi ya watu ni 2.7% kwa mwaka. Shughuli za asili za kiuchumi zinaongozwa na uzalishaji wa Korosho kama zao kuu la biashara ambalo huchangia 80% mapato ya ndani ya Halmashauri, ilihali mazao mengine ni mahindi, njegere na ufuta ambayo huchangia 20% ya mapato.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), huduma za afya hujumuisha huduma zote zinazohusu upimaji na utoaji wa tiba kwa maradhi, au kuimarisha, kuboresha na kurejesha afya ya umma katika eneo au jamii husika. Hujumuisha huduma za afya kwa mtu binafsi au kwa wote. Huduma za afya ndizo shughuli zilizo dhahiri zaidi za mfumo wa afya kwa watumiaji na umma kwa ujumla. Utoaji wa huduma huwa na maana ya namna raslimali kama fedha, watumishi, vifaa na madawa zinavyounganishwa kuruhusu utoaji wa huduma za afya. Kuboresha upatikanaji, wigo na ubora wa huduma hutegemea uwepo wa raslimali muhimu, jinsi huduma zilivyopangwa na kuendeshwa, na vivutio vya kuhamasisha watoa huduma na watumiaji. Hali halisi ya taasisi za afya katika H/W ya Masasi imeoneshwa kwenye jedwali hapa chini.

**Jedwali 1: Taasisi za Afya H/W Masasi 2016**

| Taasisi | Binafsi | Serikali | Jumla |
|---|---|---|---|
| Hospitali | 1 | 0 | 1 |
| Vituo vya afya | 1 | 2 | 3 |
| Zahanati | 10 | 30 | 40 |
| Jumla | 12 | 32 | 44 |

## 2.0 TATIZO

Upungufu wa taasisi za afya ni suala la kawaida katika nchi zinazoendelea na maeneo yanayoathirika sana ni watu wa vijijini katika nchi za Afrika Kusini mwa Sahara. Pamoja na kuwa na upungufu mwingi katika taasisi za afya, watumishi na miundombinu, mfumo wa huduma za afya wa Tanzania una sifa nyingi muhimu. Zaidi ya 70% ya taasisi za afya za Tanzania hutoa huduma nyingi za msingi za afya ikiwa ni pamoja na huduma ya mtoto, uzazi wa mpango na tiba kwa maradhi ya kuambukiza. Kutokana na hali hii, H/W ya Masasi pia ina zaidi ya 60% ya taasisi za afya zinazotakiwa kutoa huduma za kinga na tiba. Hata hivyo, kwa kuangalia wigo, H/W imekuwa ikikabiliwa na upungufu wa taasisi za afya; kati ya vijiji 166, 126 havina zahanati. Upungufu wa taasisi za afya umechangia ongezeko la vifo vya mama na mtoto.

**Jedwali 2: Hali ya Taasisi za Afya H/W Masasi**

| Taasisi | Binafsi | Serikali | Jumla | Mahitaji | Upungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| Hospitali | 1 | 0 | 1 | 2 | 1 |
| Vituo vya afya | 1 | 2 | 3 | 34 | 31 |
| Zahanati | 10 | 30 | 40 | 166 | 126 |
| Jumla | 12 | 32 | 44 | 202 | 158 |

Kijiji cha Mapili ni mojawapo ya vijiji 126 vya H/W ya Masasi ambavyo havijawahi kuwa na zahanati tangu kuanzishwa kwa Halmashauri mwaka 1978. Wanakijiji walilazimika kutembea 25km kupata huduma za msingi za afya katika Hospitali ya Wilaya ya Newala. Wale ambao hawakuweza kusafiri kwenda hospitali ya Wilaya ya Newala walilazimika kutegemea huduma za dawa za asili. Mwaka 2010 wanawake wajawazito wawili walikufa wakiwa njiani kuelekea Hospitali ya Newala kupata huduma za afya. Usafiri kati ya Mji wa Newala na Kijiji cha Mapili ni mgumu kwani kijiji kipo chini kwenye tambarare na kuna mlima mkali kuelekea mji wa Newala ambao ni eneo la Halmashauri nyingine kwani kijiji cha Mapili kipo H/W ya Masasi. Kijiji hiki hukumbwa sana na magonjwa ya malaria, kuhara na vikohozi kipindi cha mvua kutokana na hali ya hewa ya unyevunyevu, joto la juu na ukosefu wa maji safi na salama. Vyanzo vikuu vya maji kwa kijiji hiki ni matawi ya Mto Ruvuma.

Jitihada za kutafuta maji na kipato katika bonde la Mto Ruvuma huleta matukio mengi ya kuvamiwa na mamba ambayo huhitaji huduma za haraka za afya. Ni muhimu kutambua kuwa aina ya Mamba wa Nile wametawanyika napengine hupatikana katika mifumo yote ya mabonde yenye maji, bonde la Ruvuma likiwa mojawapo. Mito mingi, hasa kusini na magharibi mwa Tanzania ni ya msimu na hukauka hadi kubaki na mabwawa madogo kati ya Agosti na Januari. Mamba na viboko waishio katika mito hii hulazimika kujikusanya katika madimbwi haya. Pia, watu wa vijijini hulazimika kutumia madimbwi haya kuwapatia wanyama maji, kuoga, kufua na kuteka maji ya kunywa na kupikia. Hili huleta mafarakano kati ya Mamba na watu. Takwimu zinaonyesha kuwa Mkoa wa Mtwara ulikuwa wa tatu baada ya Ruvuma na Mwanza (1997) kuhusiana na uvamizi wa mamba na vifo. H/W ya Masasi na Kijiji cha Mapili zimo kwenye ukweli huu kwani idadi kubwa ya watu wanaishi ndani ya bonde la mto Ruvuma.

Changamoto hizi ziliwafanya watu wa Kijiji cha Mapili kutafakari, kujadili, kuweka kipaumbele na kufanya uamuzi madhubuti wa kujenga zahanati katika kijiji chao ili kuatatua changamoto za huduma za afya.

## 3.0 LENGO

Kupatikana kwa huduma za afya ni muhimu sana kwa wakazi wa vijijini. Kinadharia, wakazi wanatakiwa kuwa na uwezo wa kutumia kwa urahisi na uhakika huduma kama afya ya msingi, afya ya tiba, dharura na afya ya umma. Kupatikana kwa huduma za afya ni muhimu kwa afya ya jumla ya mwili, jamii na afya ya akili, kuzuia magonjwa, kupima na kutibu, ubora wa maisha, vifo vinavyozuilika na matarajio ya kuishi.

Lengo kuu la jitihada ya kijiji cha Mapili lilikuwa kujenga Kituo cha Huduma za faya ili kuboresha upatikanaji wa huduma za afya. Mahsusi kabisa, jitihada hii ililenga yafuatayo;

(i) Kupunguza umbali na muda uliotumika kufuata huduma za afya katika Hospitali ya Wilaya ya Newala
(ii) Kujiwekea uhakika wa upatikanaji wa haraka wa huduma za afya kwa wanakijiji wote wa Mapili
(iii) Kupunguza vifo vya mama na mtoto
(iv) Kuimarisha upatikanaji wa chanjo kwa wajawazito na watoto chini ya miaka 5

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Jitihada ya kujenga zahanati ya Kijiji ilianza kwa wananchi wenyewe. Wazee walikumbuka shughuli za kujitegemea za miaka 1960 na 1970 ambapo jamii ziligundua mahitaji yao, walijipanga katika vijiji vya ujamaa, walifanya majadiliano mazito, walitafuta majibu na walitekeleza miradi kufikia mahitaji yao. Haya yalifanyika bila usaidizi mkubwa kutoka serikalini. Kwa kufuata mfumo wa Kujitegemea wanakijiji wa Mapili walitumia mikakati mtambuka kufikia lengo la kujenga zahanati ya kijiji. Mikakati hii imeelezwa hapa chini.

Kutoa taarifa ya tatizo kwa Mkuu wa Wilaya; baada ya mikutano ya majadiliano na kupitisha maamuzi katika ngazi ya kijiji, serikali ya kijiji na diwani walimkabili Mkuu wa Wilaya Mh. Said Amanzi na kumweleza mpango wao wa kujenga zahanati. Mkuu wa Wilaya alikubali kutembelea kijiji na kukutana na wanakijiji wote ili kujiridhisha na umoja wa makundi mbalimbali ya kijamii kijijini katika kutekeleza jitihada hii. Katika Mkutano huu umoja ulithibitishwa na kila mwananchi mwenye sifa alikubali kuanzishwa kwa mradi wa zahanati kwa kuchangia sh 2,000 kwa kila mmoja mweye umri wa miaka 18 na kuendelea. Kiasi cha mchango kiliongezwa baadae na kufikia sh 5,000 kwa kichwa kwa msimu wa korosho. Kwenye mkutano wa Mkuu wa Wilaya, ramani ya jengo ilizinduliwa. Ramani ilionesha muundo wa kituo cha afya na si zahanati.

Kuunda Kamati ya Ujenzi; wanakijiji waligundua kuwa Serikali ya Kijiji ina majukumu mengi ya kila siku. Kukasimu shughuli za ujenzi kwa Serikali ya Kijiji ingeleta ucheleweshaji na tabia za urasimu. Mkutano wa kijiji uliamua kuunda kamati yenye wanakijiji 10 waliochaguliwa kati ya wanakijiji na kwa kila Kitongoji, wanawake pia waliwakilishwa. Kamati ilipewa wajibu wa kukusanya fedha taslimu na vifaa vya ujenzi, kuandaa na kufuatilia ratiba za kazi za vitongoji, usimamizi wa fedha na ufuatiliaji wa shughuli za ujenzi. Kamati ilitakiwa kutoa taarifa ya utendaji wake kwa Serikali ya Kijiji kwa kila wiki na kuwasilisha taarifa za ujenzi kila robo mwaka katika Mkutano wa Kijiji.

Maandalizi na kupitishwa kwa makadirio sanifu ya gharama za ujenzi (BOQ); Halmashauri kupitia idara ya ujenzi iliandaa na kukipatia kijiji andiko la gharama za ujenzi ili kuwezesha maamuzi kuhusu gharama halisi za vifaa, nguvukazi, muda na ufuatiliaji. Andiko hili lilipitishwa na Mkutano wa Kijiji na kukubalika kama mwongozo rasmi kwa ajili ya zabuni, manunuzi ya vifaa vya viwandani na uchangiaji wa nguvukazi za wanakijiji. Kwa kutumia andiko hili, wanakijiji waliweza kulinganisha gharama za kutekeleza mradi kati ya kutumia mkandarasi au mafundi wa kijijini ambapo namna ya pili ilionekana kuwa rahisi. Hivyo ujenzi wa zahanati ya Mapili ulifanywa na mafundi wa kijijini wakisaidiwa na nguvukazi ya wanakijiji waliojipanga kwa makundi ya Vitongoji.

Manunuzi ya Vifaa vya Ujenzi vya Viwandani; fedha zilizochangwa na wanakijiji zilitumiaka kununua vifaa na mitambo ya viwandani. Wanakijiji walishiriki katika kusafisha eneo, kutengeneza matofali, kuchimba msingi, kukusanya mawe na mchanga na kujenga kuta chini ya usimamizi wa mafundi. Hii ilisaidia kutumia gharama ndogo katika kukusanya vifaa vilivyopo kama maliasili, kusafisha eneo na kujenga kuta.

Ujenzi halisi wa Zahanati ya Mapili; mchakato wa ujenzi ulianza tarehe 23 Februari 2009. Mgawanyo asilia wa kijinsia ulielekeza ushiriki wa wanaume na wanawake katika ujenzi. Wakati wanaume walijihusisha moja kwa moja na kusafisha eneo, kuchimba msingi na kunyanyua kuta kulingana na ratiba za Vitongoji, wanawake walikuwa na wajibu wa kuteka maji na kupika chakula kwa ajili ya mafundi kwa mujibu wa ratiba za Vitongoji.



***Wanakijiji wa Mapili wakishiriki shughuli za Ujenzi***

Kutafuta fedha zaidi ili kukamilisha Ujenzi; kwa kuzingatia hali za kiuchumi za kaya, utegemezi katika uzalishaji wa msimu wa korosho na hitaji la kukamilisha mradi wa zahanati, wanakijiji kupitia Serikali ya Kijiji na Diwani waliomba msaada kutoka Halmashauri na wadau wengine. Ombi hili liliwasilishwa kwenye Halmashauri na kwa Waziri wa zamani wa Maliasili na Utalii. Undani wa msaada ulioombwa kwa namna ya fedha umeelezwa kwa kina katika sehemu ya tano ya jitihada hii.

**5.0 RASLIMALI**

Ujenzi na uanzishaji wa taasisi za afya ni mojawapo ya jitihada za gharama kubwa ambazo lazima Serikali na jamii zizifanye ili kujihakikishia uwepo na upatikanaji wa huduma za uhakika za afya. Ujenzi wa zahanati ya Mapili ulihusisha aina mbalimbali na vyanzo vya raslimali watu na fedha kama ilivyooneshwa hapa chini.

(i) Michango ya Jamii; kila mwanajamii alichangia sh 5,000 zilizoleta jumla ya sh 48,000,000. Michango hii ilifanyika kwa kukata moja kwa moja kwenye mauzo ya Korosho kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani. Michango ilianza mwaka 2009.

(ii) Serikali kuu ilichangia sh 38,500,000/= kupitia ruzuku ya maendeleo ya sekta ya afya mwaka 2013.

(iii) H/W ya Masasi ilichangia sh 5,000,000/= kwa ajili ya kununua milango 14, kufunga mfumo wa maji na ujenzi wa vyoo.

(iv) H/W Masasi ilitoa ushauri wa kitaalamu na menejimenti kupitia kwa mhandisi na mganga wa wilaya. Hawa walikuwa ndio wasimamizi wakuu kwenye ujenzi na uanzishaji wa huduma za afya.

(v) Waziri wa zamani wa Maliasili na Utalii alichangia sh 5,000,000, Mbunge wa sasa alichangia sh 5,000,000, mwenyekiti wa chama cha wananchi (CUF) alichangia 100,000 na Mbunge wa wa zamani (2005-2010) alichangia shs 1,000,000.

**(vi)** Jamii ya Mapili na Vikundi vya Vitongoji vilichangia kupitia nguvukazi kwa kufyatua matofali, kusafisha eneo la ujenzi, kuchimba msingi, kukusanya mchanga na mawe na kujenga ukuta kwa kushirikiana na mafundi wa kijijini wasio na gharama kubwa.

**6.0 MATOKEO**

Jitihada za Jamii zinaweza kutafsiriwa kama mfumo wa utafutaji raslimali katika eneo husika ambapo jitihada ya msingi na jukumu la utekelezaji linakuwa la wakazi wa eneo hilo au jamii husika. Ni namna ya

kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi ambayo michango ya mawazo, michakato, fikra na raslimali kutoka nje zinachukua nafasi ya pili. Mbinu ya kawaida ya njia hizi za mkakati wa maendeleo ni kupitia muungano wa jamii kutumia nguvukazi, michango ya fedha na matumizi yanayozingatia matakwa ya jamii. Mara nyingi mbinu hii huhusika zaidi katika eneo la kijijini ambapo maendeleo shirikishi huhamasishwa. Hii ni kwa sababu, tukiacha mchakato wa maendeleo utokao juu kwenda chini, ni kinyume chake, ambapo jitihada ya maendeleo inapendekezwa na kutekelezwa na jamii yenyewe kwa kuzingatia mahitaji yake. Jitihada za Jamii kwa kawaida zina faida kama jitihada ya Kijiji cha Mapili inavyoonesha.

Tokeo la kwanza la jitihada ya Kijiji cha Mapili ni kukamilika na kuwepo kwa zahanati iliyojengwa kwa viwango katika ardhi ya kijiji. Mwanakijiji mmoja anaeleza *“nina furaha sana kuwa na zahanati kwa kupitia nguvu na michango yetu wenyewe, tumekamilisha jengo hili zuri na la gharama la zahanati……ni kitu kipya katika kijiji chetu…….majengo yote ni ya zamani na yemechakaa lakini hili ni jipya na la muundo wa kisasa, nafikiri tumefanikiwa kitu kikubwa, na muda si mrefu tutaanza kufurahia huduma za afya hapa karibu na hakutakuwa na usumbufu wa kusafiri kwenda mjini Newala kutafuta huduma hizi……”*




***Wananchi wenye furaha baada ya kukamilisha ujenzi wa zahanati ya Mapili***

Kuimarika kwa uwezo wa Jamii ya Kijiji; jitihada za Jamii zina asili ya ushiriki. Ushiriki hujenga uwezo wa watu kuweza kuongoza maisha yao sasa na siku za mbele. Ushiriki kamilifu hujenga uwezo wa wadau katika jamii, huwafanya waweze kudhibiti matokeo na faida za mradi na zaidi sana jamii hushikamana. Jitihada ya Kijiji cha Mapili imepelekea kuwepo kwa uwezo imara ambapo wanaume na wanawake wameshikamana na kuhamasika kushiriki kikamilifu katika miradi ya maendeleo. Uwepo wa kamati ya ujenzi pia ni tokeo muhimu. Kamati hii imekuwa ya kudumu kwa muda kwani baada ya kukamilika kwa ujenzi wa jengo kuu la zahanati na vyoo, jukumu la kamati hii litaendelezwa katika kuhakikisha kukamilika kwa ujenzi wa nyumba za makazi ya watumishi (wauguzi na waganga) na miundombinu mengine ya kituo cha afya. Huku ndiko kujengeka kwa uwezo katika kubuni miradi, kutekeleza na kusimia katika ngazi za msingi.

Kuongezeka kwa hamasa ya wanakijiji katika jitihada za Jamii; hamasa ya wanakijiji kushiriki katika miradi yao ya maendeleo imeongezeka sana. Jamii ya kijiji cha Mapili ina mpango wa kupanua zahanati ili iwe kituo kamilifu cha afya kwa kujenga majengo zaidi ya kukidhi mahitaji ya Kata, nyumba za watumishi na mtambo wa kuteketeza taka za dawa. Upitishaji wa mpango huu wa kupanua zahanati haukupata upinzani na wakijiji wameonesha nia imara ya kuruhusu michango kukatwa katika mauzo yao ya korosho katika misimu ijayo. Hii inaonesha hamasa ya juu na kujitoa thabiti kwa ajili ya jitihada za Jamii za maendeleo. Kwa mfano, ujenzi wa sekondari ya kata kijijini Chikoropola unatumia mbinu ya Kijiji cha Mapili.



***Ujenzi wa Sekondari ya Kata ya Chikoropola***

Jamii ya kijiji cha Mapili imekuwa kijiji cha mfano ambapo vijiji vingine ndani ya H/W ya Masasi vinajifunza na kuiga umoja na kujitoa kwao ili kutambua matatizo ya jamii, kufanya maamuzi kuhusu utatuzi na kutekeleza miradi ya jitihada za Jamii. Kwa mfano; Kijiji cha jirani (Chikoropola) kimeiga mbinu ya Mapili na imefanikiwa kujenga jengo la zahanati ambapo tayari zahanati imepata cheti cha usajili, mtumishi wa afya, madawa na vifaa vya zahanati toka Halmashauri.



***Zahanati ya Chikoropola***

Ujenzi wa zahanati ya Mapili umeimarisha kundi la mafundi wa kijijini ambalo limeimarika kutokana na umoja, ushirikiano na usaidizi wa jamii. Mafundi hawa wametambuliwa katika ngazi zaidi ya vijiji na kata za miradi ya ujenzi na wanashiriki katika kukamilisha miradi mingine kama nyumba 4 za watumishi Mchauru, Mkululu, Nanganga na Zahanati ya Namwanga. Mafundi kutoka Mapili pia wameajriwa na Mji wa Masasi katika shughuli za ujenzi za sekta za umma na binafsi. Mafundi hawa wamekuwa kituo cha raslimali kwa ajili ya Halmashauri na Halmashauri nyingine ambazo zinaweza kuanzisha ujenzi wa vituo vya afya na majengo mengine.

Jitihada za Jamii katika ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Mapili imeanzisha funzo kwa Halmashauri nzima kuwa kama wananchi wamedhamiria kutatua matatizo yao inawezekana. Halmashauri inatarajia kuunganisha funzo hili na O&OD iliyoboresha na kuamsha vijiji vingi kujikita katika kuainisha mahitaji ya jamii, maamuzi shirikishi, upangaji miradi na utekelezaji na zaidi ya haya kujitoa ili kuanzisha miradi kuanzia ngazi ya jamii. Hili litajenga uwezo wa jamii kukabili matatizo yao mapema badala ya kusubiri hatua za Serikali kuu na Halmashauri.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Jitihada za Jamii kawaida hujiendeleza zenyewe kwani jamii na watu binafsi katika jamii huthamini michango yao na wanaweza kupambana kwa namna yoyote ile kuendeleza huduma wazitakazo. Jitithada za Jamii pia hujenga uwezo wa wananchi na makundi yote ya kijamii katika ushiriki endelevu kwenye utekelezaji wa miradi ya jitihada za Jamii. Kupitia Zahanati ya Kijiji cha Mapili wanakijiji wameonesha wazi

lengo lao la kuhakikisha kuwa huduma za afya zitakazotolewa ni bora, za uhakika na endelevu. Wanakijiji na Halmashauri wameweka mikakati ya kuhakikisha uendelevu. Mikakati hii inajumuisha:

(i) Mipango ya kupeleka watumishi katika Zahanati hii ili ianze kutoa huduma kwa jamii kuanzia mwaka wa fedha 2016/17. Wananchi watatu tayari wametoa nyumba zao zitumiwe kwa makazi na watumishi wa zahanati.
(ii) Mpango wa kuwa na fungu la kudumu katika bajeti ya mwaka kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi ili kujihakikishia utoaji wa kudumu wa huduma za afya kwa jamii.
(iii) Mpango madhubuti wa kusajili na kuunganisha zahanati kwenye mfumo wa idara ya Madawa (MSD) ili iweze kuwa na fungu katika bajeti la dawa na vifaa vya zahanati.
(iv) Kuwa na fungu la kudumu katika bajeti ya kila mwaka kwa ajili matengenezo ya mara kwa mara, maboresho na kuongeza hadhi ya zahanati.
(v) Utoaji wa kudumu wa huduma za ulinzi wa zahanati utakaofanywa na jamii ya kijiji cha Mapili.
(vi) Uhamasishaji na ujenzi wa uelewa endelevu kuhusu kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF). Hili lina lengo la kuweka msingi imara wa fedha za kuendesha huduma za zahanati hasa kwa kusajili kaya zote kwenye mfuko wa afya ya jamii na kupata fedha zaidi chini ya utaratibu wa tele kwa tele wa mfuko wa afya ya jamii.

**8.0 SIRI YA MFANIKIO**

Jitihada ya Jamii ya Kijiji cha Mapili ya kujenga zahanati ya kisasa na yenye ubora ni fanikio ambalo vijiji na jamii nyingi Tanzania hutamani. Halmashauri na vijiji vingi, hata hivyo vimeshindwa kubadili fursa zao kuleta uhalisia katika kujipatia huduma. Swali ni; nini kilichofanya kijiji cha Mapili na H/W ya Masasi kukamilisha mradi huu? Maelezo ya siri ni marefu sana. Kwa kifupi; zahanati katika kijiji cha Mapili lilikuwa hitaji la kweli na la dhati kwa kila mwanajamii. Baada ya kugundua udhaifu hasa kama kijiji cha pembezoni, jamii ilijiingiza katika kuainisha na kuchambua hitaji la wengi na kuchagua zahanati kama kipaumbele halisia cha kijiji. Hii ndio siri kuu

Kwa mujibu wa Diwani, kufanikiwa kwa jitihada ya Mapili kulichochewa na hasira, uchungu na huruma ya wanakijiji baada ya kupoteza wajawazito wawili wakiwa njiani kuelekea Hospitali iliyopo Mjini Newala, zaidi ya 18km kuelekea mlimani, kutokana na kukosekana kwa huduma za afya katika kijiji chao. Suala hili lilileta mijadala, umoja na fikra bunifu kuelekea ujenzi wa zahanati. Siri nyingine ni pamoja uongozi imara wa kijiji, kata na Halmashauri na uwepo wa zao la biashara lenye mfumo bora wa mauzo ambao ulisaidia ukusanyaji wa michango ya jamii (mfumo wa stakabadhi mazao ghalani).

# HALMASHAURI YA MJI WA MASASI

**JITIHADA YA JAMII KUBORESHA ELIMU YA MSINGI**








***UZOEFU WA KIJIJI CHA MPEKESO***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Mji wa Masasi ni mojawapo ya Halmashauri tisa katika Mkoa wa Mtwara. Halmashauri ilianzishwa Julai 2012, baada ya mgawanyiko wa iliyokuwa H/W ya Masasi. Makao makuu ya Halmashauri yapo 214km kutoka Manispaa ya Mtwara. Halmashauri hii imezungukwa na imezungukwa na H/W ya Masasi isipokuwa upande wa Magharibi ambapo inapakana na H/W ya Nanyumbu. Halmashauri ina eneo la $400km^2$. Kwa mujibu ya sense ya mwaka 2012 Halmashauri ina wakazi 102,696 ambapo 49,111 in wanaume na 53,585 ni wanawake (sawa na 8% ya wakazi wote wa Mkoa wa Mtwara). Halmashauri ina Tarafa 2, Kata 11 na Vijiji 169. Halmashauri ya Mji wa Masasi hupata mvua kwa wa 900mm – 1000mm kwa mwaka. Msimu wa mvua ni kati ya Desemba na Aprili na wastani wa joto ni $32^0$C msimu wa mvua na kupungua hadi wastani wa $25^0$C msimu wa kiangazi.




***Ramani ya Halmashauri ya Mji wa Masasi***

Kilimo ndio shughuli kuu ya kiuchumi katika Mji wa Masasi. Ardhi inayofaa kwa kilimo ni 48,761ha, kati ya hizi ni 16,380.5ha tu hutumika. Mazao makuu yanayolimwa ni mahindi, mhogo, mtama, na mpunga kama mazao ya chakula na korosho, karanga, na mbaazi kama mazao ya biashara. Ufugaji pia hufanyika ambapo kuna ng'ombe 2396, mbuzi na kondoo 2467, nguruwe 2667, bata 3881 na kuku 45925. Kipato cha wakazi wa mji wa masasi kinakadiriwa kuwa sh 700,000. Mji wa Masasi hutoa huduma za biashara ya jumla na rejareja za vifaa vya viwandani kwa wakazi wa mji, na H/W za Masasi na Nanyumbu. Sekta ya biashara ni ya pili kwa uzalishaji wa mapato baada ya ushuru wa Korosho na mazao mengine ya kilimo.

Mji wa Masasi ulianzisha dira yake ya elimu. Dira hii husema "kuwezesha upatikanaji wa elimu bora ya msingi na sekondari kwa wote, kwa haki na kwa usawa". Kutokana na dira hii Halmashauri ina jumla ya shule 35 za awali, shule 35 za msingi na shule ya 1 ya elimu maalumu kwa ajili wa watoto wenye ulemavu. Pia Halmashauri ina shule za sekondari za Serikali 9 na 1 ya binafsi. Shule zote zina wastani unaotakiwa wa watumishi na vifaa.

## 2.0 TATIZO

Haki ya watoto kupata elimu ni moja ya misingi ya mkataba wa haki za watoto (CRC: 1990) ambao uliridhiwa na nchi za Afrika, Tanzania ikiwa mojawapo. Mkataba huu pia hueleza kuwa si tu watoto wanatakiwa kupata fursa ya kuandikishwa bali kukamilisha kiwango cha shule kinachotakiwa. Elimu ya msingi inatakiwa kuwa haki ya kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule.

**Boksi 1: Mkataba wa Haki za Mtoto (CRC)**

***Mkataba wa Umoja wa mataifa kuhusu Haki za Mtoto (kwa kifupi CRC, CROC, UNCRC) ni makubaliano ya haki za binadamu ambayo yanaweka haki za watoto za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiafya na kiutamaduni. Mkataba huu humtambua mtoto kama binadamu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18, isipokuwa kama umri wa wengi unapatikana mapema kulingana na sheria za nchi.***

***Nchi ambazo zinaridhia mkataba huu hufungwa na sheria ya kimataifa. Utiifu kwa Sheria hii hufuatiliwa na Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Mtoto, ambayo ina wajumbe kutoka nchi zote duniani. Kila mwaka Kamati hii hukabidhi taarifa kwa Kamati ya Tatu ya Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, ambao pia hupokea risala ya mwenyekiti wa Kamati ya Haki za Mtoto, na Mkutano Mkuu huridhia azimio kuhusu Haki za Mtoto.***

***Serikali za nchi ambazo zimeridhia mkataba huu hulazimika kutoa taarifa na kuwepo kwenye Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Mtoto kwa vipindi maalumu ili kukaguliwa kuhusu maendeleo katika utekelezaji wa mkataba na hali halisi ya haki za watoto katika nchi husika. Taarifa zao na maoni ya kimaandishi ya Kamati pamoja na changamoto vinapatikana katika tovuti ya kamati.***

***Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa uliridhia Mkataba huu na kuufungua kwa saini Novemba 20 1989 (katika jubilei ya 30 ya Azimio la Haki za Mtoto). Mkataba ulianza kutekelezwa Septemba 2 1990, baada ya kuridhiwa na nchi wanachama. Kwa sasa nchi 196 zimeungana na mkataba huu, ikiwa ni pamoja na nchi zote zinazounda Umoja wa Mataifa, isipokuwa Marekani.***
**Imechukuliwa kutoka Wikipedia**

Pamoja na kuwepo kwa Dira hiyo, watoto wengi (kabla ya mwaka 2010) hawakuwa wameandikishwa kwenye shule za awali na msingi na wale ambao waliandikishwa waliingia kwenye utoro kwa sababu mbalimbali. Uandikishaji wa wanafunzi katika mji wa Masasi uliporomoka sana kutokana na umbali ambao wanafunzi wenye umri mdogo walitakiwa kutembea kuzifikia shule, ukosefu wa mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia na uelewa duni wa wazazi kuhusu umuhimu wa elimu kwa watoto. Pia umaskini uliokithiri katika jamii za Mji wa Masasi ulichangia kupunguza uandikishaji wa wanafunzi na kupelekea ongezeko kubwa la wasiojua kusoma na kuandika.

Katika kijiji cha Mpekeso, uandikishaji katika shule ya msingi ulikuwa ukishuka pamoja na kuwepo kwa sera ya elimu ya msingi kwa wote (UPE) iliyoanzishwa mwaka 1974. Kwa mujibu wa sera hii watoto wote wenye umri wa kwenda shule (7-8) walitakiwa kuandikishwa kwenda shule bila masharti yoyote ifikapo mwaka 1977. Hata hivyo, tangu kuanzishwa kwake mwaka 1973 hadi 1999 kulikuwa na watoto zaidi ya 592 ambao hawakuandikishwa katika kijiji hiki ikienda sambamba na utoro wa takribani 35% ya watoto wote walioandikishwa. Ingawa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 (na kurekebishwa mwaka 1995) inataka kila mtoto wa miaka 7 aandikishwe kwenye elimu ya msingi, ni 65% ya watoto wenye umri wa miaka 7 katika kijiji cha Mpekeso waliandikishwa. Utoro katika kijiji cha Mpekeso ulitokana na kukosekana kwa shule ya msingi kijijini; na kulazimu wanafunzi kutembea umbali mrefu (5km) kwenda na kurudi shule katika kijiji cha jirani cha Matawale. Ni muhimu kutambua kuwa Shule ya msingi Matatwale haikuwa ikitoa chakula kwa wanafunzi, hata kwa wale ambao waliishi katika vijiji vya mbali kikiwemo kijiji cha Mpekeso. Mara nyingi watoto walinyeshewa na mvua kubwa ikiwa ni pamoja na kukutana na wanyama wa porini na nyoka wenye sumu. Kwa sababu hizi na nyingine jamii ya Mpekeso waliona haja ya kujenga shule kwa ajili ya watoto na vijana ambao walikosa kuandikishwa hapo awali au waliacha shule kabla ya kumaliza elimu ya msingi.

## 3.0 LENGO

Ujenzi wa shule ya msingi katika kijiji cha Mpekeso ilikuwa ni jitihada za Jamii halisi. Jitihada hii ilitokana na hitaji la jamii kuwa watoto wa kijiji cha Mpekeso walikuwa wanaacha fursa ya kuhudhuria shule, kufuta

ujinga na kuendelea ngazi za juu za elimu kwa sababu tu ya ukosefu wa jengo la kuanzia. Wanakijiji walijipanga ili kutatua tatizo hili kwa pamoja. Wanakijiji waliamua kuwa lengo la jitihada yao liwe kuchangia ili kuweza kutoa fursa ya elimu kwa walioikosa (MEMKWA) hasa wasichana katika kijiji cha Mpekeso. Mahsusi kabisa wanakijiji wa Mpekeso walilenga;

(i) Kujenga darasa kwa ajili ya mpango wa elimu kwa walioikosa (wanafunzi wa COBET)
(ii) Kupunguza umbali waliotembea wanafunzi waliolazimika kuhudhuria shule katika vijiji vya jirani kwa kuanzisha shule kijiji cha Mpekeso.
(iii) Kupunguza au kuondoa kabisa utoro wa wanafunzi walioandikishwa na kuongeza idadi ya wanaojua kusoma na kuandika katika jamii ya kijiji.
(iv) Kupunguza usumbufu na hatari kwa watoto wadogo zilizotokana na kuvuka mto msimu wa mvua, wanyama wa porini na wahalifu.
(v) Kujenga madarasa mengine kwa ajili ya kuanzisha shule ya Msingi katika Kijiji cha Mpekeso iliyosajiliwa.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Ushiriki wa jamii ni sehemu muhimu ya jitihada za Jamii za maendeleo ya jamii na huakisi mfumo wa kutatua matatizo toka chini kupitia ushiriki wa wananchi. Sehemu kubwa ya jamii huhamasishwa kuainisha na kuweka bayana malengo yao, mbinu zao za mabadiliko, na kukusanya raslimali zao katika mchakato wa kutatua matatizo. Kupitia ushiriki wa wenyeji katika kufanya maamuzi na utekelezaji wa shughuli, ndipo mahitaji, mikakati ya kufikia mahitaji, na raslimali zinazotakiwa kutekeleza mikakati mbalimbali huanishwa. Zaidi ya hayo, uenezaji wa taarifa ni muhimu sana kwamba wahamasishaji wanatakiwa kutoa taarifa sahihi za kutosha kuhusu mradi kama faida za mradi, gharama za utekelezaji, fursa za ugharamiaji na utekelezaji na hatari zinazoweza kuambatana na mradi. Panatakiwa kuwa mtiririko wa aina mbili wa taarifa kati ya wahamasishaji na umma(Harrison 2000). Katika misingi hii ya ushirikishwaji wa jamii na jithada za Jamii na nia thabiti ya kufikia malengo, wanakijiji wa Mpekeso walitekeleza mikakati iliyofafanuliwa hapa chini;

Ujenzi wa Uelewa na Ukusanyaji wa Michango; Januari 1999 mwenyekiti wa Kijiji cha Mpekeso (Henry Dismas Mkoba) alianza kuwakusanya na kuwajengea uelewa wanakijiji kupitia mikutano, majadiliano na maongezi ya jamii kuhusu hitaji la kuwapatia watoto wao elimu. Wanakijiji walishawishika vya kutosha kuhusu sababu ya kuwepo kwa shule na uamuzi wa kujenga shule uliridhiwa na Mkutano wa Kijiji. Moja kwa moja Mkutano wa Kijiji uliridhia makubaliano ya michango ya fedha taslimu. Wanakijiji walikubali kuchangia fedha kati ya TZS 2,000 hadi TZS 10,000 kwa kaya. Pia walishirikisha wadau wengine kama Madiwani, Mbunge na wengine waliovutiwa.

Ujenzi wa madarasa mawili; utekelezaji ulianza kwa kuainisha eneo la ujenzi, kufyatua matofali, na ujenzi wenyewe wa jengo la kwanza la MEMKWA. Michango ya fedha taslimu na ushiriki wa nguvukazi vilipelekea kukamilika kwa madarasa mawili ya mpango wa MEMKWA ambayo yalianza kutumika rasmi Januari 2002.



***Madarasa ya zamani yaliyojengwa na wanakijiji kwa ajili ya MEMKWA***

Uandikishaji wa wanafunzi na usajili wa shule; mpango wa MEMKWA ulianza kwa kuandikisha watoto 72 waliokuwa nje ya mfumo wa kawaida wa shule za msingi katika makundi tofauti kama ifuatavyo; wanafunzi 45 kundi la kwanza (miaka 8-13) na wanafunzi 27 kundi la pili (miaka 14-18) Januari 2000 na kumalizia 2005 baada ya kupunguza idadi ya watoto wasio shuleni katika kijiji cha Mpekeso. Jedwali hapa chini linaonyesha hali ya uandikishaji wa watoto kwa ajili ya MEMKWA.

**Jedwali 1: Hali ya MEMKWA Mpekeso**

| | Idadi ya watoto walioandikishwa | | | Kundi | | Uhuishaji wa wanafunzi wa MEMKWA kwenye mfumo wa kawaida | | | Mpaka Kidato Cha Nnne | Kidato cha sita |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| mwaka | Me | Ke | Jumla | Drs 1 | Drs 2 | Drs 5 | Drs 6 | Drs 7 | Kidato 4 | |
| 2000 | 09 | 13 | 22 | 17 | 05 | 15 | 02 | 05 | 0 | - |
| 2001 | 07 | 5 | 12 | 08 | 04 | 07 | 01 | 04 | 0 | - |
| 2002 | 21 | 17 | 38 | 23 | 15 | 17 | 06 | 15 | 2 | - |
| 2003 | 06 | 03 | 09 | 05 | 04 | 05 | 00 | 03 | 4 | |
| 2004 | 04 | 01 | 05 | 05 | 00 | 03 | 02 | 00 | 2 | 1 |
| 2005 | 03 | 01 | 04 | 03 | 01 | 02 | 01 | 01 | 1 | |

Kuanzishwa kwa shule mpya ya msingi ya kijiji; lengo la kujenga shule ya msingi lilikuwa kupunguza umbali ambao watoto walitembea kuhudhuria shule za msingi katika kijiji jirani na kuondoa hatari za wanyama wa porini, wahalifu na kuvuka mto hasa msimu wa mvua. Mwenyekiti wa kijiji (Henry Dismas Mkoba) na viongozi wa jamii, wazee na mabalozi (MAMWENYE na APUYA MWENE), Rajab Heri, Athuman Amiri, Zainabu Jia, Hamisi Punguna na Thabiti waliandaa mikutano ya jamii na viongozi ili kushawishi jamii kujenga madarasa mawili kwa ajili ya kuanzisha shule ya Msingi. Hii ilikuwa nyongeza kwenye madarasa ya MEMKWA ambayo yalianza kuchakaa. Uamuzi wa kukusanya michango kwa ajili ya ujenzi wa shule ya msingi ulifikiwa kwa makubaliano. Wanakijiji waliamua kukusanya fedha kutoka kila kaya na wadau wengine; takribani TZS 36,000,000 zilikusanywa.

Ujenzi wa madarasa mawili na matundu sita ya vyoo; fedha zilizokusanywa zilitumika katika shughuli za ujenzi na utengenezaji wa madawati 46 kwa ajili ya wanafunzi wa darasa la kwanza, la pili na awali. Ujenzi ulikamilika Septemba 2013. Shughuli za shule zilianza Januari 2014 ambapo jumla ya wanafunzi 65 (wasichana 32 na wavulana 33) waliandikishwa darasa la awali.





***Madarasa mapya na choo yaliyojengwa na wanajamii***

Msaada wa Halmashauri kwa Shule ya Msingi Mpekeso; Halmashauri iliamuua kusaidia jitihada ya kijiji cha Mpekeso kwa kutumia mpango wa TASAF ambao ulilenga uendelezaji wa miundombinu. Mchakato pana wa utambuzi wa fursa za vijijini (E-PRA) uliendeshwa katika kijiji cha Mpekeso ili kuthibitisha hitaji lililoelezwa na kujiridhisha kukidhi vigezo na idadi ya wafaidika (kaya maskini). Mwishoni mradi wa "ujenzi wa madarasa mawili na matundu 4 ya choo katika shule ya msingi Mpekeso" ulianishwa.

Uundaji wa kamati ya usimamizi wa mradi; timu ya TASAF iliwezesha jamii kuchagua na kupitisha kamati ya usimamizi wa mradi. Zoezi liliendeshwa Mei 19, 2015. Matokeo yake jamii ilikubali kutekeleza mradi wenye gharama TZS 82,140,080, ambapo msaada wa TASAF ulikuwa TZS 74,140,080.00 na michango ya jamii ya nguvukazi ilikadiriwa kuwa na thamani ya TZS 8,419,000. Halmashauri ilitoa msaada wa kitaalam. Utekelezaji wa mradi ulianza Agosti 17 na kukamilika Desemba 23, 2015. Shughuli za kila siku zilisimamiwa na kamati ya kijiji ya usimamizi wa mradi.



***Wanajamii wakishiriki ujenzi wa madarasa***

## 5.0 RASLIMALI

Ujenzi wa Jengo na MEMKWA na Shule ya Msingi Mpekeso katika mfumo wa Jitihada za Jamii ulishirikisha aina mbalimbali za wadau. Hili linajidhihirisha katika namna ya ushiriki na raslimali zilizotolewa kufanikisha kufikia malengo. Funzo muhimu katika raslimali ni michango ya jamii. Kijiji cha Mpekeso kina kaya maskini lakini hili halikuzuia jamii kuchangia kwa kiasi kikubwa ili kuanzisha shule ya MEMKWA na Msingi. Raslimali zimegawanywa katika makundi mawili; fedha na watu.

**Jedwali 2: Raslimali Fedha**

| N | Shughuli | Raslimali TZS | Chanzo |
|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa madarasa 2 ya MEMKWA | 5,000,000 | Jamii |
| 2 | Ujenzi wa madarasa 2 na matundu 4 ya choo | 36,000,000 | Jamii |
| 3 | Ujenzi wa madarasa 2 ya shule ya msingi | 74,140,080 | TASAF |
| | | 8,419,000 | Jamii |
| | | 2,300,000 | Mbunge |

Raslimali watu zilijumuisha wanakijiji ambao walitoa nguvukazi kupitia ushiriki wao katika shughuli zote za mradi kama kufyatua matofali, kukusanya mawe, kuteka maji na kusafisha eneo la ujenzi. Halmashauri ilitoa ushauri wa kitaalamu kupitia wataalamu wa ujenzi na watumishi wa TASAF kama mratibu na mhasibu.

**6.0 MATOKEO**

Jitihada za Jamii katika Kijiji cha Mpekeso zilileta matokeo na mabadiliko makuu. Mara moja wanakijiji walishuhudia uwepo wa madarasa ya MEMKWA, shule ya msingi na vyoo pamoja na madarasa walosaidiwa na TASAF ambayo yana samani bora ikiwa ni pamoja na mitambo ya umeme wa jua. Mafaniko haya yana thamani kubwa sana kwa jamii maskini ambayo miaka michache iliyopita haikuwa na chochote. Mkuu wa kamati ya ujenzi anasema *"…….tuna furaha sana kuwa na majengo haya mapya, yanayong'aa kwa ajili ya watoto wetu, na sisi wenyewe……..kati yetu hakuna hata mmoja au familia yenye nyumba na vyoo bora kama hivi……acha umeme wa jua na mwanga…….kwa kweli wanakijiji wanafuraha na wamehamasika…..nadhani hivi karibuni tutaanza kujenga nyumba za walimu kwani ndio kipaumbele chetu kifuatacho"*. Picha zilizopo hapa chini zinaeleza kila kitu.




***Madarasa mawili na Choo (matundu 4) yaliyojengwa kwa msaada wa TASAF***

Kwa miaka ya mwanzo 2010 hadi 2013 kimsingi shule ilikuwa ya MEMKWA na shughuli za taaluma hazikuwa zimelenga elimu ya msingi. Lakini kukamilika kwa ujenzi wa madarasa na vyoo vya kisasa kumeifanya shule kuwa kamilifu ya msingi yenye usajili na mwaka 2016 shule iliandikisha wanafunzi 170 kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini. Wanakijiji wana furaha kuwa watoto wao wanaweza kwenda shule iliyopo karibu na makazi yao. Suala hili limehamasisha familia nyingi kuwatia moyo watoto wao kuhudhuria shule na hasa kutoa fursa zaidi kwa mtoto wa kike kuandikishwa kwenye elimu ya msingi na kuwa na matumaini ya kumaliza. Katika miaka kadhaa ijayo jitihada hii itaondoa idadi ya wasiojua kusoma na kuandika na kuboresha kiwango cha maisha.

Jedwali **3: Uandikishaji katika S/M ya Mpekeso 2016**

| N | Darasa | walioandikishwa |
|---|---|---|
| 1 | Darasa la awali | 65 |
| 2 | Darasa la kwanza | 59 |
| 3 | Darasa la pili | 46 |
| | Jumla | 170 |

Baada ya kuanzisha madarasa ya MEMKWA mwaka 2000, kiwango cha waisojua kusoma na kuandika kimepungua. Wakati vijana 90 wamemaliza MEMKWA na shule ya msingi kama matokeo ya jitihada hii, wanafunzi 9 waliendelea na kumaliza elimu ya sekondari. Tokeo kuu kabisa ni kuwa, mwanafunzi mmoja alifaulu elimu ya sekondari ya juu na kuendelea na masomo ya chuo kikuu katika Chuo Kikuu cha Dar es

Salaam. Kwa jitihada ya kijiji maskini kama hiki tokeo hili lina mchango mkubwa kuelekea kuondoa kutojua kusoma na kuandika na kuboresha viwango vya kuishi.

Kijiji kimepiga hatua kubwa kelekea kutokomeza utoro shuleni. Kiwango cha utoro wa watoto wenye umri wa kwenda shule umepungua kwa kasi kutoka 35% hadi 6% mwaka 2015. Hii imetokana na kubadilika kwa tabia ya wazazi wengi kwa kuanza kuwekeza zaidi katika kuhakikisha na kusaidia watoto wao kuandikishwa na kuhudhuria shuleni. Watoto wenyewe wamehamasika kuhudhuria shuleni kwani umbali uliokuwa kati 0.25km hadi 5km umepungua kuwa mita chache. Hali hii inaruhusu watoto kwenda nyumbani muda wa chakula cha mchana kwa mapumziko ya saa moja na kuendelea na vipindi vya jioni shuleni bila kuchelewa. Jamii pia imefanikiwa kuondoa usumbufu, taabu na hatari ambazo wanafunzi walizipata msimu wa mvua pamoja na kuvuka mito iliyofurika, kupita kwenye mapori yenye wanyama na nyoka na kupata vitisho toka kwa watu wabaya na wahalifu.

Jitihada za Jamii ya kijiji cha Mpekeso ni ya aina yake katika Mji wa Masasi. Jinsi wanakijiji walivyojipanga kuleta matokeo ilivutia wadau wengine kuchangia katika kuanzisha mradi wa shule ya msingi. Tabia hii ilihamasisha Halmashauri na Serikali kwa ujumla kupitia TASAF kuthamini juhudi za wanakijiji na kusaidia ujenzi wa madarasa mawili ya kisasa, choo chenye matundu manne na kufunga umeme wa jua.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Jamii ya kijiji cha Mpekeso inafahamu kuwa kwa kipindi cha mwaka 2010 na 2013 na kukamilika kwa shule ya MEMKWA uendelevu wa mradi ulikuwa hatarini. Hii ilijionyesha kwenye ubora wa jengo na utayari wa wanajamii kujihusisha kiendelevu na utunzaji wa shule. Kutokana na sababu hii, jitihada ya sasa ya jamii inalindwa kwa mikakati mbalimbali ili kujihakikishia uendelevu na ubora. Mikakati hii ni pamoja na kukabidhi uendeshaji wa shule ya msingi kwa kamati ya shule na Halmashauri ya kijiji, kuandaa mipango madhubuti ya kujenga nyumba za walimu, kuiomba Halmashauri ilete walimu na vifaa na kuibana Halmashauri iweke kipaumbele, itenge bajeti na itoe fedha za ruzuku kusaidia uendeshaji wa shule ya msingi kila mwaka. Nia ya wanakijiji ya kuchangia zaidi kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mengine ipo imara na huamshwa mara kwa mara na kamati ya usimamizi wa shule.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Kwa kawaida, Jitihada za Jamii zinazoanzia chini ambapo hitaji lipo, huiunganisha jamii na kujipanga kupambambana na tatizo. Hupelekea utekelezaji rahisi kwani hitaji humsukuma kila mwanajamii kuunganisha mikono na wengine kuliondoa tatizo. Hata hivyo kuna jamii nyingi ambazo zina utajiri na zimejaaliwa raslimali lakini zimeshindwa kutatua matatizo yao. Hii inaleta swali, kwanini iliwezekana katika jamii ya Kijiji cha Mpekeso. Sababu ni nyingi ila zenye mashiko zaidi zinajumuisha;

(i) Uongozi wa kijiji imara na wa kujitoa; mwenyekiti wa zamani bwana Henry Dismas Mkoba na mwenyekiti wa sasa bwana Filimon Jacob Nyaulingo walidhihirisha stadi bora za uongozi katika kuwapanga watu, kuondoa upinzani, kuleta ufuasi na kujituma.

(ii) Jamii kujikita katika hitaji la kuwa na shule ya msingi ya kijiji. Hitaji hili la wote liliamsha kila mwanajamii kuwa tayari kutumia muda na raslimali ili kukamilisha mradi.

(iii) Uwepo wa Viongozi wa jamii (Mamwenye na Apuyamwenye) ambao wana ushawishi mkubwa katika jamii kuhusu maendeleo. Jamii za Masasi zina viongozi wa kiasili ambao huheshimiwa na kutukuzwa. Hawa wakitoa maelezo na miongozo, wanajamii hufuata na kuteleza maelekezo hayo kwa hiari na ari ya kutosha.

(iv) Mpango wa TASAF; mpango huu wa kitaifa umekuwa na thamani kubwa kwenye jitihada za Jamii nyingi za vijiji Tanzania. Uanzishaji wa Shule ya Msingi ya Mpekeso ulifaidika kwa kiasi kikubwa na uwepo wa mapango wa TASAF katika Halmashauri ya Mji wa Masasi.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

**JITIHADA ZA JAMII KATIKA MIRADI YA BARABARA NA MAJI**




***UZOEFU WA KATA ZA TEMBELA, IJOMBE, ITEWE, MAENDELEO NA INYALA***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ni mojawapo ya Halmashauri saba za Mkoa wa Mbeya. Halmashauri inapatikana kati ya Latitudo $7^0$ na $9^0$ Kusini na Longitudo $33^0$ na $35^0$ Mashariki. H/W ya Mbeya hupakana na H/W za Mbarali na Makete upande wa Mashariki, Rungwe, Busokelo na Ileje upande wa Kusini, Mbozi upande wa Magharibi na Chunya upande wa Kaskazini. Halmashauri ina jumla ya eneo la 2,432km$^2$. Halmashauri imegawanyika katika Tarafa tatu za Tembela, Usongwe na Isangati, Kata 28, Vijiji 152 na Vitongoji 951. Kwa mujibu wa sensa ya 2012 Halmashauri ina juma ya wakazi 305,319 (wanaume 143,779 na 161,540).

Jumla ya eneo ni 2,432Km$^2$ ambapo 2,164Km$^2$ (88.9%) zinafaa kwa kilimo. Halmashauri ina ardhi ambayo imefunikwa na milima, vilima na tambarare zenye mito na vijito vinavyounda mfumo wa mabonde ya Ziwa Rukwa, Ziwa Nyasa na Bonde la Mto Rufiji. Hali hii ya nchi inayopanda kuanzia 2,865m hadi 3,300m juu ya usawa wa bahari huifanya Halmashauri kuwa na ukanda wa kati kwenye tarafa za Usongwe, Isangati na Inyala na ukanda wa juu katika Tarafa za Isangati na Tembela. Kwa ujumla ardhi ina misitu ya miyombo. Milima hii ina udongo kahawia wa mfinyanzi na ukanda wa kati una ardhi ya kichanga. Kuna joto kali kiasi katika ukanda wa kati isipokuwa kipindi cha kiangazi (Mei mpaka Agosti) na milimani kuna baridi mwaka mzima. Kwa wastani Halmashauri ina joto ambalo huanzia 22$^0$C hadi 30$^0$C. Halmashauri hupata mvua ndefu kipindi cha Novemba hadi Aprili zinazokadiriwa kuwa kati 650mm hadi 2700mm.

**2.0 TATIZO**

H/W ya Mbeya ni mojawapo ya Halmashauri ambazo zina wenyeji walioamka na wachapakazi wakijihusisha na kilimo cha mwaka mzima, uuzaji wa mazao ya kilimo na shughuli za mbao ndani ya ardhi tajiri na yenye rutuba. Watu waishio Maendeleo, Tembela, Ijombe na baadhi ya vijiji vya ndani katika kata za Ulenje na Itewe walikuwa na matatizo ya kuyafikia masoko ya mazao yao ya kilimo kutokana na kukosekana kwa barabara ya uhakika inayopitika misimu yote. Barabara ya jamii mbadala na ambayo ilikuwa na kilometa nyingi za ziada haikupitika msimu wa mvua. Hali hii iliathiri uwezo wa jamii kupata pembejeo na masoko ya mazao ya shambani. Usafirishaji wa mazao ya shambani ulikuwa wa gharama sana ukigharimu takribani TZS 80,000 kwa lori kupeleka mazao kwenye masoko. Ukosefu wa barabra za uhakika ulipelekea kuharibika kwa soko la mazao na kuyafanya kukosa ushindani sokoni ikiwa ni pamoja na bei za chini sana. Hatimaye hali hii ilijidhihirisha katika kupungua kwa vipato vya kaya za wakulima. Kwa mfano kipindi cha mvua bei ya gunia moja la viazi ilikuwa TZS 8000 tu likiwa shambani. Bei hii ni ya chini sana ikilinganishwa na pembejeo zilizoingizwa kwenye uzalishaji wa gunia hilo.

Kutokana na kuporomoka kwa bei kwa sababu ya barabara mbaya na ununuaji hodhi wa mazao ya shambani, Halmashauri pia ilipata ugumu katika kukusanya ushuru wa mazao ya kilimo. Ukusanyaji wa mazao usio na utaratibu na usafirishaji wa mazao uliofanywa na walanguzi kutoka Vijiji vya Ntangano, Hatwelo, Iwalanje, Galijembe, Inyala, Itewe na Iyelanyala katika Tarafa ya Tembela uliharibu mifumo yote iliyowekwa na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya ushuru wa viazi mviringo na mazao mengine. Barabara mmbadala za kuunganisha na barabara kuu ya Dar-es-Salaam – Zambia kupitia Uyole (Jijini Mbeya) zilifanya H/W ya Mbeya kushindwa kukusanya mapato ya ushuru wa Kilimo kwani barabara inayotokea Uyole ipo nje ya himaya ya Halmashauri. Njia ya Uyole ni ndefu sana ikilinganishwa na barabara inayopita muunganiko wa Inyala na kuwafanya wakulima kulipa zaidi kusafirisha mazao yao na kuathiri sana kiwango cha faida ya kujihusisha na kilimo.

***Sehemu ya barabara isiyopitika katika kata ya Maendeleo na daraja la Nkunywa kabla ya kujengwa***

Ugumu wa kuyafikia masoko ya mazao ya kilimo hupunguza fursa na matarajio ya kuzalisha na uhakika wa pato. Umbali kutoka yalipo masoko huongeza kukosekana kwa uhakika na hupunguza uwezekano wa kuchagua; hali hii hufinya fursa za masoko, hupunguza bei za shambani na huongeza gharama za pembejeo. Kwa kufanya hivi, hali hii hudhoofisha motisha wa kushiriki katika uchumi wa kifedha na husababisha mifumo ya uzalishaji kuwa ya kujikimu tu na siyo ya soko.

Tatizo jingine kubwa la H/W ya Mbeya; maji safi na salama katika jamii za kata ya Ijombe. Jamii hizi zilikumbana na ukosefu mkubwa wa maji safi na salama na walitegemea tu mito ya msimu na chemchem za Soho na Gusi katika Vitongoji vya Ikeka na Iwanda. Maji kutoka vyanzo hivi yalipatikana 2km toka katika kaya. Pia Vitongoji vya Igalama na Majengo viliathirika zaidi na tatizo la upungufu wa maji. Maji ya visima vifupi hayakutibiwa na hivyo kutokuwa safi, salama wala ya uhakika.

**3.0 LENGO**

Baada ya kutambua ukosefu wa uhakika wa barabara na maji safi na salama, jamii zilianza kujihusisha na jitihada za jamii kutatua hali iliyokuwepo. Lengo kuu la jamii na Halmashauri lilikuwa kuboresha maisha ya watu kwa kutoa huduma za uhakika na zinazotabirika za kijamii na kiuchumi. Mahsusi kabisa, jamii na Halmashauri zililenga kuboresha barabara ya Ntangano – Ijombe – Itewe (16kms) na kujenga daraja la Nkunywa katika barabara ya Ntangano – Ijombe (6m) ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya kilimo, hivyo kuboresha uzalishaji, kuongeza ushindani sokoni, kuchochea kilimo na kuongeza vipato vya kaya. Jitihada hii ya pamoja pia ililenga kuratibu ukusanyaji na usafirishaji wa mazao ya kilimo ili kurahisisha ukusanyaji wa ushuru katika mabanio ya Kata za Tembela, Ijombe, Itewe, Maendeleo na Inyala. Lengo jingine kuu lilikuwa kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama karibu na kaya kwa kuunda na kutekeleza skimu ya maji katika Kata ya Ijombe.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Uboreshaji wa barabara, ujenzi wa madaraja na usimikaji wa skimu ya maji katika H/W ya Mbeya vilianza katika ngazi ya jamii na hivyo ni sahihi kuwa ni jitihada ya jamii. Mwaka 2012/2013, jamii za Kata za Tembela, Ijombe, Itewe, Maendeleo na Inyala ziliunganisha nguvu na Halmashauri kuboresha barabara ya Ntangano – Ijombe - Itewe na kujenga daraja la Nkunywa katika barabara ya Ntangano – Ijombe. Jitihada za Jamii zilizohusisha shughuli mbalimbali zimefafanuliwa hapa chini.

Kuanisha na kufanya maamuzi kuhusu hitaji la barabara na daraja; jamii kupitia mikutano yao ya vijiji ilitambua hitaji la barabara na daraja na kuazimia kuzipa kipaumbele katika mipango ya vijiji vyao. Baada ya kuingiza katika mipango ya kijiji uhamasishaji wa jamii ulikuwa muhimu ili kuhakikisha utekelezaji rahisi wa miradi. Mikutano iliendeshwa katika kila kijiji kuzihamasisha jamii kuhusu umuhimu wa miradi na sababu za kushiriki kikamilifu kupitia michango ya fedha taslimu na nguvukazi kipindi cha ujenzi wa daraja, shughuli za uboreshaji wa barabara na baadaye uchimbaji wa mifereji ya kulaza mabomba.

Ukusanyaji wa fedha taslimu na ushiriki katika shughuli za ujenzi; mikutano ya vijiji iliazimia kuwa kila mtu (nguvukazi) achangie TZS 5,000 katika awamu ya kwanza na TZS 9,000 katika awamu ya pili. Jumla ya TZS 5.6m zilikusanywa. Fedha hizi zilitumia kununua nondo, saruji na kulipa mafundi wenyeji. Ushiriki katika kujenga daraja na shughuli za kuboresha barabara ulitangazwa kuwa "shughuli ya jamii yote" ikimaanisha kuwa kila mwanakijiji aliyeandikishwa alitakiwa kushiriki. Jamii zilianza zenyewe kutafuta ushauri kwa mhandisi wa Halmashauri kuhusu vipimo vya kujenga msingi wa daraja. Shughuli katika hatua hii zilikuwa uchimbaji wa shimo la msingi, ukusanyaji wa vifaa vya ujenzi (mawe, mchanga na kuponda kokoto), na ujenzi wa msingi wa daraja chini ya usimamizi wa mhandisi wa Halmashauri. Kuhusu uboreshaji wa barabara, jamii kwa kutumia vifaa vya asili (majembe, shoka, reki, mapanga nk) walisafisha maeneo, kuchimba na kutoa mawe, kusawazisha, kushindilia na kuchimba mifereji ya kutolea maji barabarani chini ya uangalizi wa mhandisi wa Halmashauri. Baadhi ya maeneo yalikuwa magumu kutengeneza barabara kwa mfumo wa nguvukazi. Uchimbaji wa miamba ulifanyika kwa kutumia mbinu za asili za kuchoma miamba, kutia maji na kuponda kwa kutumia nyundo.

Kuridhiwa kwa Mradi wa Jamii na Timu ya Menejimenti ya Halmashauri (CMT) na Bazara; kufuatia juhudi za wananchi katika ujenzi wa daraja na kuboresha barabara, mhandisi wa Halmashauri alipendekeza kwenye timu ya menejimenti kuwa msaada wa Halmashauri ulikuwa muhimu ili jamii hizi ziweze kukamilisha jitihada zao kikamilifu. Timu ya menejimenti iliridhia pendekezo hili na kuliwasilisha kwenye Baraza. Suala hili hata hivyo lilihusisha uandaaji wa hoja nzito za kuwashawishi Madiwani. Katika kuwasilisha pendekezo la kusaidia ujenzi wa daraja na uboreshaji wa barabara za kata za Tembela, Ijombe, Itewe, Maendeleo na Inyala, timu ya menejimenti ilitoa sababu nzito za kutenga fedha kwa ajili ya mradi ambazo ni pamoja na kupunguza gharama za usafirishaji kwa wakulima wa maeneo hayo na kurahisisha ukusanyaji wa ushuru wa mazao katika banio la Inyala. Baraza liliridhia na kupitisha.

Msaada wa Halmashauri katika ujenzi wa daraja na maboresho ya barabara. Wakati wa ujenzi wa daraja Halmashauri ilisaidia usimikaji wa jiwe la msingi wa daraja, kuweka zege la kivuko, kusimika nguzo za daraja na kupaka rangi. Katika kuboresha barabara Halmashauri ilisaidia kusawazisha barabara kwa kutumia greda na mitambo ya kuchimba na kushindilia. Katika kazi zote hizi wanavijiji walishikiriki kikamilifu katika shughuli zilizohitaji nguvukazi.

Matumizi ya Akaunti Maalumu (force account); msaada uliotolewa na Halmashauri katika ujenzi wa darasa na maboresho ya barabara ulitekelezwa kupitia akaunti maalumu ili kupunguza gharama na muda wa kufuata taratibu za manunuzi na utekelezaji wa mradi. Akaunti maalumu katika utekelezaji wa miradi huwa na maana ya kazi inayofanywa katika mradi wa ujenzi bila uwepo wa mkataba au makubaliano kuhusu gharama za kazi husika na hufanyika kwa maelewano kuwa mkandarasi atamdai mmiliki wa kazi kulingana na gharama za vifaa na mitambo zilizotumika katika kazi hiyo, pamoja na asilimia kadhaa ya gharama zilizozidi na faida. Kwa maneno mengine, Kazi zinazotekelezwa kwa Akaunti maalumu ni kazi za ujenzi zilizopatiwa kandarasi ambazo malipo hufanyika katika misingi ya muda na vifaa vilivyotumika. Licha ya umuhimu wake katika maeneo magumu kufikika ya vijijini, matumizi ya akaunti maalumu hayakubaliki sana katika kanuni za manunuzi ya umma.



*Jamii ikichimba msingi wa daraja la Nkunywa na uchimbaji wa mawe kutengeneza barabara*

Usimikaji wa Skimu ya Maji katika Kata ya Ijombe pia ilikuwa ni jitihada za Jamii. Jamii ilitambua hitaji lake na kuanzisha mchakato mzima wa skimu ya maji. Shughuli za mchakato huu zimefafanuliwa hapa chini.

Mikutano ya Vijiji na ukusanyaji wa michango ya kaya; kutokana na kuwa ni hitaji la pamoja, viongozi wa vijiji waliamua kuitisha mikutano ili kujadili na kufanya maamuzi ya wengi kuhusu namna ya kulikabili tatizo la maji. Azimio lilifikiwa la kuwa na ushirika ambao ulihusisha michango ya TZS 5,000 kwa kila kichwa ili kujenga skimu ya maji ikihusisha sehemu ya kuchukulia maji, mtandao wa mabomba, tenki la maji na vituo vya kuteka maji. Ukusanyaji wa michango ulifanyika na jumla TZS 9,884,000 zilikusanywa na wanavijiji wa Ntangano na Hatwelo.

Kupima skimu; Halmashauri ilipeleka fundi katika jamii na kwa kushirikiana na wanakijiji fundi huyu alipima eneo ili kuainisha sehemu ya kuchukulia maji, namna ya kutandaza mabomba, jinsi ya kujenga matanki ya maji na maeneo ya kujenga vituo vya kuteka maji. Jumla ya TZS 4m kutoka michango ya kaya zilitumika kwenye upimaji huu.

Kuomba ufadhili toka Halmashauri; wanajamii kupitia kwa Mh. Diwani Bwana Ramadhani Mwandala waliamua kuomba usaidizi kwa ajili ya mradi wa maji ambao walikuwa wanatekeleza. Halmashauri ilikubali ombi hilo na kupitisha matumizi ya TZS 129m kwa sharti kwamba jamii ichangie 5% ya gharama zote za mradi. Jamii ilichanga 5% ya gharama za mradi mara moja.

Ujenzi wa Skimu ya Maji; matenki mawili ya maji yalijengwa katika vijiji vya Hatwelo na Ntangano. Pamoja na kuchanga fedha taslimu kwa ajili ya skimu, wanajamii walishiriki katika kuchimba mifereji yenye umbali wa 10.3km kutoka sehemu ya kuchukulia maji mtoni. Mradi ulikamilika mwaka 2008 ukiwa na matenki mawili makubwa na vituo 10 vya kuteka maji katika makazi; vituo 5 kwa kila kijiji.

Uundaji wa Jumuia za Watumia Maji na Mafunzo; wataalamu wa maji wa Halmashauri waliendesha mchakato wa kuunda jumuia za watumia maji katika kila Kitongoji na jumuiya kuu ya skimu nzima ili kuwepo kwa uendelevu wa mradi. Uwezeshi ulihusu uchaguzi wa wajumbe wa jumuia, kutunga sheria ndogo, kuanzisha tozo za maji za kaya kwa mwezi na uendeshaji wa jumla wa skimu. TSZ 500 zilipitishwa kama tozo ya huduma kwa kaya kwa mwezi na TZS 35,000 zilipitishwa kuwa gharama za kuunganisha maji katika kaya na tozo ya huduma ya TZS 2,000 kwa kila kaya iliyounganishwa. Wajumbe wa jumuia walipatiwa mafunzo kuhusu usimamizi wa msingi wa jumuia za watumia maji, usimamizi wa fedha, utunzaji wa hesabu, tiba ya maji, ratiba za ugawaji maji na matengenezo madogomadogo ya skimu ya maji.

**5.0 RASLIMALI**

Barabara na Maji ni huduma muhimu zitolewazo na Serikali za Mitaa zote duniani. Huduma hizi ni ghali kuziunda, kujenga na kuhakikisha kuwa watu wanapata barabara bora na maji safi, salama na ya uhakika. Halmashauri nchini Tanzania bado zina changamoto nyingi katika kutoa huduma hizi kikamilifu. H/W ya Mbeya na jamii zinazofaidika na jitihada hizi zilitafuta raslimali kutoka vyanzo mbalimbali ili kuweza kufikia malengo yao. Raslimali zinajumuisha yafuatayo:

(i) Uboreshaji wa barabara; jamii ilichangia fedha taslimu na nguvukazi zenye thamani TZS 18,000,000 na msaada wa Halmashauri ulikuwa TZS 13,000,000 katika kuboresha barabara ya Ntangano – Ijombe – Itewe yenye 16kms ambapo jumla ni TZS 31,000,000. Ni vema kutambua kuwa kama shughuli hii ingepewa kandarasi kwa kufuata taratibu zote za manunuzi na kushirikisha sekta binafsi, gharama za ujenzi zingeweza kuzidi TZS 56m.

(ii) Ujenzi wa Daraja; jamii ilichangia fedha taslimu na nguvukazi za jumla ya TZS 12,000,000 na Halmashauri ilichangia jumla ya TZS 21,000,000 katika ujenzi wa daraja la Nkunywa na kuleta jumla ya TZS 33,000,000. Kama kazi hii ingepatiwa kandarasi kwa wakandarasi binafsi ingegharimu zaidi TZS 42mil kwa ubora huohuo wa daraja.

(iii) Skimu ya Maji; raslimali fedha kwa ajili ya skimu ya maji zilijumuisha michango ya jamii ya TZS 9,884,000 na ufadhili wa Halmashauri wa TZS 129m.

(iv) Raslimali watu; miradi hii ilihitaji ushiriki wa moja kwa moja wa wanakijiji katika shughuli zote kama ilivyofafanuliwa kwenye mikakati ya utekelezaji; hii ikiwa ndio sababu ya kuokoa gharama. Pia viongozi wa vijiji, wahandisi wa Halmashauri na mafundi walitoa nguvukazi katika majadiliano, usimamizi na upimaji.

**6.0 MATOKEO**

Jamii na H/W ya Mbeya zimeboresha utoaji wa huduma katika sekta za barabara na maji katika Kata za Tembela, Ijombe, Itewe, Maendeleo na Inyala ambazo zilikuwa na changamoto kubwa katika usafirishaji wa mazao ya kilimo na maji safi na salama. Tokeo la kwanza ni uwepo wa barabara iliyoboreshwa ya 16km ya Ntangano – Ijombe – Itewe. Barabara hii imeleta uhakika wa usafiri wa mazao ya kilimo na umma na kuchochea uzalishaji katika Kata hizi. Jamii zinafuraha kwani gharama za usafirishaji zimepungua na kupelekea kuongezeka kwa faida katika shughuli za kiuchumi. Kupungua kwa muda uliotumiwa na wakulima kusafirisha mazao kwenda sokoni kumepunguza hasara zilizotokana na kuoza kwa mazao kama kabichi, mchicha na matunda hivyo kuongeza mauzo na faida. Barabara zimepunguza umbali kutoka 26km kupitia kijiji cha Galijembe mpaka 16mk tu kupitia Inyala. Ufanisi huu katika gharama na muda kwa pamoja vimechangia kuongezeka na kuimarika kwa vipato vya kaya.




***Vipande vya barabara ya Ntangano – Ijombe – Itewe***

Daraja la Nkunywa katika barabara ya Ntangano – Ijombe limekamilika na ni tokeo muhimu la jitihada hizi za jamii. Daraja limeunganisha vijiji vyenye uzalishaji wa hali ya juu na limeboresha soko la mazao ya kilimo. Kwa mfano, uzalishaji wa mazao ya kilimo na bei za shambani zimeongezeka kutoka TZS 8,000 na 10,000 hadi TZS 20,000 na TZS 28,000 kwa gunia. Wakulima wameongeza uzalishaji kwa ekari kutokana

na upatikanaji wa pembejeo za ziada kutokana na kuimarika kwa bei za mazao sokoni na akiba inayotokana na kupungua kwa gharama za usafiri.




*Daraja la Nkunywa kipindi kiangazi na masika*

Kuongezeka kwa kiwango cha pato la kaya katika Kata za Tembela, Ijombe, Itewe, Maendeleo na Inyala kumebadilisha jamii kuelekea viwango vilivoboreshwa vya maisha ya jamii kama inavyojidhihirisha katika aina na nyumba na mifumo ya kuishi. Watu wameweza kujenga nyumba bora, kusaidia familia katika elimu na gharama za afya na kununua pikipiki, vyote vikidhihirisha kuongezeka kwa utajiri katika kaya na jamii kwa ujumla.




*Nyumba Bora*

Miradi ya ujenzi wa barabara na daraja imeboresha taratibu, udhibiti na mbinu katika ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kuleta ongezeko la makusanyo ya ushuru wa mazao. Kabla ya maboresho ya barabara makusanyo yalikuwa TZS 5,600,000.00 tu, lakini baada ya maboresho ya barabara Halmashauri inakusanya zaidi ya TZS 9,764,000.00 kwa msimu.

Vijiji vya jirani vimeiga jitihada hii za Jamii. Ubunifu na fikra za aina hii zimetumika katika vijiji vya jirani kukarabati barabara ya Shibolya – Idunda yenye 5km ambapo juhudi za jamii zina thamani ya TZS 20,000,000 na sasa barabara inatumika. Pia barabara ya Igosa – Mwaselela yenye 8km ilijengwa na wanajamii ambao walichangia raslimali zao kama ardhi na fedha taslimu takribani TZS 32,000,000 na barabara inatumika na inatoa huduma za usafirishaji ulioboreshwa wa mazao ya kilimo na uhakika wa kuchochea shughuli za uchumi.

Skimu ya maji katika kata ya Ijombe imeleta matokeo mengi. Tokeo moja kuu ni skimu ya maji inayofanya kazi yenye sehemu ya kuchukulia maji, matenki mawili ya maji, mabomba na vituo 19 vya kuteka maji. Jitihada hii ya jamii imezipa jamii punguzo kubwa la bei ya maji kutoka TZS 500 mpaka TZS 50 kwa ndoo moja. Mradi huu ni mkubwa kwani umezifikia kaya 264 na kuwafaidisha wanawake na watoto wengi katika vijiji vyao.

Skimu hii inaendeshwa na Jumuia ya watumia maji katika ngazi ya Kitongoji na shughuli za jumla zikiendeshwa na Kamati ya Skimu. Skimu ina akaunti ya benki ya NMB yenye TZS 776,000 na chama cha kuweka na kukopa (SACCOs) chenye mtaji wa TZS 2m. Kamati ya skimu ina jukumu la kufanya matengenezo ya mara kwa mara kuanzia chanzo cha maji, matenki ya maji hadi kwenye vituo vya kuteka maji katika makazi ya jamii kwa kutumia makusanyo yatokanayo na tozo za huduma.

Jamii yenye furaha na afya njema; licha ya kupata maji karibu na kaya, wananchi sasa wanaweza kutumia muda zaidi katika shughuli za uzalishaji, ujenzi wa nyumba bora na kufurahia afya njema kutokana na kupungua kwa matukio ya maradhi yatokanayo na maji machafu. Shule za msingi zimepatiwa vituo vya kuteka maji ili kuruhusu upatikanaji rahisi wa maji safi na salama kwa wanafunzi na walimu.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Halmashauri na Jamii zimeweka mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa barabara na skimu ya maji ni endelevu. Mkakati mkuu mojawapo ni ukarabati wa mara kwa mara wa daraja na barabara yanayofanywa na Halmashauri na jamii ikiwa ni pamoja na kuchimba mifereji ya kutolea maji yanayotuama barabarani, kufyeka majani kwenye kingo za barabara, kuondoa tope na kukarabati kingo za daraja. Mkakati wa pili kuhusu uendelevu wa skimu ya maji, Halmashauri na jamii zina mipango ya kujenga sehemu mpya ya kuchukulia maji mtoni ili kuongeza wingi wa maji kwa kuchangia TZS 20,000 kwa kichwa; upimaji wa skimu ta pili umekamilika na ujenzi wa sehemu ya kuchukulia maji unatarajiwa kuanza mwezi juni 2016. Skimu hii itagharimu TZS 74,559,000. Mikakati mingine ya uendelevu ni pamoja na ushirikiano endelevu na Halmashauri ili kufadhili upanuzi wa skimu na kufunga uzio katika vituo 19 vya kuteka maji.

**8.0 SIRI YA MAFANIKO**

Miradi ya ujenzi wa barabara ni ya gharama na hivyo jamii nyingi za Tanzania kwa ujumla hujitenga na sekta ya barabara. Jamii kwa ujumla huamini kuwa ni jukumu la Serikali kujenga barabara hata katika ngazi za vijiji na vitongoji. Jamii za H/W ya Mbeya ziliweza kujenga barabara na daraja bora kwa sababu ya hali halisi ya shughuli zao za kiuchumi na ari thabiti ya kumiliki maendeleo yao. Baadhi ya siri za mafanikio ni;

(i) Mradi unaotokana na hitaji halisi; daraja na barabara vilikuwa hitaji ambalo jamii ililitamani ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya shambani.
(ii) Utayari wa jamii kushiriki katika mradi; jamii ilichangia fedha taslimu na nguvukazi katika mradi kwani lilikuwa hitaji lao la muda mrefu.
(iii) Utayari wa Halmashauri kufadhili jitihada za jamii.
(iv) Viongozi wenye kujitolea katika ngazi zote.

Siri ya msingi katika kukamilisha skimu hii ya maji ambayo ni kubwa na ya gharama imeegemea zaidi katika umoja, ushirikiano na kujitoa kwa wanajamii wenye hitaji. Ukweli kuwa upatikanaji wa maji safi na salama lilikuwa hitaji la jamii, utayari wa jamii kuchangia fedha na nguvu kazi, uwazi ulioneshwa kupitia uwasilishaji wa taarifa za robo mwaka za mapato na matumizi, uanzishaji wa jumuia imara za watumia maji na utungaji wa sheria ndogo vyote ni siri na mafunzo muhimu ya jamii nyingine za Tanzania kujifunza.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MOMBA


**JITIHADA ZA JAMII KUJENGA MADARAJA BEMBEA**




***UZOEFU WA H/W MOMBA***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Momba inapatikana Kusini Magharibi mwa Mkoa wa Songwe, kati ya Latitudo $8^0$10 na $9^0$15 Kusini na Longitudo $32^0$5 na $32^0$45 Mashariki. Halmashauri inapakana na Mkoa wa Rukwa na Jamhuri ya Zambia upande wa Magharibi, H/W za Mbozi upande wa Mashariki, Chunya upande wa Kaskazini na Ileje upande wa Kusini. Halmashauri imegawanyika katika Tarafa 3 yaani Ndalambo, Kamsamba na Msangano, Kata 14, Vijiji 72 na Vitongoji 303. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 H/W ya Momba ilikuwa na wakazi 196,818 ambao 102,561 ni wanawake na 94,257 ni wanawake. Idadi ya wastani wa watu katika kaya ni 4.6.




***Ramani ya H/W ya Momba***

Halmashauri ina jumla ya eneo la 6217.9$km^2$ na limegawanyika kwa ujumla katika ardhi ya kilimo 4,017$km^2$, hifadhi za misitu 1,228$km^2$, makazi na matumizi mengine 409.8 $km^2$. Eneo la maji ni 351.4$km^2$ na eneo tengefu la wanyama ni 211.7$km^2$. H/W ya Momba ipo kati ya 900m - 2750m juu ya usawa wa bahari. Kwa wastani Halmashauri inapata mvua kati ya 1350mm na 1550mm kwa mwaka. Joto la wastani huanzia $20^0$C hadi $28^0$C. Halmashauri imegawanyika katika kanda mbili ambazo ni ukanda wa juu na ukanda wa bonde la ufa. Ukanda wa juu upo katika kipande kidogo cha Tarafa ya Ndalambo ambapo huinuka toka 1400m - 2750m juu ya usawa wa bahari. Sura ya nchi ya eneo hili ina milima mingi yenye mito na mabonde muhimu kwa umwagiliaji. Katika ukanda huu, aina mbili za udongo zipo dhahiri ambazo ni udongo wa volcano na mfinyanzi. Ingawa uoto wa asili umeondolewa na binadamu katika sehemu nyingi kupitia shughuli za kilimo, kiasi kidogo cha uoto wa asili bado kinapatikana hasa katika mabonde ya mito, milima na vilima. Hali ya hewa ni joto kidogo na mvua nyingi ikilinganishwa na ukanda wa chini.

Ukanda wa Bonde la Ufa (ukanda wa chini) upo upande wa Magharibi mwa Halmashauri, ukichukua sehemu kubwa za Tarafa za Ndalambo, Msangano, Ivuna na Kamsamba. Eneo hili lina joto kali linaloanzia $25^0$C hadi $28^0$C. Ukanda huu una tambarare zenye udongo wa mfinyanzi, aina za kichanga (loam) na tope (silt) zilizopo kwenye eneo kubwa. Mito mikuu hupita katika baadhi ya maeneo ya ukanda huu. Mito hii huambatana na mabonde yanayofaa kwa uzalishaji wa mpunga, maharagwe, mbogamboga, matunda na mazao mengine. Kwa sehemu kubwa uoto wa asili katika eneo hili ni aina mojawapo ya migunga.

**2.0 TATIZO**

Ni suala la uhakika kuwa 75% ya wakazi wa Tanzania wanaishi katika maeneo ya vijijini. Wakazi hawa hutegemea uchumi wa kilimo cha kujikimu. Hivyo usafiri ni wa muhimu sana kwa kila mmoja katika maeneo haya. Watu wa vijijini huhitaji kusafiri ili kupata mahitaji yao ya msingi ya kiuchumi na kijamii. Hitaji la kusafiri si mwisho wenyewe. Watu husafiri ili kwenda kufanya kazi mashambani, kutoka kijiji kimoja hadi kingine, kwenda kwenye taasisi za afya, shule, huduma za utawala na mengineyo. Kimsingi, kusafiri ni haki ya binadamu iliyoelekezwa na mikataba mbalimbali na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini ni ukweli kuwa wakazi wa vijijini nchini Tanzania hupata taabu sana katika kusafiri kwani mito, barabara za tope, barabara za vijijini, madaraja na kalavati huleta changamoto katika kusafiri.

Teknolojia ya madaraja bembea ilianza kama nyongeza katika teknolojia asilia iliyokuwepo ya madaraja bembea. Mbinu asilia zilizotumiwa na jamii katika kuvuka mito zilijumuisha ngalawa na madaraja bembea. Madaraja bembea na ngalawa yaliundwa kwa magogo na magogo yaliyochimbwa. Mbinu hizi za usafiri zilikuwa muhimu sana katika kuvuka mito. Ingawa zilikuwa na msaada kwa namna moja au nyingine, kulikuwa na hofu kuu kuhusu usalama wao. Ngalawa na madaraja bembea ya asili yalikuwa ya hatari sana kwa maisha ya wakazi waishio pembezoni mwa mito, hasa mto Momba. Pamoja na kutumiwa kwa miaka mingi, vijiji vilishuhudia vifo vya wapendwa wao kwa kuzama au kutumbukia kwenye maji kutoka kwenye ngalawa au daraja bembea. Maboresho ya mbinu hizi za kuvuka mito yalikuwa muhimu sana kwa wanavijiji ili kuokoa maisha yao.



***Daraja bembea na ngalawa ya asili***

Kwa H/W ya Momba, katika baadhi ya vijiji, usafiri msimu wa mvua huwa mgumu sana. Watu hulazimika kuvuka mito mikubwa na yenye kina kirefu ikiwa ni pamoja na maeneo mapana yenye matope. Kitabia nchi, Mto Momba, Ikana na Kalungu hupita katika vijiji vingi na kufanya changamoto katika usafiri wa watu suala ambalo hupelekea upatikanaji duni wa huduma za barabara. Asilia watu walizoea kuvuka mito hii kupitia madaraja bembea yaliyotengenezwa kienyeji na wengine walitumia ngalawa ndogondogo. Kwa mfano wanakijiji walisafiri kutoka na kurudi kati ya Vijiji vya Kaonga na Tontela kwa kuogelea au ngalawa. Ilieleweka wazi kuwa vifo vya watu kwa kuzama au kuvamiwa na mamba wakati wa kuvuka mto lilikuwa suala la kawaida. Mwaka 2004 watu nane kati yao wawili wakiwa wajawazito, walimu wawili na wakulima wane katika kijiji cha Kaonga walikufa wakiwa wanavuka mto Momba kwa kutumia Ngalawa za asili. Pamoja na hayo, usafirishaji wa mazao ya kilimo kwenda sokoni na vifaa vya ujenzi kwenda vijijini ulikuwa mgumu sana. Pia kuzifikia huduma za afya ilikuwa vigumu sana na ilichukua muda mwingi kwa sababu watu hawakuwa na uwezo wa kuvuka mto Momba kwenda zahanati ya Mkulwe. Vijiji ambavyo vilikuwa na hali hii vilibaki vimejitenga na kuwa mbali. Kwa ujumla kutengwa kwa eneo Fulani huchukuliwa ni tatizo la maendeleo na sababu inayochangia umaskini.



*Daraja bembea la asili lililoharibika*



*Daraja bembea la asili linalotumika*

**3.0 LENGO**

Binadamu waishio karibu na mito yenye maji mwaka mzima wametumia madaraja bembea tangu enzi na enzi. Katika hitaji la kuwatembelea majirani walio ng'ambo ya mto, kupeleka mazao sokoni, kununua bidhaa za viwandani na kupata huduma mbalimbali za kijamii, binadamu katika dunia nzima wamebuni, kujenga na kutumia aina mbalimbali za madaraja bembea, kuanzia madaraja bembea ya mikono, madaraja bembea ya miguu, madaraja bembea ya miguu yenye staha (sehemu pana ya kutembelea) na madaraja bembea ya kisasa yanayobeba mizigo mizito. Lengo kuu la H/W ya Momba lilikuwa kuboresha maisha ya wakazi kwa kuimarisha miundombinu ya usafiri hasa ya madaraja bembea katika Kata za Chitete, Msangano, Chilulumo na Nzoka. Mahsusi, jitihada hii ililenga:

(i) Kuboresha madaraja bembea ya miguu kuwa madaraja bembea ya kisasa kutoka 1 na kuwa 16.
(ii) Kuwezesha jamii kuendeleza na kutunza miundombinu yao ya usafiri kwa kutumia stadi za viongozi wa vikundi au mafundi wenyeji pamoja na stadi za usimamizi za Halmashauri za Vijiji.
(iii) Kuboresha namna ya kuzifikia huduma za kijamii na kiuchumi (huduma za afya, shule, mashamba, masoko, na utawala) zilizo nga'mbo ya mto.
(iv) Kupunguza vifo vya watoto na akina mama.
(v) Kupunguza muda uliotumiwa katika kuvuka mto kutoka masaa sita hadi dakika 5.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Teknolojia ya madaraja bembea iliigwa kutoka kwa Mapdre wa Kanisa Katoliki katika Kijiji cha Kamsamba ambalo lilijengwa mwaka 1984. Daraja hili la mapadre lilikuwa jepesi likiwa na Kamba mbili za chuma kutoka upande mmoja wa mto kwenda mwingine na njia (staha) ya mbao ya kutembelea ili kusaidia watu kuvuka mto kwa miguu tu. Teknolojia hii ya daraja la Mapdre iliboreshwa kwa kufunga kingo pande zote mbili na kujenga milingoti imara pembezoni mwa mto. Maboresho haya yalifanywa na ofisi ya mhandisi wa Halmashauri. Madaraja bembea yaliyoboreshwa ni salama zaidi kwani yanaweza kuchukua aina mbalimbali za watumiaji kama waoga wa kifo, walevi, waendesha baiskeli, waendesha pikipiki, watoto na wazee. Daraja bembea sasa linajulikana zaidi kama na kwa asili linaitwa kiteputepu, kwa lugha ya Kikonongo. Aina hii ya madaraja bado yanahitajika katika jamii za vijiji vingine ambavyo vina changamoto hii ya kuvuka mto.

Uaandaaji wa mipango na kufanya maamuzi; uandaaji wa mipango katika Kijiji cha Kaonga ulifanywa kwa usaidizi wa wawezeshaji kutoka Halmashauri mwaka 2004. Kupitia Mchakato wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD), wawezeshaji walizisaidia jamii kuainisha mahitaji na fursa zao. Mchakato huu ulifanyika kupitia mikutano ya kijiji ambapo vikosi kazi viliundwa ikiwa ni pamoja na viongozi maarufu, makundi ya vijana na wanawake. Vikosi kazi vililinganisha mahitaji na kuchagua tatizo la kuvuka Mto Momba kama kipaumbele namba moja kilichopelekea mradi wa ujenzi wa daraja bembea la Kaonga.

Ujenzi wa uelewa na ukusanyaji wa michango ya kaya; mwaka 2005 viongozi wa kijiji kwa kutumia mbinu shirikishi walianzisha mchakato wa kuondoa matatizo ya kuvuka mto kwa kuboresha miundombinu ya asili ya usafiri iliyokuwepo katika eneo lao. Mjadala wa kina ulifanyika kuhusu madhara ambayo jamii zilikuwa zikipata katika kuvuka mto. Mjadala huu uliepelekea kuitishwa kwa mkutano wa kijiji ili kujadili na kukubaliana kuhusu kuanza kwa mradi wa kuboresha usafirishaji. Mkutano wa kiijiji ulilenga kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuchangia fedha za ujenzi wa daraja. Baada ya uhamasishaji jamii ilikubali kuchanngia TZS 500/= kila kaya kama mchango anzia. Michango ilikusanywa na viongozi wa kijiji na kuweka fedha kwenye akaunti ya benki ya NMB iliyopo Vwawa katika Wilaya ya Mbozi. Baada ya makusanyo ya jumla ya TZS 4,416,000, viongozi wa kijiji waliomba usaidizi wa fedha kutoka Halmashauri kwani michango ya jamii haikutosha kukamilisha mradi. Halmashauri ilikubali kujazia katika jitihada ya jamii.

Ujenzi wa Daraja; Halmashauri ya kijiji na kamati ya usafiri zilipewa jukumu la kusimamia shughuli za ujenzi. Viongozi wa mafundi wenyeji walifundishwa kupitia mafunzo ya kazini na kujipatia stadi katika teknolojia inayotumia nguvukazi katika kazi za barabara na stadi za ujenzi na ukarabati wa madaraja bembea. Ujenzi wa daraja bembea ulizinduliwa mwaka 2005 na kukamilika mwaka 2007. Daraja bembea lililojengwa na njia zilizokarabatiwa zinaendelea kufanyiwa matengenezo na mafundi wenyeji walioteuliwa na kupewa jukumu la kutatua masuala ya kiufundi yanayojitokeza katika madaraja bembea. Daraja kwa sasa linahudumia wananchi 2,595 wa Kijiji cha Kaonga na wananchi 3,107 wa Kijiji cha Tontela.



***Uzinduzi wa daraja bembea la Kaonga***

**5.0 RASLIMALI**

Ujenzi wa daraja bembea la Kaonga ulikuwa ni jitihada za jamii halisi kwani jamii ilidhamiria kujenga daraja kwa kutumia michoro, raslimali na nguvu zao. Kupitia uwezeshi wa watumishi wa Halmashauri kipindi cha kuandaa mipango ya kijiji hitaji la kuvuka mto bila hofu lilipata kuwa kipaumbele cha juu. Kufikia lengo hili aina mbalimbali za raslimali zilihitajika.

Raslimali Fedha; michango ilifanyika kwa mfumo wa kukusanya vifaa vya ujenzi vilivyopo katika maeneo yao kama mbao, mawe, kokoto, nguvukazi na uongozi. Halmashauri na Serikali Kuu zilichangia vifaa vya viwandani, utaalamu na usafirshaji wa vifaa kwenda kwenye eneo la ujenzi, pamoja na usimamizi. Jedwali 1 linaonesha michango kutoka kwa jamii kwa vijiji vyote, pamoja na Kijiji cha Kaonga.

**Jedwali 1: Raslimali Fedha**

| N | Kijiji | Urefu wa daraja | Jamii | Halmashauri | Serikali kuu | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **01** | Chitete | 52m | 1,400,000/= | 630,000/= | 5,734,110/= | 7,764,000/= |
| **02** | Naming`ongo | 90m | 2,400,000/= | 1,000,000/= | 12,000,000/= | 15,400,000/= |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **03** | Mnyuzi | 74m | 1,426,000/= | 1,100,000/= | 6,000,000/= | 8,533,000/= |
| **04** | Kaonga | 100m | 4,416,000/= | 1,500,000/= | 20,708,000/= | 26,349,600/= |

Raslimali watu; Afisa Mtendaji wa Kijiji alikuwa mtu wa mstari wa mbele katika kuratibu na kutekeleza shuguli zilizopangwa wakati Mwenyekiti wa Kijiji kwa kushirikiana na wajumbe wa Halmashuri ya Kijiji walihamasisha wanakijiji kushiriki katika shughuli mbalimbali kwa mfumo wa jitihada za Jamii. Kamati ya kijiji ya masuala ya usafirishaji ilipewa jukumu la kusimamia kazi ya ujenzi. Viongozi wa vikundi vya mafundi wenyeji na mafundi wenyewe walishiriki katika ujenzi ambapo walijipatia stadi za teknolojia ya kazi za barabara kwa kutumia nguvukazi na utaalamu wa kujenga na kukarabati madaraja bembea. Wanakijiji toka vijiji vyote walishiriki katika ujenzi wa madaraja na maboresho ya njia zinazoelekea kwenye madaraja bembea kama vibarua na hawakulipwa. Afisa Mtendaji wa Kata aliwajibika katika kusaidia na kuratibu jitihada mbalimbali za vijiji katika kukamilisha mradi huu.

Halmashaauri ilitoa msaada wa utaalamu na ufundi kupitia timu yake ya mafundi na wahandisi kwa kutoa maelekezo kuhusu wigo na mahitaji ya kazi kama michoro, andiko la gharama (BOQ) na ufuatiliaji wa kitaalamu. Shughuli zote zilifanywa na jamii yenyewe; wakandarasi hawakutumika.

**6.0 MATOKEO**

Jitihada hii pekee ya wanakijiji ilileta matokeo ya aina mbalimbali. Madaraja bembea yamejengwa na kukamilika katika vijiji husika na kuondoa madaraja bembea ya zamani ya miguu ambayo yalikuwa na hatari. Madaraja bembea 16 yalijengwa katika kipindi cha mwaka 2005 na 2010 na wananchi kwa usaidizi wa Halmashauri. Madaraja haya yanajumuisha daraja la Mapadre katika eneo la Kamsamba. Njia na barabara za jamii zimeboreshwa na zinatoa huduma bora ya usafirishaji wa mizigo ya mazao ya kilimo kutoka mashambani na katika kaya kwenda kwenye masoko kwa kusaidiwa na huduma za madaraja bembea.



***Daraja Bembea la Kaonga***



***Daraja Bembea la Kamsamba***

Madaraja haya 16 yameboresha sana mawasiliano na usafirishaji. Wakati muda wa kuvuka mito umepungua mpaka dakika tano kutoka masaa sita ya zamani, wanakijiji wana furaha ya kuwatembelea Marafiki na ndugu katika pande zote za mto na tambarare. Hili limeboresha mahusiano na mardhiano kati ya wakazi. Badiliko jingine dhahiri ni maboresho na ufanisi kwa watu kuzifikia huduma za jamii na hasa afya. Watu sasa wanaweza kusafiri kutoka Kijiji cha Kaonga kwenda Zahanati ya Chilulumo kujipatia huduma za afya. Maboresho katika upatikanaji wa huduma za afya kumepelekea kupungua kwa viwango vya vifo vya akina mama na watoto kwa sababu akina mama na watoto wanahudhuria kliniki kwa muda, na kujidhihirisha katika maboresho ya jumla ya hali ya afya katika jamii zinazotumia madaraja haya. Katika huduma za elimu madaraja yanahudumia wanafunzi wengi. Kwa mfano, Februari mwaka 2016, wanafunzi 23 kutoka Kijiji cha Kaonga walikuwa wakihudhuria masomo katika Shule ya Sekondari ya Mkulwe iliyopo 15km kutoka lilipojengwa daraja bembea.

Kabla ya matumizi ya madaraja bembea watu wachache (1-3) ndio walioweza kupanda ngalawa kwa safari moja. Sasa, kati ya watu 10-20 wanaweza kuvuka mto kwa mara moja kupitia daraja bembea. Mojawapo ya tokeo la wazi ni kupungua kwa matumizi ya ngalawa kuvusha watu kwenye mito. Kupotea kwa ngalawa kumepunguza vifo vya wasafiri kutoka sita hadi sifuri. Uvamizi wa mamba ambao nao ulikithiri sana umeshasahaulika.

Daraja bembea la Kaonga limeboresha upatikanaji wa huduma za kijamii, kiutamaduni na kiuchumi, hasa huduma za soko la kati liliopo katika kijiji cha Chilulumo na huduma za utawala katika ngazi za Vijiji, Kata, na Halmashauri. Pia, wanakijiji wa Mnyuzi wanafurahia maji safi na salama. Mradi wa maji katika kijiji cha Mnyuzi ulitekelezwa msimu wa masika. Kuvusha vifaa vya ujenzi kulifanyika kupitia daraja bembea. Huduma za kilimo pia zimeimarika kwani eneo hili na kata za jirani zimeshuhudia kuongezeka kwa mazao ya kilimo. Uzalishaji wa mpunga na mazao mengine kama mahindi umeongezeka katika ngazi ya kaya kutoka tani 1 kwa hekta hadi tani 2.2 kwa hekta kutokana na hamasa ya kulima mpunga inayotokana na maboresho ya usafirishaji kwenda kwenye masoko na barabara kuu mjini Vwawa. Kuongezeka kwa uzalishaji na urahisi wa kufika kwenye masoko moja kwa moja kumeleta ongezeko la pato kwa wanavijiji ambalo limebadili viwango vya kuishi kwa kujenga nyumba bora zilizoezekwa kwa bati, matumizi ya pikipiki na kulipa ada za watoto wao wanaoendelea na Shule za Sekondari na Elimu ya Juu.

Kuiga teknolojia kumefanyika kikamilifu; teknolojia ya ujenzi wa madaraja bembea imepanuliwa na kutumiwa katika maeneo mengine, ambapo madaraja bembea yamejengwa katika Kata za Chitete, Msangano, Chilulumo na Nzoka. Katika Kata na Vijiji hivi, makundi ya mafundi wanaoweza kujenga madaraja bembea, kuyakarabati na kuboresha barabara wanapatikana kwa urahisi na kwa gharama nafuu.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Kama ilivyo kwa miundombinu mingine, madaraja bembea pia huchakaa na kuhitaji matengenezo ya mara kwa mara. Kata na vjiji katika H/W ya Momba zimeweka mikakati kuhakikisha madaraja bembea yanatoa hudumu kwa miaka mingi mpaka hapo Serikali itakapokuwa na uwezo wa kujenga madaraja ya kudumu. Mkakati wa kwanza mkuu ni; kamati za ujenzi wa madaraja za vijiji zilizo na watu sita kwa uwakilishi sawa kati ya wanawake na wanaume zimeanzishwa katika vijiji vya Kaonga na Tontela ili kutunza miundombinu ya usafirishaji ikiwa ni pamoja na madaraja bembea (kiteputepu). Jukumu kuu la kamati limelenga zaidi kuendelea kuunganisha nguvu za jamii kipindi cha matengenezo ya madaraja endapo panatokea uharibifu wowote ili kuwepo kwa uendelevu wa huduma za madaraja. Mkakati wa pili uliopo ni kuhakikisha kuwa stadi walizojifunza mafundi wa kijijini zinaunganishwa na kutumika katika tathmini za mara kwa mara za madaraja na kutoa taarifa haraka kwa viongozi wa vijiji endapo kuna ulazima wa matengenezo. Mwisho, Halmashauri inazitia hamasa jitihada pekee za jamii kwa kuzisaidia kiufundi na kifedha pale ambapo fedha zinapatikana.

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

H/W ya Momba ilifanikiwa kufikia malengo ya kujenga madaraja bembea kwa sababu ya mambo mengi ya msingi. Kiuhalisia, hitaji la kuvuka mito kwa usalama na haraka lilikuwa hitaji lililotambuliwa na jamii zote zinazoishi na kufaidika kutokana na mito. Wanavijiji wote waliamini kuwa maendeleo yao yalikabiliwa na ugumu wa kuvuka mito kwa haraka kuyafikia masoko, huduma na mapumziko. Halmashauri za vijiji zilipoanza kundaa mipango ya ujenzi wa madaraja bembea wananchi wote walikubalina na mpango huo. Sababu ya pili ni matumizi bora ya ushiriki wa jamii kupitia Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD) wakati wa kupanga na kutekeleza miradi. Mfumo huu huunganisha jamii na hurahisisha uelewa wa pamoja wa fursa na vikwazo vya maendeleo vilivyopo.

Katika H/W ya Momba watu wanaishi kwa mujibu wa kabila, koo na makazi ambayo yana uongozi wa kimila. Ushawishi wa viongozi wa kimila kama machifu na watu wengine mashuhuri katika ngazi ya vijiji ulirahisisha sana kufanya maamuzi na kushiriki katika ujenzi wa madaraja bembea na ukarabati wao. Pia imani katika jitihada za jamii kupambana na matatizo, inayoenziwa na jamii hizi kwa miaka mingi ilichangia sana kuwepo kwa urahisi wa nguvukazi toka kila kijiji. Shughuli zote zilifanyika katika mfumo wa jitihada za jamii. Halmashauri za Vijiji mara chache ziliwalipa mafundi wenyeji tu kama sehemu ya motisha. Siri nyingine ni kuiga utaalamu na teknolojia ya ujenzi wa madaraja bembea kutoka kwa Kanisa Katoliki lililopo jirani na ushirikiano bora na kusaidiana kati ya jamii na Halmashauri.

# SEKRETARIETI YA MKOA WA MBEYA

**JITIHADA YA MARAFIKI WA HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA MBEYA**




***UJENZI WA NJIA ZA NDANI YA HOSPITALI***

**1.0 UTANGULIZI**

Mkoa wa Mbeya unapatikana Kusini Magaharibi mwa Tanzania bara, maarufu sana kama nyanda za juu za kusini ukipakana na mikoa minne ya Rukwa, Tabora, Iringa na Ruvuma. Mkoa huu upo katika Latitudo $70^0$ and $90^0$31 kusini na longitudo $32^0$ and $35^0$ Mashariki. Mwaka 2015 Mkoa wa Mbeya uligawanywa na kuwa mikoa miwili ya Mbeya na Songwe. Mkoa mpya wa Mbeya hupakana na Jamhuri za Malawi na Zambia upande wa Kusini, Mkoa wa Songwe Magharibi, Mikoa ya Singida na Tabora upande wa Kaskazini, na Mikoa ya Iringa na Njombe upande wa Mashariki na Kasumulu iliyopo Wilaya ya Kyela ikiwa ndio mlango mkuu wa kuingia na kutoka nchi jirani ya Malawi.

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya ipo katika eneo la Forest Jijini Mbeya ikiwa na namba ya usajili 052. Idadi ya watu waliopo katika eneo la huduma ya Hospitali ni 2,932,685 lenye ongezeko la watu la 2.7% kiwango cha uzazi cha 6.1%. Hospitali inahudumua wagonjwa kati ya 164 hadi 400 kwa siku katika vyumba vya wagonjwa wa nje, idara za macho, meno, huduma za afya ya uzazi na mtoto, mazoezi, ustawi wa jamii, mifupa, mionzi na huduma za ushauri na upimaji wa VVU. Hospitali ina uwezo wa vitanda 145. Hospitali inatoa huduma kwa Halmashauri zote za Mikoa ya Mbeya na Songwe ambazo ni Jiji la Mbeya, H/W za Mbeya, Kyela, Busokelo, Rungwe, Mbozi. Momba, Chunya, Ileje, Mbarali na Mji wa Tunduma. Ujenzi wa Hospitali hii ulianza mwaka 1988 na ilianza kufanya kazi kama ofisi ya afya ya mkoa tangu 1990. Mwaka 2002 ilianza kutoa huduma za wagonjwa wa nje na Januari 2010 ikaanza kutoa huduma za wagonjwa wa kulazwa, madawa na upasuaji.

*Marafiki* wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya ni kikundi cha kijamii cha hiari ambacho kilianzishwa mwaka 2014. Kundi hili lina wajumbe wenye kazi na taaluma mbalimbali kama wanasheria, wakandarasi, wachora ramani, wahandisi, madaktari, wauguzi, watawala, walimu, wafanyabiashara, wahadhiri, wahasibu nk. Mchanganyiko huu wa wataalamu ulileta mafaniko makubwa katika lengo kuu la *Marafiki.* Wengi wao wanaishi na kufanya kazi mkoani Mbeya na wachache wapo Dar es Salaam. Lengo la msingi la kundi hili ni kusaidia maboresho ya miundombinu ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya. Mwanzoni kundi hili lilichagua kujenga njia za ndani ya hospitali ambazo hazikuwepo kabisa.

**2.0 TATIZO**

Mpaka katikati ya mwaka 2014, Hospitali haikuwa na njia za kuunganisha idara mbalimbali kama jengo la wagonjwa wa nje, wazazi na huduma za afya ya uzazi na mtoto na majengo ya Maabara na Mionzi, Stoo, Wadi za wanawake na wanaume, wadi za watoto na Jengo la kuhifadhia maiti. Hali hii ililazimisha wauguzi na ndugu za wagonjwa kuwabeba wagonjwa mahututi migongoni na mikononi badala ya kuwekwa kwenye machela na viti vya matairi kusogezwa kutoka idara moja kwenda nyingine kwa sababu ya ukosefu wa njia za ndani ya hospitali. Hali ilikuwa mbaya zaidi msimu wa mvua ikizingatiwa kuwa Mkoa wa Mbeya huwa na mvua nyingi na za muda mrefu. Ardhi iliyopo katika eneo la hospitali ni ya mwinuko mkali ulio na udongo unaoteleza sana kipindi cha mvua na wenye vumbi sana msimu wa kiangazi. Kukosekana kwa njia za ndani katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya kulisababisha matatizo mengi katika utoaji wa huduma za tiba na upasuaji yaliyojidhihirisha katika sura mbalimbali.

Ardhi yenye milima wima iliwaongezea maumivu wagonjwa walipobebwa kutoka idara moja kwenda nyingine na hasa kutoka chumba cha upasuaji kwenda kwenye wadi au kutoka vyumba vya wagonjwa wa nje kwenda maabara na katika wadi. Ilikuwa inachosha sana kwa wauguzi na watumishi wengine wa tiba kubeba wagonjwa wenye hali mbaya kutoka idara moja hadi nyingine kwa sababu viti na vitanda vyenye matairi havingeweza kutumika katika udongo wenye mawe, miamba, changarawe, vumbi na tope. Hali hii ilileta changamoto hatari ya kuambukizwa magonjwa kutoka kwa wagonjwa wenye maradhi ya kuambukiza kwenda kwa wauguzi, watumishi wa tiba na ndugu. Hatari hii pia ilihusisha uwezekano mkubwa wa kumwangusha mgonjwa aliyebebwa kwa mikono au mgongoni mwa watumishi au ndugu.

Eneo la Hospitali pia lilikosa mifumo ya kutolea maji ya mvua, kufanya maji kutapakaa hovyo na kuchimba makorongo na mashimo. Kwa ujumla changamoto na hatari hizi zilipelekea ucheleweshaji wa kutoa huduma za tiba zinazotolewa na wataalamu wabobezi na changamoto kubwa katika usafi na mandhari ya mazingira ya hospitali



***Mgojwa akibebwa na ndugu mwanamke kutoka idara ya wagonjwa wa nje kwenda wadi ya wanawake***

Hali hii iliifanya Hospitali kukosa sifa za Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, kufanya mazingira ya kazi yasiyo rafiki na kupelekea kuporomoka kwa huduma za tiba. Kwa kuzingatia hali hii kundi la *Marafiki* liliona umuhimu wa kuingilia kati kuondoa tatizo.

**3.0 LENGO**

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya na Secretarieti ya Mkoa kwa kushirikiana na Kundi la *Marafiki*, kwa ujumla walilenga kuboresha utoaji wa huduma za tiba na upasuaji katika mkoa wa Mbeya. Mahsusi kabisa, jitihada hii ililenga ujenzi wa njia kuunganisha idara zote za hospitali, kupunguza mzigo wa kubeba wagonjwa mgongoni na mikononi mwa wauguzi na ndugu, kuwezesha matumizi ya machela na viti vyenye matairi ili viweze kubeba na kuvusha wagonjwa kuelekea idara mbalimbali, kupunguza uwezekano wa kuambukizana maradhi kutokana na kugusana na wagonjwa na kuboresha mazingira kwa kujenga kingo za bustani, mifereji ya kuongoza maji ya mvua na mifumo ya maji taka. Maboresho haya kwa ujumla yalilenga kuboresha mazingira ya kufanya kazi kwa watumishi wa hospitali na kuwaongezea motisha.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Njia za ndani za Hospitali ni mindombinu muhimu iliyo katika hali ambayo huruhusu kuhamisha wagonjwa bila kunyeshewa na mvua kuelekea kwenye magari ya wagonjwa, huwa na faida za kuwakinga wagonjwa na hali ya hewa mbaya wakishuka kwenye magari, kwenye foleni au wakisubiri kuingia katika majengo ya hospitali, na kuwezesha mizunguko salama kati ya majengo ya hospitali na idara zake. Thamani inayoongoza ya njia za hospitali ni ubebaji wa wagonjwa kwa viti na machela zenye matairi. Kutatua changamoto ambazo zimetajwa kwenye sehemu iliyopita, Secretarieti ya Mkoa na Kundi la *Marafiki* wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya walipanga na kutekeleza mikakati kadhaa iliyofafanuliwa hapa chini.

Kuanisha Hitaji; Sekretarieti ya Mkoa na Kundi la *Marafiki* walitambua hitaji la kujenga njia za ndani ya hospitali. Wagonjwa na kundi la *Marafiki* pia waliona matatizo yaliyokabili mizunguko ya watumishi na wagonjwa ndani ya eneo la hospitali. Hitaji hili ambalo wadau wote waliliona lilihitaji suluhisho; lakini upungufu wa raslimali kwa upande wa Serikali ulifanya utekelezaji kuwa mgumu; hivyo kuhitaji ushiriki wa wadau mbalimbali.

Ushawishi na Uratibu wa Wadau; katikati ya mwaka 2014, Muuguzi Msaidizi mmoja (Anna Danie Sanga) alishuhudia matatizo yaliyotokana na ukosefu wa njia za ndani ya hospitali na kwa huruma aliona umuhimu wa kushawishi na kuongoza jitihada ya kujenga njia za ndani ya hospitali. Hivyo, Muuguzi huyu alileta wazo la kuboresha miundombinu ya hospitali kwa kuliwasilisha katika kikao cha Timu ya Mkoa ya Menejimenti ya Afya.

**Sanduku 1. Mwanzo (Hadithi ya Anna)**

*Tarehe 31 Desemba 2013, Anna (Muuguzi Msaidizi) alimhudumia mgonjwa katika jengo la wazazi ambapo aligundua kuwa paa la wadi ya wazazi lilikuwa linavuja na kusababisha usumbufu kwa wagonjwa na watumishi wa afya. Hali hii ilimfanya ajisikie huruma na kuamua kufanya jambo kwa ajili ya Hospitali ili kupunguza matatizo (ukarabati wa wadi wa wazazi na ujenzi wa njia). Siku hiyo hiyo alimshirikisha tatizo hili mume wake ambaye naye alipata huruma. Mume wake alimshauri kutafuta marafiki wa hospitali katika jamii ili kuwashirikisha changamoto za hospitali zilizopo na kutafuta suluhisho sahihi. Wakati huohuo, Anna na mume wake waliamua kuchangia TZS 3m kwa ajili ya ukarabati wa paa la wadi ya wazazi na ujenzi ulianza mara moja. Kuanzia tarehe 2 hadi 11 januari 2014 paa la wadi ya wazazi lilikamilika.*

Kuushirikisha utawala wazo la kujenga njia za ndani ya Hospitali; siku ya Januari 1 mwaka 2014, Muuguzi Anna aliushirikisha utawala wa Hospitali (Katibu na Mama Mlezi) hisia zake na kupendekeza wazo la kujenga njia za ndani ya hospitali; nao walikubalina na wazo hili. Katibu na mama mlezi walipeleka pendekezo hili kwa Timu ya Menejimenti ya Afya ya Mkoa (RHMT) ambapo pendekezo lilikubalika sawia. Menejimenti iliahidi kutoa ushirikiano timilifu katika jitihada hii.

Muungano na uratibu wa wadau; kufuatia kukubalika kwa pendekezo hili na menejimenti ya hospitali, Muuguzi Anna alichukua jukumu la kuwashirikisha Marafiki zake. Kufanikisha hili, aliandaa barua za mwaliko kwa Marafiki zake wa karibu na watu wengine maarufu Jijini Mbeya kwa kutumia vigezo vifuatavyo;

(i) Mtu mwenye roho njema na huruma.
(ii) Mtu ambaye huhisi matatizo ya wengine na kwa hiari hujitolea kuyatatua.
(iii) Mtu ambaye yupo tayari kutumia muda kwa ajili ya wengine.
(iv) Mtu anayeweza kutoa raslimali bila kuhesabu ni kiasi gani au mara ngapi ametoa.
(v) Mtu ambaye ni mkarimu na yupo tayari kusaidia wengine wenye uhitaji.
(vi) Mtu awaye na furaha wengine wakiwa na furaha.
(vii) Mtu ambaye yupo tayari kuwezesha mikutano bila kutarajia faida binafsi.

Kuendesha mkutano wa wadau; mkutano wa kwanza ulifanyika Januari 11 mwaka 2014 katika ukumbi wa mikutano wa hospitali na waalikwa 22 walishiriki. Mwenyeji wa Mkutano alikuwa Mganga Mkuu wa Mkoa (RMO) na Bodi ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya. Mganga mkuu wa mkoa aliwatembeza washiriki katika maeneo ya hospitali kuwaonesha hali halisi kuhusu njia, ardhi, bustani na mifumo ya kutolea maji. Washiriki walijionea mapungufu yaliyokuwepo katika miundombinu ya hospitali na mwishoni kukubalina kuunganisha nguvu kusaidia uboreshaji wa hospitali kupitia mfumo wa timu. Waliamua kuunda chama cha hiari kwa kuzingatia makubaliano ya pamoja na kukiita chama chao "*Marafiki wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mbeya".* Maelezo haya yanafafanua jinsi kundi la Marafiki wa hospitali ya rufaa ya mkoa wa Mbeya lilivyoanza. Katika mkutano huu masuala mengi yalianzishwa, kujadiliwa na kukubaliwa. Nayo ni:

(i) Pendekezo na upitishaji wa jina linalokubalika la kikundi; Kamati ya Marafiki wa Hospital ya Mkoa wa Mbeya. Picha hii hapa chini inaonesha baadhi ya wajumbe wa kundi la Marafiki.



***Baadhi ya wajumbe wa Kundi la Marafiki wa Hospitali***

(ii) Uchaguzi wa uongozi wa Kundi; mkutano ulifanya uchaguzi wa Mwenyekiti, Makamu mwenyekiti, katibu, Naibu Katibu, Mweka Hazina na Naibu Mweka Hazina.

(iii) Ujenzi wa njia za ndani ya hospitalini ulipewa kipaumbele cha kwanza na Kundi la *Marafiki*.

(iv) Mbinu za upatikanaji wa fedha na raslimali nyingine zilipendekezwa. Kwa mfano michango binafsi kwa fedha taslimu, raslimaliwatu kulingana na utaalamu wao, nguvukazi, vifaa vya ujenzi nk.

(v) Ukusanyaji wa fedha kwa kuendesha harambee; harambee ya kwanza ilipangwa kufanyika tarehe 6 Machi, 2014. Wazo la Kundi la Marafiki kuhusu ujenzi wa njia za ndani ya hospitali nakufanya harambee ili kupata fedha liliwasilishwa kwa Mkuu wa Mkoa na kupata jibu chanya. Ilipendekezwa kuwa mgeni rasmi wa harambee hii awe Mkuu wa Mkoa wa Mbeya.

(vi) Wajumbe wa Kundi la *Marafiki* walikubaliana kufungua akaunti katika benki ya CRDB na M-Pesa account ya kundi la *Marafiki* ili kurahisisha ukusanyaji wa fedha. Akaunti ya Marafiki ilifunguliwa katika benki ya CRDB na kuitwa Marafiki wa Hospitali ya Mkoa, No. 0150067027600 na akaunti ya M-pesa yenye namba 0762321829 ikiitwa Marafiki Mkoa.

(vii) Ilikubalika kuwa fedha zinazokusanywa zitumike moja kwa moja kwenye ujenzi wa njia za ndani ya hospitali na siyo vinginevyo (kama posho na vikao na viburudisho).

Ukusanyaji wa fedha; mbinu kuu tatu zilitumika kukusanya fedha za ujenzi wa njia za ndani ya hospitali. Michango binafsi ya wanachama wa Marafiki; kabla ya tukio la harambee, Marafiki waliweka lengo la kukusanya TZS 20m. Pili, makusanyo kupitia M-pesa; matangazo kuhusu ujenzi wa njia na michango ya fedha ya hiari kupitia M-pesa yalitolewa kwa umma kupitia radio, vipeperushi na spika. Mwisho, kufanyika kwa matukio matatu ya Harambee; Harambee ya Kwanza ya Mrafiki ilifanyika machi 6, 2014. Harambee nyingine zilfanyika katika H/W ya Momba na Jiji la Mbeya.

Ujenzi wa njia za ndani ya hospitali; shughuli za ujenzi zilianza na upimaji ili kuandaa ramani kuu ambayo ilifanywa na wataalamu Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (MUST) wa Kundi la Marafiki bila malipo. Ujenzi halisi uligawanywa katika awamu tatu ili kukamilisha meta 411 za njia; awamu ya kwanza ilihusu meta 155 ambayo ilianza Mei 25, 2014 na ilizinduliwa rasmi na Katibu Tawala wa Mkoa kwa kukabidhi eneo la ujenzi kwa mkandarasi, tayari kwa ujenzi. Ujenzi ulifanywa na mkandarasi ambaye ni mwanachama wa Marafiki bila malipo akitumia vibarua wake. Awamu ya pili ilihusu meta 101 na awamu ya tatu meta 155 za njia. Awamu mbili (meta 256) zilitumia jumla ta TZS 83m.



***Makabidhiano ya Shughuli za Ujenzi kwa Mkandarasi***



***Ujenzi wa Njia Ukiendelea***

## 5.0 RASLIMALI

Jitihada za Ujenzi ni ghali. Uamuzi wa Kundi la Marafiki ni wa pekee kwani hospitali za mikoa zinaendeshwa na Serikali Kuu na siyo Serikali za Mitaa ambapo ushirki wa jamii na wadau unatarajiwa sana. Lakini Kundi la Marafiki waliweka azimio la kujipanga, kukusanya raslimali na kujenga njia za ndani za hospitali na miundombinu mingine kama hii. Raslimali fedha na vifaa zilizotumika katika ujenzi katika hatua za mwanzo na wakati wa kuandikwa kitabu hiki zilikuwa kama ifuatavyo:

- (i) Jumla ya TZS 83m zilikusanywa kwa ajili ya ujenzi wa njia awamu ya kwanza na ya pili. Kundi la Marafiki lilichangia TZS 54m na wadau wengine kama watu binafsi, benki, makampuni, ofisi ya Mkuu wa Mkoa na taasisi nyingine za serikali zilichangia TZS 29m.
- (ii) Licha ya raslimali fedha wadau wengine walichangia mifuko 70 ya saruji.
- (iii) Utaalamu katika kupima na kuandaa ramani kuu kulikofanywa na Chuo Kikuu cha Sayansi na Technolojia bila malipo, gharama yake ni TZS 9,460,000 kama ingelipwa.
- (iv) Mkandarasi alitumia vibarua bila malipo, gharama yake ni TZS 21,500,000 kama ingelipwa.

## 6.0 MATOKEO

Wageni na wagonjwa ambao waliifahamu hospitali hii kabla mwaka 2014 sasa wanashangazwa na mabadiliko makuu hasa uzuri unaotokana na ujenzi wa njia na miundombinu husika. Jitihada ya kujenga njia za ndani ya hospitali zilitokana na huruma kwa wagonjwa waliokuwa wakibebwa mikononi na migongoni na watumishi wa hospitali au ndugu kutoka idara moja kwenda nyingine. Jitihada hii imeleta matokeo mbalimbali kwa Hospitali, Wagonjwa na Kundi la Marafiki.

Uwepo wa Kundi la Marafiki wa Hospitali; Kundi la Marafiki lenye wanachama 22 ni kikundi cha watu wenye hiari na huruma, wanaogushwa na mateso ya wagonjwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya, wenye nia ya kutia motisha watumishi wa hospitali, wenye hamasa ya kuboresha mazingira na uzuri wa hospitali; limesajiliwa rasmi na BRELLA kama "*Marafiki Social Development Initiatives*". Lengo kuu na shughuli za kundi hili huruma za kibinadamu zimeelekezwa katika maboresho ya miundombinu, hasa njia za Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya.

Paa la Wadi ya wazazi limekarabatiwa na njia zimejengwa; Hospitali ilikuwa na wadi ya wazazi iliyochakaa sana na ilikuwa ikivuja na kufanya maisha ya wagonjwa na watumishi kuwa si ya kiafya. Kwa wagonjwa wengine kwenda kwenye hospitali hii ilionekana kwenda sehemu ambayo si salama. Hali hii imebadilishwa

kwa kuboreshwa kwa paa. Kundi la Marafiki ndilo limewezesha na kufadhili ujenzi wa njia za ndani ya hospitali. Jumla ya meta 256 za njia zimejengwa kuunganisha wadi ya wazazi na idara za wagonjwa wan je, Maabara, Mionzi, huduma za upimaji na ushauri, wadi za wanaume, wanawake na watoto na kufanya uvushaji wa wagonjwa kuwa mwepesi na wa raha. Mgonjwa mmoja aliyehojiwa alikuwa na haya ya kusema *" ……….ni kweli, hospitali hii imeboreshwa sana, nilipokuja hapa mwaka 2012, nilikuwa naumwa sana, na sikuweza kutembea, wauguzi na mjomba wangu ilibidi wanibebe mikononi mwao, nilipata maumivu sana, na kidogo tuanguke wote, kwani nilikuwa mzito sana………nilipokuja wiki hii nilibebwa kwenye machela na kuzungushwa kila mahali hospitalini hapa, OPD, chumba cha mionzi, wadi………haya ni maajabu, ina raha sana……..hospitali imebadilika sana, imekuwa nzuri sana……"*




***Njia za ndani ya Hospitali zikiunganisha idara mbalimbali***

Eneo la Hospitali limeboreshwa sana; hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya ilikuwa na changamoto ya mafuriko ya maji ya mvua na machafu. Kundi la Marafiki wakilenga katika kujenga njia za ndani ya hospitali waliona kuwa bila kuboresha mfumo wa kuondoa maji, njia hazitakuwa kamilifu na ingeweza kusababisha maji kuvuka njia za ndani ya hospitali na kuleta hatari za aina mbalimbali. Kwa sababu hii Mrafiki walichora na kujenga mfumo wa kutoa maji ya mvua sambamba na njia ili kuyaongoza maji kwenda nje ya eneo la hospitali. Michoro pia ilihusu uanzishaji wa bustani zilizopambwa za kisasa. Haya yote yameleta sura nzuri, ujani wa mazingira na mzunguko bora wa hewa.




***Mfereji wa maji ya mvua na bustani***

Maboresho ya mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa tiba; moja ya mafanikio makubwa ya jitihada hii ni maboresho ya mazingira ya kufanyia kazi. Urahisi wa kuhamisha wagonjwa, paa la wadi ya wazazi lisilovuja, watumishi kuzunguka toka idara moja hadi nyingine bila kukutana na usumbufu wa tope, vumbi au jua, utumiaji fanisi wa machela na viti vya matairi, bustani za kijani na mzunguko bora wa hewa, vyote vimechangia kuwepo kwa mazingira bora ya kufanyia kazi, watumishi wenye furaha, wagonjwa

walioridhika na menejimenti ya hospitali yenye motisha. Kwa kweli, hospitali imekuwa safi sana na eneo la kiafya ambavyo vimejenga imani ya kupokea huduma za afya zenye hadhi ya rufaa.




***Mtumishi wa Tiba akimsaidia kwa urahisi mgonjwa kutumia kiti cha matairi kwenye njia***

Jitihada ya Kundi la Marafiki ni ya pekee kwa sababu imejenga muungano imara kati ya makundi ya wasamaria wema na Serikali Kuu. Mikutano ya mara kwa mara na majadiliano vimeboresha mahusiano kati ya pande hizi mbili na kuashiria matumaini ya maboresho zaidi ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya. Hii ni jitihada ambayo umma unatakiwa kuiga kwani jitihada za pamoja katika utoaji wa huduma ni muhimu siyo tu katika ngazi ya Serikali za Mitaa bali katika ngazi ya Serikali Kuu.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Hospitali za Rufaa za Mikoa zina aina mseto za majengo. Kila hospitali inatarajiwa kuwa na wigo mpana wa huduma na idara. Hizi zinajumuisha shughuli za upimaji na tiba kama maabara, mionzi, vyumba vya dharura, na upasuaji; huduma za Ukarimu kama utoaji wa chakula na usafi; na huduma za kulaza wagonjwa kama utunzaji wa wagonjwa na vitanda. Kila moja ya shughuli hizi za hospitali zenye wigo mpana na zinazobadilika mara kwa mara, pamoja mifumo migumu ya kiufundi, umeme na mawasiliano, vyote vinahitaji elimu na utaalamu maalumu. Hakuna mtu hata mmoja anaweza kuwa na elimu ya kutosha kiasi hiki, ndiyo maana wataalam maalumu huwa na nafasi muhimu katika mipango na maandalizi ya Hospitali.

Idara za hospitali zinaweza kuwa na mahitaji na vipaumbele vinavyoshindana. Fikra tofauti na mapendekezo binafsi yanatakiwa kupimwa kulingana mahitaji ya lazima, mahitaji ya utendaji (mizunguko ya ndani na mahusiano na idara nyingine) na hali halisi ya kifedha ya taasisi. Kufikia hili Kundi la Marafiki wa Hospitali wana mipango ya kujiimarisha ili kuwa na wanachama wengi zaidi, ambao wapo tayari kuchangia zaidi kuifanya hospitali iwe Hospitali Mseto ya Kisasa. Kundi la Marafiki limelenga kuimarisha ushirikiano na kupanua wigo wa wadau kwa kualika watu wote wenye uwezo wanaotoka Mkoa wa Mbeya nchi nzima na nje ya nchi kuungana na Marafiki na kuchangia ili kuboresha njia na hospitali kwa ujumla. Kundi hili pia linaelekea kuendelea na matukio ya harambee ili kufikia mpango wao wa kukusanya TZS 150m za kukamilisha awamu ya 3 ya ujenzi wa njia kabla ya mwisho wa mwaka 2016. Mwisho, Kundi hili limeweka mkakati wa kuhakikisha kuwa ushirikiano na Serikali Kuu unaimarika zaidi na kuboreshwa ili kuifanya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya moja ya Hospitali ya hadhi ya pekee nchini.

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Ujenzi wa njia za ndani ya hospitali kwa kutumia michango ya watu binafsi si suala rahisi ikizingatiwa ugumu wa ushiriki wa jamii katika miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma hapa Tanzania. Ndio maana

kuna hoja kuwa jitihada hii ni ya pekee kwani kwa ujumla hospitali katika ngazi ya mkoa zinapatiwa fedha na Serikali Kuu tu. Hivyo, upekee wa jitihada hii unaanza katika siri fulani. Siri mojawapo ni utayari na kujitoa kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Timu ya Menejementi ya Afya ya Mkoa katika jitihada hii. Kama Mkuu wa Mkoa na Timu ya Menejimenti ya Afya ya Mkoa wasingekubali mwito wa wasamaria hawa, suala hili kubwa lisingefanyika.




***Uzinduzi wa Mradi uilofanywa na Mkuu wa Mkoa***

Siri ya pili imeegemea kwa Muuguzi Msaidizi Anna Sanga ambaye ni mwema, mtu wa kujitoa, msamaria na mwenye huruma. Akiwa mtumishi wa hospitali, mgonjwa na baadaye afisa tawala katika Sekeretarieti ya Mkoa, aliongoza machakato wa kuunda Kundi la Marafiki, kuanzia katika familia, Marafiki wa familia na kuwaunganisha kwa jamii pana.



***Muuguzi Msaidizi (Anna Sanga)***

Siri ya tatu ni uwepo, utayari, ari na kujitoa kwa Wanakikundi Marafiki wa Hospitali na kuunganisha nguvu katika kuboresha miundombinu ya Hospitali. Utayari huu na ushirikiano thabiti wa wadau mbalimbali pamoja na mpango kabambe wa utekelezaji wa mradi, vyote vilijengeka kuleta mafanikio bora.

# Sura ya Tatu: Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato

Ugatuaji wa Masuala ya Fedha Nchini Tanzania huzingatia MSM kuwa na vyanzo vyao vya mapato vya uhakika, kuwepo kwa mfumo bora wa kutoa na kupokea fedha toka Serikali Kuu, utoaji wa fedha za kutosha kwa ajili ya huduma zilizogatuliwa, kuongeza ukusanyaji wa mapato, kuhakikisha uwazi na usawa katika kutenga fedha na kuhakikisha usawa katika utoaji wa huduma (rejea sera ya maboresho ya serikali za mitaa ya 1998). Kimsingi, Ugatuaji wa masuala ya fedha kwa Tanzania hujumuisha yafuatayo;

(i) Mamlaka za Serikali za Mitaa hazitakiwi kupewa majukumu ambayo hayatengewi fedha,

(ii) Mfumo wa ruzuku lazima uzingatie utekelezaji wa sera (vipaumbele) za kitaifa kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa, na ambazo zitapatiwa fedha kwa ruzuku zenye masharti na kuongozwa na viwango vya chini vya kitaifa,

(iii) Mfumo wa ruzuku lazima uzihamasishe Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka vipaumbele vyao kupitia uanzishaji wa ruzuku ambazo hazina masharti na ruzuku za shughuli za maendeleo,

(iv) Ruzuku zisizo na masharti zitatolewa kwa utaratibu wa usawa na kwa kufidia Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye uwezo mdogo wa raslimali,

(v) Ukokotoaji wa ruzuku lazima ufanyike kwa kutumia mbinu yenye vigezo vya uhakika, haki na visivyo na upendeleo,

(vi) Ruzuku kutoka Wizara za kisekta lazima zipunguzwe kadri iwezekanavyo.

Uboreshaji wa Mapato ni ile hali ya MSM kutumia madaraka waliyopewa na Serikali Kuu kukusanya mapato na kutumia kulingana na vipaumbele vyao. Uboreshaji wa mapato hujumuisha shughuli kama utafutaji wa vyanzo vya mapato, upanuaji wa wigo wa mapato, uhamasishaji wa shughuli za kiuchumi zinazoongeza vyanzo vya mapato na utungaji wa sheria ndogo zinazoongoza ukusanyaji na utumiaji wa mapato.

Katika Sura hii, mbinu bora mbili kutoka Manispaa ya Kinondoni na H/W ya Tandahimba zimewasilishwa. Mbinu Bora ya Manispaa ya Kinondoni inahusu mfumo wa digitali wa ukusanyaji wa mapato. Kabla ya mwaka 2011 Manispaa ya Kinondoni ilishuhudia changamoto nyingi katika kutoa huduma kutokana na upungufu wa raslimali fedha. Kuondoa changamoto hizi, sehemu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) ya Manispaa ilipata wazo la kuanzisha mfumo wa digitali wa kukusanya mapato na kuliwasilisha kwa Timu ya Menejementi ya Halmashauri (CMT) mwaka 2012. Sehemu hii iliendelea kwa kuunda kazidata, kuboresha taarifa za majengo na kuainisha vyanzo vipya vya mapato na walipa kodi waliokuwa hawajafikiwa. Mkakati huu ulihitaji ufungaji wa mfumo wa digitali wa ukusanyaji mapato. Halmashauri ilunda vituo vya kulipia kodi na kuandaa programu kabambe ya kujenga uelewa wa walipa kodi kuhusu mfumo wa digitali. Kuunda mfumo wa digitali wa ukusanyaji mapato ili kukusanya mapato zaidi ulileta ajira ya watumishi wengi wa teknolojia ya habari na mawasiliano na kuongeza uwezo wa kutoa huduma za kiwango cha juu kwa umma.

Mbinu Bora ya H/W ya Tandahimba inahusu matumizi mkakati ya mapato ya ndani ili kushughulikia mahitaji ya jamii. Halmashauri imekuwa ikikusanya mapato ya kutosha kutoka ushuru wa Korosho kwa

sababu mfumo wake wa manunuzi umepangika na wa uhakika (stakabadhi ya mazao ghalani). Hatahivyo, kwa miaka mingi matumizi ya mapato yaliyotokana na chanzo hiki hayakutumika kimkakati kutoa huduma bora, za kisasa na endelevu ili kukidhi mahitaji ya wananchi. Kufikia lengo hili, Halmashauri iliamua kwa nguvu zote kutumia mapato yake ya ndani kimkakati. Suala hili lilihusu kuandaa mapendekezo na kutekeleza miradi ya ujenzi wa nyumba za watumishi, kumbi za mikutano, shule kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu na miradi ya maji pamoja na kuanzisha Benki ya Wananchi wa Tandahimba. Utekelezaji ulianza baada ya majadiliano na makubaliano katika ngazi zote za timu ya menejimenti kuhusu miradi yote, uchambuzi wa kina na kamati husika za Baraza na kupitishwa na Baraza la Madiwani.

Kwa kuwa ruzuku toka Serikali Kuu zinapungua na kudhibitiwa sana, MSM zinalazimika kuchangamka katika kutafuta mapato kutoka vyanzo mbadala misitu, ushuru wa kilimo na kodi za majengo. Uchambuzi wa mbinu bora katika sura hii unaonyesha kuwa:


(i) Kwa kufuata maelekezo ya sera ya Serikali Mtandao na maendeleo katika teknolojia, MSM zinalazimika kutumia mbinu za digitali na elektroniki kuboresha ukusanyaji wa mapato. Hii inahusu kuifanya michakato iwe ya kidigitali kama utambuzi wa vyanzo vya mapato, uandikishaji wa walipa kodi, ubosheraji wa sheria ndogo na utumiaji wa wakusanya mapato. MSM zinahitaji kutumia fursa za teknolojia zilizopo kama Mfumo wa Habari za Serikali za Mitaa wa Ukusanyaji wa Mapato (LGRCIS) unaotekelezwa na OR-TAMISEMI na kuongeza wigo wa vituo vya kukusanyia mapato (POS) katika vyanzo vyote vya mapato. Halmashauri zinatarajiwa kuunda ushirikiano na taasisi ambazo hutumia teknolojia za elektroniki katika usimamizi wa fedha ili kuwa na ukusanyaji wa mapato wa digitali. Taasisi hizi ni pamoja na benki na makampuni ya simu na teknolojia ya habari na mawasiliano.

(ii) MSM ni taasisi kamilifu za kisheria na zinazojiendesha. Katika hali hii na kwa kuzingatia upungufu wa raslimali toka serikali kuu, MSM zinatakiwa kujikita katika utafiti wa kuainisha vyanzo tajiri vya mapato na kuimarisha kilimo na shughuli za biashara zenye uzalishaji mkubwa wa mapato. MSM zinatakiwa kuwa makini na bunifu katika biashara ya ardhi na majengo ili kukusanya mapato zaidi na endelevu na kutumia mikakati ya kidigitali na kielektroniki kuboresha ukusanyaji wa mapato.

(iii) Mapato yanayokusanywa kutoka vyanzo vyote yanahitaji kutumiwa kwa umakini na kuelekezwa kwa walipa kodi ili kujenga uhalali wa kulipa kodi. MSM zinatakiwa kutoa huduma bora na fanisi kwa jamii zinazolipa kodi ili kuongeza utayari wa kulipa kodi na kuleta uendelevu katika mapato ya ndani.

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI


**MFUMO WA DIGITALI WA UKUSANYAJI MAPATO**



***UZOEFU WA MANISPAA YA KINONDONI***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ni mojawapo ya Halmashauri sita za Mkoa wa Dar es Salaam. Manipaa hii hupakana na Bahari ya Hindi upande wa Kaskazini Mashariki, Manispaa ya Ilala upande wa Kusini, H/W ya Bagamoyo upande wa Kaskazini, na Manispaa ya Ubungo upande wa Magharibi. Halmashauri imeunganishwa vema na Jiji na sehemu nyingine za Nchi kwa barabara na mitandao mingine ya mawasiliano. Halmashauri in eneo la 170.6 $km^2$ ikiwa na wakazi 954,632 (sensa ya 2012). Manispaa ya Kinondoni ina tarafa mbili za Kinondoni and Kawe, Kata 20 na Mitaa 112.




*Ramani ya Mkoa wa Dar es Salaam*

Kabla ya kugawanyika kwa Manispaa Maarufu ya Kinondoni, idadi ya wastani ya wakazi waliokuwa wameajiriwa katika sekta mbalimbali ilikuwa 741,155 (452,557 binafsi, 264,857 walijiajiri na 23,741 sekta ya umma). Wengi wa wakazi ni wafanya biashara ndogondogo, wauzaji katika huduma na maduka, mafundi, wavuvi, wafugaji na wakulima. 3% tu ya nguvukazi ilijihusisha na kilimo cha kujikimu pembezoni mwa Jiji kwa kuzalisha mbogamboga na mazao kama mhogo na viazi vitamu kwa ajili ya matumizi ya kaya na ziada kwa ajili ya kuongeza kipato.

Ukusanyaji wa mapato unaratibiwa na idara ya fedha katika sehemu ya mapato. Idara hii inawajibika kwa ukusanyaji wa mapato, matumizi, utunzaji wa mali za Halmashauri, kusaidia michakato ya uandaaji wa mipango na bajeti endelevu na kuandaa taarifa za fedha za Halmashauri kuwezesha maamuzi. Halmashauri ina vyanzo vikuu vitatu vya mapato, ambavyo ni vyanzo vya ndani, ruzuku na misaada toka Serikali Kuu, fedha za wafadhili na michango ya jamii. Msingi wa kodi unahusu vyanzo kama kodi ya majengo, mabango, tozo za soko na vizimba, ushuru wa huduma na ushuru wa nyumba za kulala wageni.

## 2.0 TATIZO

Ukusanyaji wa mapato ni muhimu sana kwa maisha ya taasisi yoyote hasa Serikali za Mitaa. Tasisi zote hukusanya mapato ili kukidhi majukumu yao ya kibajeti. Mafanikio katika ukusanyaji wa mapato humaanisha lengo kuu la taasisi lazima liwe wazi vya kutosha. Pale Halmashauri zinaposhindwa kukusanya mapato halali kiufanisi, umma utaathirika kwa kunyimwa huduma muhimu. Pia Serikali Kuu itazidiwa na madai ya fedha kutoka Halmashauri ambayo yataathiri uchumi wa nchi.

Kabla ya mwaka 2011 Manispaa ya Kinondoni ilipata changamoto nyingi katika kutimiza utoaji wa huduma kutokana na upungufu wa raslimali fedha. Hali hii ilizidi kuwa mbaya kutokana na mbinu duni za ukusanyaji wa mapato ambapo walipa kodi walilazimika kwenda makao makuu ya Halmashauri kufanya malipo ya kodi, mifumo mibaya ya usafiri, majengo yasioainishwa na kusajiliwa, mistari mirefu kwenye ulipaji kodi, uelewa ndogo wa walipa kodi, kukosekana kwa utamaduni wa kulipa kodi kwa hiari ndani ya muda na kutoibuliwa kwa vyanzo vingi vya mapato. Aina nyingi za kodi katika mapato ya ndani zilikusanywa kwa

ugumu na gharama kubwa; mojawapo ikiwa ushuru wa vizimba katika masoko ikizingatiwa kuwa viwango ni vya chini sana (TZS 100 hadi 200), na zinatakiwa kukusanywa kila siku. Pia ada za uchafu zilikusanywa kwa siku na viwango vya malipo vilitofautiana kulingana na aina ya uchafu uliozalishwa. Haya yote yalipelekea ukusanyaji duni wa mapato. Tatizo moja kubwa ilikuwa matumizi duni ya maendeleo ya tekonolojia ya habari na mawasiliano ambayo huruhusu shughuli mbalimbali za Halmashauri kufanywa kwa kutumia kompyuta, kielektroniki na kidigitali ikiwa ni pamoja na mifumo na michakato ya ukusanyaji mapato.



***Usafiri wa Shida na Mistari Mirefu***

Ukusanyaji wa mapato katika Manispaa ya Kinondoni ulikuwa duni sana na usiopangwa. Kwa kuwa vyanzo vilikuwa vimetawanyika na kutapakaa kulingana na shuguli za kiuchumi za wananchi na utumiaji wa risiti za kuandika kwa mkono zilizotolewa na wakusanyaji wa mapato, kulikuwa na upotevu mkubwa wa mapato, uvujaji wa fedha, utoaji taarifa usiofaa na utayari duni wa walipa kodi; vyote vilipelekea ukusanyaji wa mapato wa chini sana wa Halmashauri. Jedwali lililopo hapa chini linaonyesha hali hii mbaya kwa miaka ya 2011 hadi 2015.

**Jedwali 1: Mtiririko wa Makusanyo**

| Na. | Chanzo | 2011/2012 | 2012/2013 | 2013/2014 | 2014/2015 |
|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Ushuru wa huduma | 7,984,442,588.92 | 8,984,045,082.00 | 13,542,200,927.00 | 15,669,184,818.43 |
| **2** | Kodi ya Majengo | 2,181,870,324.19 | 1,804,476,750.00 | 3,585,710.201.00 | 6,350,664,500.97 |
| **3** | Matangazo | 1,752,695,069.74 | 2,144,100,784.00 | 2,286,475,672.00 | 2,009,863,703.49 |
| **4** | Michango | 1,782,836,112.00 | 2,142,650,098.00 | 2,142,650,098.00 | 3,293,388,861.79 |
| **5** | Leseni za biashara | | | 2,749,264,594.00 | 4,582,101,265.00 |
| **6** | Vyanzo vingine | 3,651,803,559.31 | 6,277,497,301.00 | 11,763,872,422.00 | 7,116,461,776.79 |
| | **Jumla** | **17,353,647,654.16** | **21,352,770,015.00** | **27,001,674,302.20** | **39,021,664,926.47** |

## 3.0 MALENGO

Hapa Tanzania Serikali za Mitaa zina jukumu la kukusanya baadhi ya mapato kutoka vyanzo kama kodi, ushuru na ada mbalimbali. Serikali za Mitaa pia zimeruhusiwa kuanzisha sera zao za mapato ndani ya mipaka iliyowekwa na Serikali Kuu. MSM zinabaki na mapato yao yote na kutumia kama sehemu ya bajeti zao na kimsingi mapato haya si sehemu ya mapato ya Serikali Kuu. Kodi, ushuru, ada na vyanzo vya mapato ambavyo Serikali za Mitaa zimepewa uhuru wa kukusanya chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ni kodi za majengo, kodi za bidhaa na huduma, kodi katika huduma maalumu, leseni za bishara na utaalamu, leseni za vyombo vya moto, kodi za mauzo, kodi za mapato katika ujasiriamali na majengo, ada za utawala na tozo, faini na adhabu mbalimbali. Fursa hizi hazitumiwi kikamilifu na Serikali za Mitaa pale ambapo mifumo, taratibu na michakato ya ukusanyaji mapato ni ya kizamani.

Baada ya kugundua mapungufu katika mifumo ya ukusanyaji mapato na kufanya mapato kuwa duni na kusinyaa kwa utoaji huduma, Manispaa ya Kinondoni iliamua kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji mapato ambao ni wa kisasa, ulioboreshwa na ungekusanya vyanzo vyote, walipa kodi, wasimamizi na wakusanyaji wa kodi. Mahsusi kabisa, Manispaa ya Kinondoni ililenga kuanzisha kazidata ya kisasa, kidijitali na kijiografia na kuzidisha utumiaji wa tekonlojia ya mfumo wa habari wa kijiografia katika ukusanyaji wa mapato. Mwishoni, Halmashauri ililenga kuifanya mifumo ya ukusanyaji mapato kuwa ya digitali ili iweze kukusanya mapato kwa ufanisi, uwazi na uwajibikaji na kukusanya mapato ya uhakika zaidi yaliyoelekezwa katika kuongeza na kuboresha utoaji wa huduma ndani ya mipaka yake na umma kwa ujumla.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**


Serikali ya Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kuhimiza Serikali mtandao katika ngazi mbalimbali za Serikali tangu mwaka 2013 kupitia kwa Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Serikali mtandao ni kigezo muhimu cha kuharakisha michakato ya kazi, utoaji huduma kwa wananchi na biashara, kuongeza uwazi na uwajibikaji, na pia kupunguza gharama za uendeshaji. Kutokana na jitihada zilizofanywa na Serikali Kuu za kuhamasisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato, Manispaa ya Kinondoni ilichukua hatua mapema kuboresha mbinu zake za kodi na kuanza kutumia mfumo wa kieletroniki katika shughuli mbalimbali kama kuzalisha ankara, makusanyo ya malipo ya fedha taslimu, kutoa risiti, kitabu cha thamani kwa ajili ya kodi ya majengo na leseni za biashara.

Sehemu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya Manispaa ya (ICT section) ilianzisha wazo la kusimika mfumo wa kidigitali wa kukusanya mapato na kuliwasilisha katika Timu ya Menejimenti ya Manispaa. Timu ilijadili na kukubaliana na pendekezo ambalo mwishoni liliridhiwa na Baraza kwa ajili ya utekelezaji. Utekelezaji ulihusu uanzishaji wa kazidata, usimikaji wa mfumo wa kidigitali wa ukusanyaji mapato, kuongeza vituo vya kulipia kodi na ujenzi wa uelewa wa kutosha kwa walipa kodi na umma kwa ujumla.

Uanzishaji wa kazidata ulihusu kuboresha taarifa za majengo yote, vyanzo vipya na ambavyo havitumiki na walipa kodi. Baadhi ya vyanzo vipya vya mapato na ambavyo vilikuwa havitumiki ni pamoja na ada za usajili, tozo za maegesho ya bajaji, stendi za daladala, minara ya simu na ada za huduma za tiba. Hili lilifuatiwa na uthamini wa majengo wa marudio katika eneo lote la Manispaa. Mapitio ya viwango vya kodi za majengo ulifanyika kwa kufanya uthamini wa majengo ambayo hayakuthaminiwa na yale ambayo yalipewa thamani ya chini ikiwa ni pamoja na aina zote za majengo katika kiwanja au eneo lenye viwanja vilivyopimwa.

Mkakati huu pia ulihitaji ufungaji wa mfumo wa kidigitali wa ukusanyaji mapato. Suala hili lilihusu kuanzisha mfumo wa malipo mtandao ambapo mahitaji yote yalinunuliwa; yaani vifaa na mifumo. Vifaa hivi ni pamoja na seva, kompyuta, mifumo ya kuhifadhi kumbukumbu na vifaa vya mtandao wa ndani (LAN) ili kupata mtandao wa kimataifa. Kwa upande wa mifumo, Manispaa ilianzisha mfumo wake wa kuendesha ukusanyaji wa mapato uitwao *"Kinondoni Municipal Revenue Collection Manager"* kwa kifupi (KMRECOM).

Manispaa pia iliendesha zoezi la kuongeza vituo vya kulipia Kodi. Katika hili, Manispaa ilianzisha vituo na namna mpya za kulipa kodi kama matumizi ya simu za viganjani, vituo vya malipo vya kieletroniki (POS) na taasisi za fedha kama benki. Vituo vya malipo vya kieletroniki (POS) vilisimikwa katika ofisi za Kata, masoko, stendi za mabasi, hospitali, vituo vya afya na ofisi ya mweka hazina wa Manispaa. Usambazaji huu wa vituo vya kulipia kodi ulilenga kuwafikia walipa kodi katika meneo yao ya biashara na kuondoa misongamano iliyotawala ulipaji wa kodi na kuwapa motisha walipa kodi kulipa kwa wakati na mapema.




***Mfumo wa kidigitali wa ukusanyaji mapato***

Manispaa iliandaa programu kabambe ya kujenga uelewa kwa walipa kodi kuhusu mfumo wa kigitali wa ukusanyaji mapato. Ujenzi wa uelewa uliendeshwa kwa umma katika ngazi zote kupitia vyombo vya habari kama televisheni za umma, redio, magazeti na mitandao ya kijamii ikiwa ni pamoja na tovuti ya Manispaa, *www.kinondonimc.go.tz*. Viongozi wa kisiasa walihamasishwa kupitia mikutano ya Halmashauri kuhusu mfumo mpya kwa kutumia mifano halisi ya jinsi mfumo utakavyoongeza mapato kwa kuwafikia walipa kodi wengi zaidi popote pale walipo ndani ya Manispaa ikiwa ni pamoja na nje ya mkoa. Uelewa huu uliamsha elimu ya umuhimu wa kulipa kodi, nini kilipwe, kwa muda upi na wapi pa kufanyia malipo.

Kwa upande wa watumishi wa Manispaa, Halmashauri iliendesha mafunzo kwa watumishi kuhusu matumizi ya mfumo wa kidigitali wa ukusanyaji mapato. Mafunzo ya siku moja kwa watumishi yaliendeshwa na mkandarasi wa kusimika mfumo kuwajengea uwezo kuhusu matumizi ya mfumo. Mafunzo yalihudhuriwa pia na wakuu wa idara kukiwa na lengo la kujenga uwezo wao kufuatilia mchakato wa ukusanyaji mapato na kufanya usimamizi wa mara kwa mara wa wakusanyaji wa mapato na waendeshaji wa mfumo.

Jitihada ya ukusanyaji mapato ya Manispaa ya Kinondoni ilishirikisha aina mbalimbali za jumuia ya wadau. Hivyo, kutia saini ya hati ya makubaliano (MoU) na wadau mbalimbali lilikuwa suala muhimu ili kuelewa na kugawa majukumu kwa kila mdau. Kila mdau alipewa jukumu lake; kwa mfano Maxcom alipewa jukumu la kuunganisha na kuingiza kwenye mtandao vituo vyote vya ukusanyaji mapato wakati Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ulipewa jukumu la kukusanya ada za tiba katika Hospitali na Vituo vya Afya. Wadau wengine ni makampuni ya simu na benki mbalimbali.

Kuwezesha kuwa na mfumo wa kidigitali ili kuzalisha mapato zaidi na kupanua uwezo wa kutoa huduma za kisasa kwa umma, ilibidi kuajiri watumishi wa teknolojia ya habari na mawasiliano. Halmashauri iliajiri wataalamu 30 wa teknolojia ya habari na mawasiliano wa kudumu na wa muda ili kuendesha, kukarabari na kuboresha mfumo, ikiwa ni pamoja na kutoa msaada wa kitaalamu kwa watumishi wengine waliopo kwenye vituo vya ukusanyaji wa mapato (POS).

**5.0 RASLIMALI**

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ilitekeleza mapema sera ya taifa ya teknolojia ya habari na mawasiliano ya mwaka 2013 kwa kusimika mfumo wa kidigitali wa ukusanyaji na utumiaji wa mapato. Kuanzisha na kuusimika mfumo kulihusu shughuli na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na majadiliano

na taasisi za Serikali Kuu na Madiwani katika ngazi ya Halmashauri. Raslimali fedha zilizotumika zimeoneshwa katika jedwali hapa chini.

**Jedwali 2: Raslimali Fedha**


| Shughuli | Kiasi (TZS) |
|---|---|
| Kusimika na kuunganisha mfumo (KMRECOM) na usaidizi wa kimtandao wa miezi sita | 5,700,000/= |
| Mafunzo ya watumiaji (siku kumi) | 4,100,000/= |
| Kumpyuta zenye ubora wa juu (Server, ram 40GB & HDD 1TB) | 9,834,400/= |
| **Jumla** | **19,634,400/=** |

Manispaa pia ilitumia aina nyingine za raslimali. Hizi ni pamoja na seva, kompyuta, printa, karatasi, wino, mitandao ya ndani, samani na vifaa vya usafiri. Kuhusu raslimali watu, Manispaa ina kitengo cha teknolojia ya habari na mawasiliano chenye watumishi sita waliobobea wa kudumu na watumishi wa muda nane wanaoshughulika na uingizaji wa taarifa kwenye mfumo. Kitengo hiki hufanya kazi na idara zote na jukumu lake kubwa ni kuendesha mfumo na kutatua matatizo yote yanayokabili mfumo. Kuanzishwa kwa mfumo wa digitali wa ukusanyaji mapato ulichukua miezi mitatu kuanzia Agosti hadi Oktoba 2012; kuweza kuutumia kikamilifu na kuleta matokeo tarajiwa.

## 6.0 MATOKEO

Ukusanyaji wa mapato kidigitali una faida nyingi ikilinganishwa na mifumo isiyo ya digitali. Katika ngazi ya kitaifa majaribio ya mifumo ya malipo ya kidigitali yameonesha matokeo chanya katika mbinu za malipo. Kwa kufanya malipo kuwa ya kidigitali, Tanzania imewezesha sekta mbalimbali kupunguza upotevu wa fedha kutokana na malipo ya fedha taslimu. Pia imepunguza urasimu, ikiwa ni pamoja na udhaifu mwingine ulioambatana na malipo ya fedha taslimu kwa Serikali. Kwa upande wake, Manispaa ya Kinondoni imefanikiwa kupata matokeo mengi.

Tokeo moja muhimu ni uwepo wa mfumo wenyewe; mfumo wa digitali wa ukusanyaji mapato wa Manispaa ya Kinondoni (Kinondoni Municipal Revenue Collection Manager **-** KMRECOM) upo na unafanya kazi. Mfumo umeunganishwa na Idara za Manispaa, vituo vya malipo (POS), simu za kiganjani, benki, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), na Maxicom. Mfumo huu ni kwa ajili ya Manispaa ya Kinondoni tu na ni pekee nchini.




*Mfumo wa Digitali wa Ukusanyaji Mapato wa Manispaa ya Kinodoni*

Kwa sasa, Manispaa inajisifu kumiliki kazidata ya kweli, yenye uhakika, na fanisi ya kidigitali. Kazidata hii imejazwa taarifa na takwimu za majengo yote, vyanzo vya mapato, viwango vya malipo na walipakodi na hurahisisha uzalishaji wa taarifa, uchakataji na usambazaji wa taarifa za kodi, ada na tozo zinazotakiwa kukusanywa kutoka vyanzo mbalimbali. Pia kazidata hii hurahisisha kutambua na kuainisha vyanzo vinavyolipiwa na visivyolipiwa.




***Ukubwa wa Jengo, Mmiliki na Anuani***



***Bango***

Manispaa pia imekuwa na mfumo kamilifu wa habari za Kijiografia (GIS); yaani mfumo wa kompyuta unaosaidia Manispaa kukusanya, kuhifadhi, kukagua na kuonesha takwimu za mahali katika uso wa dunia kurahisisha utambuzi wa ardhi iliyopimwa, viwanja na majengo. Mfumo wa Kijiografia (GIS) wa Manispaa ya Kinondoni pia huonesha aina mbalimbali za ardhi iliyopimwa, viwanja na majengo katika ramani moja ya digitali. Hii husaidia Halmashauri kuchambua kwa urahisi na kufanya maamuzi kuhusu uzalishaji wa mapato. Uingizaji wa wamiliki wa viwanja kwa kutumia mfumo huu wa kijiografia (GIS) umewezesha kupatikana kwa taarifa zote za wamiliki wa ardhi.



Table

POINT PLOT

| FID | Shape * | X | Y | PLOT_NO |
|---|---|---|---|---|
| 0 | Point | 530583 | 9255006 | 585 |
| 1 | Point | 530615 | 9254978 | 873 |
| 2 | Point | 530594 | 9254961 | 874 |
| 3 | Point | 530557 | 9254987 | 587 |
| 4 | Point | 530531 | 9254956 | 589 |
| 5 | Point | 530580 | 9254939 | 875 |
| 6 | Point | 530556 | 9254911 | 876 |
| 7 | Point | 530481 | 9254897 | 877 |
| 8 | Point | 530536 | 9254890 | 878 |
| 9 | Point | 530515 | 9254869 | 880 |
| 10 | Point | 530500 | 9254845 | 883 |
| 11 | Point | 530433 | 9254836 | 881 |
| 12 | Point | 530414 | 9254808 | 882 |
| 13 | Point | 530387 | 9254777 | 888 |
| 14 | Point | 530352 | 9254736 | 892 |
| 15 | Point | 530426 | 9254757 | 887 |
| 16 | Point | 530408 | 9254730 | 889 |
| 17 | Point | 530390 | 9254705 | 891 |
| 18 | Point | 530371 | 9254680 | 893 |
| 19 | Point | 530335 | 9254706 | 894 |
| 20 | Point | 530332 | 9254633 | 897 |
| 21 | Point | 530261 | 9254625 | 958 |
| 22 | Point | 530308 | 9254604 | 957 |
| 23 | Point | 530195 | 9254526 | 1197 |
| 24 | Point | 530122 | 9254401 | 1205 |
| 25 | Point | 530101 | 9254372 | 1207 |
| 26 | Point | 530086 | 9254343 | 1209 |

(243124 out of 243140 Selected)

POINT PLOT


Table Of Contents | Table

***Taarifa za Kidigitali***

Manispaa imejihakikishia kuwa kila kituo cha malipo (POS) kina vifaa vya Maxmalipo vyenye bango lililounganishwa na KMRECOM kwa ajili ya kusafirisha miamala ya ukusanyaji mapato mara moja kwenda kwenye mfumo. Vituo vya malipo (POS) vilivyoanzishwa vipo katika Hospitali kama Mwananyamala na Sinza na kwenye Vituo vya Afya vya Magomeni na Kimara. Vifaa hivi vya kieletroniki (POS) pia vinatumika

kukusanya ada za upimaji wa afya na kodi za majengo. Manispaa pia imeanzisha POS mbili makao makuu, yaani benki ya CRDB na Maxmalipo.


**Kifaa cha Maxmalipo**


**Bango la Maxcom**



**Duka la Maxmalipo shop**



**Benki ya CRDB**

Manispaa ya Kinondoni imeunganisha Kata zote 34, maduka na walipakodi kwenye simu za kiganjani kama mfumo rahisi wa malipo. Kwa sasa wananchi wa Kinondoni wanaweza kulipa ada zao za hospitali, ankara na ushuru mbalimbali kielektroniki. Halmashauri imeweka mameneja katika vyanzo vyote vya mapato na kuwapatia magari ili kuwezesha usimamizi wa ukusanyaji mapato.



**Gari la Meneja wa Ukusanyaji Mapato**

Mfumo wa KIMRECOM unasaidia kufuatilia makusanyo katika vyanzo vyote, kuchakata taarifa za makusanyo, kufanya mlinganisho na benki na kuzalisha taarifa zote kuu za siku, wiki, mwezi, robo mwaka na mwaka. Wakuu wa Idara na mameneja walioidhinishwa wanaweza kuingia kwenye mfumo na kupata taarifa mbalimbali za ukusanyaji wa mapato popote pale wakiwa na mtandao. Kwa uwepo wa mfumo huu wakuu wa idara wanaweza kufuatilia na kudhibiti makusanyo ya siku na utendaji wa wakusanyaji.


**Mfumo wa Wavuti wa KIMRECOM**

Maboresho katika utoaji wa huduma kutokana na kuongezeka kwa mapato na uhakika wake kumejidhihirisha katika kuimarika kwa utayari wa walipa kodi. Halmashauri sasa inafurahia ulipaji wa kodi kwa wakati pamoja na uzalishaji na utoaji wa taarifa za kodi unaofanywa na mfumo. Utumiaji wa mfumo wa KIMRECOM umeongeza makusanyo ya mapato kutoka bilioni 16.9 mwaka 2009/2010 hadi bilioni 35.3 mwaka 2014/2015, kuifanya Halmashauri kuwa tajiri na kupanua uwezo wa kutoa huduma bora, za kisasa na nyingi kwa umma.

**Jedwali 3: Kuongezeka kwa Mapato**

| Mwaka | Makisio | Makusanyo | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 2010/2011 | 15,477,332,000.00 | 13,582,608,208.00 | 88 |
| 2011/2012 | 17,169,836,000.00 | 17,350,845,358.00 | 101 |
| 2012/2013 | 19,609,529,590.00 | 19,476,935,310.10 | 99 |
| 2013/2014 | 36,165,880,537.00 | 37,018,216,932.00 | 102 |
| 2014/2015 | 36,477,797,677.00 | 35,327,720,322.05 | 97 |

Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato kumeimarisha uwezo wa Halmashauri na kuleta ongezeko la bajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka bilioni 3.2 mwaka 2009/2010 hadi bilioni 16.4 mwaka 2013/2014. Miradi kadhaa imetekelezwa kutumia mapato ya ndani kama ujenzi wa barabara za lami za 14km, ujenzi wa maabara za biolojia, fizikia na kemia katika shule zote 46 za sekondari na ujenzi wa idara ya wagonjwa wa nje (OPD) na jengo la wazazi katika Hospitali ya Mabwepande.



*Barabara ya Tegeta Sokoni 1km*



*Barabara ya Tandale Sokoni*



*Barabara ya Journalism (1.1 Km)*



*Kalavati la Feza – Mikocheni*



*Maabara na Nyumba ya Mwalimu*



***Daraja la waenda kwa miguu Kata ya Mburahati na Daraja la Msigani Kata ya Msigani***



***Zahanati ya Manzese***



***Hospitali ya Mabwepande***



***Choo cha Umma na Stendi ya Daladala eneo la SIMU 2000***

Halmashauri hii imekuwa kituo cha kujifunzia ukusanyaji mapato wa digitali. Takribani Halmashauri 80 nchini zimetembelea Manispaa ya Kinondoni kujifunza mfumo. Baadhi ya Halmashauri hizi ni Lindi, Mafinga, Njombe, Morogoro, Magu, Kwimba, Bukoba, Mpanda, Sumbawanga na Mufindi. Pia majiji toka nchi jirani kama Jiji la Kampala lilifika kujifunza.

## 7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Manispaa ya Kinondoni imefanikiwa kuthibitisha kuwa ujio wa simu za viganjani na mtandao ni teknolojia muhimu katika ukusanyaji wa mapato na utoaji wa huduma. Kwa sababu hii Halmashauri ilisimika mfumo wa digitali wenye njia za kielektroniki kama maungio ya mtandao, chaguo za malipo mtandao na matumizi ya machine za kujiendesha zenyewe za huduma za benki (ATMs). Kwa kutumia njia hizi kwenye miamala rahisi ya walipakodi, Halmashauri imeongeza wigo wa walipakodi wa hiari na kuonesha kwa dhati umuhimu wake kwa umma. Mbinu hii imepunguza misongamano katika ofisi za malipo na kuondoa kizuizi cha utayari duni wa mlipakodi.

Kuimarisha na kuboresha mfumo huu wa digitali wa uboreshaji mapato; Manispaa ya Kinondoni imeweka mikakati mbalimbali. Mikakati hii ni pamoja na mafunzo yasiyokoma kwa watumiaji wa mfumo na vifaa ili kuelekeza matumizi sahihi ya mfumo, uhamasishaji endelevu wa jamii kupitia tovuti ya Kinondoni na mitandao ya kijamii, matengenezo na maboresho endelevu ya mfumo ili kuhakikisha uwepo wa mtandao

uliotulia na wa uhakika kwa masaa 24, kazidata ya walipakodi, nyongeza ya huduma za mfumo kama leseni za biashara, mauzo ya ardhi na kujikita katika jitihada endelevu za kupitia uingizaji wa taarifa za mfumo wa habari za kijiografia (GIS) ili kuwa na ulinganifu wa kudumu na mfumo wa KIMRECOM.




***Mfumo wa Taarifa za Kijiografia (GIS) na ukusanyaji Mapato***

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Manispaa ya Kinondoni imekuwa mojawapo ya Halmashauri kubwa na Kiongozi katika ukusanyaji wa mapato siyo kwa sababu ya kujaaliwa kuwa na raslimali nyingi, eneo la kitajiri na idadi kubwa ya wakazi bali kwa sababu ya nia thabiti ya kujenga msingi imara kwa ajili ya kutoa huduma na kupata uhalali kwa jamii yake. Kutokana na nia hii, siri za mafanikio zinatokana na utayari wa Halmashauri kusimika mfumo wa KIMRECOM na ushirikiano wake bora na MAXCOM katika kufunga na kuendeleza mfumo ambao umewezesha Halmashauri kuwa na wigo mpana katika ukusanyaji wa mapato na uunganishaji wa vyanzo vyote kama hospitali, vituo vya afya (Mwananyamala, Magomeni, Kimara and Sinza), stendi za mabasi, masoko na Kata zote 34, ambazo zinaweza kulipa ankara na ushuru nyinginezo kupitia mfumo wa kielektroniki. Siri nyingine muhimu sana ni uongozi imara wa Mkurugenzi wa Manispaa (Mhandisi Mussa Natty) na usaidizi toka kwa wajumbe wa Menejimenti ya Manispaa katika kukamilisha jitihada hii. Kwa upande wa menejimenti ya Manispaa na Halmshauri, jitihada hii imekuwa ya mafanikio sana na kuleta uendelevu kwa sababu ya usimamizi bora wa sheria ndogo kuimarisha utayari wa walipa kodi. Manispaa ya Kinondoni pia ina jamii ambayo ina uelewa wa kutosha wa masuala ya kiraia na maendeleo.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA


**MATUMIZI MKAKATI YA MAPATO YA NDANI KUKIDHI MAHITAJI YA JAMII**




***UZOEFU WA H/W YA TANDAHIMBA***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ni mojawapo ya Halmashauri tisa za Mkoa wa Mtwara. Inapatikana kwenye mwinuko wa Makonde uliopo 900m juu ya usawa wa bahari. Halmashauri ina eneo la 167,331Ha. Jumla ya 166,535Ha zinafaa kwa kilimo ambapo 129,507Ha zinatumika kwa kilimo. H/W ya Tandahimba hupakana na H/W za Newala upande wa Magharibi, Mtwara upande wa Mashariki, Mkoa wa Lindi upande wa Kaskazini na Mto Ruvuma upande Kusini ambao ndio mpaka wa Tanzania na Jamhuri ya Msumbiji. Kiutawala, Halmashauri ina Tarafa 3 za Litehu, Mahuta na Namikupa, Kata 31 na Vijiji 157. Kwa mujibu wa sensa ya 2012, Halmashauri ina wakazi 227,514 ambao kati yao 122,192 ni wanawake na 105,514 ni wanaume na kaya 53,790 zenye wastani wa 3.8 wa wakazi.



*Ramani ya Utawala ya H/W Tandahimba*

Shughuli kuu za kiuchumi za wakazi wa Tandahimba ni uzalishaji wa mazao na ufugaji. Korosho ndio zao kuu la biashara ikifuatiwa na mazao mengine kama ufuta na karanga. Mazao ya chakula ni pamoja na mhogo (chakula kikuu), uwele, mahindi, mpunga na jamii za maharagwe. Mifugo ni pamoja na kuku, mbuzi na ngo'mbe.

Halmashauri hupata mvua mara moja kwa mwaka ambazo huanza kwa kawaida mwishoni mwa Novemba na kuisha katikati ya Mei. Kuna msimu mfupi wa ukame wa wiki mbili au tatu mwishoni mwa Januari na mwanzoni mwa Februari. Wastani wa mvua ni 900mm; ingawa mtawanyiko wake haulingani. Joto huanzia 21$^{o}$C hadi 28$^{o}$C. Ardhi ya Halmashauri ina mwinuko tambarare wenye vilima vichache. Kuna mteremko mkali unaoelekea kwenye bonde la Mto Ruvuma. Aina ya udongo hutegemea ukanda; ukanda wa chini wa bonde la Ruvuma una udongo wa mfinyanzi na maeneo mengine yana udongo wa kichanga. Takribani 75% ya uoto uliopo katika Halmashauri hii ni mikorosho, na sehemu iliyobaki ina miti ya asili na majani marefu, mabwawa ya msimu na misitu (ya akiba na asili). Halmashauri ina kanda 3 za ikolojia na kilimo; yaani ukanda wa tambarare, juu na chini.

Ukanda wa Tambarare una ardhi ya kichanga, dhaifu kwa kutuamisha maji na imefunikwa na majani marefu na mikorosho ambayo hulimwa kwa wingi katika ukanda huu. Mazao mengine ni karanga, njugu, mhogo, uwele na njegere.

Ukanda wa juu una vilima na ardhi yake ina masalio mfu ya uoto wa asili na kina kirefu. Kuna misitu (asilia na kupandwa) na vichaka. Kuna mikorosho michache kutokana na joto kuwa la chini. Mazao makuu yanayozaliswa katika eneo hili ni mahindi, mbaazi, mtama, mhogo, na jamii za kunde. Ukanda wa chini ambao upo sambamba na bonde la Mto Ruvuma una majani marefu, misitu na vichaka. Udongo wake ni wa aina ya tope utokanao na mafuriko ya Mto. Mazao yanayolimwa ni mpunga, mahindi, ufuta na mbogamboga.

Mapato ya Ndani ya H/W ya Tandahimba hutegemea zaidi makusanyo ya ushuru wa korosho inayozalishwa na wakulima wadogo na ushirika wa wakulima. Ushuru wa korosho unakusanywa kwa mfumo wa pekee uliowekwa na wadau wa korosho ujulikanao kama Stakabadhi ya Mazao Ghalani. Mapato yaliyotokana na ushuru wa korosho kati ya 2010 – 2015 yanaoneshwa katika jedwali hapa chini.

**Jedwali 1: Makusanyo ya Ushuru wa Korosho 2010-2015**

| Mwaka | Makusanyo |
|---|---:|
| 2014/2015 | 2,983,404,273 |
| 2013/2014 | 2,197,819,369 |
| 2012/2013 | 2,210,057,733 |
| 2011/2012 | 3,103,955,071 |
| 2010/2011 | 1,973,760,052 |

## 2.0 TATIZO

H/W ya Tandahimba ni moja ya wazalishaji wakuu wa korosho, na hivyo ukusanyaji mkubwa wa ushuru utokanao na mauzo ya korosho. Halmashauri imekuwa ikikusanya mapato ya kutosha kutoka ushuru wa korosho kutokana na mfumo wake wa mauzo ambao una utaratibu maalumu na wa uhakika. Hata hivyo kwa miaka mingi matumizi ya mapato yatokanayo na chanzo hiki hayakuwa ya kimkakati ili kutoa huduma bora, za kisasa na endelevu kukidhi mahitaji ya wananchi.

Ukosefu wa mipango na matumizi ya kimkakati ya mapato yaliyokusanywa ulileta matatizo mengi kwa Halmashauri na wakazi. Halmashauri ilishuhudia kuondoka kwa watumishi wengi kutokana na ukosefu wa nyumba na mazingira mabaya ya kazi. Ni ukweli kuwa watanzania wengi huchukulia Tandahimba kama Halmashauri ya pembezoni ambayo ni vigumu kufikika. Ukosefu wa nyumba za watumishi na miundombinu haikutoa motisha kwa watumishi wapya kuitumikia Halmashauri hii. Pili, kulikuwa na utoaji duni wa huduma za jamii hasa katika elimu kwa watoto wenye mahitaji maalumu, kwa sababu suala hili halikuchukuliwa kama kipaumbele cha Halmashauri. Halmashauri hii, hata hivyo, ina idadi (mlinganisho) kubwa ya wakazi wenye mahitaji maalum, lakini kwa miaka mingi, hili halikuwa kipaumbele katika vitabu vya bajeti. Tatu, Halmashauri ilishuhudia uwazi wenye mashaka kutokana na miundombino duni ya mikutano. Ukumbi wa mikutano uliokuwepo kabla ya jitihada hii haukuweza kutosha kuingiza wananchi wakati wa mikutano ya Baraza, hivyo kuwanyima haki ya kupata habari moja kwa moja kutoka mijadala ya Madiwani. Mwisho, kulikuwa na ukosefu wa mifumo bora ya kufikisha mikopo na michango ya kisheria ya Halmashauri kwa Wanawake na Vijana kwa viwango vya chini vya riba. Licha ya ukweli kuwa baadhi ya taasisi za fedha zina viwango vya juu vya riba, usaidizi wa Halmashauri kwa Makundi haya ni elekezo la sera na kushindwa kutekeleza huleta adhabu za kinidhamu kwa Viongozi wa Halmashauri.

**3.0 LENGO**

H/W ya Tandahimba haikuwa na changamoto zinazohusu ukusanyaji wa mapato kwani ukusanyaji wa ushuru kupitia Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani uliihakikishia Halmashauri kupata mapato yake kikamilifu. Changamoto ilikuwa katika matumizi na uwekaji wa vipaumbele. Matatizo katika matumizi na uwekaji wa vipaumbele yalipelekea kuwepo kwa mahitaji mengi katika makao makuu ya Halmashauri na taasisi zake za chini. Wananchi pia walishuhudia mapengo mengi katika utoaji wa huduma. Hivyo, lengo kuu la Halmashauri katika jitihada hii ya mabadiliko lilikuwa kuanzisha matumizi mkakati ya mapato ya ndani yaliyopatikana kimfumo kutoka kwenye ushuru wa korosho ili kukidhi mahitaji ya jamii. Mahususi kabisa, jitihada hii ya mabadiliko ililenga:

(i) Kuwavutia watumishi ili wasihame kwa kuwapatia nyumba na mazingira bora ya kazi (ofisi).
(ii) Kuboresha utoaji wa huduma za jamii hasa katika elimu na maji.
(iii) Kuboresha uwazi na uwajibikaji kwa kujenga miundombinu ya kisasa ya mikutano inayoruhusu wananchi kufuatilia mijadala kwenye mikutano ya Baraza.
(iv) Kupanua wigo wa mapato kwa kukodisha kumbi za mikutano na ofisi kwa wananchi na taasisi mbalimbali.
(v) Kuboresha upatikanaji wa huduma za benki na mikopo kwa kuanzisha Benki ya Jamii.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

H/W ya Tandahimba DC hupata makusanyo ya ushuru kwenye misimu ya mavuno na mauzo ya korosho kupitia Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani. Mapato yanayokusanywa kwa namna hii hayahitaji nguvu za ziada katika kuunda mifumo ya ukusanyaji kama vile mabanio katika barabara kuu. Hii inafanya ukusanyaji wa mapato katika H/W ya Tandahimba kuwa fanisi na hakika. Changamoto kubwa ya Halmashauri hii ilikuwa katika kuleta uwiano kati ya mapato yaliyokusanywa na huduma zinazotolewa. Kufikia lengo hili, Halmashauri iliamua, kwa nguvu zote, kutumia mapato ya ndani kimkakati. Hili lilihusu Timu ya Menejimenti ya Halmashauri kuandaa mapendekezo kuhusu ujenzi wa nyumba za watumishi, miundombinu ya mikutano, shule kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu, miradi ya maji na uanzishaji wa Benki ya Wananchi wa Tandahimba. Baada ya majadiliano na makubaliano katika Menejimeneti mapendekezo ya miradi mbalimbali yaliwasilishwa kwenye kamati husika za Baraza kwa ajili ya uchambuzi wa kina. Mapendekezo yote ya miradi yalipitishwa na Baraza.

Ujenzi wa nyumba za watumishi na ofisi za Kata; jitihada ililianza kwa kuainisha upungufu wa nyumba za watumishi katika ngazi zote, kuandaa michoro ya nyumba na gharama za ujenzi (BOQ), kuwasilisha mapendekezo ya michoro na gharama kwenye Baraza ili kupata idhini, kutenga raslimali na kuziandaa Kamati za Maendeleo za Kata (KMK) kuongoza usimamizi wa miradi katika ngazi ya Kata. Mchakato huu pia ulihusu upelekaji wa fedha kwenye miradi kupitia akaunti maalumu (force account) ili kujenga umiliki wa jamii katika ujenzi wa ofisi za Kata na nyumba za watumishi; na kuunda mifumo kwa ajili ya ufuatiliaji na tahmini bora ya miradi ambayo hufanywa na timu ya kitaalamu ya Halmshauri.

Ujenzi wa Miundombinu ya Mikutano na Ofisi ya Mwenyekiti wa Halmashauri; mwaka 2013, Baraza lilipitisha mradi wa ujenzi wa kumbi za mikutano na vyumba vya ofisi. Baada ya kupitishwa shughuli zifuatazo zilitekelezwa. (i) uainishaji wa eneo la ujenzi; Halmashauri iliamua kutumia eneo lililopo karibu na makao makuu yake (ii) kufanya utafiti wa tija ya mradi ili kujiridhisha na faida zitakazopatikana (iii) kuchora na kuwasilisha gharama za ujenzi kwa Baraza kupata idhini (iv) kutenga fedha za ujenzi (v) kuendesha mchakato wa zabuni (vi) ujenzi kufanyika chini ya usimamizi na uangalizi wa Mhandisi wa Halmashauri (vii) kugawa na kukodisha ofisi kwa watumiaji mbalimbali.

Ujenzi wa shule kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu; mwaka 2007 Halmashauri iliamua kujenga shule ya watoto wenye mahitaji maalum kupunguza mzigo wa wazazi kupeleka watoto hawa huko Lukuledi, H/W ya Masasi. Kufikia lengo hili Halmashauri ilifanya yafuatayo; (i) kuhamasisha jamii kuhusu

kuwatambua watoto wote wenye mahitaji maalumu katika vijiji vyote 157 (ii) utambuzi wa watoto wote wenye mahitaji maalumu katika vijiji vyote 157 (iii) kushirikisha wadau mbalimbali katika kukusanya raslimali za ujenzi wa madarasa 3, bweni 1, chumba cha ufundi 1, nyumba 2 za walimu na chumba 1 cha mazoezi ya viungo (vi) kuajiri walimu waliobobea katika elimu maalumu na (v) uandikishaji wa watoto wanohitaji elimu maalumu.

Kuanzisha Benki ya Wananchi wa Tandahimba; Jamii ya Tandahimba ilikuwa na upungufu mkubwa wa huduma za benki na mikopo na walilazimika kupata huduma hizi H/W Newala 45km kutoka makao makuu ya H/W ya Tandahimba. Suala hili lilikuwa la gharama na hatari kadhaa kuhusu kusafirisha fedha taslimu kutoka na kwenda Newala. Mwaka 2012, Halmashauri kwa kushirikiana na jamii iliamua kuanzisha Benki ya Wananchi wa Tandahimba (TACOBA). Utekelezaji wake ni kama ifuatavyo; (i) kuunda timu ya mpito ya uhamasishaji ili kuifahamisha jamii umuhimu wa kuanzisha na kumiliki benki ya watu (ii) kukusanya mtaji wa awali kupitia uuzaji wa hisa kwa jamii na wadau wengine (iii) kuandaa miongozo ya uendeshaji wa benki na kuiwasilisha Benki Kuu kulingana na maelekezo ya mwaka 2008 (vi) kutenga fedha za kununua vifaa na (v) kuajiri watumishi na kuanza kutoa huduma zote za benki.

## 5.0 RASLIMALI

Lengo la H/W ya Tandahimba kutoa huduma na miundombinu kwa watumishi wake, madiwani, umma na makundi yenye uhitaji ni jitihada ya kusifiwa kwani mapato yanayokusanywa toka kwa umma yanatakiwa kuleta matokeo chanya kwa umma. Kukamilika kwa miradi iliyoelezwa hapo juu kulitegemea sana mapato ya ndani. Raslimali zifuatazo zilitumika kwenye utekelezaji. Jedwali liliopo hapa chini linaonesha raslimali fedha.

**Jedwali 2: Raslimali Fedha**

| Jina la Mradi | Chanzo cha Mapato | | | Jumla (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| | Jamii (TZS) | H/W (TZS) | Wadau na S/K (TZS) | |
| Ujenzi wa ofisi 30 za Kata na Nyumba 52 za watumishi | 50,000,000 | 1,800,000,000 | | 1,850,000,000 |
| Ujenzi wa kumbi za mikutano na ofisi ya Mwenyekiti | | 1,144,159,050 | | 1,144,159,050 |
| Ujenzi wa Shule ya Watoto wenye mahitaji maalumu | Nguvukazi (usafi wa eneo) | 50,000,000 | -DADPs 17,000,000<br>-TASAF 10,000,000<br>-JICA (madarasa 2, bweni 1, vitanda, magodoro) | 77,000,000 |
| Uanzishaji wa Benki ya Wananchi wa Tandahimba | Hisa 473,012,740 | Hisa 491,532,000 | | 964,544,740 |

Halmashauri pia ilitumia raslimali watu kama Madiwani na watumishi kutoa usaidizi wa kitaalamu. Wanajamii walichangia nguvukazi na Kamati za Maendeleo za Kata zilikuwa na jukumu la kutathmini na kusimamia utekelezaji wa miradi katika ngazi ya Kata. Huduma hizi ni endelevu na watumishi wengi wanaendelea kuendesha kumbi za mikutano na shule na wengine kusimamia maendeleo ya Benki ya Watu.

## 6.0 MATOKEO

H/W ya Tandahimba imefanikiwa kufikia malengo yalitotarajiwa kutoka kwa mbinu hii ya "matumizi mkakati ya mapato ya ndani". Suala moja kubwa la kimkakati lilikuwa kuhakikisha watumishi wanabaki Tandahimba. Halmashauri imefanikiwa kuwa na nyumba 30 za watumishi katika ngazi ya Kata na watumishi 30 ikiwa ni pamoja na maafisa ugani, maafisa maendeleo ya jamii na maafisa kilimo wanaishi

katika nyumba bora na familia zao. Tokeo hili limeongeza ari ya kuungana na Halmashauri na kiwango cha watumishi kusalia Tandahimba kimeongezeka.



***Nyumba mojawapo za Afisa Mtendaji Kata na mtumishi wa afya***

Wakuu wa idara ni watumishi mkakati katika Halmashauri. Hawa ndio huandaa mapendekezo muhimu na kupelekea maamuzi katika jitihada zote za maendeleo kwenye sekta mbalimbali. Kuwaweka katika nyumba za kifahari, karibu na makao makuu ya Halmashauri, huwapa motisha, hupunguza gharama, huongeza ufanisi, huboresha uzingatiaji wa kazi na kupelekea ubora wa jumla wa Halmashauri katika kutoa huduma na kuleta maendeleo kwa jamii yake. Katika hili, H/W ya Tandahimba imejenga nyumba 22 kwa ajili ya wakuu wa idara. Jamii ambayo hupata huduma bora huitika kwa wema katika ulipaji kodi na utoaji wa michango kwa ajili ya miradi ya maendeleo.



***Baadhi ya Nyumba za Wakuu wa Idara***

Kwa miaka mingi H/W ya Tandahimba ilihitaji kuwa na ukumbi mkubwa wa mikutano ambao ungeruhusu mikutano kufanyika kwa ufasaha na kuwa na nafasi ya kutosha kwa ajili ya wananchi kuhudhuria mikutano na kufuatilia mijadala ya Madiwani. Miundombinu ya mikutano imejengwa ikiwa na ukumbi mkubwa, ofisi ya Mwenyekiti na ofisi nyingine za kukodisha. Miundombinu hii imeboresha utendaji, imeleta uwazi katika shughuli za Halmashauri na Mwenyekiti pamoja na Madiwani wameridhika. Ukumbi wa mikutano una ofisi za ziada ambazo zimekodiwa na benki ya CRDB na kuongeza mapato ya ndani hivyo kupanua uwezo wa Halmashauri kutoa huduma kwa umma.



***Ukumbi wa Mikutano na Ofisi zilizokodishwa kwa benki ya CRDB***

H/W ya Tandahimba ina idadi kadhaa ya watu pamoja na watoto wenye mahitaji maalumu. Eneo hili lilichukuliwa na Halmashauri kuwa mkakati kwa sababu huduma lazima zielekezwe kwa wote bila kujali uwezo wa mwili na akili. Hivyo Halmashauri ilianzisha na kujenga majengo ya shule mahsusi kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu. Shule yenye usajili Na. MT 05.136 hutoa huduma kwa jamii ya Tandahimba na Halmashauri za jirani kama Masasi, Nanyamba na Mtwara. Shule hii pia inapokea watoto wenye mahitaji maalumu kutoka mikoa yote Kusini mwa Tanzania. Majengo katika shule hii ni ya kisasa na yenye vifaa kwa ajili ya mahitaji maalumu, yakitoa na huduma za bweni; chakula na malazi. Walimu wa shule hii wanaishi katika nyumba zilizojengwa vizuri, wana furaha na motisha wa kazi na kufundisha watoto. Majengo yanajumuisha madarasa, bweni, jengo la ufundi, nyumba za walimu na jengo la mazoezi ya viungo.



***Madarasa na Bweni***



***Nyumba ya Walimu, Jengo la Ufundi, na Jengo la Mazoezi ya Viungo***

Wakati wa kuchapa kitabu hiki shule hii maalumu katika H/W ya Tandahimba ilikuwa na wanafunzi 48 wenye mahitaji maalumu wakihudhuria elimu ya msingi. Katika elimu hii maalumu watoto wanafundishwa maisha ya kawaida katika jamii, matumizi ya viungo vyao vya mwili kufanya kazi na kuboresha uchaji na ujanja wa akili zao. Walimu wana stadi katika maeneo haya muhimu na taaluma hii isiyo ya wengi, na wanasaidia watoto kushiriki katika shughuli za shule kama usafi, upishi, kusoma, kuandika, kucheza na kuimba.




***watoto wenye mahitaji maalumu katika kipindi mojawapo***

H/W ya Tandahimba ni mojawapo ya Halmashauri zinazochukuliwa kuwa za pembezoni. Kwa miaka mingi huduma za benki zilikuwa zikifuatwa Mtwara au Newala. Kwa kutambua umuhimu wa uzalishaji wa korosho na hitaji la watu wa Tandahimba la kupata huduma za benki za kila siku, Halmashauri ilipanga kimkakati, ikaunda na kutekeleza uanzishaji wa Benki ya Wananchi wa Tandahimba. Kwa sasa, benki ipo, ikitoa huduma za akiba, mikopo na uhamishaji wa fedha. Wakulima sasa wanaweza kupata mikopo kwa ajili ya pembejeo ili kuboresha uzalishaji wa  korosho na kupelekea hali bora ya kiuchumi na maboresho ya kipato katika kaya. Huduma za benki ni za haraka na zimeondoa hatari zote,  wizi na uvamizi ambao umma wa Tandahimba ulikuwa ukipata katika kusafirisha fedha taslimu kwenda kwenye benki zilizopo Mtwara na Newala.




***Benki ya Wananchi Tandahimba***

## 7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Jitihada ya matumizi mkakati ya mapato ya ndani katika H/W ya Tandahimba imelengwa iwe ya kudumu na Menejimenti ya Halmashauri imejipanga kuifanya jitihada hii kuwa suala la kawaida na tabia bora ya Halmashauri. Dira tarajiwa ni kuifanya H/W ya Tandahimba kuwa moja ya Halmashauri bora katika ukusanyaji wa mapato na ni "moja tu" kwa matumizi bora katika utoaji wa huduma katika sekta zote. Kwa hiyo Halmashauri imejiwekea mikakati mbalimbali ya uendelevu wa matumizi mkakati ya mapato ya ndani. Mikakati muhimu sana ni pamoja na kuendelea kutenga fedha kwa ajili ujenzi na ukarabati wa ofisi na nyumba za watumishi katika ngazi za Kata na Vijiji, kuendeleza ukodishaji wa ofisi na kumbi za mikutano ili kuzalisha mapato ya kuendesha ukarabati wa mara kwa mara wa miundombinu ya mikutano, kununua samani kwa ajili ya kumbi za mikutano na kutoa kandarasi kwa kampuni ya usafi kwa shughuli za usafi na utunzaji wa maeneo wa kila siku na utengaji wa fedha usiokoma kwa ajili ya miundombinu, ajira ya walimu na uanzishaji wa mfumo wa maji katika shule ya watoto wenye mahitaji maalumu.

H/W yaTandahimba imedhamiria kuendesha uhamasishaji jamii usiokoma kuhusu matumizi ya huduma za zitolewazo na Benki ya wananchi wa Tandahimba na ujenzi wa uelewa kwa jamii ili kushiriki kikamilifu

katika jitihada hizi na huduma zitolewazo na Halmashauri. Kujihakikishia uendelevu, Halmashauri pia imeweka mkakati endelevu wa kuuza hisa na kutoa mikopo yenye viwango vya chini vya riba ili kuongeza mtaji wa benki ya wanannchi pamoja na kuifanya benki kuwa mfumo wa kudumu wa kupitishia mikopo kwa wanawake na vijana (10% ya lazima kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri).

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Lengo la kutumia mapato ya ndani kimkakati kukidhi mahitaji ya watumishi na umma, kutia motisha watumishi, kuwafanya wabaki katika Halmshauri na kutoa huduma kwa makundi maalumu wakati wote ni vipaumbele vya Halmashauri nyingi hapa Tanzania. Hata hivyo, Halmashauri nyingi hazifanikiwi sana kuwa kimkakati katika matumizi ya mapato ya ndani. Ikimaanisha kuwa kuna siri za mafanikio kwa H/W ya Tandahimba. Siri hizi ni;

(i) Kujitoa kwa Timu ya menejimenti ya Halmashauri katika kuandaa mapendekezo mkakati yanayogusa mahitaji halisi ya jamii.
(ii) Ushirikiano wa karibu na makubaliano ya pamoja kati yaTimu ya Menejimenti na Madiwani katika kutenga mapato ya ndani kwa ajili ya miradi iliyotekelezwa.
(iii) Uhamasishaji bora wa jamii kuhusu umuhimu wa kushiriki katika shughuli za maendeleo na elimu ya watoto wenye mahitaji maalumu.
(iv) Eneo la kuvutia kwa ajili ya kukodisha ofisi kwenye miundombinu ya mikutano.
(v) Uongozi imara wa Mkurugenzi na Mwenyekiti wa Halmashauri katika kuongoza na kuratibu wadau.
(vi) Mfumo ulio bora na wazi wa uuzaji wa Korosho ambao hurahisisha ukusanyaji wa ushuru (Stakabadhi ya Mazao Ghalani).

# Sura ya Nne: Ushirikishwaji wa Jamii katika Utoaji wa Huduma

Utoaji wa huduma ni jukumu muhimu katika mahusiano ya taasisi za Serikali na wananchi. Huduma ni mfumo au mpangilio unaokidhi mahitaji ya jamii. Helmsing (1995) anaeleza kuwa utoaji wa huduma ni uamuzi wa lazima unaofanywa na maafisa wa kuchaguliwa au kuajiriwa kutumikia au kutoa bidhaa na huduma kwa wapokeaji. Utoaji wa huduma ni wa namna ya mtazamo na mwelekeo, ukihusisha sifa na desturi za kimataifa..

Utoaji huduma ni mchakato endelevu na unaojirudia wa kupanga na kutoa huduma zinazozingatia mpokea huduma. Huhusu ushiriki wa mpokea huduma katika kuainisha wapokea huduma na kutambua mahitaji yao. Utoaji wa huduma pia unahitaji mchakato wa kubuni na kupanga huduma kati ya watumiaji, watoaji, wasambazaji na washirika katika kuanzisha, kubuni na kupanga huduma na kuhakikisha mahitaji ya watumiaji wa huduma yanafikiwa. Hatimaye utoaji wa huduma unahusu uzalishaji, usambazaji na uwasilishaji wa huduma ambazo zinakidhi lengo na zinafaa kwa mahitaji ya watumiaji. Katika utoaji wa huduma muda wote panahitajika mfumo wa ufuatiliaji na uboreshaji wa kukusanya maoni ya watumiaji na vipimo vya utendaji ili kuwezesha ufuatiliaji na uboreshaji wa bidhaa na huduma wa mara kwa mara.

Utoaji wa huduma ni shughuli ya msingi ya Serikali. Serikali huwepo, pamoja na sababu nyingine, kwa sababu ndio chombo pekee kinachoweza kutoa kwa usahihi maelekezo kuhusu huduma muhimu kama usalama wa raia, ulinzi, miundombinu, usimamizi na ukarabati wa barabara na kadhalika. Ulazima na umuhimu wa masuala haya huleta uhalali katika shughuli za Serikali. Imewekwa katika Katiba na mikataba ya kimataifa kwamba Serikali inawajibika na huduma za msingi katika maeneo mengi ya kijamii ambayo ni pamoja na elimu, hifadhi ya jamii, mahitaji ya msingi, ulinzi wa kisheria na makazi. Serikali lazima iwapatie wananchi uhakika wa kuendeleza utoaji huduma; kupatikana huduma kwa wote bila kujali tofauti za kijamii na kiutamaduni na kwa bei zinazofaa. Hili lina matokeo kwa taasisi za Serikali. Uwazi, ufanisi, upatikanaji na mambo mengine, huleta ubora katika bidhaa zitolewazo na Serikali kama huduma kwa wananchi wake.

Kwa wananchi wengi, Serikali yao ya Mtaa ndio Serikali yenye mashiko zaidi, pia ndiyo ngazi ya Serikali ambayo huwasiliana nayo zaidi katika maisha yao ya kila siku. Mfumo wa Tanzania wa Serikali za Mitaa unaonyesha kuwa MSM hutoa huduma ambazo zina asili ya kijamii, yaani afya, maji, elimu, ustawi, usimamizi wa taka, na zile zenye asili ya kiuchumi, yaani ardhi na makazi, muindombinu, kilimo, mazingira na maendeleo ya jamii.

Nadharia ya utoaji huduma shirikishi iliyotumika katika kitabu hiki, ina maana ya utoaji huduma ambao huhusisha wadau wote. Kiini cha ushiriki ni jamii ambayo hufaidika na huduma zitolewazo na jamii yenyewe, MSM, Serikali Kuu, mashirika yasiyo ya kiserikali na hata mashirika ya kimataifa. Utoaji huduma shirikishi huweka jamii faidika kama msingi wakati wa kupanga, utoaji wa huduma na upimaji wa ubora wa huduma. Utoaji huduma shirikishi huleta uendelevu wa huduma inayotolewa.

Katika sura hii, mbinu bora nane kuhusu utoaji huduma shirikishi zimewasilishwa kutoka Halmashauri za wilaya za Lindi, Kilwa, Ruangwa, Chunya, Busokelo, Ileje na Newala na nyingine kutoka Manispaa ya Ilala. Mbinu bora za mwazo za Halmashauri za Lindi, Chunya, Kilwa na Ruangwa zinahusiana na ushirikishwaji wa jamii katika kuhifadhi misitu. Mbinu hizi zinaeleza yaliyozikabili jamii hadi zikaamu kushiriki kwenye mpango wa kuhifadhi misitu. Baadhi ya matatizo ambayo jamii ilikumbana nayo ni pamoja na kukithiri kwa ukame, kukauka kwa vyanzo vya maji, kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo na uharibifu wa mazingira uliotokana na shughuli za kibinadamu. Kutokana na changamoto hizi, Halmashauri na wadau wa misitu waliamua kuchukua hatua ya kuwashirikisha jamii kuanzisha mpango wa kutunza na kuhifadhi misitu. Mikakati iliyotumika kwenye kutekeleza jitihada hii ni pamoja na; kuwajengea wananchi uelewa kuhusiana na utunzaji wa mazingira, kuzihamasisha jamii kuanzisha misitu yao wenyewe na kuitunza, kuanzisha kamati za kuhifadhi misitu za Vijiji, kuzijengea kamati za misitu za Vijiji uwezo wa kusimamia utunzaji wa misitu, kusaidia jamii kupanga matumizi bora ya ardhi, kutunga sheria ndogo za kulinda misitu na kusaidia jamii kupata majiko banifu yanayotumia kuni kidogo ili kupunguza matumizi makubwa ya kuni. Baada ya utekelezaji wa mradi huu, matokeo chanya yameonekana; Misitu imeweza kustawi kutokana na utunzaji wa misitu unaoendelea, jamii zimeanza kunufaika kutokana na mazao ya misitu, fedha wanazopata kutokana na mazao ya misitu zimetumika kujenga miundombinu ya kutolea huduma za jamii.

Sura hii mbali na kuzungumzia uhifadhi wa misitu, zinaelezea pia mbinu bora za Halmashauri za Busokelo, Manispaa ya Ilala, Halmashauri za Wilaya za Ileje na Newala. Mbinu bora ya Halmashauri ya Busokelo inaelezaea jinsi Halmashauri ilivyoweza kushirikiana na wananchi katika kupanga mji wa Lwangwa hivyo jina la mbinu bora ni Ushirikishwaji wa Jamii katika Upangaji wa Mji. Changamoto zilizoikabili Halmashauri ya Busokelo kabla ya utekelezaji wa mpango huu ni pamoja na; kukua kwa makazi holela kutokana na ongezeko la watu ndani ya Wilaya ya Busokelo. Ukuaji huo wa Mji ulipelekea kukosekana kwa maeneo tengefu kwa ajili ya huduma za barabara, maeneo wazi kwa ajili ya shughuli za kijamii na za kiuchumi. Kutokana na uhaba wa raslimali, Halmashauri iliamua kuupanga mji wa Lwangwa kwa kuishirikisha jamii yenyewe. Ili kufikia lengo hili, Halmashauri ilianza kwa kuunda kikosi kazi cha kushawishi jamii na kuijengea uelewa kuhusu faida za kupima ardhi na kuupanga mji. Jamii ilihamasika na kuunda vikosi kazi katika ngazi ya jamii kuratibu zoezi vikisaidiana na kikosi kazi cha Halmashauri. Kutokana na uhamasishaji uliofanyika, baadhi ya wakazi waliamaua kutoa maeneo yao bila gharama yoyote kuruhusu kupitishwa kwa barabara ambazo zinaunganisha maeneo ya mji. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Dr. Leonard Masale, kutokana na uzoefu alioupata akiwa Halmashauri ya Itilima aliweza kuutumia uzoefu huo kuishawishi jamii na kuunganisha wadau mbalimbali wa ndani na nje ya Busokelo kuhakikisha wanatekeleza lengo la kupanga Mji wa Lwangwa.

Mbinu bora ya Manispaa ya Ilala inahusu uboreshaji wa usafi, kupendezesha na ujanishaji wa mazingira ya Shule. Kabla ya jitihada hii, Shule nyingi za Msingi na Sekondari ndani ya Manispaa ya Ilala ziliathirika kutokana na mazingira machafu; mazingira kuzunguka shule yalikuwa machafu kupindukia. Wanafunzi walionekana wachafu muda wote, vumbi jingi ilikuwa ni sehemu ya shule. Vilevile shule hazikuwa na vifaa vya kunawa mikono baada ya kutoka chooni. Halmashauri ilianza kuboresha mazingira ya shule kwa kuchagua shule mbili za mfano ambazo ni shule za Msingi za Buguruni na Boma na kuziwezesha kwa kuzijengea uwezo wa kubadilisha mazingira ya shule na kuyafanya ya kuvutia ili shule nyingine zeweze kuiga kutoka kwao. Ujenzi wa uelewa kwa walimu kuhusu kuboresha mazingira na afya za wanafunzi shuleni ulifanyika, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa uelewa kwa wanafunzi ili kuwafanya wabadilike tabia na kuchukia uchafu. Vilevile wanafunzi waliwezeshwa kuanzisha klabu za mazingira na kuwafanya wawe mabalozi wa usafi katika jamii.

Mbinu Bora ya Ileje inahusu uboreshaji wa mahusiano ya ujirani mwema baina ya jamii za mpakani mwa Tanzania na Malawi katika Wilaya za Ileje (Tanzania) na Chitipa (Malawi). Kabla ya jitihada za kuboresha

mahusiano haya kulikuwa na changamoto za migogoro ya ardhi baina ya wananchi wa vijiji vya Ileje na wananchi wa Malawi. Kulikuwa na mahusiano yasiyo rasmi baina ya wananchi wa pande zote mbili, biashara za mipakani zikiendelea bila kuwepo kwa udhibiti wa namna yeyote, hapakuwa na mikakati ya matumizi ya huduma za jamii kama afya, elimu, kilimo na mifugo katika maeneo ya mpakani ambapo jamii zilitumia huduma hizo bila kujali zinatolewa na nchi ipi. Pia kulikuwa na changamoto za usafiri na usafirishaji wa bidhaa kwa kutumia njia zisizo rasimi jambo ambalo lilipelekea bidhaa zilizozuiliwa kuingia nchini kupenya kwa kutumia njia hizo. Katika kukabiliana na changamoto hizi, Wakuu wa Wilaya za Ileje na Chitipa walikutana na kujadiliana changamoto hizo na kuweka mikakati ya kuzitatua. Mikakati iliyotumika ni pamoja na kuunda timu ya uratibu wa zoezi na kuandaa mikutano ya kukutanisha wadau wa nchi zote mbili kujadili na kufikia muafaka wa kutatua changamoto hizo. Kutokana na majadiliano yaliyoendeshwa mara kwa mara iliafikiwa kuweka mazingira ya kujenga mahusiano yanayotambulika kisheria baina ya jamii za pande mbili, kuanzishwa kwa soko la mazao ya kilimo la kimataifa katika Wilaya ya Ileje ambalo litaruhusu mazao kutoka Malawi kuuzwa ndani ya soko hilo kuepuka kupenyeza biashara hizo kwa njia zisizo rasmi, kukarabati daraja la Mto Songwe ili kuwafanya wananchi kutumia njia moja kuvuka kwenda sehemu ya nchi nyingine ili kupunguza njia zisizo rasmi na kutunza mazingira ya Mto Songwe ilikuepusha kuhama hama kwa mto ambapo inapelekea kuhama kwa mpaka wa nchi hivyo kuleta migogoro ya ardhi baina ya wananchi wa pande zote mbili.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Newala inahusu kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Elimu wa Newala. Kabla ya jitihada ya kuanzisha mfuko huu, Halmashauri ilikumbwa na changamoto mbalimbali katika sekta ya elimu kwa shule za Sekondari na Msingi. Kulikuwa na miundominu mibovu ya madarasa, vyoo na madawati ambayo haikutosheleza mahitaji ya shule, jamii hazikuwa na moyo wa kuchangia elimu kwa ajili ya watoto wao kwani baadhi yao hawa kuona umuhimu wa elimu na ilichukuliwa kuwa ni jukumu la Halmashauri pekee kutekeleza mahitaji yote ya shule jambo ambalo lilikuwa gumu kutokana na ufinyu wa raslimali. Halmashauri ili amua kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Elimu Newala ili kukusanya fedha za kuhudumia sekta ya elimu. Kufikia lengo hili, Halmashauri iliunda kamati ya kuchambua changamoto za sekta ya elimu na kutoa mapendekezo kuhusu nini kifanyike. Kamati ilipewa jukumu la kutafuta wadau wa elimu na kuwashawishi kuhusu kuanzishwa kwa mfuko wa elimu, kuishawishi jamii na kuitia hamasa ione umuhimu wa elimu. Baada ya uhamasishaji, mfuko ulianzishwa mwaka 2011; taratibu za kukusanya michango kwa ajili ya mfuko ziliwekwa na jamii iliweza kushiriki vyema katika kufikia lengo la kutatua changamoto za sekta ya elimu.

Mambo dhahiri ya kujifunza yanayotokana na mbinu bora zilizopo katika sura hii yanaonyesha;

i. Utoaji wa huduma si wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa pekee, bali jamii kwa ujumla zinahitaji kupewa fursa ya kushiriki kikamilifu katika kutoa huduma zao. Jamii kupitia jitihada zao binafsi zinaweza kufanya mengi katika kutimiza mahitaji yao na ya huduma zinazohitaji. Kukiwa na mtazamo chanya wa umoja wa jamii, watu wanakuwa tayari kwa maendeleo yao.
ii. Ubunifu na kujitoa kwa watumishi wa MSM na upendo kwa watu wanaowahudumia, huleta tofauti kubwa katika utoaji wa huduma na huongeza ufanisi, uhakika na uendelevu katika huduma zinazoanzishwa na kutolewa.
iii. Hapa Tanzania hatujatumia kikamilifu raslimali zilizopo. Kuna raslimali nyingi ambazo hazitumiki zikisubiri watu wenye ubunifu kuzitumia. Ardhi iliyo wazi inaweza kubadilishwa kuwa misitu na maeneo ya utalii. Utamaduni tajiri uliopo unaweza kuunganishwa na maliasili kutunza mazingira, kuimarisha utalii na kuongeza fursa za ajira.

# HALMASHAURI ZA WILAYA ZA LINDI, KILWA, RUANGWA NA CHUNYA

**UBORESHAJI WA HUDUMA KUPITIA UTUNZAJI SHIRIKISHI WA MISITU**




***UZOEFU WA HALMASHAURI ZA WILAYA ZA CHUNYA, KILWA, LINDI NA RUANGWA***

## 1.0 UTANGULIZI


Mpango wa Taifa wa Kukukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA), unatambua kwamba jamii maskini zinategemea kwa kiasi kikubwa raslimali asilia katika kujiongezea kipato na kwa matumizi ya kaya. Ingawa misitu haitambuliki kama sekta ya kipaumbele, kuna ongezeko kubwa la ufahamu wa umuhimu wa raslilimali za misitu katika kutunza mazingira, kulinda maisha ya viumbe hai na kuongeza kipato cha jamii hususani jamii maskini. Kwa kutambua faida hizi za misitu, H/W za Chunya, Lindi, Ruangwa na Kilwa ziliamua kuhifadhi misitu kupitia njia shirikishi jamii kwa kuzifanya jamii zinazozunguka misitu husika kuwa wamiliki na wahifadhi wakuu wa misitu hiyo.


Usimamizi Shirikishi wa Misitu ni mkakati endelevu wa kuhamasisha utunzaji wa misitu na raslimali za misitu kupitia jamii zinazopakana na misitu. Mkakati huu unalenga kuzifanya jamii hizo kuchukua umiliki, usimamizi na utunzaji wa raslimali za misitu. Mkakati huu unalenga kuleta maendeleo ya vijijini kwa kuboresha hali ya maisha ya vijijini na kusaidia kupunguza umaskini wakati huo huo unalenga kulinda mazingira.

Mpango Usimamizi Shirikishi wa Misitu ulianza mwanzoni mwa miaka ya 2000. Kwa H/W ya Kilwa mpango ulianza mwaka 2002, H/W za Chunya na Lindi 2004 na H/W ya Ruangwa mpango ulianza mwaka 2005. Usimamizi Shirikishi wa Misitu ulihusisha jamii kutaka vijiji mbalimbali kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini.

**Jedwali 1: Hifadhi ya Misitu katika H/W Lindi, Ruangwa, Kilwa na Chunya**


| Jina la Halmashauri | Kijiji/Kata ya Uhifadhi Misiti | Eneo la Msitu |
|---|---|---|
| Lindi | Kata za Mipingo, Nangaru, Matimba, Rutamba, Milola na Kiwawa | 1744.75 $Km^2$ |
| Ruangwa | Kijiji cha Nandenje | 12745.48ha |
| | Vijiji vya Kipindimbi, Nga'u, Lichwachwa, Nahanga na Chingumbwa | 41436.3ha |
| Kilwa | Vijiji vya Liwiti, Nainokwe, Nambondo, Mavuji, Kikole, Ruhatwe, Migeregere na Ngea | 402,000ha |
| Chunya | Kata za Kipembawe, Kwimba and Songwe | 396,400ha |




*Eneo la misitu H/W ya Lindi*

*Eneo la misitu H/W ya Kilwa*




***Ramani ya H/W ya Ruangwa na eneo lililohifadhiwa***

## 2.0 TATIZO

Kabla ya mwaka 2000 hapakuwa na hifadhi ya misitu ya vijiji ndani ya Halmashauri za Wilaya. Matukio ya uchomaji misitu, kilimo cha kuhamahama na uvunaji haramu wa raslimali za misitu vilikithiri kwa kiasi kikubwa. Hapakuwa na mpango endelevu wa kutunza misitu wakati wa uvunaji raslimali za misitu. Ongezeko la uvunaji wa mazao ya misitu kama mbao na mkaa ulikithiri kwa kiasi kikubwa. Mwaka 2004, kutokana na shughuli za kijamii na kiuchumi, H/W ya Chunya iliathirika kwa kiasi kikubwa na uharibifu wa misitu uliosababishwa na wavamizi kutoka mikoa ya jirani (Tabora, Singida, Katavi na Shinyanga) ambao walikuja kutafuta maeneo ya kilimo na ufugaji. Uvamizi huu ulipelekea kufyekwa kwa sehemu kubwa ya misitu katika Kata za Kipembawe, Kwimba na Songwe.

Hifadhi za Misitu 11 katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya zilikuwa chini ya umiliki wa Serikali Kuu na Halmashauri. Hapakuwa na misitu ambayo umiliki wake ulikuwa chini ya Kijiji au jamii. Hali hii ilipelekea sehemu kubwa ya misitu kukosa usimamizi na kushawishi uvamizi wa misitu. Katika baadhi ya maeneo

ambayo uvamizi ulifanyika kulitokea uharibifu wa mazingira, uchomaji ovyo wa misitu, kutoweka kwa viumbe hai ndani ya misitu, kupungua na kukauka kwa maji katika vyanzo mbalimbali.

Kwa Halmashauri za Wilaya za Kilwa na Lindi, uchomaji misitu ulikuwa jadi yao, kama mkakati wa kujihami na wanyama wakali. Ufyekaji wa misitu pia ulisababishwa na kilimo cha ufuta ambapo wakulima walendesha kilimo cha kuhamahama. (Jamii za Lindi na Kilwa zinaamini kwamba zao la ufuta linastawi vyema kwenye shamba jipya ambalo limechomwa moto). Matatizo mengine ni pamoja na uvunaji holela wa mazao ya misitu katika kutafuta mkaa, kuni, mbao na uwindaji haramu wa wanyamapori. Matatizo haya yalipelekea uharibifu mkubwa wa mazingira, mmomonyoko wa ardhi na hatimaye mabadiliko katika tabia nchi. Kutokana na uharibifu huu mkubwa jamii zilianza kukumbwa na janga la ukame, kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo, kukauka kwa vyanzo vya maji na kupungua kwa mazao ya misitu. Kwa upande wa Halmashauri za Vijiji na Wilaya, mapato kutokana na vyanzo vya mazao ya misitu na kilimo vilipungua. Picha ifuatayo inaonesha uvunaji holela wa misitu.



***Uvunaji holela wa misitu H/W ya Lindi***

**3.0 MALENGO**

Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 pamoja na Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 inatoa fursa kwa vijiji kuanzisha hifadhi zao za misitu. Kwa misingi hii, Halmashari za Wilaya za Chunya, Kilwa, Lindi na Ruangwa zikishirikiana na wadau wa misitu ziliamua kushirikisha jamii kuanzisha na kuhifadhi misitu. Lengo kuu la jitihada hizi ni kuzisaidia jamii kuanzisha na kuboresha utunzaji wa misitu na raslimali za misitu ili kusaidia kuboreshaji wa maisha ya jamii hususan jamii maskini za vijijini. Malengo mahususi ya jitihada hizi ni pamoja na; kuhamasisha utunzaji endelevu wa misitu kwa mbinu ya uhifadhi shirikishi wa misitu na kujenga uwezo wa jamii katika kuhifadhi, kutunza misitu na raslimali zitokanazo na misitu ili ziwe endelevu. Malengo mahususi mengine ni pamoja na kuhifadhi mazingira ili kupunguza kiasi cha hewa ukaa na kuongeza mazingira wezeshi kwa uhai wa viumbe, kuongeza ukubwa wa eneo la misitu kwa kuzuia uvunaji holela wa raslimali za misitu na kuchochea dhana ya umiliki wa raslimali za misitu kwa jamii kwa kuhakikisha jamii zinafaidika na raslimali zinaotokana na uhifadhi wa misitu. Vilevile, jitihada hii ya uhifadhi shirikishi wa misitu ililenga kuanzisha chanzo madhubuti cha mapato kwa Serikali za vijiji kupitia mauzo ya mazao ya misitu na kuboresha kipato ndani ya kaya kutokana na mazao ya misitu; kwa mfano uuzaji wa asali; na kukuza uchumi wa vijiji kwa ujumla.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Uhifadhi Shirikishi wa Misitu kama mpango wa kitaifa unalenga kugatua usimamizi wa misitu kutoka Serikali Kuu kwenda kwa jamii. Katika kufikia lengo hili, Halmashauri za Wilaya ziliweka mikakati ya utekelezaji. Kwa kiasi kikubwa mikakati ilifanana kwa Halmashauri zote za Chunya, Kilwa,Lindi na Ruangwa. Mikakati ya utekelezaji iliyotumika ni kama ifuatavyo:

***Kujenga uelewa wa pamoja***; Halmashauri zilianza kwa kuwajengea uwezo jamii kuhusu uhifadhi shirikishi wa misitu. Ili kufanikisha zoezi hili Halmashauri zilianza kujenga uwezo wa viongozi kupitia mikutano ya kamati za kudumu na Mabaraza ya Madiwani. Wazo la uhifadhi misitu lilipokelewa na viongozi ambapo waliahidi kusaidia kusambaza uelewa huo kwa jamii kupitia mikutano ya Kata. Kila Halmashauri ilianza kushawishi jamii kupitia mikutano na viongozi wa vijiji, vijana makundi ya wanawake na jamii kwa ujumla kuhusu umuhimu wa jamii kushiriki kuhifadhi misitu. Kwa H/W ya Lindi uhamasishaji ulifanyika kwa Kata 6; Mipingo, Nangaru, Matimba, Rutamba, Milila na Kiwawa. Zoezi hili lilifanywa na Afisa misitu, Afisa maendeleo ya jamii, Afisa mazingira na Afisa ardhi wa Halmashauri. Picha ifuatayo inaonesha wananchi wakihudhuria mkutano wa uhamasishaji H/W ya Lindi.



***Wananchi wakihudhuria mkutano wa uhamasishaji***

***Uhamasishaji wa wadau kushiriki katika uhifadhi shirikishi wa misitu;*** wadau wa uhifadhi misitu ni wengi, hata hivyo uhifadhi wa misitu unatekelezwa kwa njia tofauti kulingana na mdau husika. Kwa kuzingatia hili, Halmashauri ziliamua kuhamasisha wadau katika kujenga msingi wa pamoja kufikia adhima ya uhifadhi mazingira. H/W ya Kilwa ilihusisha Wizara ya Maliasili na Utalii, Washirika wa Maendeleo kama Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD), World Wide Fund for Nature (WWF), Mpingo Conservation, Development Initiatives (MCDI) na Mtandao wa Uhifadhi Mazingira Tanzania (MJUMITA). H/W za Lindi na Chunya zilishirikisha Wizara ya Maliasili na Utalii na DANIDA ambao walitoa fedha za kuendesha zoezi la uhamasishaji wa jamii kuhifadhi misitu.

***Uundaji Kamati za Uhifadhi Misitu za Vijiji;*** ili kuchochea uhifadhi shirikishi wa misitu, Halmashauri za Wilaya zilianzisha kamati za uhifadhi misitu za Vijiji. H/W ya Chunya ilianzisha Kamati 15 za uhifadhi misitu ngazi ya kijiji na H/W ya Lindi ilanzisha kamati za aina hiyo ambazo ziliundwa na wajumbe 287. Kamati hizi zilianzishwa kusaidia timu ya Halmashauri ya Uhifadhi Misitu. Majukumu ya kamati hizi ni kutekeleza shughuli za uhifadhi misitu, kuandaa mpango kabambe wa uvunaji wa mazao ya misitu na kusimamia mapato yanayotokana na uuzaji wa mazao ya misitu. Kamati hizi za Vijiji ziliundwa na mkutano mkuu wa kijiji. Kila kamati ikiwa na wajumbe 10 wa kuchaguliwa, kati yao angalau wanawake 3 walichaguliwa kuunda kamati.

***Kuzijengea uwezo kamati za uhifadhi misitu za vijiji;*** Kamati za uhifadhi misitu za vijiji zilijengewa uwezo kupitia mafunzo. Mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na namna ya kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi, kutengeneza sheria ndogo za kulinda misitu, mbinu za kufanya doria ndani ya misitu, kutengeneza mpango wa kuvuna mazao ya misitu, ufugaji wa nyuki na utengenezaji wa majiko banifu ili kupunguza matumizi ya mkaa. Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa iliendesha mafunzo ya siku 3 kwa wawakilishi wa kamati za vijiji vya Nandenje, Kipindimbi, Lichwachwa, Ng'au na Nahanga. Mafunzo yalijumuisha faida zinazotokana

na uhifadhi wa misitu. Halmashauri za Wilaya za Lindi na Kilwa, pamoja na mafunzo haya, washiriki walifundishwa namna ya kupima kiasi cha hewa ukaa inayofyonzwa na miti ndani ya misitu pamoja na matumizi ya tekinolojia ya GPS. Mafunzo haya yaliendeshwa na wataalamu kutoka mradi wa MKUHUMI. Uhifadhi wa misitu kwa Halmashauri za Wilaya za Lindi na Kilwa ulichangia kupata mapato kutoka MKUHUMI ambapo malipo yalifanyika kutokana na kiasi cha hewa ukaa kilichofyonzwa na miti ndani ya misitu. Picha ifuatayo inaonyesha wajumbe wa kamati kutoka H/W ya Kilwa wakihudhuria mafunzo.



***Mafunzo yakiendelea***

***Kuandaa ramani ya msitu;*** kuandaa ramani ya msitu kunahusisha uandaaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi. Mpango huu unaonesha eneo kwa ajili ya misitu, makazi, mashamba na maeneo mengine kwa ajili ya huduma za jamii. Katika H/W ya Kilwa, Kijiji cha Nanjirinji wanakijiji waliandaa ramani kuonyesha maeneo ya msitu ambayo wanaruhusiwa kuvuna raslimali za msitu, maeneo ambayo hayaruhusiwi kuvunwa kwa ajili ya uhifadhi wa aina za miti adimu na viumbe wa msituni. H/W za Lindi, Ruangwa na Chunya ziliwezesha wanakijiji kuandaa ramani ya misitu kwa kutenga maeneo ya msitu kulingana na matumizi. Mipaka ya maeneo ya misitu iliwekwa kwa kuzingatia alama au mipaka ya asili kama mito na miti mikubwa.  Katika kuandaa ramani kwa ajili ya matumizi ya misitu, wajumbe wa kamati za misitu za vijiji walihusishwa. Vifaa vilivyotumika awali kuandaa mipaka ya utambuzi wa misitu ni kama mawe, majivu na mchanga. Baada ya ramani iliyoandaliwa na kijiji, wataalamu walizitumia ramani hizo kuandaa ramani ya kitaalamu inayobainisha maeneo kwa ajili ya wanyapori, maeneo ya kuvuna mazao ya misitu, na maeneo ya uhifadhi wa misitu. Picha ifuatayo inaonesha wanakijiji wakishiriki katika kuandaa mpango wa matumizi bora ya msitu.



***Wanakijjii wakishiriki kuweka mipaka ya misitu H/W ya  Lindi***

***Kuandaa mipango ya usimamizi wa misitu ya Vijiji;*** mpango wa usimamizi wa msitu wa kijiji unahusisha shughuli za ulinzi wa msitu, uvunaji wa mazao ya misitu, ukusanyaji wa mapato kutokana na raslimali za misitu na matumizi ya mapato yanayokusanywa. Ili kufanikisha zoezi la uandaaji wa mpango huu, wataalamu kutoka ngazi ya Halmashauri za Wilaya kupitia mikutano mikuu ya Vijiji walitoa mwongozo wa namna ya kuandaa mpango. Kupitia kamati za misitu za vijiji, mpango wa usimamzi wa misitu uliandaliwa na kuwasilishwa Halmashauri ambapo uliidhinishwa na timu za wataalamu na Mabaraza ya Madiwani.

***Kuanzisha sheria ndogo ya utunzaji misitu;*** Mchakato wa kuanzisha sheria ndogo ya kulinda misitu ulifanyika kwa kuwashirikisha wataalamu kutoka Halmashauri za Wilaya. Wataalamu walisaidia kutoa mwongozo kwa kamati ya usimamizi misitu ya kijiji kutunga sheria ndogo itakayosimamia mavuno ya misitu, tozo za mazao ya misitu zinazolipwa kwa Serikali za Vijiji, mpango wa matumizi ya mapato yatokanayo na raslimali za misitu, adhabu na faini atakazotozwa mwananchi atakayekiuka sheria ya utunzaji misitu. Sheria ndogo zilizoandaliwa na kamati ziliwasilishwa kwenye mikutano mikuu ya Vijiji ambapo ziliridhiwa na baadaye kuwasilishwa Halmashauri na kuridhiwa kuwa sheria ndogo za Vijiji za kutunza misitu.

***Kuanzisha timu za Ulinzi wa Misitu;*** ili kuhakikisha wananchi wanasimamia sheria, mikutano mikuu ya vijijii ilianzisha timu za ulinzi wa misitu. Timu hizi zilipewa jukumu la kufuatilia na kufanya doria ndani ya misitu ili kubaini wavamizi, kudhibiti vitendo haramu ndani ya misitu na kuwasilisha taarifa kuhusu hali halisi ndani ya misitu kwa kamati za misitu za Vijiji kila wiki. Ili kuhakikisha timu za ulinzi za misitu zinatekeleza majukumu yao kwa ufanisi, Halmashauri zilitoa vitendea kazi kama buti, hema, vifaa vya GPS, pikipiki, baiskeli na vifaa vingine kama panga na jembe.

***Kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya majiko banifu;*** H/W ya Chunya kwa kushirikiana na wataalamu kutoka shirika la TATEDO walitoa mafunzo kwa wananchi juu ya namna ya kutengeneza na kutumia majiko bora yanayotumia kuni kidogo ili kuepuka au kupunguza matumizi ya mkaa. Katika kuhakikisha elimu ya uhifadhi misitu inakuwa endelevu, walimu wa shule za msingi na waratibu wa elimu ngazi ya Kata kwa H/W za Lindi na Kilwa walipewa mafunzo juu ya uhifadhi wa misitu na namna ya kuingiza elimu hiyo kwenye mitaala ya shule ili kuwafanya watoto kufahamu umuhimu wa kuhifadhi misitu na hivyo kujifunza uhifadhi misitu na raslimali za misitu kuanzia umri mdogo.

**5.0 RASLIMALI**

Utekelezaji wa mpango wa uhifadhi misitu shirikishi ulihusisha matumizi ya raslimali. Halmashauri ziligharamia mpango kwa kutoa raslimali fedha, raslimali watu na vitendea kazi. Ufafanuzi kuhusu rasilmali kwa kila Halmashauri umeanishwa kama ifuatavyo;

***Matumizi ya Raslimali H/W ya Chunya;*** utekelezaji wa shughuli za uhifadhi misitu shirikishi kwa kiasi kikubwa ulifadhiliwa na Serikali ya Denmark kupitia shirika lake la maendeleo la DANIDA. Kwa upande wa raslimali watu, wataalamu wa Halmashauri, TATEDO na Shirika la Huduma za Misitu Tanzania walitoa mafunzo na mbinu za kusimamia, kutunza na kuhifadhi Misitu kwa Kamati za uhifadhi misitu za vijiji. Kwa upande mwingine, raslimali watu zilijumuisha wajumbe wa kamati za uhifadhi misitu za kijiji na timu za ulinzi wa misitu za Vijiji. Raslimali nyingine ni pamoja na vitendea kazi kama vifaa vya usafiri na shajala kwa ajili ya kuandika taarifa za maendeleo ya misitu. Jedwali Na. 2 linatoa ufafanuzi wa raslimali fedha zilizotumika kuanzia mwaka wa fedha 2003/2004.

**Jedwali Na 2: Raslimali za mpango wa uhifadhi misitu shirikishi**

| Na. | Mwaka wa Fedha | Kiasi cha fedha (TSh) |
|---|---|---|
| 1 | 2003/2004 | 33,000,000 |
| 2 | 2004/2005 | 21,652,000 |
| 3 | 2005/2006 | 29,085,000 |
| 4 | 2006/2007 | 54,723,000 |
| 5 | 2007/2008 | 82,000,000 |
| 6 | 2008/2009 | 3,313,000 |
| 7 | 2009/2010 | 0 |
| 8 | 2010/2011 | 40,832,000 |
| 9 | 2011/2012 | 91,055,000 |
| 10 | 2012/2013 | 100,188,000 |
| 11 | 2013/2014 | 25,000,000 |
| Total | | **480,989,000** |

***Matumizi ya Raslimali H/W ya Kilwa;*** Utekelezaji wa mpango wa uhifadhi shirikishi misitu ulitekelezwa kwa gharama ya shilingi million 48. Fedha hizi zilitumika kununulia mahitaji muhimu katika utunzaji misitu, kugharamia mafunzo kuhusu kufanya tathimini ya raslimali za misitu, utawala bora, na mafunzo juu ya namna ya kupima mzingo wa miti na namna ya kuandaa matumizi bora ya ardhi. Raslimali watu zilijumuisha wataalamu kutoka Halmashauri ambao ni Afisa Maendeleo ya Jamii, Afisa Ardhi na Mwanasheria wa Halmashauri ambao walihusika kuunganisha jamii kukubali kutekeleza uhifadhi shirikishi wa misitu. Shirika la maendeleo na Uhifadhi Misitu la Mpingo lilitoa msaada wa kitaalamu kwa kujenga uwezo wa wananchi kuhusu uhifadhi wa misitu. Kwenye ngazi za Vijiji raslimali watu zilijumuisha wajumbe wa serikali ya kijiji, wajumbe wa kamati ya maliasili na wanakijiji wote waliotekeleza mpango.

***Matumizi ya Raslimali H/W ya Lindi;*** katika kutekeleza uhifadhi shirikishi wa misitu Halmashauri ilipokea ufadhili wa raslimali fedha kutoka Serikali ya Norway kupitia shirika la Maendeleo la Norway (NORAD). Raslimali watu ni pamoja na wataalamu kutoka ngazi ya Halmashauri, jamii yenyewe, viongozi wa Kata na Vijiji waliohusika kwenye uhifadhi shirikishi wa misitu. Ushiriki wa vijiji kwenye jitihada hii katika H/W ya Lindi umebainishwa kwenye Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3: Vijiji vilivyomo kwenye Uhifadhi Shirikishi H/W ya Lindi**

| NA. | KATA | VIJIJI |
|---|---|---|
| 1 | Rutamba | Rutamba ya Sasa , Kinyope, Ruhoma |
| 2 | Milola | Milola Magharibi |
| 3 | Kiwawa | Kiwawa |
| 4 | Nangaru | Muungano, Makumba, Mkombamosi |
| 5 | Matimba | Moka, Matimba, Kikomolela, Likwaya |
| 6 | Mipingo | Lihimilo, Namkongo |

***Matumizi ya Raslimali H/W ya Ruangwa;*** utekelezaji wa uhifadhi shirikishi wa misitu ulifanyika katika vijiji vya Nandenje, Kipindimbi, Lichwachwa, Ng’au and Nahanga. Raslimali fedha zilitumika kununua vitendea kazi vya uhifadhi misitu, kugharamia mafunzo kwa kamati za uhifadhi misitu za Vijiji. Jedwali Na. 4 linafafanua kiasi cha fedha zilizotumika katika utekelezaji. Mbali na raslimali fedha, raslimali nyingine zilizotumika ni pamoja na gari aina ya Toyota Hilux 2.8 iliyotolewa kama msaada na Idara ya Ufugaji Nyuki ya Wizara Maliasli na Utalii. Gari hili lilitolewa ili kurahisisha usafiri katika kutekeleza shughuli za uhifadhi misitu.




*Gari kwa ajili ya kurahisisha shughuli za ufatiliaji misiti*

**Jeduwali Na. 4 Raslimali fedha H/W ya Ruangwa**

| Mwaka wa Fedha | Kiasi cha fedha kilichotolewa |
|---|---|
| 2005/2006 | 25,000,000.00 |
| 2006/2007 | 70,000,000.00 |
| 2007/2008 | 70,000,000.00 |
| 2008/2009 | 68,901,000.00 |
| 2009/2010 | 25,550,000.00 |
| Total | **259,451,000.00** |

## 6.0 MATOKEO

Utekelezaji wa jitihada ya uhifadhi Shirikishi wa misitu katika Halmashauri hizi 4 umechangia kuboresha maisha kwa jamii za vijijini na umeongeza mapato kwa Halmashauri za vijiji ambapo mapato hayo yamewezesha kujenga na kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo. Ufafanuzi kuhusu matokeo ya utekelezaji wa uhifadhi shirikishi wa misitu kwa kila Halmashauri ni kama ifuatavyo;

**Matokeo ya Uhifadhi Shirikishi wa Misitu H/W ya Chunya:** uhifadhi shirikishi wa misitu katika H/W ya Chunya umeleta matokeo yafuatayo; misitu ya Vijiji 15 imeanzishwa na inamilikiwa na wanakijiji wa Kata za Kipebwawe, Kwimba na Songwe. Kamati za uhifadhi misitu za vijiji 15 zimeanzishwa na zinafanya kazi kwa ufanisi, kukusanya mapato yatokanayo na mazao ya misitu, kusimamia matumizi ya mapato katika kutekeleza miradi ya maendeleo ya vijiji na kutoa taarifa ya utekelezaji kwenye mikutano mikuu ya vijiji. Kutokana na mapato ya misitu, jamii zimepunguziwa mzigo wa kuchangia fedha za miradi ya maendeleo ya vijiji. Fedha hizo hutumika kutekeleza miradi ya maendeleo kijijini; kwa mfano Vijiji 4 vimeweza kutekeleza miradi ya maendeleo kutakana na fedha zilizokusanywa kutokana na tozo ya mkaa. Kijiji cha Mapogoro kilijenga nyumba 3 za wahudumu wa afya, nyumba ya mwalimu mkuu wa shule, nyumba ya afisa mtendaji wa kijiji, kuchimba kisima kirefu cha maji na kujenga miundominu ya maji, kujenga vyoo vya shule, kutengeneza madawati 150 na kukarabati madawati 60. Utekelezaji wa miradi hii ulitumia jumla ya shilingi za kitanzania 74,000,000 kutokana na misitu. Kama sio mazo ya misitu wananchi wa kijiji cha Mapogoro wangelazimika kuchangia fedha hizo kutokana na vipato vyao wenyewe. Kufuatia jitihada za kijiji cha Mapogoro, Balozi wa Dernimak aliwazawadia shs 39,000,000 kukamilisha mradi wa maji. Mbali na matokeo haya, Kamati ya Uhifadhi Misitu ya Kijiji cha Mapogoro imekuwa ikifadhili michezo kwa kupatia vijana mahitaji ya michezo na kuandaa mashidano ya michezo katika ngazi za Vitongoji. Vitongoji 4 vya kijiji cha Mapogoro vimekuwa vikishiriki mashindano ya michezo yanayofadhiliwa kutokana na fedha inayokusanywa kutoka kwenye msitu wa kijiji. Kutokana na uhifadhi wa misitu ya kijiji cha mapogoro,

wanyapori ambao walitoweka hapo awali kutokana na uharibifu wa mazingira wameanza kurudi, simba 3, pundamilia 4 na wanyama wadowadogo wameweza kuonekana. Mafanikio haya yanaonekana kwenye picha zifuatazo.



***Miradi iliyotekelezwa kwa fedha za mapato ya  misitu katika kijiji cha  Mapogoro***

Katika Kijiji cha Shoga, fedha zilizotokana na mazao ya misitu zimewezesha kujenga zahanati ya kijiji, madarasa 2 katika shule ya Sekondari Chalangwa, Ofisi ya kijiji na chumba cha kuhifadhi wahalifu. Vilivile, fedha hizo zilitumika kukarabati madarasa 3, ofisi 1 ya mwalimu na nyumba 5 za waalimu kwa gharama ya shs 53,365,300.  Kijiji cha Mamba pia kilijenga ofisi ya kijiji,  madarasa 3 ya shule na kufanya ukarabati wa jengo la zahanati. Kutokana na fedha hizo, kijiji kilinunua bati 300 kwa ajili ya kupaua madarasa 3 na kununua pikipiki kwa ajili ya doria ya msitu. Gharama zilizotumika ni shs 18,310,200.  Kijiji cha Mbangala kimejenga madarasa 2, ofisi ya kijiji, choo cha shule, nyumba ya mwalimu na kukarabati nyumba nyingine 2 za waalimu kwa gharama ya shs 49,346,000 ambazo zimetokana na tozo ya mazao ya misitu.



***Madarasa ya shule katika kijiji cha  Mbangala yaliyojengwa kwa fedha za misitu***



***Nyumba ya mwalimu na pikipiki ya doria katika kijiji cha Mbangala***

Tokeo jingine muhimu ni kuenea kwa dhana ya utunzaji shirikishi wa misitu; Baada ya vijiji jirani kuona matokeo na faida zinazotokana na misitu, vimeanza kuiga uhifadhi shirikishi wa misitu. Hali hii inasaidia kuongeza eneo la uhifadhi wa misitu hivyo kusaidia kutunza mazingira kwa maendeleo ya sasa na ya baadae.

***Matokeo ya uhifadhi shirikishi wa Misitu H/W ya Kilwa****;* msitu wa hifadhi wa Nanjirinji pamoja na misitu mingine ya vijiji imeifanya Halmashauri kutambulika kama Halmashauri Kiongozi wa kuhifadhi Misitu ya Vijiji Afrika. Mbali na matokeo katika ngazi ya Wilaya, Kijiji cha Nanjirinji kimeonyesha matokeo makubwa kutokana na uhifadhi wa misitu. Uelewa wa jamii kuhusu kuhifadhi misitu umeongezeka kwa kiasi kikubwa, dhana ya umililiki wa misitu kwa jamii imeongezeka kutokana na mafunzo juu ya uhifadhi misitu yaliyotolewa na Mradi wa Uhifadhi Misitu wa Mpingo pamoja na Halmashauri. Wananchi wanakiri kunufaika na mazao ya misitu kama mama Hadija Makokoto alivyonukuliwa akisema;



***"Nazijua faida za misitu kwahiyo nitailinda na kuitunza "***
***Mama Hadija Makokoto Kutoka Kijiji cha Nanjirinji "A" akisimulia***

Kijiji cha Nanjirinji kimepata umaarufu mkubwa Tanzania juu ya uhifadhi shirikishi wa misitu, hivyo kimekuwa kikipokea wageni kwa lengo la kujifunza na kufanya utalii. Vijiji vya jirani kama Nanjirinji B, Nakiu, Likawage, na Makangaga vimevutiwa na faida za uhifadhi misitu na kuamua kujihusisha na shughuli za uhifadhi misitu. Mwaka 2014 mwanakijiji mmoja alipata mwaliko kwenda nchini Finland kwa lengo la kutoa uzoefu wa namna kijiji kilivyofanikiwa kuhifadhi msitu. Kutokana na kutambilika kwa H/W ya Kilwa kama kiongozi katika kusimamia uhifadhi wa misitu, ari ya wanakijiji cha Nanjirinji imeongezeka hivyo kuwafanya waongeze ukubwa wa eneo la msitu kwa 13,000ha zaidi.

Kijiji cha Nanjirinji kimegeuka kuwa sehemu ya mafunzo kuhusu namna ya kusimamia uhifadhi wa misitu. Halmashauri nyingi, kwa mfano H/W za Muheza, Korogwe, Kibaha, Tunduru na Liwale ziliweza kutembelea Kijiji cha Nanjirinji mwaka 2014 na 2015 kwa lengo la kujifunza. Kijiji pia kimekuwa kikipokea watafiti,

wanafunzi na wanavijiji wa nchi mbalimbali, kwa mfano Uingereza, China na Namibia wambao wanakuja kwa lengo la kujifunza na utalii. Mbali na matokeo haya, Kijiji pia kimeweza kuongeza mapato yake kutokana na mazao ya misitu. Kwa sasa kijiji kinapokea 90% ya fedha zinazotokana na mazao ya misitu kutoka 5% ambayo kilikuwa kikipokea hapo awali kutoka Serikalini. 10% ya mapato inayobaki ndiyo inayogawanywa kwa Halmashauri ya Wilaya na MCDI. Mwaka 2012 hadi 2015 kijiji kiliweza kukusanya jumla ya shs 287,000,000 kutokana na mazao ya misitu. Kabla ya jitihada hii mapato ya kijiji yalikuwa chini ya shs 30,000,000 kwa mwaka, ambapo baada uhifadhi mapato yaliongezeka hadi shs 95,000,000 kwa mwaka; ongezeko la shs 65,000,000 sawa na 68.42% kwa mwaka.

Mapato yaliyopatikana kutokana na mazao ya misitu yameweza kuboresha huduma za jamii; kwa mfano fedha zilizokusanywa zimeweza kutumika kuanzisha shule ya msingi ambapo madarasa 3, stoo na offisi ya waalimu zimejengwa kwa gharama ya sh 57,000,000 na nyumba moja ya mwalimu ya thamani ya shs 20,000,000 imejengwa. Huduma nyingine ni pamoja na ujenzi wa soko kwa ajili ya biashara ndogondogo kwa gharama ya shs 20,000,000 na ujenzi wa visima vifupi 5 kwa gharama ya shs 16,000,000.



***Madarasa 3 ya shule, ofisi ya walimu na store zilizojengwa kwa fedha za misitu***



***Mojawapo ya kisima kilichojengwa kutokana na fedha za misitu***

Mapato yaliyokusanywa kutokana na mazao ya misitu yamewezesha ujenzi wa shule ya awali katika Kitongoji cha Kitochi kwa thamani ya shs 20,000,000. Fedha nyingine zimetumika kujenga Kituo cha Polisi kwa gharama ya shs 10,000,000 na kununua sare za shule za watoto 323 zenye thamani ya shs 2,261,000. Mbali na matumizi haya, wajawazito wapatao 152 walipatiwa shs 50,000 kila mmoja kufanya maandalizi ya mtoto atakayezaliwa ili kupunguza vifo vya mama na mtoto. Jumla ya shs 7,600,000 zilitolewa kwa wajawazito.



***Wanafunzi wakiwa wamevalia sare zilizonunuliwa kwa fedha za misitu***



***Baadhi ya kinamama wajawazito waliopatiwa fedha za maandalizi***

Matokeo mengine ni pamoja na ununuzi wa sare 17 za kamati ya uhifadhi misitu ya kijiji kwa gharama ya shs 1,400,000, ununuzi wa pikipiki 3 kwa ajili ya kurahisisha doria kwa gharama ya shs 6,000,000, ununuzi wa viti 100 kwa ajili ya kuendesha mikutano ya kijiji kwa thamani ya shs 1,800,000, ununuzi wa turubai 2 na magodoro 6 kwa ajili ya doria vyenye thamani ya shs 650,000.  Vilevile kijiji kina akiba ya jumla ya shs 90,000,000 kwenye akaunti ya benki.

***Matokeo ya Uhifadhi Shirikishi wa Misitu H/W ya Lindi;*** Tokeo la kwanza kwa vijiji vyote viliyotekeleza jitihada hii, vimeweza kuandaa mpango bora wa matumizi ya ardhi. Picha zifuatazo zinaonesha vibao vya kuainisha maeneo yaliyopangwa kutokana na matumizi.









***Vibao vikionesha matumizi ya ardhi katika kijiji cha Likwaya***

Vijiji vyote vimeweza kuanzisha kamati imara za kuhifadhi misitu ya vijiji na kutunga sheria ndogo ya kudhibiti vitendo vinavyoweza kuhatarisha misitu. Kutokana na kuanzisha kamati hizi ugatuaji wa uhifadhi wa misitu kutoka Serikali Kuu kwenda kwa wananchi umefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Wananchi wameweza kusaidiwa kupata hati miliki za ardhi za kimila baada ya mpango wa matumizi bora ya ardhi. Halmashauri imeweza kupima eneo la hifadhi ya misitu 27,800ha. Jumla ya shs 200,000,000 zilitolewa na serikali ya Norway kama motisha wa kutunza misitu. Fedha hizi litolewa kufidia kasi cha hewa ukaa inayofyonzwa na misitu inayohifadhiwa na jamii. Fedha hizo zilitumika kutoa huduma za kijamii kama ujenzi wa nyumba za waalimu katika kijiji cha Likwaya na ofisi 8 za vijiji ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Tokeo jinginie ni udhibiti wa uvunaji holela wa misitu ambao umesaidia kutunza mazingira na kuboresha tabia nchi.



***Wanakijiji wakipokea fedha kutokana na kuuza hewa ukaa***




***Ujenzi wa ofisi ya kijiji cha Kinyope ukiendelea na ofisi ya kijiji cha Likwaya ikiwa imekamilika***




***Ujenzi wa nyumba ya mwalimu shule ya msingi  Likwaya***



***Wananchi wakiwa kwenye shughuli za kuvuna mazao ya misitu***

Kuna uboreshaji mkubwa wa mgawanyo wa mapato yatokanayo na misitu kati ya Serikali Kuu, Halmashauri ya Wilaya na Halmashauri ya Kijiji. Kulingana na mgawanyo wa sasa, Kijiji kinapokea 80%, Halmashauri ya Wilaya 15% na 5% ya mapato inakwenda Serikali Kuu. Mfumo wa doria ndani ya misitu umeboreshwa na kamati ya usimamizi wa misitu inafanya doria mara moja kwa wiki ili kutambua vitendo haramu vinavyoendelea ndani ya misitu. Jamii imeweza kufaidika na msitu kutokana na urahisi wa upatikanaji wa mbao na mahitaji mengine ya ujenzi bila gharama kwa mashariti kwamba nyumba inayojengwa ndani ya kijiji ni kwa ajili ya makazi.

Mitandao thabiti ya Vijiji vinavyotekeleza uhifadhi wa misitu imeanzishwa chini ya  MJUMITA  vijiji 8, MHIMIRO (Mtandao wa Hifadhi Misitu kata ya Rutamba) vijiji 3, UMICHITA  (Uhifadhi wa Misitu kata Chikonji na Tandangongoro) vijiji 3, MHIMINA (Mtandao wa Uhifadhi wa Misitu Nangaru)  vijiji 6 na UMIKIWAMI (Uhifadhi wa Misitu Kata ya Kiwawa na Milola) vijiji 2. Vilevile wanafuzi 5416 kutoka shule za msingi 12 wamejiunga na klabu za mazingira ambapo wanajishughulisha na upandaji miti na kuhamasisha jamii kuendelea kuhifadhi mazingira.

***Matokeo ya Uhifadhi Shirikishi wa  Misitu H/W ya Ruangwa*;** Misitu ya hifadhi ilikabidhiwa kwa kila kijiji mnamo mwezi Mei 2011 baada ya kusimamiwa na kujengewa uwezo. Vijiji vinafaidika na 90% ya mapato yanayotokana na misitu kuanzia mwaka 2012 hadi mwaka 2015. Mapato ambayo vijiji vimekuwa vikipokea yamebainishwa kwenye jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na 5: Mapato yatokanayo na mazao ya misitu**

| Na. | Kijiji | Kiasi cha mapato(TSH) |
|---|---|---|
| 1 | Nandenje | 82,347,752.00 |
| 2 | Lichwachwa | 32,340,00.00 |
| 3 | Kipindimbi | 13,770,560.00 |
| 4 | Nahanga | 30,865,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | Ng'au | 60,116,472.00 |

Kama ilivyothibitika kwenye H/W za Lindi, Chunya na Kilwa, Vijiji vya H/W ya Ruangwa vimefanikwa kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo ilishindikana hapo awali. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa zahanati na nyumba za wahudumu wa afya katika kijiji cha Nandenje. Vilevile ujenzi wa ofisi za vijiji vya Lichwachwa, Nandenje na Nahanga kutokana na fedha za mazao ya misitu



***Zahanati iliyokamilika na nyumba ya mganga ikiwa inaendelea kujengwa***



***Ofisi za vijiji vya Lichwachwa, Nandenje na Nahanga***

Shughuli za Kilimo zimeimarika baada ya Serikali za Vijiji vya Nahanga na Nga'u kununua trekta ambazo zinatumika kulima mashamba ya wananchi. Kijiji cha Nahanga pia kimeweza kujenga madarasa 2 na shule ya awali ya Kijiji kutokana na raslimali zitokanazo na misitu.



***Madarasa 2 na shule ya awali iliyojengwa katika kijiji cha Nahanga***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Matokeo ya Uhifadhi Shirikishi wa Misitu yanapaswa kuwa endelevu. Ili kuhakisha yanabaki kuwa endelevu Halmashauri zote 4 zimeweka mikakati ya uendelevu. Mikakati hii ni pamoja na; kuendelea kuhamasisha jamii kutunza misitu na kufanya mavuno kulingana na mpango wa mavuno wa kijiji kama ulivyoandaliwa. Halmashauri husika zinaendela kutoa msisitizo wa kutumia majiko banifu ili kupunguza matumizi ya mkaa na kuni nyingi. Kila mwaka Halmashauri zimekuwa zikitenga bajeti ya kuanzisha misitu mingine ili kuongeza wigo wa eneo lililohifadhiwa. Mbali na mikakati hii, Halmashauri zimekuwa zikianzisha shughuli mbalimbali za kiuchumi ndani ya misitu za kuwaongezea wananchi kipato na kuendelea kulinda misitu kama ufugaji wa nyuki. Kamati za misitu za vijiji zimekuwa zikipatiwa fedha kama motisha wa kuendelea kusimamia uhifadhi wa misitu.

Mikakati ya uendelevu kwa Halmashauri ya Kilwa  ni pamoja na kuimarisha doria ya misitu ya kijiji kwa kuanzisha zamu ya doriana motisha kwa wajumbe wa kamati ya maliasili ya kijiji ambayo inafanya doria ya kulinda misitu kwa zamu. Halmashauri imekua ikisisitiza kuzingatia mpango wa mavuno ya mazao ya misitu na kulinda misitu. Mafunzo kwa kamati za maliasili za kjiji yamekuwa yakitolewa kuwajengea uwezo na hamasa yakuendelea kutunza misitu, Katika kulinda athari za moto kwa misitu Halmashauri imekua ikiendesha zoezi la kuchoma mipaka kuzunguka misitu ili kuzuia moto kuvuka kuingia na kuteketeza misitu. Vile vile wakati wa mavuno halmasahuri imetoa muongozo wa namna ya kuvuna mti ambapo mti unakaktwa chini kabisa kwenye shina ili kuruhusu uweze kuchipua upya.



*Zoezi la kuchoma mipaka ya msitu likiendelea*



*Mfano wa Uvunaji wa mti wa mpingo unaosisitizwa*

Mikakati endelevu kwa H/W ya Lindi ni pamoja na kuendeleza ushirikano na wadau mbalimbali katika kuhamasisha utunzaji shirikishi wa misitu, kutenga maeneo ya misitu na kusisitiza matumizi bora ya ardhi, kundeleza jitihada za kuwajengea uelewa wanakijiji kutoka vijiji vingine ili kupokea dhana ya ugatuzi wa usimamizi wa misitu na kuendelea kuhamasisha kilimo hifadhi ili kulinda mazingira. Mikakati mingine ni pamoja na kutoa mafunzo na elimu kwa umma hasa viongozi wa vijiji juu ya namna ya kutunza na kukuza misitu kwa manufaa ya jamii na kundelea kufanya utafiti kuhusu misitu na raslimali za asili zinazopatikana kwenye misitu ambazo zinaweza kunufaisha jamii. Mwisho, kujenga mtandao wa mawasiliano na jamii ili kupata taarifa juu ya masuala mabalimbali na vitendo vinavyoendelea ndani ya misitu inayoweza kuharibu misitu ili vitendo hivyo vidhibitiwe mapema.

H/W ya Ruangwa imeweka mikakati ya uendelevu wa matokeo ya jitihada hii. Mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kusisitiza wanakijiji kufuata mipango ya uvunaji bora wa misitu kama ilivyoainishwa, kusimamia sheria ndogo za misitu, kuendelea kuwajengea uwezo wajumbe wa kamati za maliasili kuhusu utunzaji wa misitu, kuendelea kutenga maeneo ya kuanzisha misitu mingine na kushirikisha jamii katika kuitunza, kuendelea kutoa motisha kwa kamati za vijiji za usimamizi wa raslimali za misitu na kuelimisha jamii kwa kutumia mabango yenye ujumbe unaohamasisha uhifadhi wa misitu.



***Mabango ya kusisitiza uhifadhi wa misitu***

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Mafanikio ya utekelezaji wa jtahada ya Uhifadhi Shirikishi wa Misitu yametokana na uongozi wa pamoja, dhamira thabiti ya Timu za Menejimenti za Halmashauri, utayari wa jamii kupokea mradi baada ya kufanyiwa ushawishi, utayari wa viongozi wa kisiasa kuukubali na kuutangaza uhifadhi shirikishi wa misitu na ushirikiano wa wadau mbalimbali kama MCDI, WWF, TFCG na TFCGN MJUMITA. Halmashauri zote zilifanya suala la uhifadhi shirikishi wa misitu kuwa ajenda ya kudumu kwenye vikao katika ngazi zote. Vilevile Halmashauri zimekua zikiandaa mikutano ya wadau wa misitu kila mwaka kujadili mikakati ya kuhifadhi misitu, faida za misitu na changamoto zilizopo.

Dhana ya umiliki wa misitu iliyojengeka ndani ya nafsi za wanakijiji baada ya kupewa mafunzo ni siri ya mafanikio. Kujengeka kwa dhana ya uaminifu kwenye ngazi zote za Serikali pamoja na ugatuajii wa shughuli za usimamizi wa misitu kutoka Serikali Kuu kwenda kwa wananchi ni siri nyingine ya mafanikio. Fedha zilizotolewa na MKUHUMI kama malipo ya hewa ukaa iliyofyonzwa na miti ilipelekea jamii kuhamasika na kuwa na utayari wa kuendeleza uhifadhi wa misitu. Uwazi katika mapato na matumizi ya fedha zitokanazo na misitu kwa wananchi ni moja ya siri ya mafanikio.




***Wananchi wakipokea fedha za Mazao ya misitu kwa Uwazi***

# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO

**UPANGAJI SHIRIKISHI WA MJI WA LWANGWA**







***UZOEFU WA H/W YA BUSOKELO***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo ni moja kati ya Halmashauri mpya zilizoanzishwa hapa Tanzania. Halmashauri hii ilianzishwa mwaka 2012 baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kugawanywa kwa lengo la kusogeza huduma karibu na jamii. Kijiografia, H/W ya Busokelo ipo kati ya Latitudo $8^0$30 na $9^0$30 Kusini na Longitudo $33^0$ na $34^0$ Mashariki. Halmashauri inaambaa na safu za milima ya Rungwe na Livingstone kwa urefu kati ya 770m na 2,265m juu ya usawa wa bahari. H/W ya Busokelo inapakana na H/W za Kyela kwa upande wa Kusini, Rungwe upande wa Magharibi, Makete upande wa Mashariki, na Mbeya upande wa Kaskazini. Makao makuu ya Halmashauri yapo Mji wa Lwangwa ambao ni kilomita 47 kutoka mji wa Tukuyu. Kiutawala, Halmashauri imegawanyika tatika Kata 13, Vijiji 56, Vitongoji 231 na Kaya 2,773. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, idadi ya watu ni 96,348 ambapo kati yao 53,704 ni wanawake na 43,142 ni wanaume.




***Ramani ya H/W ya Busokelo na maeneo ya kiutawala***

Hali ya hewa katika Halmashauri hii ni nzuri na huruhusu uzalishaji wa mazao ya kilimo. Hali ya joto ni kati ya $18^0$C na $25^0$C na wanstani wa mvua kwa mwaka ni kati ya 900mm katika maeneo ya tambarare na 2700mm katika maeneo ya mwinuko. Halmashauri ina jumla ya eneo la 969.14km$^2$ ambapo 85% ya eneo hutumika kwa shughuli za kilimo na 15% iliyobaki ni eneo la hifadhi za misitu, milima na makazi. Shughuli za kijamii na kiuchumi katika Halmashauri ni pamoja na uzalishaji wa mazao, ufugaji, ufugaji wa nyuki, uvuvi na mazao ya misitu.

**2.0 TATIZO**

Kufuatia kuanzishwa kwa H/W ya Busokelo mwaka 2012, Mji mdogo wa Lwangwa uliteuliwa kuwa makao makuu ya Halmashauri. Hata hivyo, Mji huu haukuwa umepimwa na hapakuwa na mipango miji hali iliyopelekea kukosekana kwa miundombinu ya kutolea huduma za kijamii na za kiuchumi kwa umma. Vilevile ukuaji wa makazi holela uliongezeka kutokana na kuongezeka kwa uhitaji wa nyumba

uliosababishwa na ongezeko la idadi ya watu kwa kuzaliana na wahamiaji ambao waliingia Busokelo kutafuta fursa za kujiimarisha kiuchumi baada ya kuanzishwa kwa Halmashauri mpya.

Kutokana na kasi ndogo ya ugawaji wa viwanja vilivyopimwa ukilinganisha na mahitaji makubwa, bei za viwanja vilivyopimwa na ukubwa wa maeneo vilipo viwanja, ilipelekea kuendelea kuongezeka kwa ukuaji wa makazi holela katika maeneo ambayo hayajapimwa. Wamiliki wengi wa ardhi waliendelea kugawa na kuuza vipande vya ardhi bila kupata mwongozo kutoka Halmashauri. Hali hii ilipelekea kuendelea kuanzisha makazi holela. Ugawaji huu wa ardhi haukuzingatia kutenga maeneo kwa ajili ya barabara, mifereji ya maji, maeneo ya wazi na maeneo ya kujenga miundominu ya kutolea huduma za jamii kama stendi ya magari, soko, kituo cha polisi, hospitali, shule, taasisi za fedha, vituo vya afya na ofisi za Halmashauri. Usafi wa mazingira haukuwa wa kuridhisha kutokana na kukosekana kwa mikakati ya kukabiliana na taka ngumu na ukosefu wa mitaro ya maji taka. Kutokana na changamoto hizi, umuhimu wa kupanga mji wa Lwangwa ulijitokeza ili kurahisisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi wa Busokelo kwa ufanisi.



***Njia za watembea kwa miguu kabla ya kupanuliwa kuwa barabara.***

**3.0 MALENGO**

Lengo kuu la mpango huu ni kuanzisha makao makuu ya Halmashauri yaliyopangwa vizuri katika Kata ya Lwangwa ili kurahisisha utoaji wa huduma bora kwa ufanisi. Malengo mahususi ni pamoja na; kupata ardhi ndani ya mji wa Lwangwa itakayopimwa na kupangwa vyema ili kuainisha maeneo kwa ajili ya makazi, biashara na maeneo ya huduma za kijamii, kufungua fursa ya umiliki wa ardhi kisheria, kufungua barabara na kuboresha njia za watembea kwa miguu ili ziwe barabara rasmi kurahisisha kufunguka kwa mji na upatikanaji wa huduma.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Utekelezaji wa mbinu hii ulihusisha mikakati mabalimbali. Mwanzoni kabisa, Halmashauri haikuwa na fedha za kutosha kutoka kwenye vyanzo vyake kwa ajili ya kugharamia zoezi la upangaji wa mji. Hii ilipelekea Halmashauri kutafuta mbia wa kushikiana naye. Mwaka 2012 Halmashauri iliamua kushirikiana na UTT kupima viwanja katika mji mdogo wa Lwangwa. Wazo la kushirikiana na UTT liliibuliwa na Timu ya Menejimenti ya Halmashauri ambayo iliwasilisha wazo hilo kwenye Baraza la Halmashauri kujadiliwa na kupitishwa. Kama ilivyo hitaji la kisheria, Halmashauri ilipaswa kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kuingia ubia na UTT. Kwa bahati mbaya kulikuwa na ucheleweshwaji wa kibali kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, hivyo Halmashauri ililazimika kutafuta mbinu mbadala ya kuishirikisha jamii katika kuthamini na kupima ardhi katika mji mdogo wa Lwangwa. Kwa kutumia mbinu hii jamii yenyewe ilikuwa mtendaji mkuu wa kutekeleza upimaji wa ardhi.

Wazo kuhusu upangaji wa mji lilianzishwa na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Dkt. Leonard M. Masale ambaye alipata uzoefu wa upangaji wa mji kwa kushirikisha jamii akiwa H/W ya Itilima mkoa wa Simiyu. Mkurugenzi huyu aliwasilisha uzoefu wake wa kushirikisha jamii kupanga mji kwenye kikao cha timu ya wataalamu wa Halmashauri ambapo walivutiwa na wazo hilo na kukubaliana kutumia mbinu hiyo. Kutokana na uzoefu wa Dkt. Masale aliopata wakati wa kupima na kupanga Mji wa Itilima, aliweka mikakati ya utekelezaji ili kuupima na kuupanga Mji wa Lwangwa kwa kutumia raslimali zilizopo. Ili kufanikisha mpango huu mambo yafuatayo yalifanyika;

Uandaaji wa andiko kuhusu ushirikishwaji wa jamii katika upangaji wa mji; Timu ya Menejimenti ya Halmashauri iliandaa andiko na kuliwasilisha kwenye kamati ya masuala ya Uchumi, Kazi na Mazingira ikielezea mikakati ya utekelezaji wa upangaji wa mji. Andiko lilijadiliwa na kukubalika ndani ya kamati na baadae liliwasilishwa kwenye kikao cha Baraza kwa majadiliano zaidi na kuridhiwa.

Kuanzisha kikosi kazi cha Halmashauri cha kushughulikia masuala ya upangaji mji; Timu ya Menejimenti iliamua kuanzisha kikosi kazi chenye wajumbe 10 amabao walipewa mamlaka na menejimenti kuratibu na kutekeleza shughuli mbalimbili zinazohusiana na upangaji shirikishi wa mji. Majukumu yaliyotekelezwa na kikosi kazi hiki ni pamoja na; kuhamasisha jamii kuhusu mipango miji, kufanya utambuzi wa watu maarufu katika jamii na kuwatumia katika kutekeleza shughuli za uhamasishaji kwa wananchi wengine ili kuwafanya wakubali mradi na kuwa tayari kushirikiana katika upangaji wa mji. Kikosi kazi kiliagizwa kutoa taarifa ya utekelezaji kila siku ya Jumatatu kwa Menejimenti ya Halmashauri ili kubaini mbinu mbadala za kutumika katika kuhakikisha ufanisi wa zoezi. Pia, kikosi kazi kiliagizwa kutoa taarifa za utekelezaji kwa wajumbe wa kamati ya uchumi, kazi na Mazingira ili kufahamu maendeleo ya utekelezaji. Wajumbe wa kikosi kazi walichaguliwa kutoka watumishi wa makao makuu ya Halmashauri na Mtendaji wa Kata ya Lwangwa. Majina na nafasi za wajumbe wa kikosi kazi yameorodheshwa kwenye jedwali Na. 1 hapa chini:

**Jedwali Na 1: Wajumbe wa Kikosi Kazi**

| Na. | Jina | Cheo | Nafasi |
|---|---|---|---|
| 1 | Mr. Christopher Lupia | Fundi | Mwenyekiti |
| 2 | Mr. Philemon E. Chaula | Afisa Usafi na Mazingira | Katibu |
| 3 | Mr. Peter Salama | Mwanasheria | Mjumbe |
| 4 | Mr. Jemes T. Mgumba | Afisa Elimu | Mjumbe |
| 5 | Ms. Furaha Kalinga | Afisa Mipango Miji | Mjumbe |
| 6 | Mr. Nuru Hondo | Mhandisi | Mjumbe |
| 7 | Ms. Agnes Elikunda | Afisa Maendeleo ya Jamii | Mjumbe |
| 8 | Mr. Mwasanu | Afisa Mtendaji Kata-Kabula | Mjumbe |
| 9 | Mr. Ezekia Mwaipaja | Mhasibu | Mjumbe |
| 10 | Mr. Geofrey Mdalo | Mthamini | Mjumbe |



***Wajumbe wa Kikosi Kazi wakitekeleza majukumu yao***

Kujenga uelewa kwa wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kata (KMK) kuhusu mipango miji; Ili kuhakikisha wananchi wanakubaliana na mkakati na kushiriki kwenye utekelezaji, kikosi kazi kilianza kwa kujenga uelewa wa wajumbe wa Kamati za Maendeleo za Kata (KMK) za Lupata, Lwangwa na Kabula ambazo zinaunda mji mdogo wa Lwangwa wenye vijiji vya Ndembo, Mpanda na Ikamambande. Kikosi kazi kilieleza umuhimu wa kupanga mji na faida mbazo jamii zitapata ikiwa zitashiriki katika zoezi la mipango miji. Faida zilizoelezwa ni kupanda kwa thamani ya ardhi na uwezekano wa kupata hati miliki ya ardhi. Wazo lilipokewa vyema na KMK na kuahidi kusaidia kujenga ushawishi kupitia vikao vya Halmashauri za Vijiji na kuhamasisha wananchi kuhusu faida watakazopata kwa kukubali kushirikiana na Halmashauri katika zoezi la kupima na kupanga Mji. Picha ifuatayo inaonesha moja ya mikutano ya uhamasishaji iliyofanywa na kikosi kazi.



***Mkutano wa kikosi kazi na wajumbe wa KMK ya Lwangwa***



***Mkutano wa kikosi kazi na Wajumbe wa KMK ya Kabula***

Kujenga uelewa wa wajumbe wa Halmashauri za Vijiji vya Ndembo, Mpanda na Ikamambande; kikosi kazi kiliendelea na zoezi la kujenga uelewa kupitia mikutano ya Serikali ya kila Kijiji kueleza umuhimu wa upangaji shirikishi wa mji na sababu za Halmashauri kutaka kushirikiana na jamii katika kupima na kupanga mji wa Lwangwa. Uhamasishaji ulifanywa na wajumbe wa KMK kwa kushirikiana na kikosi kazi. Kwenye mikutano ya uhamasishaji, kikosi kazi kiliweza kubaini wanajamii maarufu ambao wanafahamika na kuheshimika ndani ya jamii. Kikosi kazi kiliwajengea hamasa watu hao na kuwaomba kusaidiana nao katika kujenga hamasa kwa jamii kwa ujumla kutoka kila kijiji. Msingi wa kutumia watu maarufu katika vijiji ni kuwa wanazifahamu vyema jamii na kufahamika hivyo ni rahisi kuihamasisha jamii na kueleweka na kuaminiwa kwa urahisi na jamii. Ushawishi uliofanyika ulisaidia kuongeza mahudhurio ya wananchi

kwenye mikutano ya mipango miji hivyo vijiji vyote vilikubali kushiriki kwa kina katika kutekeleza mradi. Picha zilizopo hapa chini zinaonesha mikutano ya uhamasishaji kwa wajumbe wa Serikali za Vijiji.



***Mikutano ya uhamasishaji Kijiji cha Ndembo na Kijiji cha Ikamambande***

Kujenga uelewa na ushawishi kwa wananchi wa Vijiji vya Ndembo, Mpanda na Ikamambande kuhusu upimaji na upangaji shirikishi wa mji; zoezi la kuwajengea uelewa wananchi lilifanyika kupitia mikutano ya hadhara iliyofanyika vijiji vya Ndembo tarehe 13/08/2015, Mpanda tarehe 24/07/2015 na Ikamambande tarehe 04/09/2015. Kikosi kazi cha Halmashauri kilielezea lengo la kupima na kupanga mji kwa kushirikisha jamii na faida zinazoambatana na upangaji wa mji ambazo ni pamoja na kuongezeka kwa thamani ya ardhi, kufikika kwa maeneo ya kutolea huduma za jamii kama soko, stendi ya magari na hospitali. Vilevile wananchi walihakikishiwa kwamba viwanja vitakavyopimwa vitabaki kuwa mali yao. Maelezo yaliyotolewa kwa wananchi yalihusisha hatua za utekelezaji wa zoezi la upimaji na upangaji wa mji. Hatua hizo ni pamoja na kufanya tathimini ya hali ilivyo, kuandaa ramani ya mji, kuchora michoro ya mji, kupima na kuidhinisha umiliki wa viwanja kwa wamiliki wa ardhi. Vijiji vya Ndembo na Mpanda walihamasika kwa kiasi kikubwa hivyo wakaamua kuunda kikosi kazi cha kijiji kuratibu utekelezaji wa mpango wa upimaji ardhi kwa kushirikiana na kikosi kazi cha Halmashauri. Kwa upande wa Kijiji cha Ikamambande, kilijumuika baadae baada ya kuona mafanikio kutoka vijiji jirani vilivyotekeleza mpango. Kwa ujumla uhamasishaji wa jamii katika vijiji vyote ulichukua muda wa miezi minne. Jedwali lifuatalo linaonesha wajumbe wa vikosi kazi vya vijiji vya Ndembo na Mpanda vilivyoshirikiana na kikosi kazi cha Halmashauri.


**Jedwali Na 2: Kikosi Kazi cha mipango miji Ndembo na Mpanda**

| S/n | Kijiji cha Ndembo | | Kjiji cha Mpanda | |
|---|---|---|---|---|
| | Jina | Nafasi | Jina | Nafasi |
| 1 | Ezekiel Mwaigula | Mwenyekiti | Sanke Mwambusi | Mwenyekiti |
| 2 | Joyce Mololo | Katibu | Dorice Itebele | Katibu |
| 3 | Magweda Lyandike | Mjumbe | Afwilile Mwakiwhaja | Mjumbe |
| 4 | Dickson Mwangajilo | Mjumbe | Tufwene Ikenda | Mjumbe |
| 5 | Grace Mpindi | Mjumbe | Tufigwege Mwamelo | Mjumbe |
| 6 | Sikujua Lemba | Mjumbe | Pasya Kibete | Mjumbe |
| 7 | Shadrack Magila | Mjumbe | Francis Mwambalaswa | Mjumbe |
| 8 | Esther Kipesile | Mjumbe | Lucia Ndemange | Mjumbe |
| 9 | Sanga Mwamkinga | Mjumbe | Kyela Mwaisango | Mjumbe |

Mkurugenzi alifanya mkutano wa siku moja na wananchi wa Busokelo wazalendo waishio nje ya Busokelo Desemba, 2015 ili kuomba ushiriki wao katika kukuza maendeleo ya Halmashauri. Katika mkutano huu ajenda ya upimaji na upangaji shirikishi wa mji ilijadiliwa. Washiriki wa mkutano walivutiwa na wazo hilo na kukubali kununua viwanja kutoka kwenye familia za Lwangwa na hatimaye kujenga majengo kwa ajili ya matumizi mbalimbali mfano kupangisha watumishi wa Serikali wanaokuja kufanya kazi Busokelo. Pia,


wajumbe walipendekeza eneo la mradi liongezwe kwa kiasi cha kipenyo cha Kilomita 10. Mwisho kabisa waliunda umoja wao wa mawasiliano kupitia barua pepe ili kupashana habari kuhusu utekelezaji wa upimaji na upangaji shirikishi wa mji.

Zoezi la upimaji na upangaji wa mji wa Busokelo lilienda sambamba na kutambua maeneo ya barabara katika maeneo ambayo makazi yalikwisha anzishwa. Zoezi hili lilifanywa na kikosi kazi cha Halmashauri kwa kushirikiana na kikosi kazi cha mipango miji cha kijiji, afisa mtendaji wa kijiji, mwenyekiti wa kijiji na wenyeviti wa vitongoji vya Itete na Katete katika kijiji cha Ndembo. Barabara na njia za watembea kwa miguu zilibainishwa na kuingizwa kwenye mfumo wa GPS. Kitengo cha Halmashauri cha Mipango Miji kiliunganisha taarifa ya barabara na mwisho kikatoa mwongozo wa kujenga mtandao wa barabara kama inavyonekana kwenye mchoro ufuatao.




**Mtandao wa barabara katika mji wa Lwangwa**

Uandaaji wa Ramani ya Mipango Miji ya mji mdogo wa Lwangwa kuainisha mpango wa matumizi ya ardhi. Kikosi kazi cha mipango miji kwa kushirikiana na vikosi kazi vya Vijiji kiliandaa ramani ya maeneo ya kupimwa kwa ajili ya kutenga maeneo ya Soko, stendi ya magari, kituo cha polisi, kituo cha mafuta na maeneo ya barabara za mitaa. Eneo kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya magari na kituo cha polisi lilitolewa bure na wananchi. Eneo kwa ajili ya soko lilitolewa kwa masharti kwamba ujenzi wa soko utakapokamilika, ugawaji wa vizimba vya biashara utazingatia nafasi za upendeleo kwa wale wote walioachia maeneo yao. Ramani ya mpango mji pia iilionesha maeneo ya makazi ambayo yalitambuliwa kama Kitalu cha Itete na Kitalu cha Mpanda Zahanati ambavyo kwa ujumla vina viwanja 464. Picha ifuatayo inaonesha sura ya mpango mji wa Lwangwa katika ramani.




***Sura ya mpango mji wa Lwangwa***

Baada ya kuanda mtandao wa barabara na ramani ya mji, jamii ilianza kukata miti na kung’oa visiki ili kufungua barabara za kuunganisha mji zenye upana kati ya mita 3 hadi 8. Barabara hizi zinaunganisha vijiji kutoka Mpanda kupitia Katilu hadi eneo la soko. Kuwepo kwa barabara hii, kunawezesha wananchi wa kijiji cha Katilu wanaweza kufika zahanati ya Mpanda, stendi ya magari na kituo cha mafuta. Katika kuboresha barabara, Halmashauri ilitoa vifaa vya ujenzi kama katapila kwa ajili ya kuchimba, kunyoosha kingo za barabara na kushindilia. Barabara hizi pia zinaunganika na barabara iliyojengwa na Halmashauri kutoka mahali palipojengwa nyumba za wakuu wa idara wa Halmashauri kupitia Lwangwa Mjini hadi Itete. Utekelezaji wa ujenzi wa barabara kwa kushirikisha wananchi ni kama inavyonekana katika picha kabla na baada ya ujenzi.



***Njia za watembea kwa miguu kabla ya kufunguliwa kuwa barabara***



***Ujenzi wa barabara Kutoka Mpanda hadi sokoni***



***Ujenzi wa barabara kutoka nyumba za wakuu wa idara wa Halmashauri***

Juhudi za H/W ya Busokelo kuanzisha Mji wa Lwangwa zilienda sambamba na ujenzi wa jengo la ofisi ya Halmashauri na nyumba za watumishi. Jengo la ofisi ya Halmashauri bado lilikua katika ngazi ya msingi. Nyumba 14 za watumishi zilikuwa zimekamilika kupitia mkopo wa Shirika la Nyumba la Taifa. Ujenzi wa nyumba 14 za watumishi ulitekelezwa kwa muda wa miezi nane kuanzia mwezi Julai, 2015 hadi Machi, 2016. Picha zifuatazo zinaonesha mchoro wa jengo la Halmashauri litakavyokuwa baada ya kukamilika.




***Mchoro wa jengo la ofisi ya Halmashauri na ujenzi ukiendelea.***

## 5.0 RASLIMALI

Utekelezaji wa mpango huu ulihusisha raslimali watu na raslimali fedha. Ufafanuzi wa raslimali hizi ni kama ifuatavyo; raslimali watu zinahusisha watumishi wa Halmashauri waliounda kikosi kazi cha ufuatiliaji na kuhamasisha jamii katika kushiriki kwenye zoezi. Madiwani walikuwa mstari wa mbele katika kutangaza mpango na kushawishi wananchi kushiriki, wajumbe wa KMK, Serikali za Vijiji na jamii kwa ujumla walijitolea kwa nguvu zao kuhakikisha mji wa Lwangwa unapangwa. Kwa upande mwingine raslimali fedha kiasi cha sh. 2,344,428,242.90 zilitumika kutekeleza shughuli mbalimbali kama inavyooneshwa kwenye jedwali Na. 3 hapa chini.

**Jedwali Na 3: Raslimali Fedha**


| Na. | Kazi iliyotekelezwa | Kiasi cha fedha kilichotumika (TShs) |
|---|---|---|
| 1 | Uchimbaji wa Barabara ya urefu wa kilomita 2.5 | 44,821,164 |
| 2 | Ujenzi wa nyumba 14 za wakuu wa idara na Mkurugenzi | 1,112,109,880 |
| 3 | Ujenzi wa jengo la Halmashauri awamu ya 1 | 861,846,158 |
| 4 | Thamani ya ardhi iliyotolewa na wananchi ekari 53.55 | 291,051,040 |
| 5 | Thamani ya nguvu za wananchi katika kufyeka na kung'oa visiki | 3,600,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Fidia ya ardhi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 14 za wakuu wa idara | 31,000,000 |
| **Jumla** | | **2,344,428,242** |

## 6.0 MATOKEO

Utekelezaji wa mradi wa upangaji shirikishi wa mji wa Lwangwa una matokeo chanya. Mtazamo wa jamii umebadilika kiasi kwamba jamii imehamasika kutoa ardhi bila fidia kuruhusu ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma. Mwananchi mmoja mzaliwa wa Busokelo kwa ridhaa yake amejitolea majengo yaliyopo katika kijiji cha Lufilyo ili kuanzisha chuo cha ufundi. Majengo hayo yamekabidhiwa kwa Mamlaka ya Mafunzo ya Elimu ya Ufundi (VETA) ili kuanza kutoa mafunzo.

Halmashauri imeandaa mchoro wa viwanja zaidi ya 1600 katika mgawanyo wa viwanja vya makazi, biashara, huduma za jamii na maeneo ya mtandao wa miundombinu ya barabara. Kwa kutumia njia shirikishi, kijiji cha Ndembo kimeweza kutoa eneo la ekari 9.55 ambalo hapo awali lilitumika kama shamba la kilimo cha chai kwa ajili ya ujenzi wa kituo kikuu cha polisi. Kijiji cha Kitali kimetoa eneo la ekari 18 kwa Shirika la Nyumba la Taifa kujenga nyumba 50 za gharama nafuu kwa ajili ya kuwauzia na kuwapangisha watumishi na jamii kwa ujumla. Mkataba wa makabidhiano ya ardhi baina ya NHC na Serikali ya Kijiji umekwishafanyika kwa makubaliano kwamba NHC itawajengea wananchi zahanati kama fidia ya ardhi. Halmashauri imepata eneo la ekari 20 kwa ajili ya ujenzi wa soko kwa makubaliano ya kuwapatia vizimba vya biashara waliojitolea maeneo yao. Kijiji cha Ndembo kimetoa eneo la ujenzi wa stendi kuu ya mabasi na ujenzi wa hospitali ya wilaya bila gharama yoyote. Halmashauri ilinunua eneo la ekari 5 kwa gharama ya milioni 31 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za wakuu wa idara. Picha ifuatayo inaonesha michoro ya mpango mji na ardhi iliyopatikana kwa ajili ya kujenga miundombinu ya huduma za jamii.



***Mchoro wa mipango miji***



***Eneo la kujenga kituo cha polisi***



***eneo la kujenga nyumba za NHC***



***Eneo zilipojengwa nyumba za wakuu wa idara***



***Eneo kwajili ya ujenzi wa soko***



***eneo kwajili ya ujezi wa stendi ya mabasi***

Upangaji shirikishi wa mji umechangia ujenzi wa barabara za mitaa 21. Jamii imetambua maeneo ya ujenzi wa barabara kuunganisha mji na kuamua kushiriki katika kukata miti na kung'oa visiki kuruhusu ufunguaji wa barabara. Halmashauri iliboresha barabara zilizofunguliwa na jamii ili kuzifanya zipitikie wakati wote ndani ya mwaka mzima. Ujenzi wa jengo la Halmashauri unaendelea, wakati wa uandishi wa hiki kitabu ujenzi ulikua ngazi ya msingi. Picha zifuatazo zinaonesha barabara zilizofunguliwa na jamii katika kijiji cha Ndembo na ujenzi wa jengo la Halmashauri ukiendelea.



***Barabara zilizofunguka kijiji cha Ndembo***





*Ujenzi wa jengo la Halmashauri katika ngazi ya msingi.*

## 6.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

H/W ya Busokelo imeweka mikakati katika kuyafanya matokeo kuwa endelevu; Halmashauri imeomba ombi maalum la fedha kutoka Serikali Kuu ili kukamilisha miradi iliyoanzishwa. Halmashauri iliomba kibali Serikali Kuu cha kuajiri wathamini wa ardhi wanne na afisa mipango miji mmoja ili kuhakikisha zoezi la upimaji na upangaji wa mji linaendelea. Mipango miji shirikishi katika vijiji vya Kabula, Lupata na Kata ya Lwangwa imeanza. Halmashauri imenunua vifaa vya upimaji kama GPS, compyuta na printa kurahisha zoezi la upimaji.

## 8.0 SIRI ZA MAFANIKIO

Mpango huu umefanikiwa kutokana na ubunifu na uthubutu wa aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji Dkt. Masale ambaye alijitoa kutekeleza mpango kwa kutumia uzoefu alioupata akiwa Mkurugenzi H/W ya Itilima. Mkurugenzi alionesha ushawishi kwa Baraza la Madiwani na baadae aliunda Kikosi Kazi cha kushawishi wananchi. Zoezi pia lilifanikiwa kutokana ushirikiano uliojengwa baina ya Halmashauri na wadau kama wenyeji waishio nje ya Busokelo, VETA, NHC na Dayosisi ya KKKT Konde ambao walikubali kushiriki kuhamasisha upimaji wa mji. Picha hapa chini inaonesha aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji.




Utayari wa Jamii kushirikiana na wataalam wa Halmashauri katika kupanga mji ni siri nyingine ya mafanikio. Jamii za Ndembo na Mpanda ni wapenda maendeleo hivyo ilikuwa rahisi kwa kikosi kazi kuwashawishi kushiriki kwenye mpango wa upimaji mji kwa kuunda kikosi kazi cha jamii kushiriki katika uhamasishaji na utekelezaji wa mpango. Picha ifuatayo ni Mwenyekiti wa Kikosi kazi cha jamii cha mipango miji akiongea kwenye mojawapo ya mikutano ya uhamasishaji.




***Mwenyekiti wa Kikosi Kazi***

Utayari wa kisiasa kukubali jamii kuhusika katika upangaji wa mji ni siri nyingine ya mafanikio. Uwezo mkubwa wa ushawishi wa Madiwani wa Kabula, Lupata na Lwangwa uliongeza kasi na utayari wa wananchi kukubali kutoa maeneo ya kwa ajili ya kuruhusu upimaji wa mji. Utayari wa timu ya menejimenti, Kikosi kazi na kamati ya Uchumi, kazi na mazingira katika kufanya ufuatiliaji ni siri nyingine ya mafanikio. Ufualitiaji wa mara kwa mara uliweza kuenga uwajibikaji wa kikosi kazi hivyo kufanya utekelezaji wa mradi kuwa rahisi.

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA

**USAFI, UJANISHAJI NA UPENDEZESHAJI WA MAZINGIRA KATIKA SHULE ZA MSINGI**




***UZOEFU WA MANISPAA YA ILALA***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ni moja kati ya Halmashauri sita za Mkoa wa Dar es Salaam. Manispaa hii ipo kati ya Longitudo $39^0$ na $40^0$ Mashariki na kati ya Latitudo $6^0$ na $7^0$ Kusini. Halmashauri ina eneo la $210km^2$ na inapakana na Bahari ya Hindi kwa upande wa Mashariki, Manispaa ya Temeke kwa upande wa Kusini, H/W Kisarawe upande wa Magharibi, na Manispaa za Kinondoni na Ubungo upande wa Kaskazini. Kwa mujibu sensa mwaka 2012 Manispaa ya Ilala ilikuwa na watu 1,220,611 kati yao wanaume 595,928 na wanawake 624,683 na Kaya 300,674. Wastani wa idadi ya watu kwa eneo ni 5,812 kwa kilometa za mraba. Kiutawala, Manipaa ya Ilala ina Tarafa 3, Kata 36 na Mitaa 159. Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inakadiriwa kuwa 43.97% ya wakazi wameajiriwa kwenye sekta za umma na binafsi na 56.03% wanajihusisha na ajira binafsi ambazo katika biashara rasmi na zisizo rasmi, uvuvi, kilimo, ufugaji na uhunzi. Wastani wa kipato kwa wakazi wanaoishi Manispaa ya Ilala ni shs. 1,734,842 kwa mwaka.

Usafi wa mazingira shuleni na utoaji wa elimu ya usafi hujumuisha uwepo wa mahitaji muhimu ya kufanikisha mazingira ya shule kuwa safi na kubadilisha tabia, kukataa uchafu na kupenda usafi. Mahitaji ya kusaidia usafi wa mazingira ya shule ni pamoja na uwepo wa maji safi na salama ya kunywa, vifaa vya kunawia mikono na vifaa vya kukusanya na kuhifadhi taka ngumu zinazozalishwa ndani na katika maeneo yanayozunguka mazingira ya shule. Ili kujenga tabia ya kupenda usafi ni muhimu kuhimiza utekelezaji wa vitendo vinavyochochea usafi kwa kuelimisha waalimu na wanafunzi kulinda usafi ili kuepusha kupata magonjwa yatokanayo na uchafu. Manispaa ya Ilala iliamua kujihusisha na uboreshaji wa hali ya usafi mashuleni na kutoa elimu ya usafi kwa lengo la kukuza tabia ya kupenda usafi. Manispaa iliamua kuimarisha usafi kwa kuhakisha shule zina huduma ya maji na vifaa vya kukusanya na kutunza uchafu katika maeneo ya shule. Pia Manispaa iliboresha mazingira na usafi wa shule kwa lengo la kuimarisha afya za wanafunzi.

**2.0 TATIZO**

Shule za Msingi katika Manispaa ya Ilala kwa kipindi kirefu zimekua zikiathirika na mazingira machafu, yaliyokosa mvuto na uchafu ulikithiri. Wanafuzi walioneka wachafu muda wote kutokana na vumbi, mazingira hayakuwa rafiki kwa wanafunzi kucheza kutokana na vumbi. Shule zilikosa huduma muhimu za usafi kama vile vyoo na vifaa vya kunawia mikono na sabuni. Kutokana na uchafu wa Mazingira, baadhi ya shule zilikumbwa na magonjwa ya kipindupindu, homa ya matumbo na magonjwa mengine yanayoambatana na uchafu mara kwa mara. Kusambaa kwa magonjwa kulikithiri zaidi msimu wa mvua kati ya mwezi Machi na Mei. Kutokana na hali hii baadhi ya wanafunzi walishindwa kuhudhuria masomo jambo ambalo liliathiri ufaulu wao katika mitihani. Kukithiri kwa hali ya uchafu wa mazingira mashuleni na katika jamii kulitokana na ukosefu wa uelewa wa masuala ya usafi tangu umri mdogo jambo ambalo lilipelekea kuendeleza tabia za uchafu katika jamii kwa ujumla. Uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya shule ulichangiwa na masuala yafuatayo;

Kukosekana kwa vifaa vya kukusanya taka ngumu katika maeneo ya shule, uhaba wa matundu ya vyoo ambapo ililazimu wanafunzi 45 kutumia tundu moja la choo tofauti wastani unaopaswa wa wanafunzi 22 kutumia tundu moja la choo. Kukosekana kwa tabia ya kupenda usafi wa mazingira na upendezeshaji wa mazingira ya shule kwa baadhi ya uongozi wa shule, elimu kuhusu usafi wa mazingira kutototolewa mara kwa mara shuleni, maeneo ya shule kuendelea kuwa wazi kwa kukosa miti na kuongezeka kwa vumbi kulichangia mazingira yasiyovutia katika shule. Picha ifuatayo inaonesha hali halisi ya mazingira ya shule kabla ya hatua za maboresho kuchukuliwa.





***Shule ya msingi Uhuru Wasichana*** ***shule ya msingi Diamond***

**3.0 MALENGO**

Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuimarisha hali na elimu ya usafi ambayo ili kukuza tabia ya kupenda usafi katika maisha ya kila siku. Lengo hili lingefikiwa kwa kukuza uelewa wa wanafunzi kuhusu usafi wa mazingira na uboreshaji wa hali ya usafi kwa jamii. Malengo mahususi yalikuwa ni pamoja na kuhimiza elimu ya usafi kutolewa na kutumika katika mazingira ya shule na nje ya shule hasa mazingira ya nyumbani, kuboresha usafi wa mazingira ili kupunguza magonjwa kwa shule 100 ifikapo mwaka 2020, kupendezesha mazingira ya shule, kufundisha wanafunzi usafi na kuwaandaa kuwa mabalozi wa usafi wa mazingira katika jamii.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Manispaa ya Ilala inaamini kwamba hali ya usafi itaweza kuimarika endapo vyanzo vya uchafuzi wa mazingira vitadhibitiwa. Mwaka 2008 Afisa Elimu mmoja alihudhuria mafunzo kwa muda wa miezi 3 chini Sweden yaliyofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Sweden. Katika mafunzo hayo alijifunza mbinu mbalimbali kuhusu uboreshaji wa hali ya usafi kwa kutumia ushiriki wa wanafuzi katika kuzambaza elimu ya usafi kwa jamii. Pia Afisa huyu alihudhuria mafunzo mengine ya wiki tatu nchini Afrika Kusini. Mafunzo haya yalihusu kuboresha usafi, kuanzisha na kutunza bustani na kupendezesha mazingira. Baada ya kurejea aliwashirikisha watumishi wenzake katika ngazi ya Halmashauri ambapo walivutiwa na kuamua kutengeneza mikakati ya utelekezaji wa mafunzo hayo kupitia wanafunzi mashuleni. Mikakati iliyotekelezwa na Manispaa ni kama ifuatavyo;

Kuchagua shule za mfano; katika kutekeleza jitihada hii, Manispaa ya Ilala ilichagua shule mbili za mfano ambazo ni Shule za Msingi za Buguruni na Boma. Shule hizi kama ilivyo kwa shule nyingine ndani ya Manispaa zilikuwa zimeathirika na tatizo la uchafu wa mazingira. Baada ya uteuzi wa shule hizi, Manispaa iliweka lengo la kuwezesha uongozi wa shule kuhusu mbinu za kupambana na hali ya uchafu shuleni. Katika utekelezaji wa lengo hili, Manispaa ilianza kwa kujenga uelewa wa uongozi wa shule kuhusu kuboresha na kutunza mazingira. Kila shule ilitakiwa kushirikisha wanafunzi na kuwajengea uelewa kuhusu tabia ya kupenda usafi katika maisha yao ya kila siku. Sambamba na kuwajengea uelewa wanafunzi kuhusu usafi Manispaa ilisisitiza ujenzi wa vyoo, upatikanaji wa maji safi, vifaa vya kunawia shuleni na kupendezesha mazingira ya shule. Zoezi la kujenga uelewa wa kutekeleza haya lilifanywa kwa walimu pamoja na wanafunzi. Picha ifuatayo inaonyesha baadhi ya mikutano ya kujenga uelewa juu ya usafi.



***Mkutano wa uhamasishaji  kuhusu usafi wa Mazingira***

Kutoa mafunzo kwa walimu; walimu walipewa mafunzo juu ya mbinu mbalimbali za kuboresha afya, mazingira na uendezeshaji wa shule kwa lengo la kubadilisha tabia na mienendo ya wanafunzi na kuwafanya wapende usafi. Mafunzo kwa walimu yalikuwa mihimu ikizingatiwa kwamba msingi wa mabadiliko kwa wanafunzi unaweza kutekelezeka zaidi shuleni kuliko katika ngazi ya familia. Shule ni sehemu ya ushawishi wa kujifunza na kuleta mabadiliko.  Ikiwa hali ya usafi itaboreshwa shuleni, walimu wakawa mfano wa kuigwa na wanafunzi kutapelekea kuambukiza hali ya usafi kwenye jamii kwa ujumla.

Kujenga uelewa wa wanafunzi kuhusu utumiaji na utanzaji wa raslimali na vifaa vya usafi; uelewa wa wanafunzi ulijengwa kupitia walimu baada ya kupata mafunzo. Ili kupendezesha mazingira, shule ziliwezeshwa kuanzisha vitalu vya miti na maua. Miti na maua ni kwa ajili ya kuleta kivuli, hewa safi, matunda na kupendezesha mazingira ya shule kwa kuyafanya mazingira kuwa kijani na ya kuvutia. Katika kustawisha bustani za miti na maua, iliamuliwa kila Jumamosi wanafunzi watashughulika na usafi na umwagiliaji wa bustani za maua na miti katika mazingira ya shule.

Uanzishaji wa klabu za mazingira na usafi; katika kusambaza jitihada ya usafi wa mazingira klabu za usafi wa mazingira zilianzishwa mashuleni. Wajumbe wa klabu walichaguliwa kutoka kila darasa na kupewa majukumu ya kusimamia usafi. Wajumbe wa klabu ya mazingira walikuwa na jukumu la kusimamia usafi, utunzaji  wa bustani,  upendezeshaji wa mazingira ya shule na kuhakikisha kila mwanafunzi anaheshimu na kufuata taratibu zilizowekwa za kutunza mazingira na kuboresha usafi ikiwa ni pamoja na uhakikisha elimu ya usafi inamfikia kila mwanafunzi (mtoto kwa mtoto). Inaaminika kwamba mtoto ana utayari na uwezo wa kumhamasisha mtoto mwenzake na kuaminiana katika kutekeleza jambo. Baada ya kuanzisha klabu za mazingira hali ya usafi ilianza kuimarika kama inavyonekana katika picha.



***Upendezeshaji wa mazingira ya shule***

Kutengeneza na kusimika mabango mbalimbali yenye ujumbe wa kutunza na kuboresha usafi wa mazingira;  katika kuhakikisha uboreshaji na uimarishaji wa hali ya usafi shuleni, ubunifu wa picha, mabango na sanamu za wanyama zenye ujumbe mbalimbali kuhusu utunzaji na uboreshaji wa usafi viliwekwa katika maeneo mbalimbali ya shule ili kuhimiza wanafunzi kupenda na kutekeleza azma ya usafi.

Baadhi ya maneno yaliyopo kwenye mabango ni "*MAZINGIRA BORA HUIMARISHA ELIMU*", "*MAZINGIRA BORA KWA ELIMU BORA*", *"MAZINGIRA BORA HUBORESHA ELIMU"*, *"ELIMU KWA MAENDELEO ENDELEVU"*, *"'USAFI WA MAZINGIRA HUBORESHA ELIMU''*, *"USAFI WA MAZINGIRA KWA MAENDELEO ENDELEVU".* Kwa upande mwingine, ili kuwafanya wanafunzi wanaendeleze hali ya usafi na kutunza mazingira, Manispaa iliandaa siku ya mazingira ambapo shule zilifanya mashindano. Katika maadhimisho ya siku ya mazingira ya Manispaa, mbinu mbalimbali za kuhamasisha wanafunzi zilitumika; mfano nyimbo kuhusu mazingira, maigizo, maswali na majibu, michezo, mashindano,misemo, mihadhara na majadiliano katika vikundi. Mbinu hizi zililenga kuwahamasisha wanafunzi kutekeleza usafi maeneo ya shule pamoja na maeneo ya wanayoishi.

Kuwaanda wanafunzi kama mabalozi wa mazingira; katika kusambaza elimu ya usafi kwa jamii, shule ziliandaa wanafunzi kuwa mabalozi wa usafi wa mazingira. Majukumu ya mabalozi wa mazingira ni kuhamasisha usafi, upandaji wa miti na maua na uanzishaji wa bustani ili kupendezesha mazingira katika mazingira yasiyo ya shule. Inafahamika kuwa wanafunzi ni chachu ya mabadiliko hivyo kuwatumia wao kama mabalozi italeta mabadiliko katika hali ya usafi wa mazingira kuanzia katika ngazi za kaya na jamii kwa ujumla.

**5.0 RASLIMALI**

Manispaa ilikuwa na mpango wa kusambaza jitihada hii katika shule zote. Kufanikisha hili, Manispaa ilishirikisha wadau mabalimbali katika kuboresha usafi wa mazingira katika shule. Wadau walichangia raslimali kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapa chini.

**Jedwali Na 1: Michango ya Wadau**

| Na. | Mchango | Shule Nufaika | Mdau aliyechangia |
|---|---|---|---|
| 1 | Madawati 800 | Shule za msingi na sekondari | Benki ya NMB |
| 2 | Madawati 300 | Shule za msingi na sekondari | Vodacom |
| 3 | Madwati 1000 | Shule za msingi na sekondari | Tigo |
| 4 | Madwati 200 | Shule za msingi na sekondari | Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) |
| 5 | Vifaa ya usafi (pipa 400 reki 20, toroli 20) | Shule za msingi na sekondari | TCRA, TIGO, Jamii na benki ya Standard chartered |
| 6 | Miche ya miti 8,400 | Shule za msingi na sekondari | Benki za Standard chartered, Barclays, Jamii |
| 7 | Udhamini wa mashindano miaka 5 | Shule zote zinapata zawadi, vyeti pamoja na vifaa vya usafi | Manispaa ya Ilala |
| 8 | Miche ya Miti na Maua | Shule za msingi na sekondari | Jamii |

Raslimali watu; wawezeshaji kutoka ngazi ya Manispaa walitoa mafunzo na uhamasishaji wa kukuza uelewa kupitia mikutano na waalimu na jamii inayozunguka shule. Walimu pia walitumia nguvu zao na ubunifu katika kuhakikisha wanafunzi wanajifunza na kubadili tabia kwa kukataa uchafu na kupenda usafi. Wanafunzi walitumika kama chachu ya mabadiliko; kupitia usaidizi wa walimu wao waliweza kuanzisha klabu za mazingira, kuanzisha bustani za maua na kuzitunza ili kufanya mazingira ya shule kupendeza na kuvutia.

**6.0 MATOKEO**

Utekelezaji wa jitihada ya uboreshaji wa usafi na mazingira kwa baadhi ya shule za msingi na sekondari katika Manispaa ya Ilala umeleta mabadiliko makubwa. Usafi wa mazingira na upendezeshaji wa shule unaimarika, shule zimeanzisha bustani za maua na hali ya ukijani imeongezeka. Miti ipatayo 8400 iliyotolewa na wadau mbalimbaili imeoteshwa katika mazingira ya shule hivyo kuboresha ukijani na kupunguza vumbi katika maeneo ya shule. Baadhi ya bustani zimepandwa miti ya matunda, vivuli na

mapambo, mazingira yamekuwa yakiwavutia wageni, pia wanafunzi wanapata hewa safi kutoka kwenye miti inayozunguka shule. Tabia za wanafunzi zimebadilika na sasa wamehamasika kutumia vifaa vya kuhifadhi taka ili kudumisha usafi wa mazingira. Vyombo vya kukusanyia taka vimesambazwa katika kona mbalimbali za shule na wanafunzi wanavitumia ipasavyo. Vifaa vya kunawia mikono baada ya kutoka chooni vipo na vinatumika ipasavyo. Kufanya mazingira yavutie zaidi sanamu za wanyama zimewekwa kwenye bustani za maua. Picha ifuatayo inaonesha namna mazingira yalivyoboreshwa katika Shule ya Msingi Minazimirefu.




***Mazingira safi na ya kuvutia S/M Minazimirefu***

Klabu za mazingira zimeanzishwa mashuleni na zimeimarika katika kujenga ufahamu kwa wanafunzi kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi, kuboresha hali ya ukijani ili kupendezesha mazingira ya shule. Moja ya majukumu ya Klabu ya Mazingira ni kuwa balozi wa kuhamasisha utunzaji wa mazingira nje ya mipaka ya shule. Wajumbe wa klabu ya mazingira wanatambulika kwa nembo za kijani ambazo zimebandikwa kwenye sare zao za shule. Picha hii inaonesha baadhi ya wajumbe wa klabu ya mazingira Shule ya Msingi MinaziMirefu.



***Klabu ya Mazingira S/M Minazi Mirefu***

Vyoo vya shule vimefanyiwa ukarabati pamoja na kujenga vyoo vipya ili kudumisha hali ya usafi shuleni; kwa kutambua kuwa usafi ni mojawapo ya hitaji kubwa la binadamu na kwamba ukosefu wa vyoo huhatarisha afya ya jamii, Manispaa ya Ilala iliamua kushiriana na wadau kama Tigo, NMB na Vodacom kukarabati na kugharamia ujenzi wa vyoo kulingana na mahitaji ya shule. Kwa sasa Manispaa imefikia viwango vya UNICEF (2010) vya uwiano wa tundu la choo kwa wanafunzi kuwa 1: 25 kwa wasichana na 1:

30 kwa wavulana. Uboreshaji wa vyoo na mazingira shule umesaidia kupunguza magonjwa kama Kuharisha, kipindupindu na homa ya matumbo ambapo hapo awali yaliwasumbua wanafunzi kwa kiasi kikubwa.

Ushirikiano kati ya wanafunzi, walimu, wazazi na jamii umeimarika na sasa wanaongea lugha moja kuhusu masuala ya usafi. Wanafunzi wamehamasika na wana utayari mkubwa wa kulinda mazingira ya shule na wapo tayari kutoa taarifa kwa walimu wao kuhusu tabia ovu za baadhi ya wanafunzi wanaoendelea kuchafua na kuharibu mazingira. Wazazi wanathamini kazi kubwa inayofanywa na walimu katika kuwajenga watoto kupenda mazingira na tabia rafiki kwa mazingira. Vilevile wazazi wanakiri kwamba mitazamo ya kifikra ya wanafunzi kuhusu kupenda mazingira imesambaa na kuambukiza wanafamilia wengine katika kaya. Hii inadhihirisha kwamba wanafunzi ni mabalozi wazuri katika kuchochea mabadiliko.

Manispaa ya Ilala imefanikiwa kuandaa mashindano ya shule kuhusu usafi, ujanishaji na upendezeshaji wa mazingira ya shule. Mashindano haya yanajumuisha siku ya mazingira Ilala na siku ya mashindano ya klabu za mazingira. Mshindi katika mashindano haya huzawadiwa tuzo na fedha. Mshindi wa kwanza hupewa Tshs 500,000 na vifaa vya usafi, mshindi wa pili shs 300,000 na vifaa vya usafi, mshindi wa tatu shs 200,000 na vifaa vya usafi na mshindi wane vifa vya usafi. Pamoja na zawadi hizi shule zote zinazoshiriki mashindano haya hupatiwa vyeti vya ushiriki. Jedwali Na. 2 linaonnesha mshindi wa kwanza kuanzia mwaka 2010 hadi 2015. Picha pia inaonesha tuzo za mashindano ya usafi wa mazingira kwa shule za msingi.

**Jedwali Na 2: Mshindi kati ya washiriki 100**

| Na | Mwaka | Jina la Shule iliyoshika nafasi ya kwanza |
|---|---|---|
| 1 | 2010 | Uhuru wasichana |
| 2 | 2011 | Diamond |
| 3 | 2012 | Uhuru wasichana |
| 4 | 2013 | Minazi Mirefu |
| 5 | 2014 | Upanga |
| 6 | 2015 | Minazi Mirefu |



*Tuzo mbalimbali za mashindano ya usafi wa mazingira*

Jitihada hii ya kutunza mazingira na kuboresha usafi imepelekea Halmashauri nyingine ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam kujifunza kutoka Shule za Msingi za Manispaa ya Ilala. Mwalimu Mkuu na wanafunzi wa Shule ya Msingi Mtongani katika Manispaa ya Temeke na Shule ya Msingi Lugalo katika Manispaa ya Kinondoni walitembelea Shule za Msingi za Manispaa ya Ilala na kujifunza mbinu zilizotumika katika kuboresha mazingira na hali ya usafi katika shule. Vilevile, shule za Manispaa ya Ilala zimekuwa zikiongoza katika mashindano ya Mkoa ambayo yanaandaliwa kuanzia ngazi ya shule, Manispaa mpaka ngazi ya Mkoa kwa lengo la kuhamsaisha na kuboresha usafi, ujanishaji na upendezeshaji wa mazingira ya shule.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Katika kuhakikisha uendelevu wa matokeo ya jitihada hii, Manispaa inaendea kusisitiza kujenga timu ya pamoja kati ya wanafunzi, walimu, klabu za mazingira na jamii kuendeleza mafanikio. Manispaa inaendelea kutenga fedha na kushirikisha wadau kuendelea kugharamia jitihada zilizoanzishwa kama vile kutenga fedha za kujenga mifumo ya kuvuna maji ya mvua kuwezesha umwagiliaji wa bustani mashuleni. Manispaa bado inaendelea kusisitiza upandaji wa miti, maua na majani katika mazingira kuzunguka shule zote ili kupendezesha shule. Vile vile Manispaa inaendelea kuandaa na kufadhili mashindano na kutoa tuzo kwa shule zinazofanya vizuri katika kupendezesha mazingira.

Kampeni za kuhamasisha usafi na kupendezesha mazingira imekuwa ajenda ya kudumu ya Halmashauri. Kampeni hizi zinaenda sambamba na kujenga uelewa kwa wazazi na jamii kwa ujumla kuhusu umuhimu wa kusafisha mazingira na kupanda miti kuzunguka maeneo yao. Uongozi wa shule umekuwa ukitenga muda kwa wanafunzi na klabu za mazingira kujenga hamasa na uelewa kuhusu mazingira na usafi kwa wanafunzi wengine shuleni.

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Mafanikio ya utekelezaji wa jitihada hizi yanatokana na siri zifuatazo; Mafunzo yaliyofadhiliwa na SIDA ambapo Afisa Elimu alihudhuria na baadae kuhamasika kufanya utekelezaji kwa yale aliyojifunza. Menejimenti ya Manispaa ilikuwa na utayari wa kuona mazingira ya shule yanaboreshwa na utayari wa kusaidia. Utayari wa walimu na wanafunzi katika kupokea elimu na kutekeleza na ushirikiano kati ya Manispaa na wadau kama benki,makampuni ya simu na jamii ni siri nyingine ziliyopelekea uboreshaji wa usafi wa mazingira katika maeneo ya shule.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA ILEJE


**UJIRANI MWEMA KATI YA TANZANIA NA MALAWI**



*UZOEFU WA HALMASHAURI YA ILEJE (TANZANIA) NA WILAYA YA CHITIPA (MALAWI)*

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Ileje ni moja kati ya Halmashauri tano za Mkoa wa Songwe ikipatikana kati ya Latitudo $9^0$14 na $9^0$37 Kusini na Longitudo $32^0$8 na $33^0$45 Mashariki. Halmashauri hii inapakana na H/W za Kyela kwa upande wa Mashariki, Rungwe kwa upande wa Kaskazini, Mbozi kwa upande wa Kaskazini Magharibi, Mbeya kwa upande Kaskazini na Mto Songwe kwa upande wa Kusini. Mto wa Songwe ndio mpaka kati ya Tanzania na Malawi. Eneo la Halmashauri ya Ileje ni 1908km$^2$. Kiutawala, Halmashauri imegawanyika katika Tarafa mbili, Kata 18, Vijiji 71, Vitongoji 317 na Kaya 31,113. Kwa mujibu wa sense ya mwaka 2012, idadi ya watu ni 124,451 ambapo kati yao wanaume ni 58,463 na wanawake ni 65,988.




***Ramani ya H/W ya Ileje na mipaka yake***

H/W ya Ileje imegawanyika katika kanda tatu ambazo ni uwanda wa juu, uwandanda wa juu Kaskazini Mashariki na uwanda wa kati. Uwanda wa juu za Kaskazini Mashariki una mwinuko wa kati ya 1500m na 1600m kutoka usawa wa bahari. Hali ya joto ni kati ya 16$^0$C hadi 20$^0$C na hupata mvua kati ya 900mm hadi 1200mm kwa mwaka. Uwanda huu una udongo wa tifutifu wenye rutuba kwa uzallishaji wa mazao kama kahawa, pareto, mahindi na viazi. Uwanda wa Kati upo kati ya 1300m hadi 1500m kutoka usawa wa bahari, hali ya joto ni kati ya 26$^0$C had 32$^0$C na wastani wa mvua kwa mwaka ni kati ya 750mm hadi 1000mm. Udongo katika uwanda huu ni wa kichanga usio na rutuba ya kutosha na hufaa kwa uzalishaji wa mazao kama mahindi, mtama, karanga na maharage. Uwanda wa juu ni kati ya 1600m hadi 2500m kutoka usawa wa bahari, hali ya joto ni kati ya 18$^0$C na 22$^0$C na wastani wa mvua ni kati ya 1500mm hadi 2000mm kwa mwaka.

Shughuli za kiuchumi kwa kiasi kikubwa zimejikita kwenye kilimo na ardhi nzuri kwa ajili ya kilimo ni 104,000ha ambapo 78,000ha ndizo zinatumika kwa kilimo. Vilevile 2,250ha zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji ingawa 1230ha tu zinazotumika. 90% ya wakazi wanategemea kilimo na ufugaji kama nguzo ya uchumi. Mazao ya chakula ni pamoja na mahindi, mpunga, maharage, viazi vitamu, karanga na mtama. Mazao ya biashara ni pamoja na kahawa, pareto, iliki na alizeti. Shughuli nyingine za kiuchumi ni biashara ndogondogo kama maduka na biashara za mpakani kati ya wananchi wa Ileje na nchi jirani ya Malawi.

**2.0 TATIZO**

Halmashauri ya Wilaya ya Ileje kwa kipindi kirefu imekua ikiathirika na mahusiano yasio rasmi kati ya wakazi wake na wakazi wa Wilaya ya Chitipa iliyopo nchi jirani ya Malawi. Mara nyingi kumekuwa na ukosefu wa udhibiti wa biashara kati ya wananchi wa nchi hizi mbili. Kwa upande wa huduma za kijamii, hapakuwa na uratibu wa matumizi ya huduma kama vile huduma za afya, kilimo na mifugo katika maeneo ya mipaka. Vilevile biashara zisizo rasmi ambazo zilihusisha kuvuka mipaka ya nchi zilikithiri, wahamiaji haramu kutoka nchi ya Malawi walikuwa wakiingia na kutoka bila utaratibu rasmi. Changamoto nyingine ambazo H/W ya Ileje ilikumbana nazo ni pamoja na;

Migogoro ya ardhi ya mara kwa mara kati ya wananchi wa Tanzania na Malawi. Migogoro hii kwa kiasi kikubwa ilisababishwa na kuhamahama kwa mto Songwe ambao ndio mpaka. Kuhama kwa mto kunasababishwa na shughuli za kibinadamu; mfano, shughuli za kilimo pembezoni mwa kingo za mto na ukataji ovyo wa miti unaoharibu uoto wa asili katika kingo za mto hupelekea mmomonyoko wa ardhi ambao hufanya mto Kuhama. Kutokana na tatizo la kuhama kwa mto, sehemu kubwa ya ardhi yenye rutuba takriban ekari 80 zilichukuliwa kutoka Kijiji cha Iyenga (Malawi) na wananchi wa kitongoji cha Navilolo na kijiji cha Ikumbilo kama sehemu ya ardhi ya Tanzania. Hali hii iliibua migogoro kati ya wananchi wa pande zote mbili kugombea mashamba.

Kukosekana kwa udhibiti wa biashara za mpakani kulisababisha Serikali kupoteza mapato kuokana na kutokukusanya kodi. Vilevile baadhi ya bidhaa zisizoruhusiwa kuingizwa nchini zilisafirishwa na kuingizwa nchini kwa njia zisizo rasmi. Changamoto nyingine zilikuwa ubovu wa njia za usafirishaji na mawasiliano kati ya pande hizi mbili; kutokarabatiwa kwa daraja la Mto Songwe linalounganisha Tanzania na Malawi kwa upande wa Ileje, kulileta ugumu wa usafirishaji na mawasiliano kati ya wananchi wa maeneo hayo. Hali hii iliwalazimu wananchi kutengeneza madaraja ya asili yajulikanayo kama *Kiteputepu* kuvuka mto. Madaraja haya hayakuwa salama na kwa kiasi kikubwa yalihatarisha maisha ya watu na mali zao. Picha ifuatayo inaonesha mojawapo ya daraja la K*iteputepu* katika Mto Songwe




***Daraja la Kiteputepu Mto Songwe***

H/W ya Ileje pia iliathirika na ukosefu wa udhibiti wa utoaji wa huduma za afya maeneo ya mpakani. Udhibiti wa magonjwa kama Malaria, Kifua Kikuu, Ukimwi, Homa za Matumbo na magonjwa mengine ya kuambukiza katika maeneo ya mpakani ilikuwa tatizo. Hapakuwa na utaratibu wa kupeana taarifa za kuzuka kwa magonjwa ya kuambukiza kama kipindupindu kati ya Wilaya hizi mbili jambo lililosababisha changamoto katika kuzuia milipuko ya magonjwa. Pia utoaji wa chanjo za kuzuia magonjwa ulikuwa duni kutokana na mwingiliano wa watu na kutokushirikiana kwenye taarifa zinazohusu magonjwa hivyo kukitihiri kusambaa kwa magonjwa.

Changamoto nyingine ilihusu utoaji wa elimu; Vijiji vya Malawi vilivyopo kandokando ya Mto Songwe vimeathirika kwa kukosa huduma za elimu kutokana na umbali kutoka makao makuu wa Wilaya yao (Chitipa). Hali hii ilisababisha baadhi ya watoto kutoandikishwa shuleni na kuongezeka kwa utoro na hivyo watoto wengi kuandikishwa shule za Tanzania, hali ilisababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji shule kwa H/W ya Ileje. Michezo isiyo rasmi kati ya vijiji vya Ileje na Chitipa ilisabisha mwingiliano mkubwa wa watu usio rasmi.

Kwa upande wa sekta za kilimo na ufugaji, changamoto kubwa ilikuwa ni kusambaa kwa magonjwa ya wanyama na mimea. Kukosekana kwa mfumo wa taarifa wa pamoja kati ya pande hizi mbili na ukosefu wa udhibiti wa magonjwa wa pamoja kulichangia kuenea kwa magonjwa ya wanyama kama kideri, homa ya nguruwe, ugonjwa wa miguu na midomo na kichaa cha mbwa. Magonjwa haya yalienea kwa kasi

kutokana mwingiliano wa wanyama. Magonjwa na wadudu wa mimea vilisambaa kupitia ubadilishanaji wa mbegu za mazao.

Changamoto nyingine ni kukosekana kwa usalama wa watu na mali zao; kutokana na sheria za kimataifa zinazozuia polisi kufanya upelelezi wa uhalifu wa raia wa nchi nyingine, wananchi walifanya uhalifu sehemu moja na kukimbilia upande wa nchi nyingine. Kwa mfano, mwizi anafanya tukio la wizi Tanzania na kukimbilia Malawi, inakuwa vigumu kwa polisi kumfuatilia na kumkamata kwani sheria za kimataifa haziruhusu polisi wa nchi moja kuingia na kufanya upelelezi kwenye nchi nyingine bila kibali maalumu.

**3.0 MALENGO**

Lengo kuu la utekelezaji wa jitihada hii lilikuwa kujenga uhusiano mzuri kati ya watu wa Wilaya ya Chitipa na Watu wa H/W ya Ileje ili kuboresha hali maisha ya jamii za pande zote mbili. Malengo mahususi yalikuwa; kuimarisha uendeshaji wa biashara za mpakani zifanyike kwa mujibu wa sheria za nchi, taratibu na kanuni zinazosimamia biashara kati ya nchi na nchi, kuweka mikakati ya kuhifadhi maliasili na mazingira ya Mto Songwe kwa kupanda miti kuzuia mmomonyoko wa ardhi unaosababisha kuhamahama kwa mto, kuboresha mawasiliano kwa kuimarisha njia za usafirishaji na uchukuzi wa bidhaa kati ta Tanzania na Malawi kupunguza matumizi ya njia za mpakani zisizo rasmi. Pia, jitihada hii ililenga kuboresha utoaji wa huduma katika sekta za afya, elimu, kilimo na mifugo kwa kuimarisha upashanaji wa taarifa zinazohusu sekta hizo. Malengo mengine yalikuwa kuimarisha mahusiano mazuri ili kuboresha hali ya usalama kwa kuanzisha kituo cha uhamiaji katika eneo la mpaka (Ileje), kuweka utaratibu rasmi wa kuendesha michezo na shughuli za kiutamaduni kati ya jamii hizi na kuboresha mahusiano ya kisiasa kwa kuwezesha Madiwani wa pande zote mbili kutembeleana, kuepeana uzoefu na kujifunza kati yao.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Utekelezaji wa jitihada hii ya kuimarisha ujirani mwema ilianza mwaka 2013. Wazo liliibuliwa na Mkuu wa Wilaya ya Ileje ambaye baadae alijadiliana na Mkuu wa Wilaya ya Chitipa kuhusu kuboresha mahusiano kati ya wananchi wa Wilaya hizi mbili. Wakuu wote wa Wilaya hizi waliweza kubaini changamoto zilizopo na kuamua jitihada za haraka kufanyika ili kutatua changamoto hizo. Wakuu wa Wilaya waliamua kuendesha mijadala na jamii ikuhusisha makundi ya wakulima, wafanyabiashara, na watoa huduma mbalimbali. Kutokana na mijadala hiyo mikakati kadhaa ya utekelezaji iliwekwa kama ifuatavyo;

Kuunda timu ya uratibu; timu ya uratibu wa zoezi la kuimarisha mahusiano baina ya pande mbili iliundwa ikijumuisha uwakilishi wa wajumbe kutoka Wilaya za Ileje na Chitipa. Timu ya utatibu ilipewa jukumu la kuandaa mkutano wa wataalamu kutoka idara za Misitu, Kilimo, Mifugo, Elimu, Maji, Utawala, Wakala wa Barabara, Biashara, Mamlaka za Mapato, Uhamiaji na Polisi kujadili changamoto zilizopo. Vilevile, timu ilipewa jukumu la kuaanda agenda za vikao na mikutano baada ya kupokea taarifa kutoka kwenye idara mbalimbali. Kutokana na ufuatiliaji wa mara kwa mara, timu ya uratibu iliandaa mikutano mingi kujadili mikakati ya kutatua changamoto zilizopo.

Mikutano kati ya idara za H/W ya Ileje na Wilaya ya Chitipa. Mikutano hii ilifanyika kwa mzunguko, mkutano wa kwanza ulifanyika Ileje na uliofuata ulifanyika Chitipa. Mikutano hii ilijadili mbinu za kujenga mahusiano rasmi baina ya jamii za pande mbili na kuweka mikakati ya utekelezaji. Mikutano ilihusisha wakuu wa idara kutoka Wilaya zote mbili, mambo yaliyojadiliwa ni pamoja na mkakati wa kuhifandhi kingo za Mto Songwe kwa kuimarisha uhifadhi wa uoto asili pembezoni mwa mto, biashara za mipakani, taratibu za upashanaji tarifa kuhusu utoaji wa huduma za elimu, afya, mifugo, kilimo na uchumi. Katika majadiliano haya iliamuliwa Wilaya zote mbili kuweka utaratibu wa upashanaji habari na utoaji wa huduma. Kuhusu huduma za jamii, ilikubalika kwamba jamii zilizopo karibu na sehemu za kutolea huduma kama zahanati,

hospitali na shule zitumie huduma hizo bila kujali ni za upande upi. Halikadhalika, iliamuliwa kwamba miti ipandwe katika kingo za Mto Songwe pamoja na kuzuia shughuli za kilimo katika maeneo hayo ili kulinda kingo za mto. Kuhusu biashara za mpakani, mkutano ulipitisha azimio la kuanzisha njia inayotambulika ya kupitishia bidhaa. Vilevile iliamuliwa kufanya ukarabati kwenya daraja la Mto Songwe ili kurahisha usafirishaji wa bidha na watu na kuanzisha kituo cha polisi katika eneo la mpakani kudhibiti ungizaji wa bidhaa haramu kutoka kila upande.

Kuitisha mkutano wa pamoja wa ulinzi; Mikutano kati ya Wilaya hizi mbili ilifanyika mara kwa mara ikijumuisha jeshi la polisi, uhamiaji, mamlaka ya mapato (TRA) na Wakala wa Barabara kujadili masuala mbalimbali kuhusu kuboresha ulinzi na usalama. Katika mikutano hii, mwenyekiti wa mkutano ni Mkuu wa Wilaya mwenyeji ambapo mkutano unafanyika. Baadhi ya maazimio katika mikutano hii kuziomba Serikali za pande zote mbili kujenga barabara kuunganisha Wilaya hizi; kwa upande wa Tanzania barabara kutoka kwa Mpemba hadi Isongole 51.1km na kwa upande wa Malawi kutoka Mbilima hadi Chitipa 35km, kujenga kituo cha uhamiaji katika eneo la mpaka kudhibiti uhamiaji haramu na kufanya watu kutumia njia rasmi za kuingia na kutoka kuboresha hali ya ulinzi na usalama. Wakati wa uandishi wa kitabu hiki, barabara hazikuwa zimejengwa kwa kiwango cha lami, hata hivyo matengenezo ya mara kwa mara yamekuwa yakiendelea kuzifanya zipitike muda wote. Kupitia mwendelezo wa mikutano hii, masuala ya ulinzi na usalama yameimarika. Picha ifuatayo inaonesha wajumbe kutoka kutoka pande mbili walipokutana kwenye mojawapo ya mikutano.



***Ujumbe kutoka Malawi ukikutana na wenyeji Tanzania eneo la Isongole karibu na Mto Songwe***

Kuitisha mkutano wa pamoja wa wafanyabiashara kutoka pande zote mbili ambao ulifanyika tarehe 30 Januari, 2015. Katika mkutano huu changamoto zilizowakabili wafanyabiashara, aina za biashara zinaoendeshwa na njia sahihi za uendeshaji wa biashara katika maeneo ya mpakani zilijadiliwa. Lengo kubwa lilikuwa ni kuimarisha uendeshaji wa biashara zinazovuka mpaka. Pia mkutano huu ulilenga kuelimisha wafanyabiashara kuhusu sheria, kanuni na taratibu zinazosimia uendeshaji wa biashara za mpakani na bidhaa zilizozuiliwa kuingizwa nchini. Picha ifuatayo inaonesha wajumbe walioshiriki mkutano wa wafanyabiashara uliofanyika katika Wilaya ya Ileje Tanzania.



***Wafanyabiashara kutoka Malawi walipokutana na Wafanyabiashara wa Tanzania hoteli ya Itumba***

Katika kuendelea kuboresha mahusiano, Wilaya zote mbili ziliweka mkakati wa kutembelea vituo vya watoto yatima na kuwasaidia mahitaji muhimu kama sukari, sabuni, mchele, madaftari pamoja na kuwahimiza kujiunga na shule. Ziara hii iliandaliwa kama mojawapo ya mbinu ya kuimarisha uhusianao kwa jamii za pande zote mbili. Tarehe 31 Desemba 2015, jumla ya vituo vya watoto yatima vitano vilipatiwa msaada kutoka Halmashauri ya wilaya ya Ileje.

Uhamasishaji wa utunzaji wa mazingira kwenye kingo za Mto Songwe ni mbinu iliyotumika katika kukabiliana na tatizo la kuhama kwa mto. Jamii zinazopakana na mto zilihamasishwa kupanda miti kwenye kingo za mto kuzuia mmomonyoko wa udongo unaosababisha kuhamahama kwa mto na migogoro ya ardh. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2015 jumla ya miche ya miti 560 ilitolewa na H/W ya Ileje na kupandwa kwenye kingo za mto. Kuepuka migoforo, iliamuliwa kuwa mpaka wa nchi na nchi utaendelea kubaki katikati ya Mto Songwe hata itakapobainika kwamba mto umehama. Picha ifuatayo inaonesha zoezi la upandaji miti likiendelea.



***Upandaji wa miti ukisimamiwa na Wakuu wa Wilaya kutoka Ileje and Chitipa (Ms. Senyamule and Ms. Chilwa)***

Ukarabati wa daraja la Mto Songwe; Wakuu wa Wilaya zote mbili, walikubaliana kushirikiana na kuchangia matengenezao ya daraja la Mto Songwe, lengo likiwa kuimarisha mawasiliano na usafirishaji. Tanzania ilifanya matengenezo pamoja na kuimarisha kingo za mto chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara. Wilaya ya Chitipa inategemewa kufanya zoezi kama hili la kuimarisha kingo za mto na kuboresha daraja siku zijazo. Huduma za usafirishaji zimeimarika, kumekuwepo na usafiri wa magari madogo ya abiria kila siku kati ya Wilaya za Ileje na Chitipa.

Kuandaa kazidata kuhusu wanufaika wa huduma kutoka Wilaya zote mbili ili kuwezesha kupanga na kufanya maamuzi kuhusu utoaji wa huduma. Kazi data hii ina taarifa za wanufaika wa huduma za afya, elimu, biashara, kilimo na mifugo.

Katika kuendelea kuboresha mahusiano, kila mwaka Wilaya za Ileje na Chitipa zimekuwa zikiandaa sherehe ya pamoja ambapo hutumia fursa hii kutathimini mafanikio na changamoto na kuweka mikakati ya kuendelea kuboresha mahusinao na ushirikiano. Sherehe ya mwisho ilifanyika mwaka 2015/2016 katika Wilaya ya Ileje. Mikakati ya kuandaa sherehe nyingine kwa mwaka 2016/2017 ilitakiwa kuandaliwa na Wilaya ya Chitipa. Mkakati mwingine ulikuwa ni uanzishaji wa soko la mazao ya kilimo la pande zote ambapo kwa Wilaya ya Ileje soko limekamilika, linafanya kazi na wananchi wote wa Ileje na Chitipa wanapata huduma za soko.

**5.0 RASLIMALI**

Utekelezaji wa jitihada hii ulihusisha matumizi ya raslimali watu na raslimali fedha. Raslimali watu; Wakuu wa Wilaya ambao walianzisha wazo hili na kulisimamia, Timu ya Menejimenti ya Halmashauri ambayo ilisimamia utekelezaji kwa kuunda timu ya uratibu, Madiwani, Machifu na jamii kwa ujumla. Raslimali fedha zilitumika kulipa posho mbalimbali, gharama za usafiri kutembelea pande zote mbili, sherehe mbalimbali zilizojumuisha wadau, ununuzi wa mbegu za miti, ujenzi wa soko la mazao, ukarabati wa daraja pamoja na ujenzi wa kingo za mto.

**6.0 MATOKEO**

Utekelezaji wa jitihada hii umeboresha mahusiano rasmi kati ya wananchi wa pande mbili. Mabadiliko haya yanadhihirishwa na matokeo yafuatayo;

Migogoro ya ardhi imetatuliwa na viongozi wa ngazi za msingi bila kuhusisha wanadiplomasia wa kitaifa. Wananchi wanaopakana na Mto Songwe wamekubaliana kuheshimu Mto Songwe kuwa ndio mpaka bila kujali kuhamahama kwa mto. Jamii za pande zote mbili zimepanda miti ipatayo 560 pembezoni mwa kingo za mto kuhifadhi mazingira na kupunguza mmomonyoko wa ardhi katika kingo za mto. Vilevile, mikutano ya ujirani mwema imekuwa ikifanyika mara kwa mara; mkutano wa wataalamu kujumuisha idara mbalimbali za Wilaya hizi mbili imekuwa ikifanyika mara mbili kwa mwaka kujadili masuala mbalimbali ya kuboresha utoaji wa huduma na mikutano ya ulinzi na usalama chini ya Wakuu wa Wilaya imefanyika kila mwaka ili kujenga mahusiano endelevu ya wananchi wa pande zote mbili.

Utoaji wa huduma mbalimbali umeimarika; huduma za elimu, afya na kilimo zimeimarika baada ya makubaliano kufanyika kwamba wanajamii waliopo maeneo ya karibu na huduma inapopatikana wanufaike na huduma hizo bila kujali kijiji au nchi wanayotokea. Wafanyabiashara za mpakani wamehamasika na wanatumia mifumo rasmi inayokubalika na wanafanya biashara kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia biashara za mpakani. Soko la mahindi limeanzishwa eneo la Isongole katika Wilaya ya Ileje kutokana na makubaliano ya Wilaya zote mbili. Wananchi wa pande zote mbili wananufaika na huduma za soko hili. Kujengwa kwa soko hili, mbali na kupanua wigo wa biashara ya mazao baina ya wananchi wa Wilaya hizi mbili, H/W ya Ileje imeongeza chanzo cha mapato yake ya ndani. Kutokana na kuruhusiwa kwa wananchi wa Malawi kuuza mazao yao ndani ya soko hili, imesaidia Mamlaka ya Taifa ya Hifadhi ya Chakula (NFRA) kuongeza kiasi cha hifadhi ya chakula kutokana na ongezeko la uzalishaji kutoka nchi jirani. Picha ifuatayo inaonesha soko la mahindi la Isongole.




***Soko la kimataifa la mahindi Isongole***

Magonjwa ya mazao na mifugo kwa kiasi kikubwa yamepungua; Magonjwa kama homa ya nguruwe, kichaa cha mbwa, ugonjwa wa miguu na midomo na magonjwa ya mazao yamepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na ushirikiano baina ya wataalamu wa pande mbili. Ushirikiano huo umejikita katika kupeana taarifa za magonjwa, mipango ya kudhibiti magonjwa ya mlipuko, idadi ya mifugo iliyoathirika na taarifa za chanjo. Kupatikana kwa taarifa hizi kunasaidia maafisa ugani na H/W kujipanga na kuweka mikakati ya kuzuia magonjwa hayo.

Ukarabati wa daraja la kuvuka mto Songwe umefanyika kwa makubaliano yaliyofikiwa kutokana na ushirikano ulioanzishwa. Wakala wa Barabara alianza kufanya ukarabati na kulifanya daraja liwe linapitika, makubaliano yamefikiwa kwamba Serikali za pande zote zitakuwa zinafanya ukarabati wa daraja mara kwa mara kwa kupeana zamu ili kuboresha mawiliano ya pande zote. Picha ifuatayo inaonesha daraja la Mto Songwe baada ya ukarabati na uimarishaji wa kingo za mto.




*Daraja lilikarabatiwa pamoja na ujenzi wa kingo za mto*



*Usafiri wa kila siku kati  ya Ileje na Chitipa umeboreshwa*

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Katika kuhakikisha uhusiano huu unakuwa endelevu, Wilaya zote mbili zimeweka mikakati ya uendelevu kama ifuatavyo; mikutano ya ujirani mwema na sherehe za pamoja  (Wilaya ya Ileje na Chitipa) vimefanywa kuwa ajenda ya kudumu. Kila Wilaya imekuwa ikweka mipango na kuaanda bajeti kwa ajili ya kutekeleza matukio haya.

Serikali za pande zote mbili zitaendelea na ukarabati wa daraja la Mto Songwe wa mara kwa mara kuhakikisha shughuli za usafirishaji ni endelevu na kuondoa matumizi ya njia zisizo rasimi ambazo zimekuwa zikitumika hapo awali.  H/W ya Ileje imejenga kituo cha ukaguzi katika eneo la mpaka na kuanzisha kituo cha muda cha uhamiaji ambapo kuna askari polisi wanaotoa huduma kwa masaa 24

kuhakikisha ulinzi na usalama. Halmashauri imekuwa ikifanya majadiliano na Serikali Kuu kushawishi ujenzi barabara kuu kutoka kwa Mpemba hadi mpakani ili kurahisha usafirishaji wa mazao na watu. Picha ifuatayo inaonesha kituo cha ukaguzi na ofisi ya muda ya uhamiaji.



***Ofisi ya muda ya uhamiaji na kituo cha ukaguzi***

Wilaya zote mbili zinaendelea kuhamasisha uhifadhi wa mazingira katika bonde la Mto Songwe ili kupunguza mmomonyoko wa udongo unaosababisha kuhamahama kwa mto. Wilaya zinaendelea kujenga uelewa kwa jamii kundelea kulinda na kutunza mazingira ya Mto Songwe pamoja na kuzipatia mbegu za miti ya kuotesha maeneo kwenye kingo za mto. Picha ifuatayo inaonesha bango la kuhamasisha uhifadhi wa Mto Songwe lililowekwa na H/W ya Ileje.




***Bango la kuhamasisha uhifadhi wa mazingira ya Mto Songwe***

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Mafanikio ya jitihada hii yalitokana na siri mbalimbali; uongozi thabiti wa Wakuu wa Wilaya walioanzisha na kusimamia utekelezaji. Wakuu wa Wilaya walitumia fursa na raslimali katika kuimarisha amani kati ya wananchi na Serikali za pande mbili. Siri nyingine ni Historia na mwingiliano wa tamaduni za wananchi wa pande zote mbili, hii ilisadia urahisi katika mawasiliano, kupunguza vikwazo vya ukabila ambavyo vingeweza kukwamisha utekelezaji na kuboresha amani. Uongozi wa kichifu katika maeneo ya mpakani umejumuisha wananchi wa pande zote mbili; Chifu mmoja anatumiwa na wananchi wa pande zote kama kiongozi wao. Kutokana na aina hii ya uongozi ilikuwa rahisi kuwaweka pamoja wananchi wa Chitipa na Ileje katika kufikia maamuzi.

Ushirikiano wa wadau kutoka Wilaya za Ileje na Chitipa katika kuhamasisha mkakati huu ni siri nyingine ya mafanikio. Wakuu wa Wilaya, Kamati ya Ulinzi, Katibu Tawala, Wenyeviti wa Halmashauri, Wabunge, Wakurugenzi Watendaji, Wakuu wa Idara, wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla walishirikiana katika kuhakikisha malengo yanafikiwa. Wadau wengine ni pamoja na Taasisi kama TANROAD, TRA. TFDA, TCCIA, NGOs na NMB walitoa ushirikiano katika utekelezaji wa jitihada hii.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA

**UBORESHAJI WA HUDUMA ZA ELIMU KUPITIA MFUKO WA MAENDELEO YA ELIMU**









***UZOEFU WA H/W YA NEWALA***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Newala ni moja kati ya Halmashauri tisa za Mkoa wa Mtwara ikiwa Wilaya kongwe iliyoanzishwa mwaka 1954 chini ya ukoloni wa Waingereza kwa sheria ya Serikali za Mitaa (Local Government Ordinance). Jina la Halmashauri linatokana na neno la Kimakonde *"niwaala"* kwa kumaanisha *"Karibu"*. Mwanzoni mwa karne ya 19, kiongozi wa Wajerumani akiwa kwenye harakati za kutafuta maji kwa ajili ya ujenzi wa *"boma"* alishindwa kutamka neno "*niwaala"* ambapo alitamka "Newala"hapo ndipo jina la Newala lilipoanza kutumika. Makao makuu ya Halmashauri yapo umbali wa 140km Kusini Magharibi mwa Mji wa Mtwara yalipo makao makuu ya Mkoa.

Kijiografia, Newala inapatikana Kusini Mashariki mwa Tanzania kati ya Longitudo $39^{o}$ - $40^{o}$ Mashariki na Latitudo $10^{o}$ -$11^{o}$ Kusini. H/W ya Newala inapakana na Halmashauri za Wilaya za Masasi kwa upande wa Magharibi, Tandahimba upande wa Mashariki, Mkoa wa Lindi upande wa Kaskazini na Jamuhuri ya Msumbiji upande wa Kusini. Eneo la ardhi la Halmashauri ni 2,439$km^2$ ambazo zipo katika mwinuko wa 900m juu ya usawa wa bahari. Maeneo ya kiutawala yamegawanyika katika Tarafa 5, Kata 33, Vijiji 155 na Vitongoji 492. Ifuatayo ni ramani ya H/W ya Newala ikionesha maeneo ya kiutawala.




***Ramani ya H/W ya Newala***

Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, idadi ya watu ilikuwa 205,492, kati yao 95,018 ni wanaume na 110,474 wanawake na wastani wa ongezeko la watu ni asilimia 1.2. Uchumi wa ndani kwa kiasi kikubwa unategemea kilimo na biashara ndogondogo. Mazao yanayozalishwa kwa kiwango kikubwa ni pamoja na korosho, mihogo na mahindi. Korosho ndio zao kuu la biashara ambalo linachangia ongezeko la kipato cha wananchi wa Newala na zaidi ya 77% ya mapato ya Halmashauri. Mihogo na mahindi huzalishwa kama mazao ya chakula, shughuli za ufugaji zinafanywa kwa kiasi kidogo sana.

H/W ya Newala kama ilivyo kwa Halmashauri nyingine, imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuboresha sekta ya elimu. Halmashauri imekuwa ikipiga vita ujinga kwa jamii kama vile ambavyo Serikali Kuu

ilitangaza ujinga kama sehemu ya maadui watatu wa taifa. Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa elimu waliweka jitihada mbalimbali katika kuboresha hali ya utoaji elimu ili kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ya kuwa na jamii iliyoelimika. Mwaka 2011 Halmashauri ilifanya tathimi katika sekta ya elimu ili kutambua changamoto zinazokabili sekta hiyo.

**2.0 TATIZO**

Kabla ya mwaka 2011, hali ya utoaji wa huduma ya elimu katika Halmashauri ulikua duni kwa Shule za Msingi na Sekondari. Changamoto zilizo kabili sekta ya elimu ni pamoja na uhaba wa miundombinu ya kutolea elimu; kwa shule za sekondari, kati ya shule 26, shule 22 hazikuwa na miundominu ya kutosha kama vyumba vya madarasa na maabara. Japokuwa baadhi ya shule chache zilikuwa na majengo ya maabara, vifaa muhimu havikuwepo. Vilevile, Halmashauri ilikabiliwa na changamoto ya uhaba wa nyumba za waalimu, vyoo vya wanafunzi na madawati. Upungufu wa nyumba za waalimu ulikuwa nyumba 276, upungufu wa madarasa 28, Matundu ya vyoo 189 na Madawati 220.

Upungufu katika shule za msingi ulikuwa nyumba za walimu 527, madarasa 265, madawati 3200 na matundu ya vyoo 654. Kutatua changamoto hizi, ilikuwa ni jukumu la Halmashauri pekee kwani jamii za Wamakonde kwa kipindi kirefu hazikuthimini elimu na umuhimu wake, hivyo uchangiaji wa fedha kutatua changamoto za elimu kwao haikuwa kipaumbele. Hali hii iliwafanya wawe wagumu wa kuchangia ujenzi wa miundominu ya elimu hata pale walipohimizwa kufanya hivyo. Vilevile, jamii za Wamakonde zina kasumba ya kutokutoa michango ya fedha taslimu; huona ni bora kuchangia nguvukazi kuliko fedha taslimu. Ili kutatua changamoto hizi, Halmashauri iliamua kuchukua hatua kwa kuanzisha Mfuko wa kuchangia maendeleo ya elimu Newala *(“Newala Education Development Fund” (NEDF).*

**3.0 MALENGO**

Lengo la Halmashauri katika kuanzisha Mfuko wa Elimu lilikuwa kuboresha utoaji wa huduma ya elimu kwa kuhakikisha mahitaji yote ya msingi yanapatikana na kutoa elimu inayokidhi viwango. Malengo mahususi ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Elimu wa Halmashauri kama mbinu ya kuishurutisha jamii kuchangia maendeleo ya elimu ndani ya Wilaya yao, kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuchangia maendeleo ya elimu na miradi mingine ya maendeleo, kubuni na kuanzisha mkakati wa kukusanya fedha kutoka katika jamii na wadau wa elimu, kuboresha na kujenga miunduminu ya shule kama madarasa, maabara, matundu ya vyoo, nyumba za waalimu, madawati, meza na viti kwa shule za msingi na sekondari. Halmashauri vilevile ililenga kuwatambua watoto wenye mahitaji maalum na kuwasaidia kupata elimu na kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu na watumishi wengine katika sekta ya elimu ili kuwafanya wafurahie mazingira ya kazi na kuboresha utendaji wao.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Elimu Newala kulitokana na wazo la Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Wazo la kuanzishwa kwa Mfuko lilijadiliwa na Timu ya Menejimenti ya Halmashauri na baadae wazo liliwasilishwa kwa wajumbe wa Baraza pamoja na Mbunge wa Newala Mh. Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika. Mfuko huu ulianzishwa kusaidia katika ujenzi wa miundombinu ya shule. Ili kufanikisha ukusanyaji wa fedha kwenye mfuko, mbinu ya kukata fedha moja kwa moja kutokana na mauzo ya korosho ilitumika. Baraza liliidhinisha ukusanyaji wa michango kupitia mfumo wa stakabadhi mazao ghalani. Mpango huu wa kukusanya kupitia stakabadhi mazao ghalani ulibuniwa kutokana na ukweli kwamba jamii za Wamakonde hazina utayari wa kuchangia fedha taslimu pindi zinapotakiwa kufanya hivyo. Kutokana na kukubalika kwa wazo la kuanzisha mfuko wa elimu na msukumo wa nguvu ya kisiasa, hatimaye mfuko wa maendeleo ya elimu Newala ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa namba 7 sura ya 287 sehemu ya 153. Kufikia malengo yaliyokusudiwa, mbinu/mikakati ifuatayo ilitekelezwa;

Kukusanya taarifa za elimu na kuzichambua ili kutambua hali halisi katika sekta ya elimu ndani ya Halmashauri; zoezi hili lilifanywa na kikosi kazi kilichoanzishwa na Halmashauri na kupewa hadidu za rejea kama ifuatavyo: kufanya tathimini ya hali halisi ya sekta ya elimu ndani ya Halmashauri, kubaini matatizo yanayokabili sekta ya elimu, kubaini ukubwa wa tatizo, madhara na njia mbadala za kuondoa matatizo hayo kwenye sekta ya elimu. Kikosi kazi kilifanikisha zoezi na kubaini changamoto mbalimbali kama upungufu wa miundombinu ya shule, upungufu wa waalimu kwa shule za msingi na sekondari, mazingira magumu ya kazi kwa watumishi wa elimu na uwepo wa idadi kubwa ya watoto wenye mahitaji maalum. Kikosi kazi kilishauri Halmashauri kujenga miundombinu kama madarasa, matundu ya vyoo, nyumba za walimu kwa lengo la kuboresha utoaji wa elimu na kuweka mpango wa usaidizi wa watoto wenye uhitaji wa huduma maalum.

Kikosi kazi kilikabidhi taarifa yake kwa Timu ya Menejiment ya Halmasahuri tarehe 15/11/2010. Baada ya kupokea taarifa, Halmashauri pamoja na Mbunge wa Newala waliaandaa andiko la kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Elimu Newala. Tarehe 18/11/2010 andiko liliwasilishwa kwenye kamati ya Fedha, Mipango na Utawala kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa kwenda kwenye Baraza. Wakati wa kuanzisha mpango huu, Mbunge wa Newala alikuwa bega kwa bega katika kuhakikisha wazo hili linakubalika. Baada ya taarifa kufikishwa kwenye Baraza la Madiwani ilijadiliwa na hatimaye baraza liliidhinisha kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Elimu Newala.

Kuanzishwa kwa kamati ya mipango na uratibu; Baada ya Baraza kuridhia kuanzishwa kwa mfuko wa elimu, kamati ya uratibu ikijumuisha wataalamu kutoka Halmashauri ilianzishwa. Kamati hii iliundwa na wajumbe wafuatao; Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Mweka Hazina, Afisa Mipango na Maafisa Elimu wa shule za Sekondari na Msingi. Kamati ilipewa jukumu la kuandaa andiko, kuweka mikakati ya uendeshaji wa mfuko na kutathimi kiwango fedha kinachohitajika kuanzisha mfuko wa maendeleo ya elimu Newala. Kamati iliweka mpango wa kuhusisha wadau wa sekta ya elimu ndani ya Wilaya kwa kueleza mpango wa kuchangia mfuko, kupanga kiwango cha michango na kuanzisha bodi ya usimamizi wa mfuko wa maendeleo ya elimu.

Kamati ya uratibu ilibaini na kuunganisha wadau wa elimu ndani ya Halmashauri. Wadau hawa ni pamoja na taasisi za Serikali zinazotekeleza majukumu yake ndani ya eneo la Halmashauri, watumishi wa Serikali, taasisi binafsi zenye kupenda maendeleo ya elimu, jamii za watu wa Newala na wazawa wa Newala wanaoishi nje ya Newala. Wadau walifahamishwa kuhusu wazo la Halmashauri katika kuendeleza sekta ya elimu na kuhamasishwa kuhusu umuhimu wa kuchangia mfuko wa elimu. Baada ya hamasa hii watumishi wa Umma wanaofanya kazi kwenye taasisi zilizopo ndani ya eneo la Halmashauri waliridhia kuchangia shs 2,000 kwa mwaka.

Uhamasishaji wa jamii; kamati ya uratibu wa mfuko, baada ya kuwatambua wadau mabalimbali wa elimu, iliendesha mikutano ya Vijiji kuhamasisha jamii na kujenga uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa kuwa na mfuko wa elimu. Uhamasishaji ulihusu kutambulisha mkakati ya ukusanyaji wa fedha kutoka kwa wananchi na michango yao itatokana na mauzo ya korosho kupitia mfumo wa stakabadhi mazao ghalani. Kamati pia ilipendekeza kiwango cha kuchangia kutokana na mauzo ya kila mkulima kwa kiasi cha shs 20 kwa kila kilo ya korosho. Viongozi wa kisiasa kama madiwani, wenyeviti, na wazee maarufu walihusika katika kutoa hamasa ya kukubalika kwa mpango huu. Jamii ilihamasika na kukubaliana kiwango kilichopendekezwa na njia ya ukusanyaji kupitia mfumo wa stakabadhi mazao ghalani.

Kamati ya uratibu kuandaa mpango wa utekelezaji wa mfuko; Mpango huu uliandaliwa kuonesha utaratibu wa kuendesha mfuko wa maendeleo ya elimu. Mpango uliwasilishwa kwenye Timu ya

Menejimenti kwa ajili ya majadiliano na maboresho. Baada ya kikao cha menejimenti, mpango uliwasilishwa kwenye kamati ya Elimu, Afya na Maji na kamati ya fedha kabla ya kufikishwa kwenye Baraza kwa ajili ya kuidhinishwa. Baraza liliidhinisha mpango na kuwasilishwa Ofisi ya Rais –TAMISEMI kupata kibali cha uchangishaji. Mfuko wa Maendeleo ya Elimu Newala ulitangazwa kwenye gazeti la Serikali namba 257 la tarehe 02/09/2011.

Kuandaaa kanuni na taratibu za kuendesha Mfuko wa Elimu; Halmashauri iliandaa kanuni na taratibu za kusimamia uendeshaji wa mfuko. Kanuni hizi ziliundwa kutokana na matakwa ya sheria mama (Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287 sehemu ya 153 na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa sura ya 290. Kanuni ziliundwa ili kuhimiza ukusanyaji wa fedha kutoka kwa wadau na kuanzisha bodi ya udhamini ya kusimamia mfuko.

Uundaji wa Bodi ya Mfuko; Bodi ya udhamini iliundwa na wajumbe 11 kutokana na wadau wa elimu ikiwa na Mwenyekiti, Katibu wa Bodi ambaye ni Afisa Elimu aliyeteuliwa na Timu ya Menejimenti ya Halmashauri, Mkurugenzi Mtendaji, Afisa Mipango, Katibu Tawala wa Wilaya, Mjumbe mmoja kutoka vyama vya ushirika na jamii, pamoja na wawakilishi wawili kutoka shule za sekondari na shule za msingi. Bodi hufanya kazi kwa muda wa miaka 3. Majukumu ya Bodi ya udhamini ni kusimamia uendeshaji wa Mfuko, kuidhinisha mipango na bajeti ya utekelezaji wa miradi kwa kushirikiana na kamati ya uratibu wa mfuko na kusimamia fedha na taarifa za kibenki. Baada ya uundwaji wa Bodi ya udhamini, Mfuko ulianza rasmi kufanya kazi mwaka wa fedha 2013/2014.

Mwaka 2013/2014, mfuko ulikusanya fedha taslimu kiasi cha shs 337,021,280, Fedha hizi zilitumika kuboresha miundombinu ya shule za Sekondari na Msingi. Jumla ya shs 275,000,000 zilitumika katika ujenzi wa chumba kimoja cha maabara kwa kila shule. Shule za sekondari 12 zilinufaika na fedha hizi. Kiasi cha fedha kilichosalia cha jumla ya shs 51,000,000 kilitumika kuboresha miundumbinu ya shule 17 za msingi. Fedha hizi zilitumika kujenga matundu ya vyoo, kukamilisha ujenzi wa madarasa ambayo yalianza kujengwa kwa nguvu za wananchi. Kila shule ilipokea shs 3,000,000 kuimarisha miundombinu.

Kuanzisha mkakati madhubuti wa kukusanya michango kutoka kwa jamii na wadau wa elimu; kamati ya uratibu iliweka mikakati ya kukusanya fedha kutoka kwa wakulima kupitia mfumo wa stakabadhi mazao ghalani. Mfumo huu wa stakabadhi mazao ghalani kwa Tanzania ulianzishwa mwaka 2007 chini ya progamu ya kuboresha kilimo na masoko (AMSDP). Mfumo huu unaendeshwa kupitia vyama vya msingi vya wakulima (AMCOS) na Vyama Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS). Kupitia mfumo huu, wakulima hulipwa 70% ya bei ya mazao mapema kabla ya mauzo na kupatiwa risiti ambayo wanapaswa kuitunza hadi mauzo halisi ya mazao yatakapofanyika na hulipwa 30% iliyobaki na ongezeko ambalo litakuwa limepatikana. Pamoja na fedha wanazolipwa, gharama za mnada na uhifadhi wa mazao katika ghala zinalipwa na uongozi uliosimamia mnada na uhifadhi wa mazao. Mfumo wa stakabadhi mazao ghalani uliibuliwa katika kudhibiti wanunuzi wakubwa wanaopenda kununua moja kwa moja kutoka kwa mkulima ambao hutumia fursa hiyo kuwalaghai kwa kuwalipa bei ndogo. Kupitia mfumo huu wakulima huuza korosho zao kwa pamoja kupitia mnada. Kupitia mfumo huu wakulima walikubali kukatwa shs 20 kwa kila kilo moja ya korosho iliyouzwa. Kwa wananchi ambao sio wakulima wa korosho, iliamuliwa wachangie shs 2,000 kwa mwaka. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 mfuko wa elimu ulikusanya jumla ya shs 424,686,810.

**5.0 RASLIMALI**

Uanzishaji na usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Elimu Newala ulimbatana na matumizi ya raslimali. Raslimali fedha zilitumika kulipa gharama za vikao vya kamati na mikutano ya Baraza iliyoipitia na kuidhinisha mpango huu, gharama za usafiri na posho kwa kikosi kazi cha kukusanya na kuchambua

taarifa za hali halisi ya sekta ya elimu ndani ya Halmashauri, fedha za usafiri na posho wakati wa kuwasilisha mpango OR-TAMISEMI, gharama za usafiri katika uhamasishaji wa jamii na gharama za kutangaza Mfuko kwenye gazeti la Serikali. Kuhusu raslimali watu, watumishi wa Halmashauri, Madiwani, Mbunge wa Newala, wajumbe wa Bodi ya Udhamini, wajumbe wa kamati ya uratibu, Watendaji wa Kata na Vijiji na viongozi maarufu walitumika katika kuhamasisha jamii kukubali na kuchangia Mfuko wa Maendeleo ya Elimu Newala.

**6.0 MATOKEO**

Mfuko wa Maendeleo ya Elimu Newala ulianzishwa ili kusaidia kuboresha sekta ya elimu ndani ya Halmashauri kwa kuhusisha michango ya jamii ya Wamakonde na wadau wengine wa elimu. Utekelezaji wa Mfuko huu umeleta watokeo yafuatayo;

Mfuko wa Maendeleo ya Elimu Newala upo na unafanya kazi. Mfuko unaendeshwa vizuri kwa kufuata kanuni na taratibu, uwepo wa Bodi ya udhamini na Kamati ya watalamu wa kusimamia uendeshaji wa mfuko wa elimu. Kuna mpango madhubuti wa kukusanya michango ambao uliwezesha kukusanya shs 337,021,280 mwaka 2013/2014 na shs 424, 686,810 kwa mwaka 2014/2015. Fedha zilizokusanwa ziliwezesha kutengeneza miundombinu ya shule za Msingi na Sekondari. Jedwali lifuatalo linaonesha matokeo ya mfuko kwa kuainisha miundumbinu iliyojengwa katika shule tofauti za Msingi na Sekondari kutokana na fedha za mfuko.

**Jedwali Na1: Miradi iliyotekelezwa kwa fedha za Mfuko**

| Mwaka wa fedha | Mradi uliotekelezwa | Kiasi cha fedha (TShs) | Picha |
|---|---|---|---|
| 2013/14 | Ujenzi wa maabara kwa shule 12 za sekondari | 275,000,000 |  (Picha ya maabara shule ya sekondari Dr. Alex Mtavala) |
| | Kuimarisha miundombinu ya shule za msingi kama madarasa | 51,000,000 |  |
| 2014/15 | Ujenzi wa maabara kwa shule 22 za sekondari (picha– maabara shule ya sekondari Mpotola) | 408,000,000 |  |

Jamii imebadilika kimtizamo; wanajamii wamekuwa na moyo wa kuchangia miradi ya maendeleo ndani ya Halmashauri. Kabla ya kuanzisha Mfuko ilikuwa ni vigumu kwa jamii za Wamakonde kuchangia fedha taslimu katika miradi ya maendeleo hususan sekta ya elimu. Uhamasishaji uliofanywa na Halmashauri kupitia Mikutano ya Vijiji umesaidia katika kubadilisha mtazamo wa jamii kuhusu elimu.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Uendelevu wa Mfuko wa Maendeleo ya Elimu ni jambo la msingi. Ili kuhakisha matokeo yanakuwa endelevu Halmashauri imeweka utaratibu wa kuteua Bodi kila baada ya miaka mitatu. Lengo la kufanya mabadiliko ya bodi ni kukuza uwajibikaji na kuleta mawazo na ubunifu mpya wa kuongeza ufanisi wa

Mfuko. Halmashauri inaendelea kubuni vyanzo vingine vya fedha kupunguza utegemezi kwa zao la korosho kwa kuwa bei ikishuka au uzalishaji ukipungua utapelekea kuathiri mapato ya Mfuko. Vilevile Halmashauri imeweka mpango wa kushawishi watumishi wa umma kuongeza michango kutoka shs 2,000 kwa mwaka hadi kufikia shs 5,000.

Halmashauri inaendelea kukuza hamasa kwa jamii na wadau kuongeza utashi katika kulipa michango yao kwa wakati, kuongeza uzalishaji wa zao la korosho na kuendelea kutumia mfumo wa stakabadhi mazao ghalani. Ili kuboresha uzalishaji wa korosho, Halmashauri imekuwa ikitenga 40% ya mapato kutokana na korosho kusaidia wakulima kununua pembejeo za kilimo. Halmashauri ina mpango wa kufungua akaunti maalumu ya benki kwa ajili ya mfuko wa maendeleo ya elimu ili kuepuka kuchanganya fedha za elimu kwenye akaunti ya maendeleo ya Halmashauri.

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Mafanikio ya mpango huu yanatokana na utayari na uthubutu wa viongozi wa Halmashauri ya Newala; Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri alikuwa na maono ya kuibadilisha jamii ya Newala, alitumia maarifa na uzoefu wake kubuni na kutekeleza mpango wa Mfuko wa Maendeleo ya Elimu Newala. Mbunge wa Newala pia alikuwa na utayari wa kuisaidia jamii yake, alijitolea kwa raslimali na muda wake katika kupigania uanzishwaji wa Mfuko wa Elimu. Vile vile Mbunge alifanya mawasiliano na kufuatilia OR-TAMISEMI iweze kuridhia kuanzishwa kwa mfuko na kutangazwa katika gazeti la Serikali.

Timu ya Menejimenti ya Halimashauri, Madiwani, na viongozi wa kimila walikuwa na utayari na hamu ya kuona jamii ya watu wa Newala iliyoelimika; hii ilipelekea kila mmoja kuhamasisha jamii kuchangia kwenye mfuko wa elimu. Uwepo wa zao la korosho, chama cha ushirika na mfumo wa stakabadhi mazao ghalani ni siri nyingine iliyopelekea kufanikiwa kwa mpango huu. Uwepo wa watumishi wa umma na utayari wao katika kuchangia mfuko kupitia makato kwenye mshahara ni sababu nyingine iliyowezesha kufanikiwa kwa mfuko. Vilevile uwepo wa wadau wa elimu na wazawa wa Newala wanaoishi nje ya Newala ambao walikuwa tayari kuchangia ni siri nyingine ya mafanikio.

# Sura ya Tano:
# Maendeleo ya Jamii Kiuchumi

Sura ya tano ina mbinu bora tatu zinazohusu jitihada za wananchi kujiletea maendeleo ya kiuchumi kwa dhana mpya ya "Kijiji Kimoja Zao Moja". Dhana hii husisitiza maendeleo yanayotokana na jamii yenyewe kwa kuibua miradi yenye upekee na vijiji vingine. "Kijiji Kimoja Zao Moja" (OVOP) ni harakati zilizoanza miaka ya 1970 katika eneo la Oita nchini Japani malengo yakiwa kuinua uchumi vijijini. Lengo mahususi la dhana hii lilikuwa ni kuhamasisha kila kijiji cha Oita kuibua mradi wa uzalishaji ambao unautofauti wa aina fulani katika mkoa na kuzalisha kwa viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

Dhana ya "Kijiji Kimoja Zao Moja" inalenga kuinua maendeleo ya jamii na uchumi katika mkoa kupitia kujitolea kuinua uwezo wa wananchi wa ngazi ya chini kabisa. Kabla ya kuanzisha harakati hizi katika eneo la Oita, waanzilishi walipata ushirikiano mkubwa wa jamii kupitia mashindano ya mpira na walikuwa na ushirikiano na miji rafiki ya nchi za nje. Mbinu hizi ziliwaweka watu pamoja, ziliwajengea uwezo wa kimaendeleo, na walishirikishana ujuzi waliopata. Mikakati mingine iliyofuata ilikuwa ni kuanzisha sera za jamii kuongeza thamani ya bidhaa, kuboresha mifumo, kuanzisha zao jipya au la kipekee, ufundi wa kuchakata mazao ya kilimo, utalii, na kubadili mtazamo juu ya hali ya jamii.

Dhana ya "Kijiji Kimoja Zao Moja" inaonekana kuwa ni njia ya kuimarisha ujasiriamali wa watu wa vijijini kwa kutumia raslimali, elimu na uzoefu, kufanya kazi zinazoongeza thamani kwa kuzipa utofauti bidhaa zao na kujenga uwezo wa raslimali watu katika shughuli za uchumi kijijini. Kutumia ujuzi na raslimali zilizopo bila kuathiri mazingira ni jambo linalotiliwa mkazo sana katika shughuli za dhana hii. Hii pia ina uhusiano na dhana ya maendeleo yanayotokana na jamii yenyewe. Katika harakati za Kijiji Kimoja Zao Moja, kuna msemo maarufu usemao "Fikiri kimataifa lakini tenda kulingana na Mazingira".

Sura ya tano ina mbinu bora tatu kutoka Halmashauri za Wilaya za Mbinga, Masasi na Tunduru. Mbinu bora ya H/W ya Mbinga inahusu jitihada za Halmashauri katika kukuza zao la Kahawa na kuboresha hali ya kipato cha wakulima. Kabla ya kuanza kwa jitihada hii wakulima waliathirika kutokana na kushuka kwa bei ya kahawa kwenye soko la kimataifa, kupungua kwa uzalishaji kutokana na kukosekana kwa utaalamu wa kuzalisha kisasa, hapakuwa na; miundombinu ya kuchakata kahawa yenye ubora, mahusiano baina ya wakulima wa kahawa na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania kwa ajili ya usaidizi kwa wakulima, maghala yaliyothiishwa kwajili ya kuhifadhi kahawa na wakulima walikosa umoja wa kuwasidia kutafuta masoko na kushughulikia changamoto zao hasa kushughulikia bei ya kahawa. Kutokana na changamoto hizi, Halmashauri ilendesha mikutano na wadau wa kahawa na kuwashawishi kutoa usaidizi kwa wakulima kuimarisha uzalishaji wa kahawa. Halmashauri ilianza kutoa mafunzo kwa maafisa ugani kuwajengea uwezo wa kuelimisha wakulima. Vilevile, Halmashauri ilianza kukarabati maghala ya kutunzia kahawa kuyafanya yapate hadhi ya kutunza kahawa. Halmashauri pia iljenga vinu vya kisasa vya kukobolea kahawa iwe na ubora na kuwaunganisha wakulima kuanzisha cha cha wakulima wa kahawa (AMCCOs). Utekelezaji wa mikakati hii uliimarisha ubora wa kahawa ya Mbinga na kuifanya itambulike na kupata bei nzuri kwenye soko la kimataifa.

Mbinu Bora ya Halmashauri ya Masasi inahusu juhudi za Halmashauri kuboresha minundombinu ya umwagiliaji kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mpunga na kuimarisha uhakika wa chakula na kipato kwa

wakulima wa vijiji vya Njenga, Mpoera na Mwena katika Kata ya Ndanda. Jamii hizi kwa kipindi kirefu zimekuwa zikijihusisha na kilimo cha mpunga, mahindi na mbogamboga kwa kutumia miundombinu duni ya umwagiliaji. Miundombinu ya umwagiliaji haikuwa imeboreshwa hivyo kusababisha upotevu mwingi wa maji ambayo yangeweza kutumika kwa umwagiliaji. Changamoto hizi zilipunguza kwa uzalishaji wa mazao na kudidimiza kipato cha mkulima. Mwaka 2002 wakati wa uendeshaji wa Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD), jamii ziliibua hitaji la kuboresha skimu ya umwagiliaji ya Ndanda. Halmashauri iliamua kutoa usaidizi kwa jamii hizo kutekeleza mpango wao. Halmashauri iliunda Timu ya Maendeleo ya Umwagiliaji ya Wilaya (DIDT) kuratibu shughuli za kujenga miundombinu ya skimu na kuunganisha wadau mbalimbali kutoa usaidizi kwenye skimu ya umwagiliaji ya Ndanda. Wakulima waliwezeshwa kupitia mafunzo kuanzisha umoja wao na kuusajili. Kabla ya kupokea usaidizi jamii zilianza kujipanga kuboresha miundombinu ya umwagiliaji. Baada ya kukamilika kwa skimu uzalishaji umeongezeka na kipato kuimarika. Pia Halmashauri imenufaika kwa kuongezeka kwa mapato ya ndani kutokana na ushuru wa mazao yanayotakana na skimu ya umwagiliaji ya Ndanda.

Mbinu Bora ya H/W ya Tunduru inaeleza jitihada za Halmashauri kuboresha uzalishaji wa mpunga na kuongeza thamani. Lengo lilikuwa kuboresha uzalishaji na kuimarisha kipato cha mkulima. Changamoto zilizopelekea kuanzishwa kwa jitihada hii ni kushuka kwa bei ya zao la korosho kwenye soko la dunia kuanzia mwaka 2011. Jambo hili liliwafanya wakulima kuachana na kilimo cha korosho na kuamua kulima mpunga. Uzalishaji wa mpunga ulikuwa duni kwa sababu; zao lilikuwa jipya, wakulima hawakuwa na utaalamu wa kutosha, kulikuwa na uhaba wa mvua jambo ambalo lilipelekea mavuno hafifu na ukosefu wa teknolojia ya umwagiliaji. Hali hii ilisababisha kushuka kwa kipato cha wakulima na mapato ya Halmashauri. Katika kukabilina na changamoto hizi, Halmashauri iliamua kujikita kutoa usaidizi wa kuboresha uzalishaji wa zao la mpunga na kuongeza thamani. Mikakati iliyotekelezwa ni pamoja na kujenga uelewa wa jamii kuhusu mbinu bora za uzalishaji na kujenga miundombinu ya umwagiliaji (mifereji ya umwagiliaji, bwawa la kukusanya maji na vituo vya kutawanya maji). Mbali na miundombinu ya umwagilaji Halmashauri ilijenga barabara kurahisha uchukuzi wa mazao kutoka mashambani na kujenga kiwanda cha kuchakata mpunga na kuupanga mchele kwenye madaraja. Kutekelezwa kwa jitihada hii kumeboresha kipato na maisha ya wakulima. Vilevile, Halmashauri imeboresha mapato yake kutokana na ushuru unaokusanywa kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mpunga.

Mbinu hizi Bora katika sura hii ya tano zina mafunzo makuu yafuatayo:

"Kijiji Kimoja Zao Moja" sio mbinu inayoanzia ngazi ya juu; hivyo ili Halmashauri ifanikiwe kuleta maendeleo ya kiuchumi ngazi ya chini ni lazima itumie wataalamu na viongozi kwa ajili ya maandalizi na ijikite katika kuhamasisha jamii zitambue fursa zilizopo, kuandaa na kujenga uwezo wa vikundi vya uzalishaji, kutunga sheria ndogondogo na kuunda mahusiano kati ya wazalishaji na taasisi za kifedha. Hii inaonesha kuwa Halmashauri lazima isimamie mchakato huu hadi wazalishaji wawe tayari kuendesha shughuli zao zote.

Ni changamoto kwa Halmashauri zote kupata masoko ya mazao ya wananchi. Penye soko la uhakika wazalishaji hupeleka bidhaa. Ni wajibu wa maafisa ugani kuwapa wakulima taarifa muhimu na kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo na soko la mazao yao.

Uwezeshaji thabiti ni muhimu katika mchakato wa Kijiji Kimoja Zao Moja. Wawezeshaji huwakutanisha wazalishaji na taasisi za utafiti na teknolojia, taasisi za huduma za kifedha, walaji/wateja kwa ajili ya kujua matakwa yao na kupeana uzoefu. Ubora na umahiri wa wawezeshaji ndiyo kiini cha mafanikio. Ni muhimu

Halmashauri kuandaa na kutumia wawezeshaji wenye elimu na ujuzi wa kutosha kwa ajili ya kuwajengea uwezo wananchi ili wainue maendeleo yao kiuchumi. Hivyo ubora wa wawezeshaji na idadi yao ni kigezo kikubwa katika kufanikisha dhana hii.

Maono ya uongozi ni ufunguo wa mafanikio ya Kijiji Kimoja Zao Moja. Ni dhairi kuwa Mkurugenzi au mtu mwingine anapoanzisha dhana hii katika Halmashauri lazima apewe muda wa kutosha ili asimamie shughuli hizo hadi matokeo yaonekane. Hakuna uhakika kama wanaorithishwa shughuli hizi huwa na maono kama waliozianzisha. Pasipokuwa na mwendelezo wa shughuli kama hizi wakulima hukatishwa tamaa kwa kutofikia malengo yao.


Ni lengo la wadau kuongeza thamani za mazao kwa kutumia vifungashio vizuri na kutumia nembo na alama zinazokubalika kimataifa. Wazalishaji hawana budi kuacha kuuza mazao yasiyochakatwa ili wadau wasaidie vikundi vyao katika shughuli za mchakato wa mnyororo wa thamani. Kuongeza thamani na mnyororo wa ongezeko la thamani ndilo jibu la uzalishaji mdogo na uhaba wa chakula.

Mnyororo wa ongezeko la thamani unaweza kuongeza thamani kila hatua kama kila kitu kimepangwa vizuri. Dhana ya Kijiji Kimoja Zao Moja inabidi ikidhi soko la mlaji wa eneo husika, kitaifa na kimataifa. Zaidi ya yote siyo lazima shughuli hizi ziwe za mazao ya kilimo tu. Zipo raslimali nyingi; maporomoko, mapango, chemichemi za maji moto, mawe ya kipekee, miti, vyakula, na nyumba za kale ambavyo vinaweza kutumika kwa ajili ya kutekeleza dhana hii. Hii inaonesha kuwa zipo raslimali nyingi za Tanzania ambazo hazijatambulika na zinazoweza kuleta maisha bora ya mtanzania.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MBINGA

**UBORESHAJI WA KIPATO KUPITIA UZALISHAJI BORA WA ZAO LA KAHAWA**










***UZOEFU WA H/W YA MBINGA***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ni moja kati ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Ruvuma. Inapakana na H/W za Songea kwa upande wa Mashariki, Ludewa (Mkoa wa Njombe) kwa upande wa Kaskazini na Nyasa kwa upande wa Kusini Magharibi. Kiutawala, H/W ya Mbinga imegawanyika katika Tarafa 6, Kata 29, Vijiji 118, Vitongoji 787 na Kaya 7,052. Mazingira ya Halmashauri ni ya milima ambayo imeinuka kati ya 900m hadi 1,350m kutoka usawa wa bahari. Baadhi ya maeneo kama Matengo yana mwinuko mkali kufikia 2000m juu ya usawa wa bahari. Hali ya joto ni kati ya $10^0$C hadi $19^0$C katika miezi ya Mei hadi Agosti na $20^0$C hadi $30^0$C katika miezi ya Septemba na Machi. Wastani wa mvua ni kati ya 1,200mm maeneo ya ukanda wa chini na 2,000mm katika maeneo ya mwinuko kama Matengo. Vipindi vya mvua ni kati ya mwezi Desemba na Mei. H/W ya Mbinga ina eneo la 631,931ha na 27,474ha kati ya hizo zinatumika kuzalisha zao la kahawa. Sehemu kubwa ya ardhi imefunikwa na Miombo, ni sehemu ndogo tu ambayo ina mchanganyiko wa misitu midogo na majani. Hali ya udongo imegawanyika katika sehemu tatu; maeneo ya mwinuko yana udongo mwekundu wa mfinyanzi uliochanganyika na Kichanga, kadri mwinuko unavyo pungua udongo hubadilika na kuwa udongo wa tifutifu uliochanganyika na mawe madogomadogo, na katika maeneo ya tambarare udongo ni wa mweusi, tifutifu na wenye rutuba ya kutosha.




***Ramani ya H/W ya Mbinga***

Kwa mujibu wa sensa yam waka 2012, idadi ya watu ni 385,363 kati yao 196,535 ni wanawake na 188,828 ni wanaume. Ongezeko la watu ni 2.9% kwa mwaka. Wastani wa pato la wananchi ni Shs 1,206,830 kwa mwaka. Zaidi ya 95% ya wakazi wa Mbinga ni wakulima wanaojihusisha na kilimo cha mazao na ufugaji. Kilimo cha mazao kinahusisha mazao ya biashara na chakula. Mazao ya biashara yanayolimwa ni pamoja kahawa, ufuta na tumbaku, kwa upande wa mazao ya chakula ni mahindi, mihogo, mpunga, maharage, viazi, ndizi, ngano, mtama, uwele na mbogamboga. Jedwali Na.1 na 2 hapa chini yanaonesha mtiririko wa uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula kwa H/W ya Mbinga.

**Jedwali Na 1: Uzalishaji wa Mazao ya Biashara**

| Aina ya Mazao | Uzalishaji 2011/2012 | | | Uzalishaji 2012/2013 | | | Uzalishaji 2013/2014 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Lengo (Ha.) | Halisi (Ha.) | Uzalishaji (Tani) | Lengo (Ha) | Halisi (Ha) | Uzalishaji (Tani) | Lengo (Ha) | Halisi (Ha) | Uzalishaji (Tani) |
| Kahawa | 36,679 | 35,172 | 7,510 | 35,893 | 35,537 | 11,717 | 36,254 | 35,937 | 18,336 |
| Tumbaku | 194 | 183 | 88.6 | 208 | 176 | 142.6 | 190 | 215 | 194.3 |
| Korosho | 183 | 154 | 54 | 196 | 177 | 62 | 208 | 187 | 26 |
| Ufuta | 105 | 68 | 54 | 100 | 55 | 44 | 113 | 70 | 56 |
| Alzeti | 159 | 169 | 169 | 153 | 147 | 134 | 161 | 61.25 | 49 |
| Karanga | 35 | 48 | 44.8 | 58 | 51 | 46 | 62 | 76 | 67 |
| Jumla | 37,355 | 35,794 | 7,920 | 36,608 | 36,143 | 12,146 | 36,988 | 36,546 | 19,728.3 |

**Jedwali Na 2: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula**

| Aina ya Mazao | Uzalishaji 2011/2012 | | | Uzalishaji 2012/2013 | | | Uzalishaji 2013/2014 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Lengo (Ha.) | Halisi (Ha.) | Uzalishaji (Tani) | Lengo (Ha) | Halisi (Ha.) | Uzalishaji (Tani) | Lengo (Ha) | Halisi (Ha) | Uzalishaji (Tani) |
| Mahindi | 44,572 | 47,852.7 | 129,202.4 | 49,184 | 50,698 | 140,000 | 52,520 | 52,520 | 147,146 |
| Mpunga | 2,148 | 2,048.2 | 5,166 | 2,035 | 2,009 | 4,620.7 | 950 | 2,050 | 5,740 |
| Muhugo | 23,418 | 23,399 | 51,325.8 | 19,000 | 19,544 | 42,977.1 | 21,550 | 20,611 | 44,628 |
| Maharage | 13,350 | 14,227 | 14,512.3 | 19,164 | 20,436 | 20,989 | 21,200 | 21,200 | 22,038 |
| Viazi mviringo | 159 | 152 | 912.8 | 147 | 151.5 | 909 | 159.5 | 132 | 790 |
| Uwele | 1,365 | 1,394.4 | 975 | 1,995 | 1,970.9 | 1,378.2 | 2,121 | 2,121 | 1,447 |
| Viazi vitamu | 6,700 | 6,847.5 | 28,759.5 | 6,551 | 6,770 | 28,450 | 7,000.2 | 7,000 | 29,873 |
| Ngano | 3,042 | 3,078 | 3,652 | 3,002 | 3,139 | 3,724 | 3,200 | 3,204 | 3,914 |
| Ndizi | 80 | 85 | 29.34 | 75 | 59.4 | 2050 | 62.9 | 65 | 2,225 |
| Jumla | 94,834 | 99,083.8 | 237,439.8 | 101,153 | 104,777.8 | 245,118 | 108,924.6 | 108,955 | 257,800 |

## 2.0 TATIZO

Mbinga ni Halmashauri pekee kwa Mkoa wa Ruvuma inayozalisha kahawa ambapo aina ya kahawa inayozalishwa ni Arabika. Wastani wa uzalishaji ni kati ya tani 15,000 hadi 18,000 kwa mwaka. Uzalishaji wa kahawa kwa H/W ya Mbinga uliathiriwa na changamoto mbalimbali kama; kushuka kwa bei ya kahawa kwenye soko la kimataifa, uzalishaji duni kutokana na mbegu zisizo bora zenye uwezo mdogo wa kuhimili wadudu na magonjwa na teknolojia duni ya usindikaji wa kahawa baada ya kuvuna. Miundombinu duni ya barabara ilisababisha wanunuzi wa kahawa kushindwa kufika Mbinga. Hali hii iliwalazimu wakulima kusafirisha kahawa yao hadi Mji wa Makambako umbali wa kilomita 400 kutoka Mbinga. Gharama za usafirishaji zilikuwa kubwa; iliwalazimu kutumia shs 80,000 kusafirisha tani moja ya kahawa kutoka Mbinga hadi Makambako. Changamoto nyingine ilikuwa kukosekana kwa maghala yaliyoidhinishwa kutunzia kahawa katika H/W ya Mbinga. Hii ilifanya wakulima kutegemea maghala ya kuhifadhi kahawa ya Makambako jambo ambalo lilipelekea kahawa ya Mbinga kupoteza uasilia (jina) wake na kuonekana ni kahawa ya Makambako.

Changamoto nyingine ilikuwa ukosefu wa umoja wa wakulima wa kahawa ambao ungeweza kuwasaidia katika kutafuta masoko na ushawishi wa bei ya kahawa yenye manufaa kwa wakulima na kuwaunganisha wakulima kuweza kupata mikopo kutoka taasisi za kifedha, wanunuzi wa kahawa na Serikali ili kupata usaidizi wa kitaalamu. Hapakuwa na mitambo ya kutosha ya kukoboa kahawa kwa wakati baada ya kuvunwa na kusababisha baadhi ya wakulima kushindwa kukoboa kahawa zao kwa wakati baada ya kuvunwa hivyo kupelekea kupungua kwa ubora wa kahawa. Wakulima pia walikabiliwa na upungufu wa pembejeo za kilimo kutokana na uchache wa wasambazaji wa pembejeo hizo. Vilevile hapakuwa na uhusiano kati ya wakulima na taasisi ya utafiti wa kahawa ambayo huwajibika kusaidia wakulima mbinu bora za uzalishaji. Changamoto hizi ziliathiri uzalishaji wa kahawa na kusababisha kushuka kwa kipato cha wakulima na kuwafanya washindwe kumudu gharama za huduma mbalimbali kama afya, ada za shule na ujenzi wa nyumba bora.

## 3.0 MALENGO

Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuimarisha uzalishaji, uchakataji, uhifadhi wa kahawa, usafirishaji, soko la kahawa na kusaidia Halmashauri kuongeza mapato kupitia ushuru wa kahawa. Malengo mahususi yalikuwa; kujenga uelewa kwa wadau wa kahawa kuhusu mbinu za kuboresha uzalishaji wa zao la kahawa, kuweka mfumo wa pamoja wa kuchakata kahawa, kusafirisha, kutafuta soko la kahawa na kuweka mikakati ya kuwezesha wakulima kupata mbegu bora za kahawa, pembejeo na viuatilifu. H/W ya Mbinga pia ililenga kuwaunganisha wadau kujenga vituo maalumu vya uchakataji wa kahawa kwa pamoja kudhibiti ubora wa kahawa na kuhakikisha kahawa inanunulika kwa bei nzuri sokoni. Vilevile Halmashauri

ilienga kuhamasisha ujenzi wa ghala za kuhifadhi kahawa ndani ya maeneo ya Mbinga kulinda uhalisia wa kahawa ya Mbinga na mwisho ujenzi wa barabara kuwezesha wanunuzi wa kahawa kuingia Mbinga hivyo kupunguza gharama kwa wakulima kusafirisha kahawa kwenda Makambako.

Malengo mengine mahususi yalikuwa; kuanzisha na kuimarisha umoja wa wakulima (AMCOs) na vyama vya akiba na mikopo (SACCOS), kuwaunganisha wakulima kuanzisha vyama vya msingi vya ushirika kwa lengo la kuimarisha nguvu ya kupanga bei ya kahawa katika soko na kuwezesha wakulima kukopesheka kupitia SACCOS. Pia kujenga mahusiano na ushirikiano baina ya wakulima na taasisi za utafiti wa kahawa ili kupata ushauri wa kuboresha mbegu za kahawa na kupanua wigo wa huduma za ugani kwa wakulima.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

H/W ya Mbinga ilikuwa na shauku ya kuboresha maisha ya wakazi wake kwa kuimarisha maendeleo ya uchumi wa wananchi. Katika kuhakikisha lengo hili linafikiwa, Halmashauri iliweka mikakati ya utekelezaji kama inavyofafanuliwa katika aya zifuatazo;

Menejimenti ya Halmashauri ilitambua uhitaji wa kuimarisha uzalishaji wa kahawa, kuboresha kipato cha wakulima na mapato ya Halmashauri. Kwa kuzingatia msingi huu, Timu ya Menejimenti ya Halmashauri ilizitambua changamoto zinazokwamisha uzalishaji hivyo iliandaa mpango wa kuboresha uzalishaji wa kahawa kuanzia hatua za uvunaji wa matunda ya kahawa, uchakataji, uhifadhi, usafirishaji na uuzaji. Mpango huu pia uliainisha uboreshaji wa miundombinu ya barabara kati ya Mbinga na Songea ili kurahisisha usafirishaji wa kahawa. Mpango huu ulijadiliwa na kupitishwa na Baraza la Madiwani.

Mwaka 2010 Halmashauri ilifanya mkutano wa wadau; mkutano huu ulihudhuriwa na wakulima, wachakataji wa kahawa, wanunuzi na watumishi wa Halmashauri. Ajenda kuu ya mkutano ilikuwa kujadili namna ya kuimarisha uzalishaji wa zao la kahawa, mfumo wa uchakataji, gharama zinazoambatana na usafirishaji wa kahawa na utegemezi wa soko la kahawa la Makambako. Lengo lilikuwa kupata mawazo ya wadau katika kujenga msingi wa utekelezaji wa mpango wa kuboresha zao la kahawa. Mkuu wa Wilaya, aliitisha mikutano miwili na wamiliki wa maghala ya Makambako (TUTUNZE Kahawa Ltd na DAE Ltd), MCCCO na wasafirishaji wa kahawa kujadili uwezekano wa kujenga maghala ya kuhifadhia kahawa Mbinga kwa faida wahusika wa pande zote. Wakulima na wadau wengine walishawishika na maamuzi ya Halmashauri na kukubali kushirikiana kufikia lengo hilo.

Halmashauri ilitafuta na kushawishi wafanyabiashara kujenga maghala mapya na kukarabati ya zamani ndani ya Halmashauri kurahisisha uhifadhi wa kahawa kabla ya kupelekwa kwenye mnada. Lengo likiwa kuepuka kutumia maghala ya Mji wa Makambako ambapo gharama za kuhifadhi zilikuwa kubwa na pia kahawa ya mbinga ilipoteza uhalisia na jina lake kwa kuhifadhiwa Makambako. Kuhifadhi kahawa Mbinga lilikuwa jambp la msingi katika kuitambulisha Kahawa ya Mbinga (EX–MBINGA) badala ya EX–MKAMBAKO. Mkutano mwingine na wafanyabiashara ulihusu kuhamasisha ujenzi wa hoteli za kisasa kuwavutia wanunuzi wa kahawa kuja Mbinga.

Ujenzi wa Barabara ya Mbinga – Songea km 98; kurahisisha usafirishaji wa kahawa ilikuwa ni mkakati mwingine uliotekelezwa. Halmashauri kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Mkoa iliomba Serikali Kuu kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Songea hadi Mbinga. Baada ya majadiliano ya kina na maridhiano kuanzia mwaka 1998, Serikali Kuu ilikubali kujenga barabara kwa kiwango cha lami. Ujenzi ulianza mwaka 2012/2013 uliotekelezwa na kampuni ya Syno Hydro Corporation kutoka China.

Katika jitihada ya kuongeza uzalishaji, bora wa kahawa na kuimarisha soko la kahawa, Halmashauri ilihamasisha wakulima kubadilisha aina ya kilimo cha mazoea badala yake watumie miche ya kahawa

iliyoboreshwa, pembejeo na matumizi ya samadi katika kuongeza uzalishaji. Ili kuhakikisha wakulima wanapata mbolea ya samadi ya kutosha, Halmashauri iliwekeza katika kukopesha wakulima ng'ombe wa kisasa katka mradi wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe. Mradi huu ulisaidia wakulima kupata samadi na maziwa kwa afya zao. Katika mradi huu Halmashauri iliwakopesha wakulima jumla ya ng'ombe 740 wenye thamani ya shs 629,000,000. Kati ya mwaka 2012 na 2015, Halmashauri ilitoa jumla ya shs 70,000,000 kwa Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TACRI) kwa ajili ya kuzalisha miche ya kisasa 576,000 na kuwapatia wakulima kwa gharama nafuu ya shs 300 kwa kila mche badala ya shs 800 hadi 900 ambayo ndio bei ya soko. Lengo la Halmashauri lilikuwa kuwezesha wakulima kupata miche bora ya kahawa ambayo inazalisha kwa kiasi kikubwa kwa muda mfupi. Kwa upande wa viuatilifu, Halmashauri iliwapatia wakulima lita 11,800 za Tanzacron kwa muda wa miaka 3 kuanzia mwaka 2013 – 2015 zilizogharimu jumla ya shs 259,600,000 kwa ajili ya kukinga ugojwa wa vidung'ata.

Halmashauri pia ilitoa mafunzo kwa vitendo kwa maafisa ugani kuhusu utunzaji bora wa kahawa, muda sahihi wa kuvuno, kukoboa, kuloweka na kukausha kahawa. Jumla ya Maafisa Ugani 60 walifundishwa na kupelekwa kwa wakulima ili kushirikiana kwa karibu na wakulima katika kuboresha ustawishaji na uvunaji bora wa kahawa. Pia, Halmashauri kwa kushirikiana na TACRI ilitoa mafunzo kwa wawezeshaji 105 wa ngazi ya kijiji kuhusu uzalishaji bora wa kahawa. Hawa, walijengewa uwezo ili kufanya kazi kama maafisa ugani katika vijiji vyao. Mafunzo haya kwa wawezeshaji wa vijiji yalitolewa kama mbinu ya kukabiliana na upungufu wa maafisa ugani.

Halmashauri kupitia DADPs ilijenga vituo 50 vya kukobolea kahawa (CPU). Hizi ni mashine rahisi za kukobolea kahawa mara baada ya kuvuna. Kutunza ubora wa kahawa, inashauriwa baada ya kahawa kuvunwa mbegu za kahawa zikobolewe mapema iwezekanavyo. Kutokana na uhaba wa vituo hivyo vya kukobolea na kukausha kahawa, Halmashauri iliamua kujenga vituo 50 na kuvikabidhi kwa vikundi vya wakulima kuwezesha kukoboa na kukausha kahawa kwa wakati kuepuka kupoteza ubora.

Halmashauri ilifanya jitihada za kuwasiliana na Bodi ya Kahawa Tanzania ili kupata leseni ya kuuza kahawa moja kwa moja kutoka Mbinga. Kibali cha kuruhusiwa kuuza kahawa moja kwa moja kutoka Mbinga kilitolewa baada ya kukidhi masharti ya kuwa na vifaa bora vya uchakataji wa kahawa na maghala bora ya kuhifadhi kahawa jambo ambalo Halmashauri ilikamilisha. Kupata kibali kuliwezesha kahawa ya Mbinga kuuzwa moja kwa moja kutoka Mbinga. Sampuli zilipelekwa kwenye mnada wa Moshi lakini kwa kiasi kikubwa kahawa inabaki Mbinga. Katika kuunganisha wakulima na taasisi mbalimbali, soko na wadau, Halmashauri iliwezesha wakulima kuunda Umoja wa Wakulima wa Kahawa (AMCOS). Umoja huu ulisaidia kuunganisha wakulima na taasisi kama benki kwa ajili ya kupata mikopo, masoko na wauzaji wa pembejeo za kilimo kwa bei nafuu.

## 5.0 RASLIMALI

Katika kufanikisha jitihada ya kuboresha kahawa ya Mbinga, raslimali mbalimbali zilitumika. Hizi ni pamoja na raslimali watu na fedha. Raslimali fedha zilizotumika ni kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 3 hapa chini.

**Jedwali 3: Raslimali Fedha**

| Na. | Shughuli iliyofanyika | Kiasi cha fedha | Chanzo |
|---|---|---|---|
| 1 | Kununua viuatilifu (Tanzacron – 11,800 liters) | 259,600,000 | Halmashauri |
| 2 | Uzalishaji wa miche bora 576,000 | 70,000,000 | Halmashauri |
| 3 | Posho wakati wa kwenda Kushawishi Bodi ya Kahawa kuruhusu soko lifanyike Mbinga | 1,200,000 | Halmashauri |
| 4 | Kujenga uelwea kwa wakulima | 10,000,000 | TUTUNZE KAHAWA Ltd. |
| 5 | Ununuzi wa Ng'ombe wa Maziwa 740 | 629,000,000 | Halmashauri |
| 6 | Ujenzi wa vituo vya kukoboa kahawa | 450,000,000 | Halmashauri |

Raslimali watu; Mkuu wa Wilaya alitumia nguvu na maarifa katika kuunganisha wadau na kushawishi ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi kahawa katika eneo la Mbinga. Watumishi wa TACRI, Maafisa Ugani, maafisa wa AMCOS, Mashirika binafsi kama TUTUNZE Kahawa Ltd, DAE, MCCO, MBIFACU na TCB walishirikiana na Halmashauri katika kufikia lengo la kuboresha kahawa ya Mbinga.

**6.0 MATOKEO**

Utekelezaji wa jitihada hii ya kuboresha uzalishaji wa kahawa umepelekea mabadiliko chanya kwa wakulima wa kahawa na Halmashauri kwa ujumla. Eneo la uzalishaji wa kahawa limeongezeka kutoka hekta 35172 mwaka 2011/2012 na kufikia hekta 35,937 mwaka 2013/2014. Ongezeko hili, limeongeza uzalishaji kutoka tani 7,510 mwaka 2011/2012 hadi tani 18,336 mwaka 2013/2014. Matokeo zaidi ya jitihada hii yamejadiliwa kama ifuatavyo;

Uelewa wa wakulima wa kahawa kuhusu kilimo bora cha kahawa umeongezeka. Wakulima wameanza kutumia miche bora ya kisasa ya muda mfupi, wanatumia viuatilifu kukinga magojwa ya kahawa na usindikaji kwa njia za kisasa. Hii imesababisha uzalishaji wa kahawa bora inayokidhi vigezo. Picha ifuatayo inaonesha miti bora ya kahawa.



***Mti bora wa kahawa***

Vinu vya kukoboa kahawa vipatavyo 50 vimejengwa na Halmasahauri na vinafanya kazi ya kukoboa kahawa mara baada ya kuvunwa. Mbali na vinu vya kukoboa vilivyojengwa na Halmashauri, Mashirika binafsi pia yamewekeza katika kujenga vinu vya aina hii katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri kusaidia wakulima kuchakata kahawa kwa wakati. Tokeo jingine ni kuanzishwa kwa vyama 48 vya wakulima (AMCCOS) na taasisi 14 za ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS) ambazo zinahudumia wakulima ndani ya Halmashauri. AMCCOS zinaunganisha wakulima na Serikali, Bodi ya Kahawa Tanzania, Taasisi ya utafiti wa kahawa Tanzania (TACRI) na Taasisi za kifedha. Mbali na kuunganisha wakulima na wadau hawa, AMCCOS pia zinatafuta soko na kuhudhuria minada ya kahawa kwa niaba ya wakulima. Moja ya AMCCOS iliyoanzishwa ni KIMULI AMCCOS ambayo ilianzishwa mwaka 1993 ikiwa na wanachama 360; hadi sasa wanachama wameongezeka kufikia 1623, imeajiri wafanyakazi 15 ambapo kati yao 6 wanafanya kazi katika ofisi kuu ya AMCCOS na wengine 9 wapo kwenye ofisi zilizopo katika vijiji kuwahudumia wakulima.

Mapato yameongezeka kwa kiasi kikubwa; AMCCOS ya KIMULI pekee imekuwa na rekodi ya kufikisha mapato ya shs bilioni 3.4 kwa mwaka. Ongezeko hili la mapato limechangiwa na ongezeko la uzalishaji kutoka tani 381 mwaka 2013 hadi tani 683 mwaka 2015. Kutokana na faida ambayo KIMULI imepata imeweza kusadia utoaji wa huduma za jamii; KIMULI imefanya ukarabati wa shule ya msingi Kitanda na

kununua madawati kwa kutumia jumla ya shs Milion 47, ukarabaiti wa zahanati ya Kitanda uliogharimu shs million 5, ukarabati wa shule ya msingi Lupilo kwa shs milioni 2 na ukarabati wa zahanati ya Lipumba kwa gharama ya shs milioni 7. Mbali na ongezeko la pato la AMCCOS, kipato cha wakulima pia kimeongezeka na kuboresha maisha yao. Jedwali Na.4 linaoneesha wakulima walionufaika na ongezko la uzalishaji, kaasi cha pato na mambo waliyoboresha.

**Jedwali 4: Mafanikio kwa wakulima wa Kahawa**

| S/N | Jina la mnufaika | Kata Kijiji | Ha. | Uzalishaji (Magunia) | | | Kipato (mil TshS) | | | Mafanikio | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 2013 | 2014 | 2015 | 2013 | 2014 | 2015 | Nyumba /bati | Maji | Umeme wa jua | samani |
| 1 | Seleman A. Tilia | Mitanga | 3 | 17 | 28 | 39 | 1.53 | 5.6 | 5.88 | √ | √ | √ | √ |
| 2 | Ditric S. Tilia | Mitanga | 0.5 | 10 | 16 | 8 | 1.75 | 2.0 | 1.6 | | √ | | √ |
| 3 | Yordan S. Komba | Nyoni | 2 | 28 | 12 | 42 | 3.36 | 4.4 | 6.72 | | √ | | √ |
| 4 | Simon Mapunda | Nyoni | 1 | 20 | 28 | 35 | 3.0 | 4.5 | 3.0 | | √ | | √ |
| 5 | Filbert Mbunda | Nyoni | 3.8 | 24 | 18 | 47 | 2.62 | 1.95 | 6.82 | | √ | | √ |
| 6 | Aron Milinga | Likwela | 2.3 | 52 | 50 | 50 | 10.0 | 11.6 | 10.0 | √ | √ | √ | √ |
| 7 | Joakim Kowelo | Mpapa | 0.6 | 6 | 4 | 5 | 1.05 | 0.86 | 1.0 | √ | √ | √ | √ |
| 8 | Adolfina Komba | Mpapa | 2.3 | 30 | 15 | 20 | 5.25 | 3.37 | 4.0 | | √ | | √ |
| 9 | Sairis Ndimbo | Ngima | 4 | 80 | 70 | 40 | 14.0 | 10.5 | 5.0 | √ | √ | √ | √ |
| 10 | Erick Mbepera | Ngima | 1.6 | 20 | 15 | 40 | 3.05 | 2.62 | 5.0 | √ | √ | √ | √ |

Hali ya usafirishaji na uhifadhi wa kahawa imeboreshwa; barabara ya Songea – Mbinga yenye urefu wa 98km imejengwa kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa maghala ya kuhifadhia kahawa umeongezeka, maghala 8 ndani ya mji wa Mbinga, kati ya hayo, maghala 5 yanamilikiwa na MCCCO, MBIFACU, CMS, DAE na MDC na mengine 3 yalijengwa na DAE Ltd (1), TUTUNZE Kahawa LTD (1) na GOMEZ (1). Picha ifuatayo inaonyesha Barabara iliyojengwa kuunganisha Songea na Mbinga.



***Barabara kuu ya Songea-Mbinga***

Ushirikiano kati ya Halmashauri, Bodi ya Kahawa Tanzania, Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania na wakulima wa kahawa umeimarika. Tawi la TACRI la Kijiji cha Ugano linasaidia wakulima kupata miche bora inayozalishwa kisasa kwa kutumia vikonyo vya kahawa vilivyoboreshwa. Pia, TACRI inashirikiana na wakulima kutoa elimu kwa wakulima kuhusu kilimo bora cha kahawa na imetoa mafunzo kwa wakulima 25 kuhusu uzalishaji wa miche bora ya kahawa. Kutokana na uwepo TACRI aina mbalimbali zipatazo 19 za kahawa zinazohimili magonjwa zinazalishwa kwa njia ya vikonyo.



*Uandaaji wa miche mama*




*Maandalizi ya miche kwa njia ya vikonyo*

Kutokana na utekelezaji wa jitihada hii wadau wa kahawa na kampuni binafsi za kuchakata, kuhifadhi na kufungasha kahawa wameongezeka.  Baadhi ya kampuni hizi ni Mbinga Coffee Curing Company (MCCCO) Ltd; kampuni hii inasaidia vikundi vya wakulima, kampuni ndogondogo za kahawa na mkulima mojamoja kuhusu uboreshaji, uchakataji,  uhifadhi na uuzaji wa kahawa. Mbali na usaidizi huu kampuni imejenga ghala la kuhifadhi kahawa lenye uwezo wa tani 25,000 hadi 30,000. Picha hapa chini inaonesha ghala lililojengwa na MCCCO.




*Ghala la MCCCO*

Kampuni nyingine ni TUTUNZE Kahawa Company Ltd (TKL) amabayo inamiliki ghala lenye thamani ya shs 1,520,000,000 na inatoa ushauri kwa wakulima kupitia mafunzo juu ya namna ya kutunza taarifa za uzalishaji, kilimo mseto, utunzaji wa mazingira, na matumizi sahihi ya fedha wanazopata kutokana na kahawa katika kuboresha maisha ya familia.  Kampuni hii inasaidia  uzambazaji wa pembejeo za kilimo na miche iliyoboreshwa. Pia inasaidia kudhamini wakulima kupata huduma za kibenki na taasisi za Serikali. Kampuni imewekeza mitambo 3 ya kuchakata kahawa yenye thamani ya Dolla za kimarekani 35,000 kila moja kwa ajili ya kuhakisha kahawa inaandaliwa katika ubora unaohitajika. Pia inawaunganisha wakulima na soko na wanunuzi wa kimataifa na kuhamasisha uzalishaji wa kahawa kwa kutumia msemo wa " *Kahawa safi kwa furaha ya familia".* Picha ifuatayo inaonyesha shamba la kahawa la TKL na ghala.




***Shamba la kahawa la KTL na ghala***

DAE Ltd ni kampuni nyingine binafsi;  inajishughulisha na uzalishaji, uchakataji na uuzaji wa kahawa. Kampuni hii imetoa ajira 500 kwa wakazi wa Mbinga kujishughulisha na biashara ya kahawa, imeajiri maafisa ugani 5 ambao wanatoa elimu kwa wakulima kuhusu uzalishaji wa kahawa kwa kutumia miche iliyoboreshwa. Vilevile Kampuni inamiliki vinu 50 vya kukoboa kahawa ambavyo imevikabidhi kwa wakulima na vinasimamiwa na vikundi vya wakulima. Mbali na jitihada hizi, kampuni inaendesha mgahawa wa kisasa (Coffee shop) ambapo wageni mbalimbali wanatembelea kupata kinywaji cha kahawa bora  inayoandaliwa katika mazingira safi.




***Ghala la kahawa la DAE na Mgahawa wa kuuza kinywaji cha kahawa***

Kutambuliwa kwa Kahawa ya Mbinga (EX-Mbinga Coffee) ni moja ya tokeo la jitihada zilizofanywa na Halmashauri.  Ushirikiano kati ya Halmashauri na wadau mbalimbali wa kahawa umewezesha kuboresha uzalishaji wa kahawa bora iliyozalishwa, kuchakatwa, kuhifadhi na kusafirishwa  katika hali ya ubora  na kuuzwa kwenye masoko ya kitaifa na kimataifa kwa utambulisho wa kahawa ya Mbinga (EX-Mbinga Coffee). Kutokana na jitihada hii , mapato ya Halmashauri yameboreshwa na pia kipato na maisha ya wakulima vimeboreshwa. Picha ifuatayo inaonyesha kahawa inayozalishwa Mbinga ikiwa katika vifungashio vya kisasa vinavyoitangaza kahawa ya Mbinga.



***Kahawa ya mbinga ikiwa sokoni wakati wa Maonyesho ya nanenane***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Katika kuhakisha matokeo ya jitihada hii, Halmashauri ya wilaya ya Mbinga imeweka mikakati ya uendelevu. Mikakati hiyo ni pamoja na kutoa kiwanja kwa Bodi ya Kahawa Tanzania kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kuonja kahawa. Fedha kwa ajili ya ujenzi zimetengwa. Kujengwa kwa kituo cha kuonja kahawa

kutasaidia uonjaji wa kahawa kufanyikia Mbinga tofauti na hali iliyopo ya kusafirisha kahawa hadi Moshi Kilimanjaro ambapo uonjaji wa kahawa hufanyika. Kujengwa kwa kituo hiki kutapunguza gharama za usafirishaji wa kahawa hadi Moshi.

Halmashauri inaendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kwa kushirikiana na TACRI kuhusu uzalishaji na uchakataji wa kahawa. Ujenzi na ukarabati wa maghala ya kuhifadhia kahawa na kuimarisha soko la kahawa umefanyika. Halmashauri inaendelea kusisitiza matumizi ya vinu bora vya kukoboa kahawa (CPU) kudhibiti ubora wa kahawa. Mikakati mingine ni pamoja na kuimarisha mahusiano baina ya wakulima na taasisi nyingine kama soko, TUTUNZE, DAE na MCCCO kudhibiti ubora wa kahawa. Halmashauri inaendelea kuimarisha vyama vya wakulima (AMCCOS), kuwekeza kwenye shughuli nyingine za kiuchumi kama upandaji wa miti na kuhimiza ukaguzi wa hesabu wa mara kwa mara na kutoa mafunzo ya kuziwezesha AMCCOs kudumu kwa kipindi kirefu.

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Mafanikio ya jitihada hii yanatokana na utashi na uthubutu wa wadau mbalimbali; utayari wa viongozi wa wilaya (Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Halmashauri, Madiwani na Wakuu wa Idara), uwepo na utayari wa wadau mbalimbali kama wakulima, AMCOS, wanunuzi na Bodi ya Kahawa katika kuhimiza uzalishaji wa kahawa bora ya Mbinga. Pia, uwepo wa AMCCOs madhubuti kama KIMULI na SACCOS katika kusaidia wakulima kupata pembejeo za kilimo na uwepo wa vinu bora vya kukobolea kahawa (CPU) za kutosha ni siri nyingine za mafanikio. Uwepo taasisi za kifedha kama CRDB, NMB, Benki ya Wananchi wa Mbinga na NSSF zinazotoa mikopo na Maafisa Ugani kutoka Halmashauri na kampuni binafsi za TKL na DAE wanaotoa elimu kwa wakulima kuboresha uzalishaji wa kahawa pamoja na jamii ya watu wa Mbinga ambao ni wachapakazi wazuri walioshiriki kikamilifu kuhakikisha uzalishaji wa kahawa bora ni siri nyingine za mafanikio.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI

**UBORESHAJI WA UMWAGILIAJI KWA UHAKIKA WA CHAKULA NA KIPATO**









***UZOEFU WA SKIMU YA NDANDA***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ni moja kati ya Halmashauri tisa za Mkoa wa Mtwara ambayo ina fursa kubwa ya maendeleo ya kiuchumi. Halmashauri ina hali ya hewa na ardhi inayofaa kwa kilimo na uwekezaji wa shughuli nyingine za kiuchumi. H/W ya Masasi inapakana na H/W za Nachingwea kwa upande wa Kaskazini, Lindi na Newala kwa upande wa Mashariki, Nanyumbu kwa upande wa Magharibi na Jamhuri ya nchi ya Msumbiji kwa upande wa Kusini. Halmashauri inapatikana kati ya Latitudo $10^0$ na $12^0$ Kusini na Longitudo $36^0$ na $38^0$ Mashariki na ipo umbali wa 214km kutoka makao makuu ya mkoa wa Mtwara. Halmashauri ina eneo la 3,829.9$km^2$ ambalo ni 20.8% ya eneo lote la Mkoa wa Mtwara ambalo ni 16,720$km^2$.




***Ramani ya H/W ya Masasi***

Kiutawala, H/W ya Masasi ina Tarafa 5 ambazo ni Lisekese, Mchauru, Mkundi, Chiungutwa na Lulindi, Kata 34, Vijiji 166 na Vitongoji 889. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, idadi ya watu ilikuwa 260,854 kati yao wanaume 125,151 na wanawake 135,703. Kiwango cha ongezeko la idadi ya watu ni asilimia 2.7. Wastani wa kipato cha wakazi kwa mwaka 2014/2015 ilikuwa shs 700,000. Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo na mazao ya nayozalishwa ni korosho kama zao kuu la biashara linalochangia 80% ya pato la wananchi na Halmashauri. Mazao mengine ni mahindi, mpunga ufuta ambayo huchangia 20% ya pato kwa mwaka.

Mfumo wa kilimo cha umwagiliaji kama teknolojia mpya kwa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi unafanyika kwa kutumia maji ya bonde la Mto Ruvuma. Bonde hili lina ardhi nzuri yenye rutuba ambayo inapata maji kwa ajili ya umwagiliaji kutoka Mto Lukuledi na vyanzo vingine vya maji kutoka mito ya Mwiti, Mbwinji, Mkungu, Ndanda na Mkululu. Bonde hili linawanufaisha wananchi wa vijiji 3 vya Njenga, Mpowora na Mwena kwa kilimo cha umwagiliaji na kuachana na utegemezi wa kilimo cha kusubiri mvua.

Skimu ya umwagiliaji ya Ndanda ipo katika Kata ya Mwena, Tarafa ya Chikundi, Skimu ipo pembezoni wa barabara ya Masasi – Mtwara umbali wa kilomita 40 kutoka Mji wa Masasi. Chanzo cha maji ya umwagiliaji ni Mto Ndanda unaoanzia kwenye miinuko ya milima ya Makonde na kuambaa kutoka kusini kuelekea kaskazini kupitia eneo la umwagiliaji. Skimu hii ya umwagiliaji iliibuliwa kipindi cha kuandaa mipango ya vijiji kwa Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD).

**2.0 TATIZO**

Mwanzoni mwa miaka ya 1990, wakulima ambao walijiunga kwenye vikundi vya Upendo (Kijiji cha Njenga), Mkombozi (Kijiji cha Mpowora) na Jipemoyo (Kijiji cha Mwena) walianzisha kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia miundombinu asilia ya umwagiliaji kwa kuchimba mifereji na kuielekeza kwenye mashamba yao. Mfumo huu wa umwagiliaji haukuwa na tija kwa sababu kiasi kikubwa cha maji kilipotea kutokana na kutosakafiwa kwa mifereji ya kupitishia maji kwenda mashambani. Vilevile hapakuwa bwawa la kukusanya maji na vituo vya kugawa maji kutokana na kukosa ujuzi na raslimali. Kupitia vikundi hivi wakulima waliweza kulima mazao kama mpunga, mahindi na mbogamboga mara mbili kwa mwaka. Hata hivyo uzalishaji haukuwa mkubwa. Uzalishaji wa mpunga ulikuwa ni kati ya gunia 8 hadi 10 kwa ekari, hali hii ilipelekea wakulima kuwa na vipato vidogo ambavyo havikukidhi mahitaji kama kujenga nyumba bora, kulipa ada za shule, huduma za afya na gharama za kuunganisha umeme. Kutokana na hali hii wazo la kuanzisha skimu ya umwagiliaji ya kisasa lilionekana jambo lisiloepukika.

**3.0 MALENGO**

Lengo Kuu la ujenzi wa skimu ya umwakiliaji ya Ndanda lilikuwa kuboresha hali ya maisha ya watu wa Vijiji vya Mwena, Mpowora na Njenga kupitia ongezeko la uzalishaji wa mazao na hatimaye uhakika wa chakula na ongezeko la kipato cha wakulima na Halmashauri kwa ujumla. Malengo mahususi yalikuwa; kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji ya skimu na kuifanya sehemu ya mafunzo kwa vijiji vingine vinavyoendesha kilimo cha umwagiliaji, kuongeza uzalishaji wa mbogamboga na mpunga na kuanzisha chama cha ushirika cha wakulima wa mpunga ambacho kitakuwa na jukumu la kusaidia wakulima kupata soko na kupanga bei ya mazao. Vilevile kujenga mahusiano kati ya wakulima na taasisi za kifedha ili wakulima wapate mikopo kwa urahisi na kupata usaidizi wa kitaalamu kutoka Halmashauri.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Katika Kupambana na changamoto zilizoainishwa hapo awali na kufikia malengo, jamii kwa kushirikiana na Halmashauri ilitekeleza mikakati ifuatayo;

Mwaka 2002 Halmashauri iliwezesha mchakato wa upangaji mipango wa vijiji kupitia Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD) kwa jamii za Njenga, Mpowora na Mwena. Kupitia mchakato huu vijiji viliibua fursa ya uwepo wa ardhi nzuri ya uzalishaji na maji ya umwagiliaji. Upande wa vikwazo waliorodhesha teknolojia duni na kukosekana kwa ujuzi wa kuendesha kilimo cha umwagiliaji cha kisasa. Mchakato huu uliibua mradi wa skimu ya umwagiliaji kama hitaji kuu la jamii. Picha hapa chini inaonesha jamii zikishiriki kwenye mchakato wa O&OD.



***Wanavijiji wakishiriki kwenye Mchakato wa O&OD***

Mradi wa umwagiliaji wa kisasa uliibuliwa kama hitaji kuu la wanavijiji na kuingizwa kwenye mipango ya vijiji. Mikutano mikuu ya vijiji iliridhia na kuthibitisha kwamba mradi wa kisasa wa umwagiliaji kama hitaji

kuu. Mipango iliwasilishwa katika ngazi ya Kata na Kamati ya Maendeleo ya Kata (KMK) ilipitisha skimu ya umwagiliaji kuwa ndilo hitaji la jamii za vijiji vya Njenga, Mpowora na Mwena. Baada ya ngazi ya Kata mpango uliwasilishwa katika ngazi ya Halmashauri ili kuingizwa kwenye mpango wa Halmashauri na kupangiwa bajeti. Kutokana na skimu ya umwagiliaji kuwa hitaji kubwa, jamii zilianza kupanua skimu ili kukidhi hitaji lao kabla ya kupata usaidizi kutoka Halmashauri na wadau.

Mwaka 2006/2007, Timu ya Menejimenti ya Halmashauri ilitembelea skimu ya umwagiliaji ya asili iliyojengwa na wananchi na kuona ni kiasi gani jamii imewajibika katika kutoa nguvu zao kujenga skimu na kuangalia hali ya uzalishaji wa mpunga na mazao mengine. Timu ya Menejimenti ilhamasika na jitihada zilizooneshwa na jamii na kuamua kutoa usaidizi ambapo Halmashauri ilitenga fedha kiasi cha shs 12,000,000 kwenye bajeti ya mwaka 2008/2009. Kati ya fedha hizi shs 4,500,000 zilitumika kufanya upembuzi yakinifu na Tshs 7,500,000 zilitumika kufanya utafiti wa miundombinu ya umwagiliaji.

Mwezi Agosti, 2008 Halmasahuri ilianza kufanya uhamasishaji na kujenga uelewa wa jamii kupitia mikutano katika vijiji vya Mwena, Mpowora na Njnga kuhusu skimu ya umwagiliaji ya kisasa. Wakati wa mikutano ya uhamasishaji jamii zilielekezwa kuanzisha kamati za usimamizi wa mradi. Kamati ya wajumbe 9 ilianzishwa, kati ya wajumbe hao 6 wanaume na 3 wanawake. Kamati ilipewa jukumu la kuunganisha wakulima na Halmashauri na kusimamia utekelezaji wa mradi wa umwagiliaji.

Katika Ngazi ya Halmashauri, timu ya maendeleo ya umwagiliaji (DIDT) iliundwa ikiwa na wajumbe 13. Kwa kushirikiana na Kamati iliyoundwa na wakulima, DIDT ilikuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mradi na kuunganisha wadau wa kilimo na wakulima. Halmashauri ilianza kutafuta fedha kutoka kwa wadau mbalimbali kwa lengo la kuongeza raslimali za ujenzi wa skimu ya kisasa ya umwagiliaji. Halmashauri ilishirikisha wadau mbalimbali kusaidia skimu; wadau hao ni pamoja na JICA, AGHA KHAN FOUNDATION, DIDF na Waziri Mkuu Mstaafu Mh. Mizengo Kayanza Peter Pinda.

Mwaka 2010, wakulima walianzisha umoja wa umwagiliaji wenye usajili Na. SA16783. Umoja huu ulianzishwa kwa lengo la kujenga uwezo wa kukabiliana na changamoto zao na kuweka mahusiano na wadau mabalimbali. Kupitia umoja huu, wakulima waliunganishwa na kituo cha Utafiti wa Kilimo cha NALIENDELE na Skimu ya Umwagiliaji ya KITELE. Hii ilisaidia wakulima wa Ndanda kutembelea skimu ya Kitele na kujifunza mbinu bora za umwagiliaji wa kisasa.

Baada ya kupokea fedha kutoka kwa wadau mbalimbali, Halmashauri ilishirikiana na kitengo cha Umwagiliaji cha kanda Mtwara kutengeneza mchoro na kutafuta mkandarasi wa kujenga bwawa la kukusanya maji. Mwaka 2009/2010 Halmashauri ilikamilisha ujenzi wa bwawa la kukusanya maji na mwaka mwaka 2010/2011 Halmashauri ilijenga mifereji mikubwa 2 yenye urefu wa 4332m (mfereji wa upande wa kushoto 1882m na wa upande wa kulia 2450m) kuruhusu maji kwenye mashamba ya mpunga. Picha hapa chini zinaonesha bwawa la kukusanya maji na mifereji ya kusambaza maji.




***Bwawa la kukusanya maji na mifereji ya kuzambaza maji***

Mwaka 2011/2012 Halmashauri iliendelea kutoa fedha za ujenzi wa mifereji ya kusambaza maji ambapo jumla ya mifereji 24 ilijengwa na kusakafia mifereji 5 kati ya hiyo yenye urefu wa 838m. Vilevile, Halmashauri ilitoa fedha nyingine kujenga mifereji midogo 18 ya kuingiza maji mashambani, vituo 35 vya kugawa maji pamoja na kuimarisha kalavati 11. Miundombinu iliyojengwa wakati huu ilisaidia kuongeza eneo la skimu na kupunguza muda wa umwagiliaji. Mwaka 2014/2015 Halmashauri ilitoa fedha za kujenga mifereji mingine 7 ya usambazaji wa maji, vituo 4 vya kugawa maji na kutoa mafunzo kwa wakulima kuhusu matumizi ya skimu ya umwagiliaji ya kisasa na kuboresha kilimo cha mpunga. Mafunzo haya yalitolewa kwa wawakilishi wa wakulima ambapo waliwashirikisha wenzao waliokosa fursa ya kuhudhuria mafunzo hayo.

**5.0 RASLIMALI**

Katika utekelezaji wa jitihada hii, raslimali mbalimbali zilitumika, raslimali hizo zinajumuisha fedha, watu na vitendea kazi. Kwa upande wa raslimali watu, wakulima walijitoa kukusanya baadhi ya vifaa vya ujenzi vinavyopatikana katika mzaingira yao kama vile mchanga, mawe, kokoto na kushiriki kuchimba mifereji ya kusambaza maji. Wajumbe wa DIDT mara kwa mara waliwatembelea wakulima na kuwajengea uwezo wa matumizi ya skimu ya umwagiliaji ya kisasa na huduma za ugani. Wataalamu kutoka Skimu ya Umwagiliaji Kitele mara kwa mara walitoa elimu kwa wakulima wa mpunga wa skimu ya Ndanda. Picha ifuatayo inawaonesha wakulima wakishiriki katika ujenzi wa skimu kwa kukusanya vifaa vya ujenzi.




***Wakulima wakikusanya mawe na mchanga kwa ajili ya ujezi wa skimu***

Raslimali fedha zilizotumika katika ujenzi wa vituo vya kugawa maji zilitolewa na Aga Khan Foundation na Halmashauri ilitoa vifaa vya ujenzi. Jedwali Na. 1 linaonyesha raslimali fedha zilizotumika katika ujenzi wa skimu ya umwagiliaji ya Ndanda.

**Jedwali 1: Raslimali fedha za ujenzi wa skimu**

| Na. | Shughuli | Kiasi TZS | Chanzo |
|---|---|---|---|
| 1 | Upembuzi yakinifu | 14,000,000 | H/W ya Masasi |
| 2 | Kuandaa michoro na mchakato wa zabuni | 21,361,257 | Halmashauri ya Masasi |
| 3 | Ujenzi wa Bwawa la kukusanya maji | 62,361,257 | DADPS |
| 4 | Ujenzi wa mifereji ya usambazaji wa maji | 300,000,000 | DIDF |
| 5 | Ujenzi wa mifereji ya uzambazaji maji awamu ya pili | 184,000,000 | DIDF |
| 6 | Ujenzi wa vituo vya kugawa maji | 153,051,240 | Aghakhan Foundation |
| 7 | Ujenzi wa mifereji 4 | 8,500,000 | JICA |
| 8 | Ujenzi wa bwawa | 10,000,000 | Waziri Mkuu (Pinda) |
| 9 | Kukusanya vifaa vya ujenzi kama mawe, mchanga na kokoto | 140,180,948 | Wakulima |

**6.0 MATOKEO**

Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa skimu ya umwagiliaji ya Ndanda umeleta matokeo mbalimbali kama ifuatavyo;

Uzalishaji wa mpunga umeongezeka; ongezeko la uzalishaji ni kutoka gunia 8 mwaka 2002 hadi kufikia gunia 30 kwa ekari mwaka 2015. Ongezeko hili limetokana na kujengwa kwa skimu ya umwagiliaji ya kisasa, matumizi mazuri ya pembejeo za kilimo na kufuata mbinu bora za kilimo. Kutokana na ongezeko la uzalishaji, matatizo ya uhaba wa chakula na kipato kidogo cha mkulima yametatuliwa. Wastani wa pato la mkulima limeongezeka kutoka shs 960,000 hadi shs 3,600,000 kwa mwaka na kuwezesha wakulima kumudu kulipia huduma za afya, ada za shule za shule, ujenzi wa nyumba bora na kuwepo kwa uhakika wa chakula.

Umoja wa wakulima wa mpunga umeanzishwa na umesajiliwa kwa namba ya usajili SA 16783. Umoja huu umeunganisha wakulima na soko pamoja na taasisi za fedha ili kupata mikopo chini ya mwavuli wa umoja. Umoja pia umeuganisha wadau wengine kushiriki katika skimu ya umwagiliaji kwa lengo kujifunza kutoka kwa wadau hao. Kutokana kuunganishwa kwa wakulima na wadau mbalimbali, wakulima wamejifunza mbinu bora za kilimo endelevu, kama vile upandaji wa mpunga kwa nafasi, utunzaji wa ardhi na matumizi ya mbolea . Picha zifuatazo zinaonesha mashamba ya mpunga yaliyoboreshwa na hatua za uvunaji wa mpunga.



***Shamba la mpunga, uvunaji na usafirishaji wa mpunga***

Mfumo wa utunzaji wa skimu ya umwagiliaji umeanzishwa kuhakikisha skimu inatunzwa. Uongozi wa skimu umepewa majukumu ya kufuatilia matumizi ya raslimali ya maji na kuhakikisha matengenezo ya skimu yanafanyika pale tatizo linapotokea. Meneja wa mradi anasimamia uendeshaji wa skimu na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu skimu mara kwa mara. Kutokana na kujengwa mfumo mzuri wa umwagiliaji ambao una mifereji ya kutosha na vituo vya kugawa maji, kumepunguza migogoro ya kugombania maji baina ya wakulima ambayo ilikithiri hapo awali. Picha zifuatazo zinaonesha miundombinu ya umwagiliaji iliyojengwa katika skimu ya umwagiliaji ya Ndanda.




***Kituo cha kugawa maji na mifereji ya uzambazaji wa maji mashambani***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Skimu ya Umwagilaji ya Ndanda imeleta matokeo makubwa kwa kuboresha hali ya maisha ya jamii za vijiji vya Mwena, Mpowora na Njenga. Kutokana na matokeo haya Halmashauri haipo tayari kuona matokeo haya yanapotea. Hivyo Halmashauri imeweka mikakati ya uendelevu wa mradi kama ifuatavyo;

Halmashauri inaendelea kutoa msaada wa kitaalamu kupitia Maafisa Ugani kuboresha mbinu za kilimo, ushirika na ushiriki wa jamii katika kutunza skimu ya umwagiliaji. Lengo ni kuhakikisha wakulima wanajenga uelewa wa kutunza skimu na kujenga dhana ya umiliki.

Halmashauri imekuwa ikitenga bajeti kila mwaka na kutafuta fedha kwa wadau wengine kwa lengo la kupanua skimu ya umwagiliaji na kuendelea kuiboresha. Vile vile, Halmashauri imekuwa ikiwajengea wakulima uwezo kwa kuwapatia fursa ya kujifunza nje ya Halmashauri kuona ni namna ambavyo wakulima wa maeneo mengine wanaendesha shughuli za umwagiliaji na kuimarisha mbinu za kilimo.

Halmashauri ina mpango wa kuwekeza katika viwanda vya kuchakata mpunga; Halmashauri imetenga bajeti ya kununua mashine za kuchakata mpunga zinazojumuisha mashine ya kuvuna, kukoboa na kupanga mchele kwenye madaraja, kuweka mchele kwenye vifungashio na kuweka nembo ya kuutambulisha Mchele wa Ndanda. Lengo kuu ni kuutangaza mchele wa Ndanda na kuongeza kipato cha mkulima kwa kuuza mchele badala ya mpunga.

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Mafanikio ya mradi huu yanatokana na sababu mbalimbali: kwanza skimu ya umwagilaji ilikuwa ni hitaji la jamii; Halmashauri iliheshimu hitaji la jamii na kuamua kutoa usaidizi katika kuhakikisha jamii inapata kile inachohitaji, hali hii ilichangia kutoa hamasa kwa jamii na kujenga dhana ya umilii wa mradi. Sababu nyingine ni uhamasishaji wa jamii uliowezesha jamii kujitambua na kufahamu umuhimu wa ushiriki wao katia mradi. Hivyo, jamii kwa ujumla ilishiriki kwa kiasi kukubwa katika ujenzi wa mradi wa umwagiliaji. Sababu nyingine ni ushirikano uliojengwa baina ya wakulima na kituo cha utafiti wa kilimo cha NALIENDELE, wataalamu kutoka Taasisi ya umwagiliaji ya kanda ya Mtwara ambapo wakulima walinufaika na utaalamu wa kilimo cha kisasa na mbinu bora za uendeshaji wa kilimo cha umwagiliaji.

Siri nyingine ni utayari wa jamii za Ndanda katika kupokea na kutekeleza mradi wa skimu ya uwagiliaji na kujifunza mbinu za kilimo cha kisasa kutoka kwa wataalamu. Vilevile kulikuwa na uongozi thabiti chini ya Mkurugezi wa Halmashauri na Wakuu wa Idara katika kusaidia wakulima na kuwaunganisha na wadau mbalimbali. Katika ngazi za msingi, uongozi wa vijiji ulishiriki kikamilifu kuwaunganisha wakulima na kuanzisha umoja wa wakulima chini ya kauli mbiu " *tukitaka tunaweza".* Kauli mbiu hii iliwatia hamasa wakulima katika kufanikisha mradi huu. Picha ifuatayo inaonesha wakulima wakifanya kazi kwa umoja.



***Wakulima chapakazi wakisafisha mfereji wa umwagiliaji***

# HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU

**UZALISHAJI WA MPUNGA NA UONGEZAJI WA THAMANI**





***UZOEFU H/W YA TUNDURU***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ni moja kati ya Halmashauri sita za Mkoa wa Ruvuma. Halmashauri ipo kati ya mwinuko wa 200m hadi 500m juu ya usawa wa bahari upande wa kusini mwa mkoa wa Ruvuma. Kijiografia, Halmashauri ipo kati ya Latitudo $100^0$15 na $110^0$ 45 Kusini na Longitudo $360^0$30 na $380^0$ 00 Mashariki. H/W ya Tunduru inapakana na H/W za Namtumbo kwa upande wa Magharibi, Liwale na Nachingwea kwa Upande wa Kaskazini, Nanyumbu kwa upande wa Mashariki na Jamhuri ya Msumbiji kwa upande wa Kusini. Halmashauri ina eneo la 18,78$km^2$ ambapo 413$km^2$ (2.2%) ni maji na 18,365$km^2$ (97.8%). 15,700$km^2$ (83.6%) ni ardhi ya kilimo na 2,665$km^2$ (14.2%) ni misitu. Halmashauri imegawanyika katika Tarafa 7, Kata 37, Vijiji 153, Vitongoji 1,097 na Kaya 57,162. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, idadi ya watu ilikuwa 298,275 kati yao wanaume 143,660 na wanawake 154,619. Wastani wa kipato cha wakazi wa Tunduru ni shs 462,000 kwa mwaka.

H/W ya Tunduma imegawanyia katika kanda tatu za ikolojia ambazo ni Matemanga, Tunduru Kusini na Nakapanya. Ukanda ya Matemanga unajumuisha eneo la Kaskazini Magharibi, eneo hili ni la milima na lina asili ya udongo mweusi ambao umestawisha Miombo kwa wingi. Katika eneo hili ufugaji sio mkubwa kutokana na kukithiri kwa mbung'o. Ukanda wa Kusini mwa Tunduru unajumuisha Tarafa za Lukumbule, Nalasi, Namasakata, Nampungu na Kata ya Mlingoti Magharibi. Eneo hili pia limezungukwa na milima, hali ya udongo ni kichanga cha rangi nyekudu na weusi, eneo hili kwa kiasi kikubwa kuna miti jamii ya Miombo. Ukanda wa Nakapanya ni eneo la tambarare ambalo lina asili ya udongo wa kahawia na linastawisha misitu jamii ya miombo.

H/W ya Tunduru inapata watani wa mvua chini ya 1000mm kwa mwaka, ambapo vipindi vya mvua vinaanza kati ya mwezi Desemba na Mei na kipindi cha mwezi Januari na Machi. Kipindi cha kiangazi huanzia mwezi Juni hadi Novemba, hali ya joto inatofautina baina ya vipindi, kipindi ambacho joto linakuwa juu ni kipindi cha mwezi Novemba ambapo joto linafikia nyuzi joto $36^0$C. Kipindi cha baridi ni kati ya mwezi Julai na Agosti ambapo joto hushuka hadi kufikia nyuzi joto $10^0$C.

Shughuli za Kiuchumi katika H/W ya Tunduru ni kilimo, biashara ndogo ndogo na uchimbaji mdogo wa madini. Kilimo ndio shughuli kuu ya kuchumi ambayo inaajiri karibu 95% ya wananchi wa Tunduru ambao wanalima wastani wa ekari 10 hadi 20 kwa kaya. Mazao ya chakula yanayolimwa ni muhogo, mpunga, mahindi na kunde. Mazao ya biashara ni korosho, karanga, tumbaku, ufuta na nazi. Hata hivyo, mpunga na mahindi japo kuwa ni mazao ya chakula huhesabika pia kama mazao ya biashara. Asilimia 5 ya wananchi wanajihusisha na biashara ndogondogo na uchimbaji wa madini katika maeneo ya Muhuwesi na Ngapa. Jedwali Na.1 linaonesha hali ya uzalishaji wa mazao Tunduru.

**Jedwali Na 1: Uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kati ya 2011/ 2012**

| Aina ya Mazao | Makisio | | Uzalishaji | |
|---|---|---|---|---|
| | Eneo (Ha) | Tani | Eneo (Ha) | Tani |
| Mahindi | 29,158.0 | 52,484.0 | 27,992.0 | 50,385.6 |
| Mpunga | 44,334.0 | 124,135 | 46,551.0 | 130,342.6 |
| Muhogo | 30,000.0 | 90,000.0 | 28,500.0 | 85,500.0 |
| Uwele | 2,000.0 | 1,200.0 | 1,900.0 | 1,140.0 |
| Kunde | 13,677.0 | 10,942.0 | 12,720.0 | 10,176.4 |
| Maharage | 200.0 | 140.0 | 180.0 | 126.0 |
| Mtama | 1,200.0 | 480.0 | 960.0 | 384.0 |
| Viazi vitamu | 6,295.0 | 18,885.0 | 5728.0 | 17,184.0 |
| Jumla ndogo | 126,864.0 | 298,266.0 | 124,531.0 | 295,238.6 |
| Karanga | 5,800.0 | 2,900.0 | 4,814.0 | 2,407.0 |
| Ufuta | 3,500.0 | 1,050.0 | 2,800.0 | 840.0 |
| Alizeti | 150.0 | 90.0 | 153.0 | 91.8 |
| Tumbaku | 300.0 | 150.0 | 270.0 | 135.0 |
| Korosho mbegu ya zamani | 20,000.0 | 10,000.0 | 12,000.0 | 6,000.0 |
| Korosho mbegu iliyoboreshwa | 530.0 | 0.0 | 128.0 | 0.0 |
| Jumla ndogo | 29,750.0 | 14,190.0 | 20,165.0 | 9,473.8 |
| **Jumla kuu** | **156,614.0** | **312,456.0** | **138,696.0** | **304,712.4** |

## 2.0 TATIZO

Kabla ya mwaka 2011/2012 zao kuu la biashara katika H/W ya Tunduru lilikuwa ni korosho. Mapato ya Halmashauri kwa kiasi kikubwa yalitegemea ushuru kutokana na zao la korosho na kipato cha mwananchi halikadhalika kilitegemea mauzo ya zao la korosho. Hata hivyo, kuanzia mwaka 2011, bei ya korosho kwenye soko la dunia ilishuka kwa kiasi kikubwa. Hali hii ilipelekea kushuka kwa kipato cha mkulima na Halmashauri kwa ujumla. Katika kukabiliana na tatizo la kushuka kwa kipato, wakulima waliamua kuachana na zao la korosho na kuzalisha zao la mpunga kwa wingi ambao bei yake ilikuwa nzuri ukilinganisha na korosho. Hata hivyo uzalishaji wa mpunga bado ulikumbwa na changamoto; wakulima wengi walilima katika maeneo ya bondeni wakitegemea umwagiliaji wa maji ya mvua. Kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, pale mvua inapopungua uzalishaji wa mpunga ulipungua na wakati mwingine kukosa mavuno. Hali hii iliwafanya wakulima kukosa mazao ya kutosha na kudhoofisha kipato. Mbali na utegemezi wa kilimo cha mvua, uzalishaji wa mpunga uliathiriwa na sababu mbalimbali kama zilivyoelezewa kwenye aya zifuatazo.

Kukosekana kwa teknolojia bora ya uzalishaji wa mpunga; idadi kubwa ya wakulima hawakuwa na ujuzi wa kuzalisha kisasa kwa kutumia pembejeo za kilimo katika kukabiliana na wadudu, magonjwa na magugu yaliyoathiri mpunga. Mfano mdogo ni pale walipokuwa wanatumia mbolea za viwandani chini ya kiwango kinachostahiki. Wakulima walitumia 9kg kwa ekari badala ya 16kg kwa ekari kama inavyoshauriwa kitaalamu. Mifumo ya umwagiliaji ya asili iliyokuwepo haikuwa inatunzwa ipasavyo hivyo kupelekea kupotea ovyo kwa maji ambayo yangetumika kumwagilia mashamba. Picha zifuatayo zinaonesha skimu ya umwagiliaji ya asili iliyotumika.



***Bwawa la kutunzia maji ya umwagiliaji kabla ya kuboreshwa***

Hapakuwa na vyama ushirika na umoja wa wakulima madhubuti wa kusaidia wakulima kutafuta masoko na kuwaunganisha na wadau wa mpunga. Vilevile miundombinu ya mawasiliano haikuwa na ubora; hapakuwa na barabara za uhakika kusafirisha mazao kutoka shambani, nyumbani hadi sokoni, mifumo ya mawasiliano ya simu haikuwepo na ukosefu wa umeme vilichangia wanunuzi wa mpunga kushindwa kufika kwa wakulima kununua mpunga. Vilivile hapakuwa na kiwanda cha kuchakata mpunga na maghala ya kuhifadhia jambo ambalo liliwafanya wakulima kulazimika kuuza mpunga kwa bei ndogo badala ya kuuza mchele uliopangwa kwenye madaraja kwa bei kubwa.

Ongezeko la uhitaji wa ardhi nzuri ya kuzalisha mpunga ilikuwa ni changamoto nyingine; ongezeko la uhitaji wa ardhi lilichangiwa na ongezeko la watu na wakulima wa mpunga kutoka kwenye zao la korosho. Kutokana na uhaba wa ardhi kulitokea migogoro baina ya wakulima wakigombea ardhi. Changamoto hizi ziliilazimu Halmashauri kuboresha miundombinu ya umwagiliaji ili kutumia maji yaliyopo kwa ufanisi na kupanua eneo la uzalishaji wa mpunga kufikia hecta 10,000.

**3.0 MALENGO**

Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuboresha maisha ya wakulima na mapato ya Halmashauri kwa kuongeza uzalishaji wa mpunga na thamani.  Malengo mahususi ni pamoja na;kusaidia wakulima kuongeza uzalishaji wa mpunga kutoka magunia 5-8 hadi kufikia 25-35 kwa ekari, kuanzisha ushirika wa umwagiliaji na kuunganisha wakulima na soko, wauzaji wa pembejeo, na taasisi za fedha ili kupata mikopo. Halmashauri pia ililenga kuboresha skimu ya umwagiliaji, kupanua eneo la uzalishaji wa mpunga na kujenga kiwanda cha kuchakata mpunga na kupanga mchele kwenye madaraja na pia kuanzisha soko la mchele unatambulika kama mchele wa Tunduru.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Katika kufikia malengo Halmashauri kwa kushirikiana na wakulima wa mpunga  ilitekeleza mikakati mbalimbali kama ifuatavyo;

Kuwajengea wakulima uwezo; Halmashauri ilianza kwa kuwajengea uwezo wakulima kuhusu mbinu bora za kilimo kupitia mafunzo mbalimbali. Wakulima walifundishwa kuhusu mbinu za kisasa za kilimo kupitia mwezeshaji wa mafunzo kutoka KATC Moshi.  Mafunzo haya yalihusisha wakulima waliochaguliwa kutoka vijiji mbalimbali na yalitolewa kwa njia mbili: ziara ya mafunzo kwa kutembelea KATC Moshi na MATI Ilonga na kupitia mafunzo kwa vitendo. Mafunzo yalijikita katika namna ya kutengeneza majaruba ya maji, kusawazisha shamba, kuandaa kitalu cha miche na kuhamisha miche kutoka kwenye kitalu na kuipanda shambani. Gharama za ziara za mafunzo kwenda KATC Moshi na MATI Ilonga ziligharimiwa na Halmashauri. Baada ya mafunzo washiriki waliwashirikisha wakulima wengine ambao hawakupata fursa ya kuhudhuria mafunzo hayo.  Picha zifuatazo ni wakulima wakihudhuria mafunzo.




***Wakulima wakipata mafunzo darasani na kwa vitendo***

Ujenzi wa mabwawa 3 ya kuhifadhia maji ya umwagiliaji; wakulima kwa kushirikiana na Halmashauri walijenga mabwawa 3 ya kukusanya maji ya umwagiliaji katika Skimu za umwagiliaji za Legezamwendo, Kitanda, na Madaba. Wakulima walishiriki kwa kuchangia nguvu kazi kwenye kuchimba mabwawa, kukusanya vifaa vya ujenzi kama mawe, mchanga na kokoto. Halmashauri ilitoa vifaa vya viwandani kama saruji na nondo. Picha zifuatazo zinaonesha ujenzi wa mabwawa ukiendelea.




***Ujenzi wa mabwawa skimu za umwagiliaji za Legezamwendo na Madaba***



***Bwawa la skimu ya umwagiliaji ya Madaba***

Uchimbaji wa mifereji ya umwagiliaji na vituo vya kugawa maji katika skimu za Legezamwendo na Madaba; baada ya ujenzi wa mabwawa ya kukusanyia maji, ujenzi wa mifereji ya kupitisha maji na vituo vya usambazaji wa maji vilijengwa kuruhusu maji kutoka kwenye mabwawa kwenda mashambani. Zoezi la kuchimba mifereji lilifanywa na wakulima wenyewe na Halmashauri ilisaidia kuijenga na kuisakafia. Picha ifuatayo inaonesha wakulima wakichimba mfereji mkuu wa umwagiliaji kutoka kwenye bwawa.




***Uchimbaji wa mfereji mkuu skimu ya Madaba***

Ujenzi wa barabara 9km kuanzia Lekindo hadi skimu ya umwagiliaji ya Madaba na ujenzi wa vituo vya mafunzo ya kilimo; barabara ilijengwa kurahisha usafirishaji wa mpunga kutoka skimu ya Madaba hadi kwenye kiwanda cha uchakataji wa mpunga na soko la mchele kurahisisha wakulima kusafirisha mpunga kwa kutumia magari, tofauti na ilivyokuwa hapo awali. Halmashauri imejenga vituo vya mafuzo ya kilimo 5 katika Kata za Matemanga, Mtina, Nakapanya, Mbesa na Marumba kwezesha wakulima kupata usaidizi wa huduma za kilimo zinapohitajika. Picha ifuatayo inaonesha barabara iliyojengwa kuunganisha Skimu ya Madaba na Lekindo.



***Ujenzi wa barabara ya Lekindo Madaba***

**5.0 RASLIMALI**

Uboreshaji wa uzalishaji wa zao la mpunga na kuongeza thamani ulihusisha matumizi ya raslimali. Halmashauri ilitoa raslimali fedha, utaalamu na vifaa, na jamii ilichangia nguvu kazi kwa kukusanya vifaa vya ujenzi kama mawe, kokoto na mchanga pamoja na kuchimba mabwawa na mifereji. Mchanganuo wa raslimali zilizotumika umebainishwa kwenye jedwali Na.2.

**Jedwali Na 2: Matumizi ya Raslimali**

| Na. | Kazi zilizotekelezwa | | Aina ya Raslimali | Thamani Tshs |
|---|---|---|---|---|
| 01 | Ujenzi wa baraba ya Lekindo Madaba | | -Nguvu kazi, vifaa vya ujezi kama katapila | 50,000,000.00 |
| 02 | Kuimarisha skimu 5 za umwagiliaji | Lekindo | - Nguvu kazi, vifaa vya ujezi | 220,000,000.00 |
| | | Misyaje | - Nguvu kazi, vifaa vya ujezi | 435,000,000.00 |
| | | Kitanda | - Nguvu kazi, vifaa vya ujezi | 655,000,000.00 |
| | | Madaba | - Nguvu kazi, vifaa vya ujezi | 600,000,000.00 |
| | | Legezamwendo | - Nguvu kazi, vifaa vya ujezi | 140,000,000.00 |
| 03 | Ujenzi wa ghala | | - Nguvu kazi, vifaa vya ujezi | 800,000,000.00 |
| 04 | Ujenzi wa mashine ya uchakataji mpunga | | - Nguvu kazi, vifaa vya ujezi | 130,000,000.00 |
| **Jumla** | | | | **3,030,000,000.00** |

**6.0 MATOKEO**

Uboreshaji wa uzalishaji wa mpunga na uongezaji wa thamani umeleta matokeo mbalimbali; wakulima wamenufaika na mafunzo ya kilimo bora cha mpunga na wanatumia ujuzi waliopata katika kuboresha uzalishaji wa mpunga. Jumla ya wakulima 150 walinufaika na mafunzo yaliyotolewa na KATC Moshi na MATI Ilonga. Kutokana na ujuzi waliopata wakulima, wameongeza uzalishaji kutoka tani 1.2 - 1.8 kwa hekta hadi kufikia tani 1.9 - 2.9 kwa hekta kwa mwaka 2015. Ongezeko la uzalishaji limeimarisha uhakika wa chakula na kipato cha mkulima. Picha ifuatayo inaonesha mashamba ya mpunga yaliyoboreshwa.



***Mashamba ya mpunga yaliyoboreshwa***

Skimu za umwagiliaji zimejengwa na kuimarishwa; skimu 5 kati ya 13 zimeimarishwa kwa kusakafiwa kupunguza upotevu wa maji. Utunzaji wa skimu upo chini ya kamati za umwagiliaji zilizo chini ya uangalizi wa kitengo cha umwagiliaji cha idara ya kilimo ya Halmashauri. Picha ifuatayo inaonesha mwonekano wa skimu ya umwagiliaji kabla na baada ya ujenzi.



***Ujenzi wa skimu na baada ya kukamilika***

Halmashauri imefanikisha ujenzi wa maghala 11 ya kuhifadhi mazao kwenye vijiji 11 yenye ujazo tofauti. Vilevile Halmashauri imejenga vituo 5 vya mafunzo ya kilimo. Maghala yaliyojengwa ni kwa ajili ya kuhifadhi mazao mbalimbali zaidi ya mpunga kama korosho, mahindi na kunde. Kujengwa kwa maghala haya kumesaidia wakulima kuhifadhi mazao kwa gharama nafuu. Usimamizi wa maghala upo chini ya Serikali za Vijiji. Picha zifuatazo zinaonesha baadhi ya maghala yaliyojengwa.



***Ghala la kijiji cha Chingulungulu,***




***Ghala la kijiji cha Namasakata***



***Ghala la kijiji cha Muhuwesi***

Tokeo jingine ni kujengwa kwa baraba ya 9km kuunganisha eneo la skimu la Madaba na Lekindo ambapo usafirishaji wa mazao umeboreshwa; wakulima wanaweza kusafirisha mpunga kutoka shambani kwa gharama nafuu na bidhaa kutoka maeneo mbalimbali hadi eneo la skimu. Wafanyabiashara wanaweza kununua mpunga na kusafirisha kutoka eneo la skimu ya madaba. Picha ifuatayo inaonesha barabara iliyojengwa.



***Baraba ya Lekindo - Madaba***

Kiwanda cha kuchakata mpunga kimejengwa kwenye kiwanja Na. 31 na 32 kilichopo kwenye kijiji cha Nakayaya-bias. Kiwanda hiki kimekamilika na kinafanya kazi. Kiwanda kimefanyiwa majaribio na kuonekana kinafanya kazi kwa mujibu wa vigezo vinavyokubalika. Kiwanda hiki mbali na kukoboa mpunga, kinapanga mchele kwenye madaraja na kuufungasha kwenye vifungashio vya ujazo tofauti. Kiwanda kina uwezo wa kuchakata na kufungasha tani 20 za mchele kwa siku. Picha ifuatayo inaonesha kiwanda cha kuchakata mpunga.




***Kiwanda cha kuchakata mpunga***

Halmashauri imewawezesha wakulima kuunda ushirika wa umwagilijaji; baada ya kupata mafunzo wakulima wameanzisha vyama 13 vya umoja wa wakulima wa mpunga na chama 1 cha ushirika. Vyama vya wakulima na ushirika vinafanya kazi ya kutafuta soko la mpunga na kuunganisha wakulima na taasisi za fedha ili kupata mikopo. Ushirika unaweka dhamana kwa mikopo ya wakulima na vyama vya wakulima vinaunganisha wakulima na wauzaji wa pembejeo za kilimo.

## 7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Kuhakikisha matokeo ya jitihada yanakuwa endelevu, Halmashauri ina mikakati ifuatayo;

Halmashauri inaendelea kuhamasisha jamii kwenye skimu za umwagiliaji kushiriki kikamilifu kutunza na kusimamia skimu. Uhamasishaji unafanywa na Maafisa Ugani, vilevile Halmashauri imewapa jukumu Madiwani na viongozi wa kisiasa wa maeneo husika kuendelea kuhamasisha jamii kulinda na kutunza skimu za umwagiliaji.



*Mkutano wa uhamasishaji ukiendelea*

Halmashauri imekuwa ikiendelea kutoa mafunzo kwa wakulima kupitia Maafisa Ugani wa kilimo kuboresha uwezo wao wa kulima kisasa. Halmashauri inaendelea kujenga vituo vya mafunzo ya kilimo kwenye kata mbalimbali ili kuwapelekea wakulima huduma na taarifa za kilimo na masoko kwa ukaribu zaidi. Jitihada hizi zinaenda sambamba na kuimarisha umoja wa wakulima wa umwagiliaji waweze kutumia raslimali ya maji kwa ufanisi na uendelevu. Uimarishaji wa umoja wa wakulima kusimamia matumizi ya maji unafanywa kwa mujibu wa mwongozo wa matumizi ya raslimali maji ambao upo chini ya Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya (DADPs).

Halmashauri inaendlea kuboresha mazingira ya kazi ya Maafisa Ugani kuwezesha kudumu katika vituo vyao vya kazi. Halmashauri imekuwa ikitenga bajeti kwa ajili ya motisha kwa maafisa ugani wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu na kuwanunulia vitendea kazi kama vile pikipiki.

Halmashauri inahimiza kusimamia sheria ndogo za Vijiji na umoja wa watumia maji, kuwezesha matumizi ya maji kwa mujibu wa sheria na kuzingatia mwongozo wa Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya 2010 na Sheria ya Umwagiliaji ya 2013. Sheria ndogo pia inahimiza ukusanyaji wa ada kwa ajili ya fedha za kutunza na kufanya matengenezo ya miundombinu ya skimu. Halmashauri ina mpango wa kuanzisha kituo cha taarifa za biashara cha kukusanya na kutawanya taarifa za biashara ya mazao ya kilimo kwa wakulima.

Halmashauri inaendelea kuboresha mahusiano na wadau wengine kwa kuhamasisha kuingia ubia na sekta binafsi na kuhimiza sekta binafsi kuwekeza kwenye viwanda vya kuchakata mpunga na kuwezesha wakulima kuuza mchele badala ya mpunga ili kuongeza kipato. Vilivile Halmashauri ina mpango wa kuendelea kujenga barabara kwenye skimu zote za uzalishaji wa mpunga kurahisisha usafirishaji wa mazao ya kilimo na kupanua eneo la skimu ili wakulima wengi waweze kunufaika. Picha ifuatayo inaonesha ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji.



***Ukarabati na Upanuzi miundombinu ya skimu***

**8.0 SIRI ZA MAFANIKIO**

Siri zilizopelekea matokeo chanya ya jitihada hii ni ubunifu na utayari wa Timu ya Menejimenti ya Halmashauri kusaidia jamii katika kuboresha miundombinu ya umwagiliaji. Matumizi sahihi ya kutumia feha za maendeleo kutoka Serikali Kuu kupitia mradi wa DADPs DIDT na MIVARF, mahusiano imara baina ya Timu ya Menejimenti, Madiwani na wadau kama Taasisi ya utafiti wa Maendeleo ya Kilimo Naliendele Kanda ya Mtwara na KATIC Moshi ni siri nyingine ya mafanikio. Taasisi hizi kwa kushirikiana na

Halmashauri walitoa mafunzo kwa wakulima kuhusu kilimo cha kisasa yaliyowezesha kufikia matokeo makubwa.

# Rejea


Abiona, A. I. and Bello, W. N. (2013). Grassroots Participation in Decision-Making Process and Development Programmes as Correlate of Sustainability of Community Development Programmes in Nigeria, *Journal of Sustainable Development; Vol.* 6 (3):47-57. Canadian Centre of Science and Education, [www.ccsenet.org/jsd] site visited on 19 /03/ 2013.

Apolo, Kansiime (2013). The Impact of Public Procurement Reforms on Service Delivery in Uganda; Bishop Stuart University.

Chibehe, M.M. (2004). Factors Affecting Sustainability of Farmer Groups: the case of Twikinde Malimbichi Cooperative Society. MA Dissertation, SUA, Unpublished, 90pp.

Helene Bie Lielleor and Ulrik Lund-Sorensen (2013). FARMERS' CHOICE evaluating an approach to agricultural technology and adoption in Tanzania, Rockwool Foundation research Unit, PRACTICAL ACTION Publishing, pp. 154.

Helmsing, A. H. J. (1995). *Local Government Central Finance.*An Introduction: NewYork USA

Howlett. D and J. Nagu. (1997). *Agricultural Project Planning in Tanzania, A handbook on cycles and sequences, participation, identification, planning and design, economic and financial analysis, and environmental assessment of agricultural projects.* ISBN 1898828261. pp 89.

Kusago, Takayoshi. (2008). *Sustainable Livelihood and Happy Generation in Minamata-City Japan*: A Model for Endogenous Community Development.

Makonda, K.S.C. (2003). Partnership and sustainability of water supply systems in Bukombe District, Tanzania. *MA Dissertation*, Sokoine University of Agriculture, Morogoro, Tanzania. Unpublished. pp.154

Mwanga, J.N. (2011). Empowerment of Local Society in Tanzania –the Nucleus for Development- With Experience from Indonesia and Japan, *Rare Series Policy Paper*, Local Government Training Institute, Dodoma Tanzania. 100 pp.

Ohama, Y. (2002). Basic Framework and viewpoints of Participatory Local Social Development (PLSD) and construction of its evaluation framework.

Porter, Michael E. (1998). *Competitive Advantage: Creating and Sustaining Superior Performance*, 397

pp, Amazon.

Pretty, J.N. (1995). Participatory learning for sustainable agriculture. *World Development* 23(8): 1247-1263.

Scoones, I. and John Thompson (1994). *BEYOND FARMER FIRST: Rural people's knowledge, agricultural research and extension practice*. Intermediate Technology Publications LTD, London, UK, pp.301.

Sharma, P.N. and Ohama, Y. (2007*). Participatory Local Social Development-An Emerging Discipline*, Bharat Book Centre Publishers & Distributors, Lucknow India. pp. 467.

Shikuku, O.M. (2012). Community related Variables influencing sustainability of water projects in Nyando District a case. *MA Dissertation*, University of Nairobi, Digital Repository

URT (1998). Local Government Reform Agenda

URT, (2010). Public private partnership (PPP) *Act*, no 18 of 2010, pp 21

URT (2011). Millennium Development Goals, Tanzania country report. Ministry of Finance and Economic Affairs, Dar es Salaam – Tanzania.

Zadeh, B.S. and Nobaya, A. (2010). Participation and Community Development. *Current Research Journal of Social Sciences* 2(1): 13-14, 2010. [http://maxwellsci.com/print/crjss/v2-13-14.pdf] site visited on 22/07/2014.